# MAPENDEKEZO YA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU

## KUHUSU HALI YA HAKI ZA BINADAMU KATIKA KIJIJI CHA MSOMERA, TARAFA YA NGORONGORO, TARAFA YA LOLIONDO NA SEHEMU YA TARAFA YA SALE



APRILI - SEPTEMBA 2023

# MAPENDEKEZO YA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU KUHUSU HALI YA HAKI ZA BINADAMU KATIKA KIJIJI CHA MSOMERA, TARAFA YA NGORONGORO, LOLIONDO NA SEHEMU YA TARAFA YA SALE

## APRILI- SEPTEMBA 2023

# YALIYOMO

**MUHTASARI** ........ **vii**
A. Kijiji cha Msomera ........ viii
B. Tarafa ya Ngorongoro ........ xi
C. Loliondo na Sale ........ xvii

*SHUKURANI* ........ *xxiv*
*VIFUPISHO* ........ *xxv*

***SURA YA KWANZA* ........ *1***
**UTANGULIZI WA JUMLA ........ 1**

**1.0 Utangulizi wa Jumla** ........ **1**
1.1 Muundo wa Taarifa Hii ........ 2
1.2 Malengo ya Taarifa Hii ........ 2
1.3 Methodolojia ya Taarifa Hii ........ 3
1.4 Matarajio ya Taarifa hiii ........ 3
1.5 Changamoto za Uandaaji wa Taarifa Hii ........ 4

***SURA YA PILI* ........ *5***
**MAREJEO YA NYARAKA MBALIMBALI ........ 5**

**2.0 Utangulizi** ........ **5**
**2.1 Sheria na Sera Mbalimbali** ........ **5**
2.1.1 Sheria na Miongozo ya Kimataifa ........ 5
2.1.2 Sheria na Miongozo ya Kikanda ........ 7
2.1.3 Sheria za Kitaifa ........ 8

**2.2 Nyaraka Mbalimbali** ........ **11**
2.2.1 Muhtasari wa kikao cha halmashauri ya Kijiji cha Msomera ........ 11
2.2.2 Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji cha Msomera ........ 11
2.2.3 Sheria ndogo za (Usimamizi wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi) za Halmashauri ya Kijiji cha Msomera za Mwaka 2016 ........ 11

***SURA YA TATU* ........ *13***
***SEHEMU YA KWANZA* ........ *13***
**TAARIFA YA HALI YA HAKI ZA BINADAMU KIJIJI CHA MSOMERA WILAYA YA HANDENI MKOANI TANGA ........ 13**

**3.1 Maelezo ya Awali** ........ **13**
3.1.1 Kuhusu Kuhamishwa kwa Wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro ........ 13
3.1.2 Historia ya Kijiji cha Msomera ........ 14

3.1.3 Chimbuko la Mgogoro wa Ardhi katika Kijiji cha Msomera ....15
3.1.4 Malengo ....15
3.1.5 Methodolojia. ....16
3.1.6 Eneo la ziara na Muda wa Ziara ....16
3.1.7 Changamoto za Ziara....16

SEHEMU YA PILI .... 17

MATOKEO YA ZIARA....17

3.2 UTANGULIZI.... 17

3.2.1 Hali ya Haki za Binadamu kwa Wananchi waliohama kutoka Ngorongoro.... 17
3.2.2 Huduma za Jamii na Miradi ya Maendeleo .... 17
Picha 3.1: Josho jipya lilijengwa Msomera ambalo tuliliona wakazi wa ziara....17
Picha 3.2: Bwawa la kisasa lililojengwa Msomera ....18
Picha 3.3: Jengo la Kituo cha Afya kinachochengwa Msomera....19
Picha 3.4: Kisima cha maji kilichojengwa katika kitongoji cha katikati kilichopo Msomera ....20
Picha 3.5: Picha ya Kamati ya Ulinzi ya Wilaya Handeni, Timu ya Ziaea wakiongea na baaadhi ya wanafunzi wa Sekondari ya Msomera wakati wa ziara. Pembeni ni moja wapo ya madarasa ya kisasa ya shule hii. .... 20
3.2.3 Changamoto za Wananchi waliohama kutoka Tarafa ya Ngorongoro ....21
Picha 3.6: Nyumba ya vyumba 3 ya mfano wa nyumba zilizojengwa Msomera...21
3.2.4 Mahitaji ya Wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro....29
3.2.5 Ufafanuzi wa Serikali....29
3.2.6 Hali ya Haki za Binadamu kwa Wenyeji wa Msomera....30
3.2.7 Ufafanuzi na Hoja za Serikali ....34

SEHEMU YA TATU.... 37

UCHAMBUZI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI .... 37

3.3 UTANGULIZI....37

3.3.1 Uchambuzi wa Madai ya Wananchi wa Ngorongoro na Ufafanuzi wa Serikali.... 37
3.3.2 Uchambuzi wa Madai wa Wenyeji wa Msomera na Ufafanuzi wa Serikali....41
3.3.3 Mapendekezo Mahususi ``( Specific Recommendations) ....44

SEHEMU YA NNE .... 47

MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO.... 47

3.4 UTANGULIZI....47

3.4.1 Mapendekezo ya Jumla .... 47
3.4.2 Hitimisho .... 47

## SURA YA NNE..................................................49
### SEHEMU YA KWANZA..................................................49
### HALI YA HAKI ZA BINADAMU TARAFA YA NGORONGORO..............49
**4.1 UTANGULIZI**.................................................. **49**
4.1.1 Kuhusu Tarafa ya Ngorongoro..................................................49
4.1.2 Kuhusu Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro..................................................50
4.1.3 Historia ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)..................................................51
4.1.4 Malengo ya Kuanzishwa kwa NCAA..................................................51
4.1.5 Malengo ya Ufuatiliaji..................................................51
4.1.6 Matarajio ya Ufuatiliaji..................................................52
4.1.7 Methodolojia..................................................52
4.1.8 Eneo la ziara na Muda wa Ziara..................................................52
4.1.9 Changamoto za ziara..................................................52
### SEHEMU YA PILI..................................................53
### MCHAKATO WA KUONDOA WATU KATIKA HIFADHI..........................53
**4.2 UTANGULIZI**.................................................. **53**
4.2.1 Chimbuko la Nia ya Kutaka kupunguza Watu katika Hifadhi..................................................53
4.2.2 Hatua zinazochukuliwa Kutatua changamoto za Uhifadhi..................................................54
4.2.3 Changamoto ya Zoezi la Kuhama kwa Hiari..................................................55
Picha 4.1 : Wananchi wakiwa katika mkutano wa hadhara..................................................55
Picha 4. 2: Mhe. Waziri Mkuu pamoja na Wajumbe na Wananchi kutoka Ngorongoro baada ya kuwasilisha ripoti jijini Dodoma..................................................57
Picha 4.3: Barua ya Mkurugenzi Ngorongoro Ikielekeza Million 190 za Tarafa ya Ngorongoro kwenda Wilaya Handeni..................................................60
Picha 4.4: Barua za kuhamisha fedha za miradi ya uviko 19 kutoka Ngorongoro kwenda Msomera..................................................61
Picha 4.5: Shule ya Msingi ya Bweni Endulen ambayo kwa sasa haina vyoo na watoto takriban 700 wanalala hadi wanne kwa kitanda katika mabweni mawili pekee. Kila bweni lina uwezo wa kubeba watoto 40 pekee..................................................62
Jedwali 4.1 : Changamoto za Huduma za Elimu Tarafa ya Ngorongoro..................................................62
Jedwali 4 2: Changamoto Huduma za Afya kwa baadhi ya kata za Tarafa ya Ngorongoro..................................................63
Picha 4.5:Choo ambacho hakijakarabatiwa kwasababu ya kukosa kibali S/M Endulen..................................................65
Picha 4.6: Ofisi ya kijiji cha Mokla iliyoezuliwa na upepo na hadi sasa haijakarabitwa..................................................65
Picha 4.7: Mabaki ya ng'ombe waliokufa kutokana na kupewa chumvi yenye sumu..................................................66
Picha 4.8 : Barua kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuelekeza watumishi wenyeji kuhamishwa..................................................67
Picha 4.9: Dekezo kuhusu kuhakiki mali za Watumishi Wazawa (Wamasai) kwa lengo la Kujua Mali zao kwa ajili ya hatua zaidi hasa kushinikizwa kuhama... 68
Picha 4.10: Formu Maalum kwa Watumishi wa Kimasai katika Mamlaka ya Ngorongoro..................................................68

4.2.4 Mahitaji ya Wananchi Kuhusu Zoezi la Kuondolewa Wananchi Ngorongoro...69
4.2.5 Ufafanuzi wa Serikali Kuhusu Changamoto za zoezi la Kuhama kwa Hiari.....70
4.2.6 Matumizi ya Vyombo vya usalama Unaoendelea Tarafa ya Ngorongoro.......72

**SEHEMU YA TATU...75**

**UCHAMBUZI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI...75**

**4.3 Utangulizi...75**
4.3.1 Ufafanuzi wa Serikali Kuhusu zoezi la Kuhama...75
4.3.2 Uchambuzi kuhusu Changamoto ya Huduma za Kijamii...76
Picha 4.9: Ripoti ya Flying Medical Service 1985-2021...79
4.3.3 Mapendekezo Mahususi...83
4.3.3.1 Kwa Serikali...83
4.3.3.2 Kwa Wananchi...84
4.3.3.3 Kwa Wadau wa Maendeleo...85
4.3.3.4 Kwa Watetezi /CSOs...85

**SEHEMU YA NNE...86**

**MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO...86**
4.0 Utangulizi...86
4.1 Mapendekezo ya Jumla...86
4.2. Hitimisho...89

**SURA YA TANO...91**

**SEHEMU YA KWANZA...91**

**HALI YA HAKI ZA BINADAMU TARAFA YA LOLIONDO NA SEHEMU YA SALE...91**

**5.1 Kuhusu Tarafa ya Sale na Loliondo...91**
5.1.1 Kuhusu Pori Tengefu la Pololeti...91
5.1.2 Malengo ya Ufuatiliaji Katika Eneo la Kilometa za Mraba 1,502...93
5.1. 3 Matarajio ya Ufuatiliaji...93
5.1.4 Methodolojia...94
5.1. 5 Eneo la ziara na muda wa ziara...94
5.1.6 Changamoto za Ziara...94

**SEHEMU YA PILI...95**

**MCHAKATO WA KUTWAA ENEO LA KILOMITA ZA MRABA 1,502 NA KULIFANYA KUWA ENEO LA PORI LA AKIBA LA POLOLETI...95**

**5.2 Utanngulizi...95**
5.2.1 Chimbuko la Nia ya Kutaka Kutenga Eneo la Kilometa za Mraba 1,502...95
5.2.2 Uwepo wa Vijiji Kisheria...95
5.2.3 Vichocheo vilivyo Pelekea Kutwaliwa kwa Eneo la Kilometa za Mraba 1,502.... 96
5.2.4 Kubadilishwa kwa Sheria ya Wanyamapori Mwaka 2009...99

5.2.5 Kukiukwa kwa Makubaliano ya Mwaka 1958 ........ 99
5.2.6 Utaratibu Uliotumika Kutwaa Ardhi ya Vijiji `( Kilometa za Mraba 1,502) ......100
5.2.7 Changamoto za Zoezi la Uwekaji Mipaka ........105
Picha 5.1: Sehemu ya Wajumbe wa Kamati ya Wananchi kutoka Tarafa za Loliondo na Sale wakiwa katika Mapitio ya rasimu ya Kwanza ya Taarifa. ........106
Picha 5.2: Sehemu ya Wananchi kutoka tarafa ya Loliondo na Sale katika Kikao cha pamoja kujadili mgogoro wa Ardhi ........107
Jedwali 5.1 : Orodha ya mikutano ya ukusanyaji wa tarafa ya Loliondo na Sale ...107
Jedwal 5.2 : Baadhi ya Viongozi wa kisiasa, wa kimila na watetezi wa haki za binadamu walioendelea kukamatwa, kuitwa vituo vya polisi na kuhojiwa wakati wa zoezi la kukusanya maoni ya wananchi (Machi-Aprili 2022). ........113
Jedwali 5.3 : Makazi na Miundo Mbinu iliyobomolewa ........115
5.2.8 Mahitaji ya Wananchi kuhusu Zoezi la Uwekaji Mipaka ........115
5.2.9 Ufafanuzi wa Serikali Kuhusu Changamoto Zoezi la Uwekaji Mipaka ........116

***SEHEMUYA TATU ........ 119***

**CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA BAADA ENEO LA KILOMITA 1,502 KUGEUZWA KUWA HIFADHI ........ 119**

**5.3 UTANGULIZI ........ 119**
5.3.1 Changamoto Zinazoendelea Kujitokeza Baada ya Eneo la Vijiji Kutwaliwa ........119
Jedwali 5.4 : Idadi ya Mifugo iliyokamatwa pamoja na Fedha zilizotumika kukomboa kwa kila Kata ........120
Jedwali 5.5 : Eneo Kata Mbili kabla na baada ya kuchukuliwa na Serikali...122
5.3.2 Hoja za Wananchi ........123
5.3.3 Ufafanuzi wa Serikali kuhusu Changamoto Hizi ........123

***SEHEMU YA NNE ........ 124***

**UCHAMBUZI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI ........124**

**5.4 UTANGULIZI ........124**
5.4.1 Kukosekana kwa maeneo ya malisho, maji na chumvi ........124
5.4.2 Wananchi Kukosa Makazi ya Kuishi ........125
5.4.3 Mifugo Kufa kutokana na Ukame na hakuna vyanzo mbadala vya maji......125
5.4.4 Mifugo kukamatwa, kutaifishwa na kutozwa faini ........126
5.4.5 Uamuzi wa Mahakama dhidi ya Tangazo la Waziri ........126
5.4.6 Mapendekezo Mahususi ........ 127

***SEHEMU YA TANO ........ 129***

**MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO ........129**

**5. 0 UTANGULIZI ........129**
5.1 Mapendekezo ya Jumla ........129
5. 2. Hitimisho ........130

# MUHTASARI

Taarifa hii ni ya watetezi wa haki za binadamu Tanzania iliyoandaliwa baada ya kufanya ziara katika Kijiji cha Msomera kilichopo wilaya ya Handeni mkoa wa Tanga, ziara katika tarafa ya Ngorongoro, Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale zinazounda wilaya ya Ngorongoro iliyopo mkoa wa Arusha. Ziara hiyo ilifanyika baada ya Serikali kuwahamisha baadhi ya wakazi wa tarafa ya Ngorongoro kwenda katika Kijiji cha Msomera mwaka 2022 kwa madai ya ongezeko la watu pamoja na kuhifadhi eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Lengo la ziara lilikuwa ni kufuatilia hali ya haki za binadamu Ngorongoro na kwa wakazi wa Msomera (wenyeji na wageni waliohamia kutoka Ngorongoro). Lengo la ziara katika tarafa ya Ngorongoro lilikuwa ni kufuatilia hali ya haki za binadamu na katika tarafa ya Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale lilikuwa pia ni kufuatilia hali ya haki za binadamu na mifugo baada ya Serikali kutwaa eneo la vijiji 14 lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,502 mwezi Juni mwaka 2022 na kisha kulitangaza kuwa pori tengefu na baadae kuwa pori la akiba la Pololeti.

Taarifa hii ina sura kuu tano ambapo sura ya kwanza inaelezea utangulizi wa jumla kuhusu taarifa hii. Sura ya pili inaelezea marejeo ya nyaraka mbalimbali tulizorejea wakati wa kuandika taarifa hii ikiwa ni pamoja na sheria na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Sura ya tatu inaelezea hali ya haki za binadamu katika kijiji cha Msomera. Sura hii ya tatu imegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza inaelezea kijiji cha Msomera pamoja na kilichotokea baada ya wakazi wa Ngorongoro kuhamishiwa kijijini hapo ikiwemo mgogoro wa ardhi uliopo baina ya wananchi wenyeji na wageni waliotoka Ngorongoro. Sehemu ya pili inaelezea matokeo ya ziara hii ikiwa ni pamoja na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali katika Kijiji hicho pamoja na changamoto zilizopo. Sehemu ya tatu inaelezea uchambuzi na mapendekezo mahususi kwa Serikali, wananchi, watetezi wa haki za binadamu na wadau wa maendeleo. Sehemu ya nne inaelezea mapendekezo ya jumla na hitimisho.

Sura ya nne inaelezea hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Ngorongoro, kuhusu huduma za kijamii na hali ya mifugo katika tarafa hii. Sura hii pia ina sehemu nne. Sehemu ya kwanza inaelezea utangulizi, sehemu ya pili inaelezea mchakato na namna jinsi ambavyo watu waliondolewa katika ardhi mseto kwenye eneo la hifadhi ya Ngorongoro. Sehemu ya tatu inaelezea uchambuzi wa hoja au madai ya wananchi na mapendekezo mahususi kwa Serikali, wananchi, waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu na wadau wa maendeleo. Sehemu hii pia inaelezea hali ya huduma za kijamii ikiwemo fedha za maendeleo kuhamishwa kwenda Msomera na kusitishwa kwa miradi ya maendeleo katika tarafa hii. Sehemu ya nne inaelezea mapendekezo ya jumla na hitimisho.

Sura ya tano inaelezea hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale. Sura hii ina sehemu tano. Sehemu ya kwanza inaelezea utangulizi, sehemu ya pili inaelezea jinsi mchakato wa kutwaa eneo la kilometa za mraba 1,502 na kulipa hadhi ya kuwa Pori la Akiba la Pololeti. Eneo lililochukuliwa na Serikali lilikuwa ni mali ya vijiji 14 lakini Serikali ilichukua bila ya kuwashirikisha wananchi kikamilifu. Sehemu ya tatu inaelezea changamoto mbalimbali zilizojitokeza baada ya eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa na Serikali na baadae kugeuzwa kuwa pori la akiba la Pololeti. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa eneo la malisho na maji kwa mifugo, utozwaji wa faini kubwa na kutaifishwa kwa mifugo ya wananchi inayodaiwa kukutwa kwenye pori la akiba la Pololeti, kuongezeka kwa umasikini kutokana na mifugo kufa kwa kukosa malisho na ukame. Sehemu ya nne inaelezea uchambuzi na mapendekezo mahususi kwa Serikali, wananchi, watetezi wa haki za binadamu na wadau wa maendeleo. Sehemu ya tano inaelezea mapendekezo ya jumla na hitimisho katika sura hii.

Ifuatayo ni muhtasari wa matokeo ya ufuatiliji wa ziara hii uliofanyika katika eneo la Msomera, Loliondo na Ngorongoro. muhtasari huu unalenga kutoa kwa ufupi matokeo ya ufuatiliaji huu pamoja na mapendekezo yake kwa ufupi kama ifuatavyo;

### A. Kijiji cha Msomera

Katika ziara hii kwenye kijiji cha Msomera tulikutana na wananchi takriban 100 kati ya waliohamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro na sasa wanaishi Msomera. Lakini pia tulikutana na wenyeji wa Msomera pamoja na kufanya nao mkutano kijijini hapo.

#### (i) Mambo yaliyobainika kwa ufupi

- **Kaya 48 hazikupewa nyumba za kuishi.** Idadi ya wananchi waliohamishwa katika awamu ya kwanza kutoka Ngorongoro ni 3,010 ambazo ni jumla ya kaya 551. Lakini nyumba zilizojengwa ni 503. Hivyo kaya 48 hazikupewa nyumba za kuishi katika Kijiji cha Msomera.
- **Wananchi kutoka Ngorongor o wamepewa nyumba moja bila kuzingatia ukubwa wa kaya au idadi ya wanafamilia.** Kila kaya imejengewa nyumba moja yenye vyumba vitatu na sebule bila kuzingatia idadi ya wanafamilia. Kwa mfano, moja ya kaya tuliyoitembelea ina wanafamilia 10: mume, mke, watoto wawili, mama mzazi, kaka mwenye wake wawili na watoto wawili wote hawa wamepewa nyumba moja yenye vyumba vitatu hali ambayo imeathiri utamaduni, malazi na hivyo kupelekea kutafuta hifadhi kwa wenyeji.
- **Maji ya kunywa yaliyopo Msomera ni ya chumvi.** Wananchi ikiwemo na wanafunzi wa shule ya sekondari Msomera walitueleza kwamba maji hayatoki mara kwa mara lakini pia ni ya chumvi hivyo kwa ujumla walisema miundombinu haijakaa sawa kulingana na mahitaji yao.
- **Wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro hawakushirikishwa kikamilifu.** Wananchi wamelalamikia mchakato wa uhamishwaji ulifanyika bila kuwashirikisha viongozi wao wa kisiasa wa ngazi mbalimbali kuanzia Kijiji hadi ngazi ya Wilaya (Halmashauri ya Wilaya). Hadi sasa hawajui ni

lini utaratibu huu ulijadiliwa na kupitishwa katika vikao vya Halmashauri ya Wilaya na pia katika Baraza la Wafugaji la Ngorongoro ambalo ni chombo cha Kisheria chenye mamlaka ya kusimamia mambo yote ya wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro.

- **Uwepo wa Mgogoro wa Ardhi kati ya Wageni na Wenyeji wa Msomera.** Wageni waliohamishiwa Msomera walitueleza uwepo wa mgogoro wa ardhi kati yao na wenyeji. Ardhi waliyopewa inamilikiwa kihalali na wenyeji kwani wenyeji waliwaonyesha hati za umiliki wa maeneo hayo.
- **Kuna hatari ya kufa au kutoweka kwa utamaduni wa jamii ya kimaasai na Kidatoga.** Katika ziara hii wananchi walitueleza wasiwasi wa kutoweka au kufa kwa tamaduni na mila zao kwani mazingira ya sasa ya Msomera hayaruhusu jamii ya wamaasai na wadatoga kufurahia na kuendeleza utamaduni wao kwa mfano utamaduni wa kukaa na mifugo nyumbani, matambiko, sherehe za kimila, maeneo ya kuabudia, kuvusha rika na kustaafisha rika.
- **Uhaba wa chakula kwa wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro.** Wananchi wanakabiliwa na njaa kwasababu ya kutokupewa chakula kwa wakati kama ambavyo awali waliahidiwa na mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro. Wananchi waliahidiwa kuletewa mahindi kila baada ya miezi mitatu wakiwa Msomera wakati wa ziara tulikuta wana miezi mitatu bila kuletewa chakula.
- **Mifugo kufa kwa kukosa malisho.** Mazingira ya Kijiji cha Msomera hayana malisho kwa mifugo hasa ng'ombe hali hii imepelekea ng'ombe wengi waliohamishwa kutoka Ngorongoro kufa kwa kukosa malisho. Hivyo, wananchi wamelazimika kuhamisha mifugo iliyobaki kwenda sehemu mbalimbali nje ya Msomera kama vile kilindi, gendagenda, kabuki, korogwe, mzeri n.k.
- **Ukosefu wa Zahanati na Vituo vya afya.** Msomera kuna uhaba wa zahanati hivyo huwalazimu wananchi kutembea umbali mrefu kwaajili ya kupata huduma za kijamii. Kwa mfano wakazi wa kitongoji cha Mkababu ambapo nyumba 100 zilijengwa na kupewa wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro hawana zahanati, hivyo kulazimika kutembea takribani kilomita 16 ili kufuata huduma hizo katika kitongoji cha katikati kilichopo Kijiji cha Msomera.
- **Uhaba wa Walimu na Shule kulingana na Wingi wa wanafunzi.** Wananchi wakazi wa kitongoji cha Mkababu hawana shule na hivyo kulazimika kutembea takribani kilomita 16 ili kufuata huduma hizo katika Kitongoji cha katikati kilichopo kijiji cha Msomera. Shule ya Msingi Samia Suluhu Hassan iliyopo kitongoji cha katikati kijiji cha Msomera, ina jumla ya wanafunzi 883 lakini walimu ni 7 tu (5 kiume na 2 kike) hivyo kuna uhaba wa walimu 12, madawati 186 na vyumba vya madarasa. Shule ya sekondari Msomera ina jumla ya wanafunzi 206 lakini walimu wapo 8 tu na wa kike ni mmoja tu na ndio mwalimu pekee anayefundisha masomo ya sayansi.

- **Wananchi wenyeji wa Msomera hawakushirikishwa wakati wa utwaaji wa ardhi yao.** Wananchi wenyeji wa Msomera katika mkutano wa hadhara na katika usahili wa mtu mmoja mmoja, walitueleza kwamba hawakushirikishwa wakati wa uandaaji wa makazi na baadae uhamisho wa wananchi kutoka katika tarafa ya Ngorongoro kwenda kijiji cha Msomera. Wananchi wote ambao tuliweza kuwafikia katika ziara yetu katika kijiji cha Msomera walieleza kuwa maeneo yao ya makazi, mashamba, makaburi na malisho yalitwaliwa kwa nguvu na kujengwa makazi ya watu wa Ngorongoro na miradi mbalimbali bila kushirikishwa.
- **Wananchi hawakupewa taarifa sahihi kuhusu eneo la Msomera.** Wananchi kabla ya kuhamishwa kwao waliahidiwa kwamba sehemu wanapohamishiwa kuna mandhari mazuri, ardhi yenye rutuba na ambayo haimilikiwi na mtu yeyote. Pia waliambiwa eneo hilo ni pori tengefu linalomilikiwa na Serikali hivyo hakuna mtu anayeishi katika eneo hilo. Na pia eneo hilo ni zuri na linafaa kwa mashamba na malisho. Lakini baada ya kufika katika eneo la Msomera walikuta ni ardhi ya kijiji na ina wamiliki wake, hakuna maeneo ya malisho kwakua maeneo mengi ni ya watu na yaliyobakia ni mapori yasiyokuwa na nyasi. Eneo la Msomera ni kame na lisilofaa kwa malisho.
- **Ardhi ya wenyeji wa Msomera kutwaliwa bila utaratibu wa kisheria.** Kijiji cha Msomera kilisajiliwa mwaka 1992 na baadhi ya wananchi walikuwa wanaishi katika Kijiji hicho kabla ya uhuru, wengine walihamia baada ya uhuru. Baada ya Kijiji kusajiliwa kilikuwa na mamlaka kamili na tangu hapo miradi mbalimbali ya maendeleo kama josho, mabwawa, soko, zahanati, shule, ofisi ya Kijiji na hivi karibuni mwaka 2014 Rais wa awamu ya nne Mhe. Jakaya Kikwete alizindua mradi wa madume ya mbegu ya ng'ombe wa kisasa. Mwaka 2016 waliandaa na kupitisha mpango wa matumizi bora ya ardhi wa hadi mwaka 2026. Wananchi wengi walituonyesha hati za kumiliki ardhi katika Kijiji cha Msomera ambazo walipata kihalali. Na pia kuna kesi zilizoamuliwa na Mahakama Kuu ya Tanzania juu ya umiliki wa ardhi katika Kijiji cha Msomera. Mfano kesi ya *Juma Iddi Chambo dhidi ya Julius Leki [Rufaa ya Kesi ya Ardhi Na. 12 ya Mwaka 2019]* Mahakam Kuu ya Tanzania, masjala ya Tanga ilitambua uhalali wa ardhi iliyogawiwa na Kijiji cha Msomera tarehe 01/02/2010.
- **Vitisho na Kunyimwa Uhuru wa Kujieleza .** Tangu zoezi la wageni kuhamishiwa katika Kijiji hicho lianze, wenyeji wa Msomera wamekuwa wakikumbana na vitisho mbalimbali ikiwemo kupigwa, kuwekwa ndani, kutishiwa kufungwa n.k.
- **Msomera kuitwa Wavamizi.** Wananchi wenyeji wa Msomera, walilalamika juu ya kauli ya Serikali ya kuwa wao ni wavamizi katika Kijiji cha Msomera ilihali wao ni wakazi halali wa Kijiji hicho. Walidai pia kwamba Serikali iliwapelekea maendeleo tangu zamani kama vile shule ya msingi, zahanati, barabara, bwawa, soko na mradi wa madume ya mbegu ya ng'ombe za kisasa mwaka 2014.

#### ii) Mapendekezo kwa Ufupi

- Tunishauri Serikali iwachukulie hatua baadhi ya watumishi wake wanatoa vitisho dhidi ya wanachi wa Ngorongoro hasa pale ambapo wanadai haki zao
- Tunaishauri Serikali kutatua changamoto ya maji ya chunvi kule msomera
- Tunaishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa shule mpya ya msingi mkababu na ujenzi wa bweni kwa wanafunzi wa sekondari
- Tunamuomba Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusitisha zoezi la kuondoa wananchi katika tarafa ya Ngorongoro ili kutoa nafasi ya kufanyia kazi changamoto hizi na pia kutoa nafasi ya kuandaa kwa pamoja mpango wa uhamaji kwa hiari wa muda mrefu na mfupi wenye kuzingatia misingi ya haki za binadamu na shirikishi.
- Tunawaomba wananchi kudumisha amani na wazingatie njia ya kimahakama katika kudai haki zao
- Tunawaomba wananchi kufanya mikutano na kujadiliana juu ya namna ya kutatua changamoto za huduma za kijamii
- Tunawaomba wananchi kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo ambayo wamepewa
- Tunawaomba wadau wa maendeleo kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo katika Kijiji cha Msomera
- Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika Kijiji cha Msomera
- Kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kutatua changamoto katika Kijiji cha Msomera na tarafa ya Ngorongoro
- Tunawasihi baadhi ya waandishi wa habari waache kueneza propaganda za chuki na uongo dhidi ya wananchi wa Kijiji cha Msomera na tarafa ya Ngorongoro
- Waandishi wa habari wazingatie misingi ya taaluma yao kwa kutoa taarifa ambazo sio za upande mmoja na watoe taarifa za kweli
- Serikali iandae "resettlement plan" kwanza kabla ya kuhamisha watu kutoka eneo moja kwenda kwingine.
- Wananchi wenyeji wa Ngorongoro wameitaka Serikali wapitie mchakato wa ulipaji fidia kwa kuwa sio shirikishi na wala hauko wazi. Na kuwa kiwango cha Milioni Kumi kama pesa ya fidia kwa kila kaya iongezeke hadi kufikia million 50 au million 100 kwa atakayetaka kuchagua kuchukua hela na kwenda anakotaka.

### B. Tarafa ya Ngorongoro

#### (i) Katika ziara hii kwenye Tarafa ya Ngorongoro yalibainika mambo yafuatayo;

- **Wananchi Kutokushirikishwa.** Mnamo Januari 11, 2022 Serikali kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ilitangaza wito kwa wananchi kuhama kwa hiari kutoka katika tarafa ya Ngorongoro kwenda katika Kijiji cha Msomera kilichopo Handeni mkoani Tanga. Baada ya maagizo hayo ya Mkuu wa Mkoa, wananchi kwa kushirikiana na viongozi wao wa kimila na kisiasa

walifanya mikutano na jitihada mbalimbali kutaka ushirikishwaji lakini hawakushirikishwa. Mbali na mikutano ya hadhara, wananchi walifanya vikao mbalimbali wakijadili hatua za kuchukua ili kunusuru ardhi yao kuchukuliwa bila ridhaa yao pamoja na kujadili changamoto zilizokuwa zinawakabili watetezi wa ardhi Ngorongoro. Mashirika ya haki za binadamu pia yaliratibu vikao vya wananchi, watetezi wa ardhi na haki za binadamu kwa ujumla ili kujadili kwa mapana na kuandaa mapendekezo yao kabla ya utekelezwaji wa amri ya Mkuu wa Mkoa ya watu kuhama kwa hiari katika tarafa ya Ngorongoro, jitihada zote hizi hazikuzaa matunda kwa kuwa hakukua na nafasi yoyote ya kuwashirikisha wananchi na makundi ya kijamii.

- **Kufifishwa kwa Huduma za Msingi za Jamii.** Wananchi walitueleza kwamba moja ya changamoto kubwa wakati wa zoezi la kuhama kwa hiari ni kunyimwa huduma za kijamii kwa wananchi ili kuwalazimisha kuhamia katika kijiji cha Msomera. Huduma mbabalimbali za jamii kama vile huduma za mabweni kwa shule za msingi na secondari, huduma za vyoo mashuleni, huduma za afya , huduma za barabara, huduma za maji , vibali vya ujenzi n.k.
- **Wananchi wa Ngorongoro hawakuwa na uhuru wa kuchagua.** Wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro hawakupewa chaguo kama wanataka kwenda Msomera au sehemu nyingine ambayo wao wangependa kuhamia.
- **Mchakato wa tathmini ya fidia ulighubikwa na usiri.** Mchakato ulikuwa wa siri na wananchi hawakupewa mrejesho wa tathmini iliyofanyika na kiwango ambacho walistahili kulipwa. Fedha pekee iliyofahamika tangu awali ni fedha taslimu za kitanzania shilingi milioni kumi maarufu kama ***"asante mama" wanayosema ni hela ya Rais Samia.*** Lakini pia fidia haikuzingatia ukweli kwamba wananchi wa Ngorongoro walizuiliwa kufanya shughuli za kimaendeleo kama vile kujenga nyumba za kisasa, kilimo na kumiliki vyombo vya usafiri. Wananchi wengi walipewa fidia ya kuanzia milino moja hadi milioni tatu.
- **Wananchi walipewa fidia ndogo ambayo haiendani na uhalisia. Matoeko** ya kutokuwa na utaratabu shirikishi wa kuhamisha watu kwa hiari umechangia watu wengi kupata fidia ndogo na hata wengine kutokupata fidia hadi sasa. Wananchi hawakushirikishwa kikamilifu na kwa uwazi katika kukokotoa fidia zao. Walidai hawakuwahi kupewa nafasi ya kujadiliana na kukubali utaratibu utakaotumika kukokotoa fidia zao ukizingatia aina ya maisha wailiyokuwa wanaishi katika Tarafa ya Ngorongoro. Mamlaka ya hifadhi ndio iliwafungulia akaunti za benki kwaajili ya kuwekewa fedha za fidia. Wale ambao walikuwa na akaunti zao tayari zilikataliwa.
- **Kuhamishwa kwa fedha za huduma za Kijamii**
  Kiasi cha shilingi za kitanzania, 355,500,000 cha fedha za mradi wa uviko-19 (Covid-19 relief funds) zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro zilihamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni bila kuazimiwa na baraza la madiwani wa Halmashauri

ya Wilaya ya Ngorongoro. Fedha hizo zilihamishwa kwa barua mbili zenye Kumb. No.NGOR/DC/F.1/02/VOLIII/68 na Kumb. No.NGOR/DC/F.1/02/VOLIII/69 za tarehe 31/03/2022. Fedha hizo zilikuwa kwaajili ya kujenga madarasa na mabweni ya wanafunzi katika shule tatu za Serikali ambazo ni Nainokanoka, Embarway na shule ya Wasichana ya Ngorongoro pamoja na shule za msingi Endulen, Misigiyo na Esere. Baada kwa barua ya Mkurugenzi wa Halmashauri zilihamishwa kwenda Wilayani Handeni Tanga. Kwa ujumla zaidi ya billion 3 za kitanzania zilizotengwa kwa kuendesha miradi mbalimbali katika Tarafa ya Ngorogoro zilielekezwa kwenda kwingine.

- **Kukosekana kwa mabweni, madarasa na matundu ya vyoo Mashuleni**
  Wanafunzi katika shule zote Ngorongoro kwa sasa hawana madarasa, mabweni pamoja vyoo hali inayoweza kupelekea madhara ya kiafya kwa wanafunzi na magonjwa ya mlipuko kwani imewalazimu wanafunzi kulala wawili kwenye kitanda kimoja kutokana na upungufu wa mabweni. Kwa mfano shule ya msingi Enduleni pekee ina upungufu wa matundu 42 ya vyoo.

- **Kuzorota kwa huduma za afya na kuzuiwa kwa Huduma ya Afya ya Dharula**
  Huduma za afya zimezorota sana katika tarafa ya Ngorongoro. Tarafa ya Ngorongoro ina kituo cha afya kimoja, zahanati Nane, Hospitali Moja ya Enduleni inayosimamiwa na Kanisa Katoliki. Huduma hizi zinahudumia Tarafa nzima yenye kata 11 na vijiji 25 na takriban watu 110,000. Pia kulikuwa na huduma ya dharua pamoja na chanjo kupitia mradi wa Flying Medical Service ulioko chini ya Kanisa Katoliki ambayo initoa huduma za chanjo na huduma za dharura katika sehemu za pembezoni ikiwemo Ngorongoro. Mnamo 08/04/2022 Serikali ilisitisha huduma ya afya ya dharura iliyokuwa inatolewa na Flying Medical Service. Flying Medical Servive ilizuiliwa kuanya shughuli zake na kupelekea watu wengi sana kuadhirika. Huduma zote hizi zimezorota kwa njia mbambali zikiwemo kukosa ukarabati, kukosa majengo mapya , kuzuiwa kwa ndege kuruka, kuondolewa kwa fedha za miradi, kunyimwa vibali vya ujenzi,ukarabati na kunyimwa kuwa na makazi ya kisasa.

- **Wananchi kukatiwa huduma ya maji na NCAA**
  Huduma za maji zimezorota haswa kwenye kata zote za Ngorongoro. Wananchi walitueleza pia kuwa, hata kwenye kata ya Ngorongoro, Misigiyo na Nainokanoka ambazo zilikuwa zikipata huduma za maji baada ya kuzuiliwa kupeleka mifugo yao ndani ya kreta kwa ajili ya maji na chumvi,sasa wanadai kukatiwa huduma ya maji na NCAA.

- **Changamoto ya barabara**
  Wananchi walilamika kuwa kumekuwa na changamoto ya barabara, wakati barabara zinazoenda kwa wananchi na kuunganisha vijiji zikiwa na changamoto na wakati mwingine kutopitika kabisa lakini barabara zinazoenda katika maeneo ya wawekezaji kama mahoteli, loji na kambi za kitalii zinawekewa miundombinu nzuri.

- **Kunyimwa Vibali vya Ujenzi**
  Wakati wa zoezi la kuhama kwa hiari, mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ilisitisha vibali vya kufanya ujenzi au ukarabati wa aina yoyote kwa kwa nyumba za wananchi na taasisi zinazotoa huduma za jamii. Kwa mfano ukarabati wa hospital, shule za msingi, nyumba za watumishi n.k. Kwa mfano shule ya msingi Endulen vyoo vimejaa na imewalazimu wanafunzi kujisaidia nje au porini. Kwa mfano katika shule ya Enduleni, wanafunzi wanalala 4 kwenye kitanda kimoja kutokana na ujenzi wa mabweni uliokuwa unaendelea kusitishwa. Shule hii ina jumla ya wanafunzi 1,900 (wakike 785 na wa kiume 1054) ina mabweni mawili tu. Kati ya hao wanafunzi 617 wanaishi bweni (wakike 272 na wa kiume ni 345) na kuna mabweni mawili tu. Hospitali ya Enduleni pia imeshindwa kufanya ukarabati wa nyumba zinazotumika kutoa huduma kwa wananchi kwa kukosa vibali. Suala la vibali inatumika kama silaha kubwa kuhakikisha hakuna kinachoendelea tena katika Tarafa ya Ngorongoro. Majengo ya serikai pia kama ofisi za kata zimeshindwa kufanya ukarabati wowote. Mfano shule na ofisi ya Mtendaji wa Kijiji cha Mokilal zilipata changamoto ya kuezuliwa paa na mvua na hadi tunapoandika taarifa hii ofisi hiyo haijaezekwa.

- **Ng'ombe kupewa chumvi yenye sumu na hatimae kufa**
  Kabla ya mwaka 2016 wafugaji wa kata zilizopo karibu na bonde la kreta la Ngorongoro walikuwa wanalisha mifugo yao kwenye bonde la kreta kwasababu ni eneo lenye malisho, maji na chumvi ya mifugo. Mwaka 2016 Serikali kupitia kwa Mhe.Waziri Mkuu ilizuia wafugaji kuingiza mifugo katika bonde la kreta na Waziri Mkuu aliamuru kwamba Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro iwe inaleta chumvi mbadala, kuweka na kuboresha huduma ya maji katika maeneo hayo ambayo ni; Kata ya Ngorongoro, Kata ya Misigiyo na Kata ya Nainokanoka. Mamlaka ilifanya hivyo lakini mwaka 2021 wananchi waligundua kwamba chumvi iliyokuwa inaletwa ilikuwa na sumu na hili lilithibitishwa na vipimo vya maabara ikiwemo maabara ya taifa ya mifugo ambapo tarehe 27/12/2021 sampuli ya chumvi katika vijiji vya, Kayapus, Mokilal, Erkeepus na Misigiyo ilipelekwa maabara ya taifa ya mifugo na kufanyiwa uchunguzi tarehe 27/12/2021 na majibu ya kiuchunguzi yalibaini chumvi hiyo kuwa na sumu. Baada ya janga hilo kutokea mifugo mingi ilikufa hali iliyopelekea umasikini kwa wananchi, na hadi sasa hakuna hatua zozote za kisheria au kiutawala zilizochukuliwa dhidi ya mamlaka na hakuna fidia iliyotolewa kwa wananchi.

- **Wenyeji wa Ngorongoro kunyimwa ajira**
  Katika mahoteli na maeneo mengine ya ajira ndani ya tarafa ya Ngorongoro wenyeji hawapewi kipaumbele kutokana na propaganda zilizoenezwa kuwa wenyeji wakipewa ajira wataenda kufuga ng'ombe ndani ya eneo la hifadhi ya mamlaka ya Ngorongoro. Hii pia inadhibitishwa na barua inayotoka NCAA yenya kumb.No. DE 70/341/04/40 kwenda kwenye maloji, kambi za kitalii na mahoteli ambayo imetoa maelekezo ya kuhamishwa kwa watumishi wenyeji wanaofanya kazi katika maeneo hayo tajwa na kupelekwa katika sehemu zingine.

- **Kuna madai ya unyanyapaa na ubaguzi kwa watumishi wenyeji/ wamaasai**
  Kumekuwa na vitendo vinavyoashiria ubaguzi dhidi ya watumishi wenyeji wanaofanya kazi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, watumishi wenyeji ndani ya NCAA wamekuwa wakipewa dodoso za kueleza mali wanazomiliki na burua hizo inalenga watumishi wenyeji pekee na sio watumishi wote ndani ya NCAA.
- **Gharama ya kupaki gari (Parking fee) kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro**
  Wakazi wa tarafa ya Ngorongoro wanakumbana na changamoto ya kulipia gharama ya kupaki gari ndani ya makazi yao. Mtu yeyote anayemiliki gari na ni mkazi wa tarafa ya Ngorongoro anatakiwa kulipa kiasi cha Tshs. 118,000 kwa gari binafsi na Tshs 300,000 kwa gari ya biashara kwa mwaka. Mbali na gharama ya kupaki gari, ikifika 11:30 Jioni kama mtu hajaingia getini hatoruhusiwa tena kuingia hata kama mtu huyo ni mkazi wa Ngorongoro.
- **Kudhoofishwa kwa Shughuli za Baraza la Wafugaji**
  Baraza la wafugaji ni chombo kilichoanzishwa kwa Tangazo la Serikali la mwaka, 2000 kwa lengo la kusimamia maslahi ya wenyeji ndani ya NCAA. Kwa sasa shughuli za Baraza la Wafugaji zimedhofika na kusimama kabisa baada ya Baraza kunyang'anywa fedha za uendeshaji na pia baada ya miradi yote ya Baraza kuhamishiwa Halmashauri chini ya usimamizi wa Afisa Maendeleo ya Jamii.

**ii) Mapendekezo kwa ufupi Kuhusu Ngorongoro**

- Tunapendekeza Serikali katika ngazi ya Wilaya na Mkoa kupeleka miradi / huduma za kijamii zinazotengwa katika bajeti ya TAMISEMI katika tarafa ya Ngorongoro kwa kuwa ni haki ya wananchi wa Ngorongoro kuendelea kupata huduma za jamii kama watanzania wengine.
- Tunaishauri Serikali,Wizara ya maliasili na utalii, Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro, mashirika yanayojihusha na uhifadhi kujadili pamoja na wananchi na kutathmini upya hoja zinazoisukuma Serikali kupunguza idadi ya watu Ngorongoro.
- Tunaisihi Serikali kuruhusu vyombo huru vya habari kuchunguza na kupata ukweli katika eneo la Ngorongoro, yaani upande wa jamii na uhifadhi, ili kuja na matokeo ambayo yatasaidia kupata ufumbuzi wa changamoto zinazoikumba jamii na uhifadhi.
- Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro inapaswa kuboresha nyumba za asili zilizopo Ngorongoro kwani ni kivutio cha utalii na zimependesha eneo hilo.
- Mamlaka husika kama wizara ya Habari na mawasiliano, iwahoji na kuwachukulia hatua wamiliki na wahariri wa baadhi ya magazeti na vyombo vingine, ambavyo kwa nyakati tofauti zimetumia muda mwingi kueneza chuki na uongo, kutoa kauli za kudhalilisha dhidi ya wenyeji wa Ngorongoro

- Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ione umuhimu wa kutoa vibali kwa ajili ya huduma muhimu za kijamii kwa maisha ya wanadamu kama vile ujenzi wa vyoo, majengo ya huduma za jamii, hospitali ya Endulen, vituo vya afya, zahanati, madarasa, makazi na mabweni ya wanafunzi.
- Ili kuepusha watu kufa kwa kukosa matibabu Serikali iruhusu huduma ya afya ya dharura kwa jamii iliyokuwa inatolewa na Flying Medical Service Ngorongoro.
- Serikali isitisha zoezi la uhamishwaji wa wananchi ili kufanya tathimini shirikishi juu ya changamoto zilizojitokeza katika awamu ya kwanza ya kuhamisha watu kwa hiari.
- Tunaomba Serikali kuwachukulia hatua za kisheria na kuwaamuru maofisa wa Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kulipa fidia kwa wananchi waliopoteza mifugo yao baada ya kula chumvi iliyothibitishwa na wataalamu kuwa na sumu.
- Tunaiomba Serikali iwashauri na kuwataka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itoe vibali kwa asasi za kiraia na wadau wengine kwenda kutoa huduma za msingi kwa jamii katika Tarafa ya Ngorongoro
- Serikali ione umuhimu wa kuwarudishia wananchi wa tarafa ya Ngorongoro fedha ya mradi wa Covid-19 zilizohamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.
- Serikali ya wilaya iandae na kutangaza utaratibu wa uchaguzi wa nafasi za madiwani na viongozi wengine waliohama ili wananchi wapate uwakilishi katika vyombo vya maamuzi.
- Asasi za kiraia zinashauriwa kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro. Kwa mfano miradi ya afya, maji, elimu, kuwawezesha kiuchumi hasa kwa wakina mama n.k.
- Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Ngorongoro.
- Serikali kwa kushirikiana na Asasi za kiraia, viongozi wa jamii na jamii na viongozi wa Wilaya iandae mpango wa kuhama kwa hiari (Voluntary-relocation Plan) , itakayotoa dira ya namna gani wananchi wa Ngorongoro wanaweza pungua kwa njia ya kuhama kwa hiari bila kuvunja haki za binadamu. Mfano mpango huu utakuwa na fursa za wananchi kuchagua namna gani wanataka kuondoka kwa hiari, kwani wengi wamependekeza wapewe nafasi ya kuchagua.
- Fidia ya sasa inayotelewa ni kidogo sana , tunapendekeza wale watakao kuwa tayari kwa hiari yao kuhama wote kila kaya ipewe hela million 50 kama fudia wakati wa kuhama pamoja na nyumba na ardhi au milioni 100 kwa wale ambao watahitaji kwenda wanapochagua wao.
- Kuendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro

### C. Loliondo na Sale

Katika tarafa za Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale tulibaini mambo yafuatayo wakati na baada ya Serikali kutwaa eneo la kilomita za mraba 1500.

#### i) Mambo yaliyobainika kwa ufupi katika ufuatiliaji huu

- **Utwaaji wa eneo la kilomita za Mraba 1502 haukuzingatia sheria**
  Serikali imetwaa eneo la vijiji 14 lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1502 kuwa Pori Tengefu la Pololeti na baadae kutangazwa tena na Raisi kuwa Pori la Akiba. Utwaaji wa ardhi hiyo ulighubikwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu kama vile; watu kupigwa risasi, watu kupotezwa,wananchi kukamatwa na kuwekwa ndani kwa muda mrefu pamoja na ukamataji na utozaji wa faini kwa mifugo na maelfu ya watu wengine kukimbilia nchi jirani ya Kenya kwa hofu ya kukamatwa na kuteswa.
- **Eneo la kilometa za mraba 1502 ni eneo halali la vijiji 14**
  Eneo la kilometa za mraba 1502 ni eneo la vijiji 14 vilivyopo tarafa za Loliondo na Sale. Vijiji vyote hivyo vimesajiliwa na vina hati na hivyo utwaaji wake ni lazima kuwepo na ushirikishwaji wa viongozi na wadau wa vijiji vyote ambao ndio waathirika kama maeneo yao yatatwaliwa. Utwaaji wa ardhi wa vijiji kuwa pori tengefu na baadae kuwa pori la akiba haikufuata utaratibu wa kisheria ikiwemo kushirikisha viongozi na wadau ambao ndio waathirika wakubwa wa ardhi hiyo kutwaliwa. Kwenye kesi ya **Ndalamia Taiwap na Wenzake 4 dhidi Waziri wa Mali Asili na Utalii na Mwenzake, No.21 ya 2022**, Mahakama imeamuru kuwa Waziri wa Mali Asili na Utalii hakufuata utaratibu wakati anatwaa eneo la vijiji kuwa pori la tengefu. Wakati huo huo, mahakama kuu ya Tanzania katika kesi ya **Latang'amwaki Ndwati na Wenzake 7 v. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shauri No. 178 ya 2022** imesimamisha operesheni ya tangazo la Raisi hadi kesi inayopinga tangazo hilo itakapo sikilizwa na kuamuliwa na mahakama.
- **Utwaaji wa eneo la Km 1502 halikuwa zoezi shirikishi**
  Zoezi la kumega eneo la kilomita za mraba 1502 halikuwa shirikishi na kwa maana hiyo halikuwa na ridhaa ya wananchi wala viongozi wao. Taratibu za utawala bora na pamoja na taratibu za utawala wa sheria unalazimisha zoezi lolote linalogusa maeneo yanayotumiwa na wananchi kihalali kuwe na mchakato shirikishi na kisheria katika kufanya maamuzi yoyote.
- **Matumizi makubwa ya nguvu za vyombo vya usalama**
  Taarifa mbalimbali za wananchi katika kata zote nane ambazo operesheni ya utwaaji wa eneo imepita inaonyesha kuwa kulikuwa na matumizi makubwa ya nguvu katika zoezi hili la utwaaji wa eneo la km za mraba 1502. Takriban magari zaidi ya 50 ya vikosi mbalimbali vya usalama yanasadikiwa kuwa yalikuwa yanasimamia zoezi hili katika ukanda wote huu wa kata nane zenye eneo hili la km za mraba 1502. Vikosi vingi vyenye silaha za moto, mabomu

ya machozi yalionekana yakizingira maeneo yote ambayo vigingi vilipangwa kupitishwa. Katika zoezi hili wananchi wamelalamika kuwa kulikuwa kuna matumizi holela ya risasi na mabomu. Risasi zilipigwa mara kwa mara juu na mabomu pale palipoonekana kuna watu. Milio ya silaha iliweza zua taharuki na mshtuko mkubwa kwa jamii. Wapo waliokimbia walitoa mimba kutokana na mshtuko, mifugo kupigwa risasi na mingine kupotea.

- **Kupoteza uhai na kupotea kwa Watu**
  Zifuatazo ni baadhi ya taarifa za kupotea kwa watu siku ya oparesheni na vifo vilivyotokana na oparesheni hiyo kama ilivyoelezwa na waathirika katika kila kata.

  i. Kutokana matumizi makubwa ya nguvu katika zoezi hili, watu Katika zoezi hili hadi sasa kutokana na matokeo ya ufuatiliaji huu , tumebaini uwepo wa taarifa za kifo cha Askari ( Jina) mmoja anayedaiwa kupigwa mshale katika mvutano wa wannchi na askari katika kata ya Ololosokwan.
  ii. Imebainika kuwa yupo mzee Oriasi ole Ng'iyo, mwenye umri wa miaka 80 aliyekeruhiwa na vikosi vya Operesheni na kupotea hadi leo
  iii. Imebainika kuwa pia kuna mtoto mmoja kutoka Kijiji cha Piyaya alipotea wakati wa oparesheni hii na hadi leo hajulikani alipo.
  iv. Pia wananchi wa Piyaya walitueleza kuhusu mtoto aliyepoteza uhai wakati wanawake waliokuwa wanakimbia kumwangukia mtoto na hatimaye kupoteza maisha.
  v. Wapo pia watu zaidi ya 30 waliopigwa na kuumizwa na kulazimika kutafuta matibabu nje ya nchi.
  vi. Kuna taarifa pia kuwa yupo mtu wa kata ya Malambo aligongwa na magari ya Oparesheni na kupoteza maisha.

- **Kukamatwa kwa watu wengi wakiwemo viongozi wa kisiasa na Jamii**
  Zoezi la uwekaji vigingi lilikwenda sambamba na ukamataji holela wa wananchi katika maeneo husika. Utafiti huu umebaini kuwa walau kila kata ilikuwa na watu wasiopungua 30 waliokamatwa wakati wa zoezi hili. Toka zoezi hili lianze takribani jumla ya watu 200 walikamatwa na kupewa makosa mbalimbali kama ya mauaji, makosa ya uraia, makosa ya kuingia katika eneo linalotengwa pamoja na makosa mengine. Wengi walishia katika vituo vya polisi na kulipa kila mtu hongo ya million tatu kwa polisi. Waliofika mahakamani ni pamoja na wananchi 27 wakiwemo viongozi waliobambikiziwa kesi ya mauaji katika Mahakama ya Hakimu mkazi Arusha (Kesi ya Awali Na 11 ya Mwaka 2022 Jamhuri dhidi ya Molongo Daniel Paschal na wenzake 26) na kukaa gerezani kwa muda wa Zaidi ya miezi sita na badaye Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini kuiondoa kesi hiyo mahakamani. Pia wananchi 62 walikuwa kesi tofauti tofauti wakituhumiwa kuwa wao sio raia wa Tanzania na badaye kuamuliwa na mahakama kwa kuwaachia huru watuhumiwa baada ya upande wa mashitaka kushindwa kuthitibtisha madai yao (Mfano kesi ya Jamhuri dhidi ya Paulo Yale Mako

na wenzake 4, Kesi na 15 ya mwaka 2022, Kesi na 16 ya 2022 Jamhuri dhidi ya Samson Joseph Kipukya na wenzake 6 nk, kesi hizi zilifunguliwa katika mahaka ya wilaya ya Ngorongoro iliyopo Loliondo).

- **Watu kukimbia Nchi**
  Kutokana na nguvu kubwa iliyokuwa inatumika wakati wa oparesheni hii, wananchi takriban elfu mbili (2,291) waliweza kukimbilia nchi Jirani ya Kenya kuepuka kupigwa , kukamatwa na kuunganishwa katika kesi mbalimbali. Katia ya wananchi hawa 2,291 (Watoto walikuwa 1,652 Wanawake 528 Wanaume 100 na Watetezi wengine 30). Pi kuliwa na wagonjwa 30 waliondoka pamoja na ndugu zao. Kati ya watu waliokimbia walikuwepo pia watetezi wa haki za binadamu takribani 30 ambao walikuwa katika hali ya kutafutwa pengine kuunganishwa na shauri la mauaji liliokuwa mahamani. Hadi sasa hakuna taarifa kamili kama watu wote hawa wamesharudi katika jamii na kuendelea na shughuli zao za kawaida.

- **Watu kupigwa na majeruhi kunyimwa matibabu**
  Kutokana na mvutano uliojitokeza kati ya vikosi na wananchi, wapo wananchi walioumizwa na kupelekea kuhitaji matibabu ya haraka. Mfano katika kata ya Olosokwan pekee watu 30 pekee walipigwa na kujeruliwa kwa silaha za mpira pamoja na risasi za moto. Wengi wanaeleza walikosa ushirikiano wa matibabu katika vituo vya afya vya Loliondo kwa kuwa walitakiwa wawe na PF3 form ya polisi kitu ambacho kwenda polisi wao waliona ni kujipeleka kwenye shida zaidi.

- **Kuibuka kwa zoezi la Watu kuwa sio raia**
  Changamoto nyingine iliyoambatana na zoezi la uwekaji vigingi au inayofanya zoezi hili kuwa na sura ya matumizi makubwa ya nguvu ili kutisha watu ni suala la uraia. Kutokana ukweli kuwa jamii ya kimasai ipo pande zote mbili za mpaka (Kenya na Tanzania). Suala hili la uraia lilisababisha watu wengi kukamatwa takriban 150 kwa swala la uraia. Wengi waliishia katika hatua za awali lakini waliofika mahakamani na mashauri yao kusikilizwa ni watu 62.

- **Kukosekana kwa uhuru wa Habari**
  Katika ziara hii tumebaini pia kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa uhuru wa kujieleza na pia uhuru wa vyombo vya habari kutoa taarifa za operesheni hii. Vyombo vingi vya ndani vilipata vitisho na maelezo yasiyo rasmi kuwa taarifa zozote zinazonyesha uhalisia wa zoezi hili zisitolewe badala yake zipo baadhi ya vyombo vya habari vilitumika kufanya propaganda dhidi ya wananchi wa Loliondo. Waandishi wengi walishindwa kwenda Loliondo kutoa taarifa za kweli kutokana na hali ya vitisho wakihofi usalama wao. Kwa mfano Februari 03, 2022 jumla ya waandishi wa Habari 6 walikamatwa na askari wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro baada ya kufuatilia mkutano wa wanakijiji zaidi ya 200 waliofanya mkutano katika kata ya Nainokanoka katika tarafa ya Ngorongoro.

- **Kukosekana kwa uhuru wa Watetezi wa Haki za Binadamu**
  Watetezi wa haki za binadamu pamoja na mashirika ya utetezi wa haki za wafugaji wamekuwa katika wakati mgumu sana kufanya kazi zao za utetezi kipindi chote cha zoezi hili hadi hivi sasa.  Baadhi ya watetezi wa jamii walijikuta wakikimbia nchi kunusuru maisha yao huku wengine wakiunganishwa katika kesi ya mauaji. Kila kiongozi wa Serikali aliyefika katika eneo la Loliondo alitamka wazi wazi kupambana mashirika ya utetezi wa jamii pamoja na watetezi waengine wa jamii. Mashirika haya yalipekuliwa mara kwa mara na viongozi wao kutakiwa kwenda kuripoti katika vyombo vya usalama. Mwezi Februari mwaka 2022 Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) kwa kushirikiana na mashirika 20 ya kidini na ya haki za binadamu ulizuiwa kufanya ziara katika wilaya ya Ngorongoro kufuatilia hali ya haki za binadamu. Hata hivyo, ziara hiyo ilizuiliwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha baada ya mashirika hayo kufika Arusha kwa madai ya kwamba hayakuwa na kibali cha kufanya zaiara hiyo kutoka ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

- **Kupotea kwa mifugo na kuliwa na Wanyama wakali**
  Mifugo ilipotoea wakati wa oparesheni na mingine kuliwa na wanyama wakali kwa mfano mbuzi , kondo, ngombe na punda na wengine kupigwa risasi na askari wa oparesheni. Mfano kata ya Arash ng'ombe 17 walipigwa risasi.

- **Watu kuvunjiwa makazi yao na wengine kuacha mali zao**
  Katika zoezi hili wapo pia wanachi waliovunjiwa makazi yao ya kudumu. Kata zilizoadhirika zaidi na watu kuvunjiwa nyumba zao wakati wa zoezi hili ni pamoja na kata ya Arash, Ololosokwan na Malambo.  Mfano katika kata ya Malambo, vitongoji viwili vya ndinyeka na Sanjani ndio vilivyoathirika zaidi na zoezi hili. Vitongoji hivi vimepoteza mifugo mingi , nyumba , maeneo ya huduma za jamii kama makanisa, vituo vya afya pamoja na visima vya maji.  Mfano kitongji cha Sanjani nyumba 120 (81 maboma ya kiasili pamoja na nyumba za bati 40)  zilibolewa zilokuwa na kaya 450  sawa na jumla ya watu 1982, shule za awali mbili , zahanati  4 na kanisa moja kubwa., matenki matatu ya maji ya mvua. Kitongoji kingine katika kata hiyo hiyo ya malambo kilichoadhirika ni cha Ndinyeka , kilikuwa na nyumba 100 ( Maboma 89 nyumba za bati 11)  yenye kaya 287 sawa na watu 1468.  Kulikuwa na shule moja ya awali, vituo viwili vya kutolea huduma za chanjo kwa wanawake na watoto mbili , kanisa kubwa ambalo hadi sasa halijavujnwa;  mabwawa saba ya maji.

- **Mifugo kukamatwa, kutaifishwa na kutozwa faini. Hii ni changamoto** kubwa sana kwa wakazi wa maeneo ya Kirtalo, Soitsambu, Arash, Malambo, Sale, Piyaya, Loliondo, Ololosokwan, n.k. Mifugo yao imekamatwa kwa wingi, kuuzwa kwa mnada na mingine kutaifishwa. Wananchi walitueleza kuwa wahusika wa mifugo wakigundulika wamekuwa wanafunguliwa kesi mahakamani na kutozwa faini ya shilingi laki moja (Tshs. 100,000) kwa

ng'ombe na shilingi elf ishirini na tano (Tshs. 25,000) kwa mbuzi au kondoo. Kwa mfano kwa mwezi Novemba pekee mwaka 2022 ng'ombe 2,276 walitaifishwa katika kata ya Arash kwa kudaiwa kuingia katika hifadhi ya taifa ya Serengeti. Kwa kata nzima ya Arash kuanzia Juni 2022 hadi Aprili 2023 faini iliyolipwa na wafugaji ni milioni 860 kwa kudaiwa mifugo yao kuingia katika pori tengefu la Pololeti na hifadhi ya taifa ya Seerengeti.

- **Askari Kuswaga Mifugo na Kuwaingizwa kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti**

  Askari wanaolinda pori la akiba la Pololeti wamekuwa na tabia ya kuswaga mifugo na kuwaingiza kwenye pori la Pololeti na hatimaye kwenye hifadhi ya taifa ya Serengeti kwa lengo la kutoza faini au kutaifisha mifugo endapo mmiliki hatajitokeza.

- **Mifugo Kufa kutokana na Ukame na Kukosa Maji**

  Mifugo mingi imekufa kwa wingi kutokana na ukame ndani ya miezi 8 toka eneo hili litwaliwe. Eneo lililochukuliwa na Serikali ndio lilikuwa chanzo cha maji na malisho kwa mifugo kwa tarafa nzima ya Loliondo na Sale hasa wakati wa kiangazi.. Ni eneo ambalo lilikuwa na vyanzo vya maji hasa mito ya maji safi na salama kwa mifugo na binadamu. Mito hiyo yenye vyanzo vya maji ni ormungushi, orkereyani, esiyaiti na emurgur na yote imechukuliwa. Kabla ya eneo la Pololeti kutwaliwa na Serikali kulikuwa na mifugo takriban 973,745 lakini mara baada ya eneo kutwaliwa kata zote zinazo zunguka eneo hili la km za mraba 1502 zilipungua karibu nusu ya mifugo hasa ng'ombe. Mfano kata ya Arash ilikuwa na ng'ombe 56,000, lakini baada ya eneo kutwaliwa na Serikali ng'ombe 25,000 wamekufa kutokana na ukame.

- **Wananchi Kukosa Makazi ya Kuishi**

  Wakati wa zoezi la uchukuaji wa eneo la kilometa za mraba 1,502, wananchi walipewa notisi ya kuhama kwenye maboma yao ndani ya saa 24. Nyumba zao zilizungukwa na askari waliokuwa wanafanya oparesheni na kuwataka wahame mara moja. Hivyo wengi iliwalazimu kuhama bila kujua kuwa wanaenda kuishi wapi hali ambayo imewasababishia kutokuwa na nyumba na hivyo hawana makazi ya kuishi. Pia hakuna maeneo kwaajili ya wao kujenga nyumba kwani eneo liliobaki ni dogo sana. Mfano katika kata ya Malambo pekee , zaidi ya kaya 600 zimekosa mahali pa kuishi baada ya makazi yao kubomolewa wakati wa zoezi la uwekaji mipaka.

- **Watoto Kushindwa kwenda Shule kwa sababu ya kukosa ada**

  Wananfunzi wameshindwa kwenda shule kutoakana na umasikini uliosababishwa na mifugo kutaifishwa, kupigwa mnada na kupigwa faini na mifugo kufa kutokana na kukosa malisho. Asilimia 90 ya shughuli za kiuchumi kwa jamii ya kifugaji katika eneo hili ni shughuli za ufugaji asili unaotegemea sana eneo liliochukuliwa.

- **Kukosekana kwa maeneo ya malisho, maji na chumvi**
  Wananchi kwasasa hawana maeneo ya malisho kutokana na kwamba eneo ambalo walitenga kwa ajili ya malisho limechukuliwa na Serikali. Kwa mfano ukubwa wa Kijiji cha Ololosokwan ulikuwa ni hekari 51,230 kabla ya kuchukuliwa na Serikali. Serikali imechukua hekari 25,000 na kuwa sehemu ya pori tengefu la Pololeti na eneo hili lote ndio lilikuwa la malisho tu na sio makazi.

- **Miradi na Huduma Mbalimbali Kusitishwa**
  Wananchi wa kijiji cha Ololosokwan walikuwa wamewekeza kwenye mradi wa ubia na kampuni ya kitalii ya **And Beyond** kabla ya eneo kutwaliwa ambapo walikodisha ardhi yao. Kutokana na uwekezaji huo kjiji kilikuwa kinapata faida ya shilingi milioni 240 hadi 250 kwa mwaka na walikuwa wanalipia bima za afya kwa kaya masikini 30 katika kila Kijiji kwa mwaka, gharama ya matibabu kwa wagonjwa mahututi, na kusomesha wanafunzi wanaotoka kaya masikini ,hadi kufikia mwaka 2022 wanafunzi 600 walinufaika na mpango huo. Baada ya ardhi yao kuchukuliwa vijiji vimekosa mapato na huduma zilizokuwa zinatolewa kusitishwa.

- **Njaa na Umasikini Kuongezeka**
  Wakazi wa Loliondo na Sale ni wafugaji kwa asili na ndio shughuli pekee iliyokuwa inawaingizia kipato ikiwa ni pamoja na kupata chakula kama nyama na maziwa. Baada ya eneo kuchukuliwa na mifugo kufa, wamepoteza uchumi wao hali ambayo imewaletea umasikini mkubwa na hivyo wanakabiliwa na njaa. Hali hii imewalazimu kuchangiana chakula ili wasife njaa na kuna madai kuwa baadhi ya watu wamefariki kwa kukosa chakula.

- **Wananchi Kukosa Huduma ya Maji**
  Baada ya eneo la kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa ambalo ndio sehemu ya chanzo cha maji ya kunywa kwa binadamu, wananchi hawana huduma ya maji ya kunywa kwasasa. Hivi sasa wamama hutembea umbali wa kilometa za mraba 18 kutafuta maji ya kunywa na maji hayo mengi yanapatikana kwenye madimbwi. Hakuna visima vya maji kwaajili ya matumizi ya binadamu.

### ii) Mapendekezo kwa Ufupi

- Tunapendekeza Serikal kuingilia kati na kusitisha utaratibu wa sasa wa kukamata mifugo katika eneo la Pololeti na kutoza fedha nyingi kwa wananchi.
- Tunapendekeza Tume Huru ya Majaji iundwe kuchunguza ukiukwaji wa Haki za Binadamu uliotokea wakati wa zoezi la utwaaji wa ardhi ya Vijiji na kugeuzwa kuwa eneo la Pori la Akiba.
- Serikali ione umuhimu wa kurudisha fedha zilizokusanywa kwenye vijiji husika kwa ajili ya kutoa huduma za chakula, kulipia ada za wanafunzi.

- Kutokana na ukweli kwamba wamasai wamekuwa mstari wa mbele katika kutunza mazingira, basi Serikali iwaruhusu wananchi kuchunga katika eneo la Pololeti na kuendelea kutumia mbinu za kiasili katika kuhifadhi maeneo hayo kwa matumizi ya mifugo na wanyama
- Serikali ione umuhimu wa kufanya majadiliano na wananchi juu ya matumizi ya eneo la kilometa za mraba 1,502 ambalo ndio lilikuwa tegemeo pekee kwao.
- Serikali ikamilishe ujenzi wa barabara ya Loliondo - Mto wa mbu kwa kiwango cha lami
- Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa ifungue milango na kuweka mazingira mazuri kwa mashirika na watetezi wa haki za binadamu kufanya kazi Wilayani Ngorongoro.
- Serikali kufanya tathimini shirikishi juu ya changamoto zilizojitokeza wakati wa oparesheni ya kuwaondoa watu na kuweka vigingi katika tarafa ya Sale na Loliondo. Kuwepo na tume ya majadiliano na maridhiano ili kuhakikisha yaliyotokea hayatajirudia tena.
- Wananchi pamoja na viongozi wa kimila na kisiasa watafute fursa ya kufanya majadiliano na Serikali ili waweze kutatua changamoto ya mifugo kukamatwa na suala zima la faini na eneo la malisho ya mifugo.
- Wananchi wanapaswa kufanya mikutano mbalimbali na kujadiliana juu ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabili.
- Wananchi wanapaswa kubuni shughuli nyingine mbalimbali za kufanya ili kukuza uchumi wao tofauti na kutegemea ufugaji pekee ambao kwa kiasi kikubwa umezuiliwa na mazingira yalivyo kwasasa.
- Tunawaomba wadau wa maendeleo kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Loliondo na Sale.
- Kwa upande wa asasi za kiraia ni wakati sasa wa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Loliondo na Sale.
- Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Loliondo na Sale.

# SHUKURANI

Taarifa hii isingeweza kukamilika bila ushirikiano wa wananchi katika maeneo yote ya ziara, hivyo shukrani za kipekee ziwaendee wakazi wa Msomera, Ngorongoro, Loliondo na Sale kwa ushirikiano wao mkubwa waliotuonyesha. Wananchi wamekuwa na mchango mkubwa sana katika kutupatia taarifa za hali ya haki za binadamu na mifugo katika maeneo yao.

Tunashukuru pia kwa ushirikiano wa ofisi ya mkuu wa wilaya ya Handeni kwa kutukaribisha vizuri na kutupa ushirikiano wakati wa ziara kwenye Kijiji cha Msomera. Maelezo ya mkuu wa wilaya ya Handeni kuhusu historia na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali katika Kijiji cha Msomera yalikuwa ni muhimu sana kwetu.

Tunawashukuru pia wale wote kwa namna moja ama nyingine walituwezesha kufanya ziara hii. Tunawashukuru kwa muda na mchango wao katika kufanikisha ziara hii. Tunatambua pia ushirikiano wa uongaozi wa Baraza la Wafugaji Ngorongoro, madiwani pamoja na viongozi wa kijamii na kimila Ngorongoro.

Mwisho, tunashukuru mashirika yote yaliyojitolea kwa muda na rasilimali watu kufanya ufuatiliaji wa hali ya haki za binadamu Msomera, Ngorongoro, Loliondo na Sale. Mashirika hayo ambayo mengi ni wanachama wa THRDC, ni pamoja na Baraza la Wanawake Wafugaji (PWC), Shirika la Uraia na Msaada wa Kisheria (CILAO), Shirika la Uhifadhi wa Utamaduni wa Kimaasai (Tanzania Maasai Heritage), Taasisi ya Wanahabari ya Kusaidia Jamii za Pembezoni (MAIPAC), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Haki Madini, Shirika la Kusaidia Ustawi wa Wanawake na Watoto (WOCWELS), Jukwaa la Ardhi Tanzania (TALA), Mtandao wa Mashirika ya Kifugaji (PINGOs Forum), Shirika la Uhifadhi wa Mifumo ya Asili na Jadi (TEST), Shirika la Utafiti wa Kijamii na Huduma za Maendeleo (CORDs), Shirika la Kuwabariki Watoto wa Kike na Wanawake wa Jamii za Kifugaji Maasai (NAMGWO), HakiArdhi, Ujamaa Community Resource Team (UCRT), Shirika la Kuinua na Kusaidia Maisha ya Wafugaji (PALISEP), Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF), Shirika la Maendeleo ya Jamii ya Wafugaji wa Kimaasai (MPDO – LARETO), Chama cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania na Umajumui wa Afrika wa Uwezeshaji wa Kisheria (PALEI).

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **BBC** | – | Shirika la Utangazaji Habari la Uingereza |
| **CCM** | – | Chama Cha Mapinduzi |
| **CILAO** | – | Shirika la Uraia na Msaada wa Kisheria |
| **CSO** | – | Asasi za kiraia |
| **FPCT** | – | Kanisa la Pentekoste |
| **NCA** | – | Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro |
| **NCAA** | - | Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro |
| **NLUPC** | – | Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi |
| **NPC** | - | Baraza la Wafugaji Ngorongoro |
| **OBC** | – | Kampuni ya Uwindaji kutoka Falme za Kiarabu |
| **PGCA** | – | Pori la Uhifadhi ya Pololeti |
| **PWC** | – | Baraza la Wanawake Wafugaji |
| **TAMISEMI** | – | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **THRDC** | – | Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania |
| **UNESCO** | – | Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni Duniani |
| **KM** | - | Kilomita |



# SURA YA 1

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

Sura hii inaelezea utangulizi wa jumla kuhusu taarifa hii iliyoandaliwa na watetezi wa haki za binadamu baada ya kufanya ziara katika kijiji cha Msomera wilaya ya Handeni mkoani Tanga na kwenye tarafa tatu za wilaya ya Ngorongoro (Ngorongoro, Loliondo na Sale). Sura hii pia inaelezea muundo wa taarifa hii kwa ujumla. Taarifa hii ni ya watetezi wa haki za binadamu wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC). Wanachama hawa wanafanya kazi katika maeneo ya haki ya ardhi, mabadiliko ya tabia ya nchi, haki za wafugaji, ulinzi wa maliasili, haki za kiraia, haki za wananwake wa kifugaji, haki za kitamaduni na haki za binadamu kwa ujumla.

Mnamo mwezi Aprili mwaka 2023 watetezi wa haki za binadamu chini ya uratibu wa Mtandao walifanya ziara katika Kijiji cha Msomera wilaya ya Handeni mkoani Tanga. Ziara hiyo ililenga kufuatilia hali ya haki za binadamu na changamoto zinazojitokeza katika Kijiji cha Msomera baada ya wananchi kuhamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro kwenda Kijijini hapo ili kuweza kuwa na taarifa sahihi za pande zote kwa lengo la kuishauri Serikali, wananchi na wadau mbalimbali namna bora ya kutatua changamoto hizo kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu.

Mnamo mwezi Mei mwaka 2023 watetezi hao hao pia kama walivyofanya ziara katika Kijiji cha Msomera, walifanya ziara pia katika tarafa ya Ngorongoro, Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale ili kupata taarifa sahihi juu ya ushirikishwaji wa wananchi wa Ngorongoro kuhusu mchakato mzima wa uhamishwaji na kuangalia iwapo utaratibu wa kutwaa ardhi ulizingatiwa kabla ya eneo la kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa na Serikali kwenye tarafa ya Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale.

Baada ya kufanya ziara katika maeneo tajwa, masuala kadhaa kuhusu hali ya haki za binadamu, mifugo na wanyamapori yalijitokeza ambayo yalitulazimu kuandika barua kuomba ufafanuzi wa Serikali kwa ujumla. Kwa bahati mbaya mpaka tunaandaa taarifa hii hatukuweza kupata ufafanuzi wa Serikali kwenye maeneo ambayo tuliomba ufafanuzi na hivyo ilitulazimu kufuatilia kwenye mitandao ya kijamii kurejea kile ambacho Serikali iliwahi kutolea ufafanuzi siku za nyuma.

Hivyo katika taarifa hii tumeelezea hali ya haki za binadamu, hali ya mifugo na changamoto ambazo zinawakabili wananchi katika maeneo ya ziara pamoja na mapendekezo kwa wananchi, Serikali, watetezi/mashirika ya haki za binadamu, waandishi wa habari na kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

### 1.1 Muundo wa Taarifa Hii

Taarifa hii ina sura kuu tano ambapo sura ya kwanza inaelezea utangulizi wa jumla kuhusu taarifa hii. Sura ya pili inaelezea marejeo ya nyaraka mbalimbali zikiwemo sheria na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Sura ya tatu inaelezea hali ya haki za binadamu katika kijiji cha Msomera wilaya ya Handeni mkoa wa Tanga. Sura hii ina sehemu nne. Sehemu ya kwanza inaelezea mgogoro wa ardhi uliopo katika kijiji cha Msomera kutokana na wananchi wa Ngorongoro kuhamishiwa katika kijiji hicho. Sehemu ya pili inaelezea matokeo ya ziara hiyo. Sehemu ya tatu inaelezea uchambuzi na mapendekezo mahususi kuhusu hali ya haki za binadamu katika Kijiji cha Msomera. Sehemu ya nne inaelezea mapendekezo ya jumla na hitimisho.

Sura ya nne inaelezea taarifa za msingi kuhusu Tarafa ya Ngorongoro, Hifadhi ya Ngorongoro, kuhusu ziara hii ya ufuatiliaji pamoja na changamoto zake. Sura hii ina sehemu nne. Sehemu ya kwanza inaelezea utangulizi, sehemu ya pili inaelezea mchakato wa kuondoa watu kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Sehemu ya tatu inaelezea uchambuzi wa mapendekezo mahususi. Sehemu ya nne inaelezea mapendekezo ya jumla na hitimisho. Sura ya tano inaelezea hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale. Sura hii ina sehemu nne. Sehemu ya kwanza inaelezea utangulizi, sehemu ya pili inaelezea jinsi mchakato wa kutwaa eneo la kilometa za mraba 1,502 na kulipa hadhi ya kuwa Pori la Akiba la Pololeti. Sehemu ya tatu inaelezea changamoto mbalimbali zilizojitokeza baada ya eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa na Serikali na baadae kugeuzwa kuwa pori la akiba la Pololeti. Sehemu ya nne inaelezea uchambuzi na mapendekezo mahususi. Sehemu ya tano inaelezea mapendekezo ya jumla na hitimisho.

### 1.2 Malengo ya Taarifa Hii

(a) Lengo la taarifa hii ni kuonyesha na kutoa mapendekezo kuhusu hali ya haki za binadamu na changamoto zinazojitokeza katika Kijiji cha Msomera baada ya wananchi kuhamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro katika awamu ya kwanza ambapo wananchi zaidi ya 3,000 walihamishwa.

(b) Taarifa hii imefuatilia kwa kina hali ya haki za binadamu kwa wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro hasa mara baada ya zoezi la watu kuhamishwa kuanza mwaka 2022. Imefanya pia uchambuzi wa utaratibu unaotumika kuhamisha wato kutoka katika tarafa ya Ngorongoro pamoja na mapendekezo ya namna ya kuendesha zoezi hili kwa kuzingatia haki za binadamu na sheria.

(c) Pia taarifa hii imelenga kuonyesha hali ya haki za biandamu katika tarafa ya Loliondo na sehemu ya Sale baada ya eneo la kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa na Serikali mwaka 2022. Lengo jingine pia ni kuonyesha changamoto zinazowakabili wananchi na mifugo baada ya Serikali kuchukua eneo hilo ambalo ndio lilikuwa tegemezi kwa makazi ya wananchi, malisho ya mifugo na maji kwa binadamu na Wanyama. Taarifa hii pia ina mapendekezo ya msingi kuhusu changamoto hizi.

### 1.3 Methodolojia ya Taarifa Hii

Taarifa hii imeandaliwa kama ilivyo taratibu za kawaida za ufuatiliaji wa hali ya haki za binadamu na sio utafiti wa kisayasi. Kama watetezi wa haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania na misingi ya haki za binadamu tunajukumu la msingi la kufuatilia hali ya haki za binadamu na kuadaaa taarifa kwa ajili ya kushauri mamlaka husika. Katika kuandaa taarifa hii tumetumia methodolojia mbalimbali kupata taarifa kwa lengo la kuandaa taarifa hii. Tulitumia njia zifuatazo katika kukusanya taarifa:

iii) Vikao na vioongozi wachache wa serikali waliokuwa tayari kukutana na timu ya watetezi

iv) Njia ya usahili na Kusambaza dodoso

v) Mahojiano ya mtu mmoja mmoja na mahojiano ya makundi na taasisi mbalimbali, mahojiano na viongozi wa kijamii na kisiasa katika tarafa ya Loliondo na Ngorongoro na Msomera. Zaidi ya watu 600 wamefikiwa katika ziara hii katika maeneo yote matatu ( Msomera, Ngorongoro na Loliondo).

vi) Kutembelea maeneo husika na kufanya mikutanao na wananchi wakazi wa maeneo tuliyoyatembelea.

vii) Uchambuzi wa nyaraka mbalimbali,

viii) Lakini pia kilifanyika kikao cha kuhakiki na kupitia kwa pmaoja taarifa na madiwani wa tarafa ya Loliondo, Sale na Ngorongoro pamoja na badhi ya mashirika na watetezi wa kijaamii mjini Moshi Kilimanjaro tarehe 8 na 9 August 20231.5

### 1.4 Matarajio ya Taarifa hiii

Matarajio ya taarifa hii ni kuoona utekelezaji wa mahitaji ya wananchi katika maeneo yote ambayo ziara ilifanyika na kama ambavyo mapendekezo yake yameainishwa katika taarifa hii. Utekelezaji wake ni pamoja na kusitishwa kwa muda kwa zoezi la uhamishwaji wa wananchi kutoka Ngorongoro ili kutoa nafasi ya wananchi kushirikishwa kwa uwazi.. Hii ni kutokana na kutokuwepo kwa ushirikishwaji wa wananchi na kupewa fidia isiyoendana na uhalisia.

Matarajio mengine ni wananchi kuruhusiwa kuendelea kutumia eneo la kilometa za mraba 1,502 katika tarafa ya Loliondo na sehemu ya Sale kwaajili ya malisho ya mifugo yao ambapo kwasasa mifugo haina malisho wala sehemu ya kunywa maji hali ambayo imepelekea mifugo kufa na mingine kutaifishwa au wamiliki kutozwa faini kubwa pale mifugo yao inapoingia kwenye hifadhi kwaajili ya malisho na maji.

Tunategemea pia kupitia taarifa hii nafasi ya mazungumzo katika ya Serikali na watu Ngorongoro pamoja na watetezi wao itapatikana. Hii ni kutokana na ukweli kuwa hadi sasa hakuna mikutano yoyoe kati ya Serikali na wananchi, viongozi wa wananchi pamoja na watetei wa haki za binadamu katika kupanga mikakati ya pamoja na yenye

kuzingatia haki za binadamu. Matukio yote ya ukiukwaji wa haki za binadamu na vilio vya kila siku vitaondoka na wananchi watakuwa sehemu ya mikakati ya kulinda maeneo ya hifadhi.

Matarajio mengine ni pamoja na kupatatikana kwa Mpango wa Pamoja wa Kuhama kwa Hiari ( Voluntary -Relocattion plan and Resettlement Plan) ambayo itakuwa mwarobaini wa hizi changamoto ambazo zinajitokeza katika utataribu wa sasa wa kuhamisha watu.

### 1.5 Changamoto za Uandaaji wa Taarifa Hii

Katika kuandaa taarifa hii kuna changamoto kadhaa ambazo tulikumbana nazo. Changamoto kubwa ni kukosa ushirikiano wa Serikali na taasisi za Serikali ambazo tuliziomba ufafanuzi wa masuala mbalimbali ambayo tuliyabaini kutoka kwa wananchi. Licha ya kuandika barua na kuziwasilisha kwenye ofisi husika na kukumbushia kwa njia ya barua pepe lakini hatukufanikiwa kupata majibu juu ya malalamiko ambayo wananchi waliyatoa wakati wa ziara yetu. Taasisi hizo za Serikali ni Ofisi ya Waziri Mkuu, ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, wizara ya elimu, wizara ya afya, wizara ya ardhi, wizara ya maliasili na utalii na TAMISEMI.

Changamoto nyingine ni upatikanaji wa takwimu kwa baadhi ya maeneo katika wilaya ya Ngorongoro, baadhi ya wananchi hawatunzi kumbukumbu za matukio hivyo walishindwa kutoa taarifa za baadhi ya maeneo.

SURA YA 2

# MAREJEO YA NYARAKA MBALIMBALI

## 2.0 UTANGULIZI

Sura hii imelenga kutoa maelezo mafupi yaliyotokana na marejeo ya sheria, sera na nyaraka mbalimbali zinazohusiana na taarifa hii. Sura hii imechambua sheria, sera, miongozo mbalimbali ya ndani na ya Kimataifa kuhusu suala la wafugaji, umiliki wa ardhi, uhifadhi na haki za binadamu hapa nchini hususani kwa wakazi wa sasa wa Kijiji cha Msomera Handeni, Tarafa ya Ngorognoro, Loliond na sehemu ya Sale.

### 2.1 Sheria na Sera Mbalimbali

Katika ripoti hii tuliweza kurejea na kuchambua Sheria na nyaraka mbalimbali za Kimataifa Kikanda na kitaifa kuhusu umiliki, usimamizi na utwaaji wa ardhi nchini Tanzania. Pia kuhusu haki za binadamu, utawala bora, utawala wa Sheria na dhana ya ushirikishwaji wa wananchi.

#### 2.1.1 Sheria na Miongozo ya Kimataifa

#### 2.1.1.1 Tangazo la Dunia Kuhusu Haki za Binadamu

Tangazo la dunia la mwaka 1948 ndio chimbuko la haki zote msingi ambazo kila mwanadamu anastahili kuwa nazo kwa misingi ya ubinadamu wake. Miongoni mwa stahili hizo ni haki ya kumiliki mali pasipo kupokonywa na mtu mwingine. Baada ya Azimio hili, mikataba mingine ya haki za binadamu ilifuata.

#### 2.1.1.2 Tamko la Umoja wa Mataifa Juu ya Haki za Watu wa Asili

Tamko hili la mwaka 2007 limeeleza wazi katika ibara ya 10 kwamba watu wa asili hawataondolewa kwa nguvu kutoka kwenye ardhi au maeneo yao, uhamisho wowote wa watu wa asili hauwezi kufanyika bila idhini yao huru, lakini pia bila ya kuwa na fidia stahiki na ikiwezekana wawe na chaguo la kurudi. Maana ya watu wa asili imeelezwa na Tume ya Afrika juu Haki za Binadamu na Watu kuwa inahusiana na utumiaji wa ardhi, lugha, maeneo ya kuabudiana na tamaduni zao.

Kwa mujibu wa ripoti ya Kikundi cha Wataalamu kutoka Tume ya Afrika Juu ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu watu wa asili ya mwaka 2005, hakuna tafsiri kamili kuhusu maana ya watu wa asili ambayo inatumika duniani kote lakini ripoti hiyo imeelezea sifa

ya watu wa asili katika mtazamo wa Umoja wa Afrika.[1] Sifa hizo ni kwamba utamaduni wao na namna wanavyoendesha Maisha yao ni tofauti na utamaduni wa kawaida, lakini pia kuishi kwao kunahusishwa moja kwa moja na utumiaji wa ardhi yao ya asili na maliasili zilizopo kwenye ardhi hiyo, watu hawa wanakuwa wanabaguliwa kutokana na mtazamo hasi dhidi yao kuwa ni watu ambao hawajaendelea ukilinganisha na makabila mengine yenye utamaduni wa kawaida. Ubaguzi wa aina hiyo huwapelekea kuvunjwa kwa haki zao kama jamii na kuhatarishwa kwa uendelevu wa utamaduni na maendeleo yao.

Miongoni mwa watu waliotambuliwa na Tume ya Afrika juu ya Haki za Binadamu na Watu kuwa ni watu wa asili ni Wamaasai ambao ndio wenyeji wa Ngorongoro. Hii imeelezwa vizuri na Tume ya Afrika juu ya Haki za Binadamu na Watu kwenye kesi ya **Centre for Minority Rights Development (Kenya) and Minority Rights Group International on behalf of Endorois Welfare Council v Kenya, Communication 276 / 2003.**

Sifa zilizoelezwa kwenye kesi tajwa zimefafanuliwa pia katika kesi ya **African Commission on Human and Peoples' Rights v Kenya (merits) (2017) 2 AfCLR 9** maarufu kama **"Kesi ya Ogiek".**

Kwa maelezo haya Wamaasai kutoka Ngorongoro wanakidhi vigezo vilivyosemwa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na pia Mahakama ya Afrika juu ya Haki za Binadamu na Watu.

#### 2.1.1.3 Mkataba wa Kimataifa Juu ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966

Mkataba huu katika utangulizi wake unaeleza wazi kwamba nadharia ya binadamu kuwa huru na kufurahia uhuru wake bila uoga inaweza kufanikiwa tu pale ambapo kutakuwa na mazingira ya kila mtu kufurahia haki zake za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni pamoja na haki zake za kiraia na kisiasa. Vilevile ibara ya 1,3,6 na 15 ya mkataba huu inaeleza kwamba kila mtu anyo haki ya kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na inatoa wajibu kwa Serikali kuhakikisha kwamba inaweka mazingira sawa kwa watu wote ili waweze kufurahia haki hizo. Katika mazingira ambayo wamaasai wamehamishwa kutoka Ngorongoro na utofauti wa mazingira ya Msomera ambayo wanaishi kwasasa, ni dhahiri kwamba kuna dalili kubwa ya wao kutojiendeleza kiutamaduni na hivyo utamaduni wao unaweza kufutika.

1 Report of the African Commission's Working Group of Experts on Indigenous Populations/Communities 2005 P 87-89

### 2.1.2 Sheria na Miongozo ya Kikanda

#### 2.1.2.1 Mkataba wa Afrika Juu ya Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981

Mkataba huu unataka nchi wanachama kuheshimu haki za binadamu ambazo zimeainishwa kwanye mkataba. Katika ibara ya 14, 21 na 22 ya mkataba huu imeainisha haki ya kumiliki mali kuwa ni miongoni mwa haki za binadamu. Ardhi ni mali hivyo ni miongoni mwaka haki za binadamu zilizotamkwa kwenye mkataba huu. Wamaasai waliohamishwa Ngorongoro na wananchi wenyeji wa Msomera wote wana haki ya kumiliki ardhi ambayo ni mali yao, utwaaji wa ardhi ambayo ni mali ya wananchi lazima ufuate utaratibu wa kisheria wa fidia. Wananchi wenyeji wa Msomera wamelalamikia suala la wao kunyang'anywa ardhi yao bila kupewa fidia stahiki.

#### 2.1.1.2 Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Huu ni mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1999. Mkataba umeeleza kuwa nchi wanachama izingatie utawala wa sheria, haki za binadamu, demokrasia na utawala bora. Katika ziara yetu, wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro walitueleza kwamba, sheria na haki zao kama binadamu hazikuzingatiwa mfano haki ya kupewa taarifa sahihi, hawakushirikishwa kikamilifu kabla ya kuhamishwa. Wananchi wenyeji wa Msomera vilevile madai yao ni kwamba hawakushirikishwa wala kupewa fidia stahiki ambayo ni haki yao kwa mujibu wa sheria.

#### 2.2.2.3 Mkataba wa Utamaduni wa Afrika (Cultural Charter for Africa)

Mkataba huu umeridhiwa na nchi 55 za Afrika ikiwemo Tanzania ambayo iliuridhia mwaka 1976 na ulianza kutumika mwaka 1990 kwa nchi zote wanachama. Ibara ya 1 ya mkataba huu inasisitiza mojawapo ya malengo ya mkataba huu ni ukuzaji wa utamaduni wa Afrika ikiwa ni pamoja na kutambua kwamba utamaduni hujengwa na watu wa nchi husika. Mazingira ya sasa ya Kijiji cha Msomera na kwa namna jinsi Kijiji kilivyopangwa, hakiweza kukuza utamdani wa jamii ya wamaasai wanaoishi katika Kijiji hicho kwani hakuna mfano maeneo ya matambiko na shughuli za kimila yaliyotengwa na Serikali.

#### 2.2.2.4 Sera Juu ya Ufugaji Afrika: Kuhifadhi, Kutunza na Kuboresha Uhai, Maisha na Haki za Jamii za Kifugaji

Muongozo huu wa Kisera juu ya kulinda uhai na maisha ya jamii za kifugaji barani Afrika ya 2010 imeweka pia bayana haja za kuheshimu haki za wafugaji na nyanda za malisho barani Afrika. Mwongozo huu wa kisera pia ulitaka nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kuheshimu mifumo ya maisha ya watu wa asili.

Katika Sakata la kuhamisha wananchi kutoka Ngorongoro unakiuka mwongozo huu wa Kisera unayotaka nchi wanachama kuheshimu na kulinda ufugaji na nyanda za malisho.

### 2.1.3 Sheria za Kitaifa

#### 2.1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

Katiba ndio mama wa Sheria zote za Tanzania hivyo Sheria yoyote, sera, tamko, miongozo na maelekezo mbalimbali lazima yazingatie matakwa ya Katiba, kinyume na hapo ni ukiukwaji wa Katiba na hivyo ni batili. Kwa mujibu wa ibara ya 24 (1) ya Katiba, kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo. Haki ya kumiliki mali ni moja ya haki msingi ya binadamu. Katika tafsiri za kimahakama, mali inajumuisha ardhi kuwa ni mali kama mali zingine. Mahakama ya Rufaa imetoa tafsiri ya haki ya ardhi kama mali kuwa;

> *"Haki za ardhi chini ya mila na desturi, ingawa kwa uhalisia wake ni haki ya kukaa na kutumia ardhi, bado ni mali ambayo inalindwa na ibara 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utwaaji wa haki za mila bila fidia ya haki inazuiliwa na Katiba."*[2]

Katiba imeeleza zaidi katika ibara 24 (2) kwamba ni marufuku mtu yoyote kunyang'anywa mali yake  isipokuwa kwa kuzingatia taratibu za kisheria ikiwepo ulipwaji wa fidia stahiki.

#### 2.1.3.2 Sheria ya Ardhi Na. 5 ya Mwaka 1999

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Ardhi kina tamka kwamba ardhi yote ya Tanzania itaendelea kuwa ardhi ya kiumma na itaendelea kuwa mkononi mwa Rais kama mdhamini kwa niaba ya wananchi wa Tanzania.

Sheria inatumia neno '*itaendelea*' kwa sababu ya historia kuanzia mwaka 1923 ambapo Sheria ya Ardhi ya kikoloni ili tamka kwamba ardhi yote nchini ni ardhi ya kiumma na ikawekwa mkononi mwa Gavana. Mfumo huo uliendelea baada ya Uhuru isipokuwa tu neno 'Gavana' lilikawekwa neno 'Rais'. Sheria ya Ardhi imeendeleza mfumo huu wa umiliki wa ardhi nchini Tanzania.

Hivyo, tafsiri sahihi ya kifungu ni kwamba ardhi sio mali ya umma, bali ni mali ya kiumma kwasababu kuwa mdhamini haimaanishi umiliki wa ardhi.  Sheria haitoi umiliki wa ardhi kwa umma, Rais au Serikali ila mmiliki ni mwenye hati rasmi au hati ya kimila.

Kifungu cha 4 (3) kimetoa jibu la nani ni mmiliki wa ardhi nchini Tanzania. kifungu hicho kinaeleza kwamba wote waliokuwa wana kalia ardhi kabla ya Sheria ya mwaka 1999 kwa hati rasmi au kwa mfumo wa mila na desturi wataendelea kukalia ardhi hiyo, na ukaaji huo wa ardhi utafasiriwa kama mali. Hii pia itajumuisha matumizi ya ardhi kama vile ardhi ya malisho, kilimo na matumizi mengine ya ardhi.

---

2 Mwanasheria Mkuu wa Serikali *Dhidi ya*  Lohay Akonaay na Joseph Lohay [1995] TLR 80, ukurasa wa 81.

Zaidi ya hapo, kifungu cha 4(6) cha Sheria ya Ardhi kinasisitiza kwamba, mtu aliyekuwa anamiliki ardhi kwa hati rasmi au kwa mujibu wa mila na desturi, kabla ya mwaka 1999 ataendelea kuwa mmiliki halali. Kwa ujumla, Sheria ya Ardhi ni sheria mama katika suala zima la umiliki wa ardhi na hivyo ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa ardhi, ardhi yote nchini imegawanywa katika maeneo matatu ambayo ni: ardhi ya Kijiji, ardhi ya hifadhi na ardhi ya jumla, hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 4(4) cha Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999.

#### 2.1.3.3 Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 4 ya Mwaka 1999

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7 hadi cha 21 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji, usimamizi wa ardhi ya vijiji umeelezewa kwa kina. Kwa mfano Kifungu cha 8 (1) kinaeleza kwamba Serikali ya Kijiji ndio chombo pekee chenye mamlaka ya kusimamia ardhi ya Kijiji kwa niaba wa wanavijiji. Kifungu cha 8(5) kimeweka ulazima kwamba Halmashauri ya Kijiji haiwezi kugawa au kutoa hati ya umiliki wa ardhi wa kimila bila ridhaa ya mkutano mkuu wa Kijiji, na lazima izingatie maoni na ushauri wa mkutano mkuu.

Katika ziara yetu tulibaini kwamba mwaka 2016 kijiji cha Msomera kilipitisha mpango wa matumizi bora ya ardhi na kuutungia Sheria ya usimamizi wa mpango huo. Katika mpango huo, ardhi ya Kijiji ilipangiliwa katika maeneo ya makazi, mashamba na maeneo ya malisho ambayo yalikuwa yanamilikiwa pamoja (communal land). Mgawanyo huo unaendana na matakwa ya kifungu cha 13 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji ambacho kinaeleza kwamba, halmashauri ya Kijiji inaweza kutenga eneo na kuwa mali ya pamoja na kupanga matumizi ya eneo hilo litumike kwa shughuli fulani kama vile malisho.

#### 2.1.3.4 Sheria ya Utwaaji wa Ardhi

Sheria hii imeweka bayana taratibu za kufuata na kuzingatia pindi ambapo Serikali inataka kutwaa ardhi ya mtu kwa maslahi ya umma. Taratibu hizo ni kama ifuatavyo: Rais lazima apate azimio la Bunge na kuchapishwa kwenye gazeti la Serikali kwamba ardhi hiyo itatwaliwa kwa maslahi ya umma, notisi ya kusudio la kutwaa ardhi kwa mtu ambaye ardhi yake itatwaliwa na kupewa fidia stahiki.

#### 2.1.3.5 Sheria ya Serikali za Mitaa (Tawala za Wilaya) ya mwaka 1982

Sheria hii inasimamia usajili wa Kijiji na Serikali za mitaa ikiwemo halimashauri ya Kijiji. Baada ya kufanya ziara tulibaini kuwa Kijiji cha Msomera kilisajiliwa mwaka 1992 kwa mujibu wa Sheria hii Pamoja na kupewa hati ya usajili. Kijiji hiki pia tangu kuanzishwa kwake hadi hivi sasa kina mamlaka kamili ya kiuongozi kama vile Mwenyekiti wa Kijiji, Halmashauri ya Kijiji na Mtendaji wa Kijiji.

#### 2.1.3.6 Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro

Sheria ya NCA ilianzisha Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro (The Ngorongoro Conservation Area Authority **(NCAA).** NCAA ni mamlaka iliyoundwa na sheria yake mwaka 1959 kwa lengo la kusimamia hifadhi hii pamoja na kusimamia matumizi mengine mseto ya eneo hili.

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ni eneo la kipekee lenye matumizi ya mesto ya ardhi. Sheria ya NCA inatambua eneo hili lipo kwa ajili ya kuhifadhiwa, lipo kwa ajiil ya utalii lakini pia kwa matumizi ya watu hasa jamii ya wamaasai ambao sheria imewataja. Eneo hili linatumika pia kwa shughuli za kifugaji na shughuli mbalimbali za kimila. Asilimia kubwa ni msitu , pia kuna uoto wa asili wa nyanda za juu kaskazini lenye kuchukua asilimia 20 za NCA, pia milima ipo mingi na maeneo mengineyo ni tambarare na mabonde kama mabonde 5 ya kreta.

Mamlaka hii ya Ngorongoro ambayo ipo katika Tarafa ya Ngorongoro, ilianzishwa ikiwa na malengo makubwa matatu;

(a) Kuhifadhi eneo hili
(b) Kusimamia shughuli za utalii
(c) Na Kuendeleza Jamii ya Kifugaji katika eneo hili

Jamii ya kimaasai kutokana na utamaduni wao na historia yao ya kuishi na Wanyama bila kuwa na madhara makubwa , walionekana wanafaa kuendelea kuishi katika eneo hili kwa kuwa hawana madhara yoyote kwa shuguli za uhifadhi. Hivo NCAA ilipewa jukumu la kisheria la kuendeleza jamii hiii sambamba na shughuli zingine za utalii na uhifadhi.

#### 2.1.3.7 Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009

Sheria hii ilitungwa mwaka 2009 na kufuta sheria ya awali iliyokuwepo ya mwaka 1974. Sheria hii hutumika katika maeneo yote ya hifadhi nchini isipokuwa kwenye Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi za Taifa Tanzania.[3] Kifungu cha 16 kwa ujumla wake kimeweka utaratibu wa uanzishwaji wa mapori tengefu. Sheria imeweka bayana kwamba Waziri mwenye dhamana anaweza kutangaza kwenye gazeti sehemu ya Tanzania kuwa pori tengefu baada ya kushauriana na mamlaka husika katika ngazi za Serikali za mitaa. Kwakuwa Sheria hii ilitungwa mwaka 2009 na tayari kulikuwa na mapori tengefu 48 nchi nzima, kifungu cha 16 (4) kilimtaka Waziri afanye mapitio ya mapori tengefu yote nchini ili kujiridhisha ni mapori yapi yalikuwa yanasifa za kuendelea kuwa mapori tengefu na ayatangaze ndani ya miezi 12.

**Mapori hayo tengefu yalikuwa ni:**

Burunge, Chabula Marsh, Enduleni, Gombe, Handeni, Igombe Dam, Kalimawe, Kigosi, Kihirumira Pool, Kilombero, Kitwai, Kongwa, Lake Daramatai, Lake Kwela, Lake Manka, Lake Natron, Lihogosa, Loliondo, Lolkisale, Longido, Luganzo, Lunda Mkwambi, Masasi River, Maswa, Meserani Dam, Mkungunero, Mlele, Moyowosi, Msima, Mto-Wa-Mbu, Muhuwesi, Mwadui Diamond Mine, Mwambesi, Nchwa-Nkima, Ngeju-Njiro Dam, Ngorongoro, Nyonga, Rau Forest, Rukwa, Rungwa River, Ruvu Masai, Ruvu Same, Sanya-Lelatema, Simanjiro, Speke Gulf, Ugunda, Umba River na Utengule Swamps.

---

3 Kifungu cha 8 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009.

Hata hivyo, Waziri hakutekeleza takwa hilo la lazima la kisheria ndani ya muda uliowekwa na sheria. Kifungu cha 16(5) cha Sheria hii kilimkataza Waziri kujumuisha ardhi ambayo ipo katika eneo la kijiji kuitangaza kuwa pori tengefu. Hii ni kwasababu Sheria za awali zilizosimamia mapori tengefu kama vile ya mwaka 1951 na 1974 hazikuzuia watu kuishi na kufanya shughuli za kijamii, kiutamaduni na shughuli za kiuchumi ndani ya mapori tengefu. Hii maana yake ni kwamba, Waziri alitakiwa afanye mapitio ya mapori tengefu yote, na yale anayoona hayaangukii ardhi ya eneo la Kijiji ayatangaze ndani ya miezi 12. Kutokufanya hivyo, maana yake ni kwamba hakutakuwa na mapori tengefu.

## 2.2 Nyaraka Mbalimbali

### 2.2.1 Muhtasari wa kikao cha halmashauri ya Kijiji cha Msomera

Katika ziara yetu, tuliweza kupata muhtasari wa kikao cha halmashauri ya Kijiji cha Msomera kujadili mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji kilichofanyika katika eneo la ukumbi wa kanisa la pentekoste (FPCT) tarehe 24/08/2016. Katika kikao hicho ajenda zilizojadiliwa na kupitishwa ni mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji cha Msomera, mipaka ya Kijiji, wajumbe wa kamati ya mpango wa matumizi bora ya ardhi pamoja na umiliki wa ardhi.

### 2.2.2 Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji cha Msomera

Katika ziara hiyo, tuliweza kupata mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji cha Msomera, kata ya Misima, tarafa ya Sindeni Wialaya ya Handeni wa mwaka 2016 mpaka 2026. Mpango huo uliwezeshwa na wananchi wa Kijiji cha Msomera na kupitishwa na mkutano mkuu wa \Kijiji cha Msomera mnamo Agosti 2016.

Katika mpango huo ardhi iligawanywa katika makundi manne: eneo la makazi, eneo la huduma za kijamii (shule za msingi, zahanati, bwawa la maji, eneo la mnada, uwanja wa michezo, uwanja wa mikutano, josho), eneo la kilimo na ufugaji wa ndani pamoja na eneo la malisho.

### 2.2.3 Sheria ndogo za (Usimamizi wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi) za Halmashauri ya Kijiji cha Msomera za Mwaka 2016

Sheria hizo ndogo zilitungwa ili kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji na zinatumika katika eneo lote la mamlaka ya Kijiji cha Msomera. Sehemu ya pili ya Sheria hizo imeainisha matumizi ya ardhi yaliyopangwa na kuainishwa ambayo ni: makazi na kilimo, mashamba, huduma za jamii, misitu, vyanzo vya maji, pori na malisho na manyatta. Sheria hizo zinaeleza wazi kwamba mabadiliko ya matumizi ya ardhi katika eneo lolote lililoainishwa yatafanyika tu kwa halmashauri ya Kijiji kurejea na kurekebisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji na kupata ridhaa ya mkutano mkuu wa Kijiji. Katika ziara yetu, wananchi walitueleza kwamba halmashauri ya Kijiji haijawahi kurejea au kurekebisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji wa mwaka 2016.



SURA YA 3
SEHEMU YA KWANZA

# TAARIFA YA HALI YA HAKI ZA BINADAMU KIJIJI CHA MSOMERA WILAYA YA HANDENI MKOANI TANGA

## 3.1 MAELEZO YA AWALI

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) pamoja na baadhi ya wanachama wake ambao ni Baraza la Wanawake Wafugaji (PWC), Shirika la Uraia na Msaada wa Kisheria (CILAO), Mtandao wa Mashirika ya wafugaji (PINGOs Forum Ujamaa Community Resource Team ( UCRT) na Shirika la Uhifadhi wa Utamaduni wa Kimaasai (Tanzania Maasai Heritage-TMH) kwa pamoja tulifanya ziara kati ya Aprili 24-25, mwaka 2023 katika Kijiji cha Msomera Wilayani Handeni mkoani Tanga. Ziara hiyo ilifanyika baada ya kusikia kwamba wananchi wenyeji wa Msomera wamenyang'anywa ardhi yao na kugawiwa kwa wageni waliohamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro mwaka 2022. Siku ya kwanza ya ziara tulionana na kufanya majadiliano na uongozi wa wilaya ya Handeni na baadae uongozi huo chini ya Mkuu wa Wilaya Mhe. Albert Msando tulitembelea miradi ya maendeleo inayojengwa na Serikali katika Kijiji cha Msomera.

Sura hii ya kwanza inaelezea historia ya kuhamishwa kwa wananchi kutoka tarafa ya Ngorongoro, historia ya Kijiji cha Msomera, mgogoro wa ardhi katika Kijiji cha Msomera, malengo ya kufanya ziara katika kijijini cha Msomera, njia tulizotumia kukusanya taarifa pamoja na changamoto tulizokumbana nazo wakati wa kufanya ziara katika Kijiji cha Msomera.

### 3.1.1 Kuhusu Kuhamishwa kwa Wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro

Mnamo Januari 11, 2022 Serikali kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ilitangaza wito kwa wananchi kuhama kutoka katika tarafa ya Ngorongoro kwenda katika Kijiji cha Msomera. Baada ya agizo hilo la Mkuu wa Mkoa, wananchi walifanya mikutano mbalimbali kujadili hatima ya maisha yao pamoja na ardhi yao katika tarafa ya Ngorongoro. Katika mikutano yao, wananchi walijadili na kujiuliza ni kwanini Serikali haijawashirikisha kikamilifu kuhusu mpango wa watu kuhamishwa kwa hiari? Huo uhiari ukoje ukizingatia kwamba wao kama wahusika hawakushirikishwa? Walikosa majibu na hivyo waliendelea kufanya maombi ya kutaka kukutana na viongozi wa Serikali. Walifanya jitihada mbalimbali ikiwemo kuandaa mapendekezo juu ya namna

bora ya kuhifadhi eneo la mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro huku wao wakiendelea kuishi katika eneo hilo. Waliandaa mapendekezo yao na yaliwasilishwa rasmi kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini hayakufanyiwa kazi hali iliyowatia hofu kuwa hawasikilizwi na Serikali.

Mnamo Februari 17, 2022 Waziri Mkuu alienda Ngorongoro na kuongea na wananchi akifafanua kuhusu kinachoitwa "zoezi la kuhama kwa hiari". Hata hivyo, wananchi wenyeji hawakupata muda wa kutosha wa kuwasilisha hoja zao kuhusiana na zoezi hilo la kuhama kwa hiari. Mnamo Juni 07, 2022 takribani baada ya miezi 4 tangu Waziri Mkuu alipowatembelea waliona vikosi vya askari wakiwa na silaha nyingi za moto wakizunguka maeneo yao ya makazi. Vikosi hivyo vilitapakaa katika maeneo mbalimbali kwenye tarafa ya Ngorongoro.

Wakati huohuo wananchi walipata ugeni wa viongozi wa Serikali wakiwemo katibu tarafa, muwakilishi kutoka wizara ya maliasili na utalii, muwakilishi kutoka ofisi ya mkuu wa wilaya, muwakilishi kutoka mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na muwakilishi kutoka idara ya ardhi walifika na kufanya tathmini na makadirio ya vitu ambavyo familia inamiliki na kisha kuondoka. Siku moja kabla ya kuhamishwa walipigiwa simu wakitakiwa kufika makao makuu ya mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro yaliyopo Karatu ambapo walisainishwa kiasi cha fedha walichotakiwa kulipwa kama fidia. Wakati wakienda karatu, maboma yao yalikuwa yanabomolewa. Karatu ndio ilikuwa mwanzo wa safari ya kuelekea Kijiji cha Msomera.

Kabla ya kuhamia Msomera, wananchi waliahidiwa kuwa eneo wanalohamishiwa lina malisho ya kutosha, ni eneo la Serikali ambalo halikaliwi na mtu yeyote. Jumla ya wananchi 3,010 wamehamia katika Kijiji cha Msomera. Wakati wa ziara walitueleza kuwa hali waliyoikuta Msomera inakinzana na taarifa walizopewa awali kwani eneo hilo halina malisho, ni ardhi ya Kijiji kilichosajiliwa tangu mwaka 1992 na sehemu ya wazi ni mapori ambayo hayana nyasi kwaajili ya malisho ya mifugo.

### 3.1.2 Historia ya Kijiji cha Msomera

Msomera ni Kijiji kilichopo katika kata ya Misima, tarafa ya Sindeni, wilaya ya Handeni, mkoa wa Tanga. Kijiji cha Msomera kilisajiliwa mwaka 1992 na kupewa hati ya usajili yenye namba TA/KIJ/576. Kabla ya Kijiji cha Msomera hakijasajiliwa, kilikuwa ni sehemu ya Kijiji cha Mbagwi ambacho kimesajiliwa katika oparesheni vijiji miaka ya 1970. Tangu kiliposajiliwa, Kijiji cha Msomera kiliendelea kupata huduma mbalimbali za kijamii kama vile shule, zahanati, mradi wa maji, ofisi za Kijiji na huduma zingine muhimu za kijamii.

Mwaka 2014 Rais wa awamu ya nne Mhe. Jakaya Kikwete alizindua mradi wa madume ya mbegu ya ng'ombe wa kisasa katika Kijiji cha Msomera. Wakati akizindua mradi huo Rais aliwahimiza wananchi kuongeza maeneo kwaajili ya ufugaji na malisho. Kufuatia maagizo hayo ya Mhe. Rais, mwaka 2016 wananchi waliandaa na kupitisha mpango wa matumizi bora ya ardhi wa mwaka 2016-2026. Kupitia mpango huo, halmashauri ya Kijiji ilitenga maeneo ya makazi, kilimo, malisho, na maeneo ya huduma za kijamii pamoja na kutunga sheria ndogo kwaajili ya kusimamia mpango huo.

### 3.1.3 Chimbuko la Mgogoro wa Ardhi katika Kijiji cha Msomera

Mnamo mwaka 2022, Kijiji cha Msomera kilianza kuwa gumzo katika vyombo mbalilmbali vya habari kufuatia uhamisho wa wananchi kutoka tarafa ya Ngorongoro kwenda katika kijiji hicho. Uhamisho wa wananchi kutoka katika tarafa ya Ngorongoro ulifuatia uwepo wa taarifa kuwa eneo la Msomera ni pori tengefu na hivyo hakuna mtu yeyote anayekalia eneo hilo. Hata hivyo, baada ya wananchi kuhamia katika Kijiji hicho, malalamiko kadhaa yalizagaa kwenye vyombo vya habari kuwa Serikali imetwaa ardhi ya wananchi wenyeji na kuwapa wageni waliotoka Ngorongoro bila fidia ya aina yoyote ile.

Mkuu wa Wialaya ya Handeni alitueleza kuwa ni kweli baadhi ya maeneo katika Kijiji cha Msomera wamepewa wageni kutoka Ngorongoro. Alitueleza zaidi kwamba kila familia iliyopo Msomera imepewa hekari 2.5 za makazi na hekari 5 kwaajili ya kilimo bila kujali kuwa ni mgeni au mwenyeji. Uamuzi wa kugawanya ardhi sawia ulitokana na alichotueleza Mkuu wa Wilaya kuwa Kijiji cha Msomera kilisajiliwa mwaka 1992 lakini kimakosa kwasababu eneo lote hilo lilikuwa ni pori tengefu la Handeni tangu mwaka 1974.

Kwa mujibu wa ziara yetu, tuligundua kuwa wananchi wenyeji hawakuridhishwa na uamuzi huo wa Serikali. Wengi wao walidai kuwa wameanza kuishi kijijini hapo kabla ya uhuru na miaka yote wamekuwa wakilima na Serikali iliwapelekea huduma mbalimbali za kijamii kama vile shule, zahanati, barabara, mradi wa maji, mradi wa madume ya mbegu ya ng'ombe uliozinduliwa mwaka 2014 na Rais Kikwete. Hivyo wananchi wenyeji wanaona kuwa wao sio wavamizi wa eneo hilo bali eneo hilo ni amali yao halali na Serikali ilikuwa inawatambua.

Hoja nyingine ya wananchi wenyeji wa Msomera ni kwamba wageni kutoka Ngorongoro walifanyiwa tathmini na kupewa fidia kabla ya kuhamishwa. Lakini wao hawajafanyiwa tathmini ya maeneo yao isipokuwa Serikali imetwaa maeneo yao kwa nguvu bila fidia yoyote na wao kuendelea kuitwa wavamizi. Namna ardhi yao ilivyotwaliwa ndio malalamiko yao makubwa zaidi kwamba, waliona tu vikosi vya askari vimezunguka maeneo yao na nyumba mpya kujengwa walizopewa wageni na wao kupewa taarifa tu kuwa eneo lao wamepewa watu kutoka Ngorongoro.

Wananchi wenyeji walidai zaidi kuwa hawana maeneo ya kulima kwasababu maeneo waliyokuwa wanalima wamepewa wageni ambao tayari wameshalima. Hivyo, wenyeji walitishia kuwa wanaweza kuwa na ugonvi wa kung'oleana mazao kwasababu kila mtu anataka kulima kwaajili ya chakula.

### 3.1.4 Malengo

#### 3.1.4.1 Lengo Kuu

Lengo la ziara ni kufuatilia hali ya haki za binadamu na changamoto zinazojitokeza katika Kijiji cha Msomera baada ya wananchi kuhamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro kwenda Kijiji cha Msomera ili kuweza kuwa na taarifa sahihi za pande zote kwa lengo kushauri Serikali, wananchi na wadau mbalimbali namna bora ya kutatua changamoto hizo kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu.

#### 3.1.4.2 Malengo Mahususi

i. Kupata taarifa sahihi kuhusu malalamiko ya wananchi wenyeji wa Msomera na wale waliohamishiwa katika Kijiji cha Msomera

ii. Kupata taarifa sahihi juu ya ushirikishwaji wa wananchi wenyeji wa Msomera na wale waliotoka Ngorongoro kuhusu mchakato mzima wa uhamishwaji wa wananchi

iii. Kuangalia iwapo utaratibu wa kugawa ardhi katika Kijiji cha Msomera ulizingatia haki za binadamu na utawala bora

iv. Kupata taarifa kuhusu uwajibikaji wa Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi wa Kijiji cha Msomera.

### 3.1.5 Methodolojia.

Katika ziara yetu tulifanikiwa kuwafikia watu zaidi ya 400 wakiwa ni wananchi wenyeji wa Msomera (300) pamoja na wale walihamishwa toka Ngorongoro (100) pamoja na viongozi mbalimbali. Tulitumia njia zifuatazo katika kukusanya taarifa: kikao na uongozi wa Wilaya ya Handeni chini ya Mkuu wa Wilaya Mhe. Albert Msando pamoja na kamati ya usalama ya Wilaya ambapo tulipata maelezo mafupi kuhusu hali ya Msomera. Pia kupitia njia ya usahili, dodoso, mahojiano kati ya makundi lengwa, kutembelea maeneo husika, uchambuzi wa nyaraka mbalimbali, mkutanao na wananchi.

### 3.1.6 Eneo la ziara na Muda wa Ziara

Ziara hii ya ufuatiliaji katika Kijiji cha Msomera ilifanyika Aprili 24 – 25 mwaka 2023. Siku ya Kwanza tulifanya kikao na uongozi wa Wilaya ya Handeni na badae kutembelea miradi yote ya huduma za jamii katika Kijiji cha Msomera chini ya uongozi wa Mkuu wa Wilaya na baadhi ya wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama. Siku ya pili tulitembelea wananchi katika maeneo yao, kufanya usahili wa mtu mmoja mmoja, usahili wa makundi madogo madogo pamoja na kufanya usahili katika mikutano ya hadhara.

Ziara yetu ilijikita katika eneo la Kijiji cha Msomera pamoja na vitongoji vyake (Orkung', Ormoti, Mkababu na Katikati). Ili kupata ufafanuzi zaidi tulitembelea pia katika Kijiji cha Mbagwi ambacho ni Kijiji mama cha Msomera. Tulifanikiwa kukutana na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji pamoja na Kaimu Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Mbagwi.

### 3.1.7 Changamoto za Ziara

Changamoto kubwa katika ziara hiyo ni muda ulikuwa mchache kwani watu walikuwa ni wengi sana na walitaka kufikiwa kila mmoja kwenye maeneo yao. Hali hiyo ilipelekea kushindwa kumfikia kila mwananchi. Baadhi ya wananchi hasa waliohamishwa kutoka Ngorongoro walikuwa na hofu ya kuzungumza. Kwa mfano mmoja alisema kwamba ***"tumeshalipwa na kuhama, hata nikisema itanisaidia nini na nilishaondoka Ngorongoro?".*** Baadhi ya viongozi ngazi ya Kijiji hawakutoa ushirikiano wa taarifa tulizohitaji. Wapo wananchi pia hasa wa kutoka Ngorongoro ambao walikuwa na woga mkubwa wa kueleza changamoto zao wakidai wamepewa maelekezo wasieleze changamoto zozote wanazokumbana nazo.

SURA YA 3
SEHEMU YA PILI

# MATOKEO YA ZIARA

## 3.2 UTANGULIZI

Sura hii imeelezea hali ya haki za binadamu katika Kijiji cha Msomera, changamoto zilizopo kwa wageni na wenyeji wa Kijiji cha Msomera, hoja za wananchi, hoja za Serikali pamoja na uchambuzi na mapendekezo kwa wananchi wa Msomera, Serikali na uongozi wa Wilaya ya Handeni , wadau wa maendeleo, watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia.

### 3.2.1 Hali ya Haki za Binadamu kwa Wananchi waliohama kutoka Ngorongoro

Katika ziara yetu tulikutana na wananchi takriban 100 kati ya waliohamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro na sasa wanaishi katika Kijiji cha Msomera. Idadi kamili ya wananchi waliohamishwa ni 3,010 ambazo ni jumla ya kaya 551. Nyumba zilizojengwa ni 503. Katika sura hii ndogo taarifa hii imewasilisha hali ya utoaji wa huduma za jamii kwa wananchi wa Ngorongoro waliohamia Msomera pamoja na changamoto mbalimbali walizoelezea wananchi wa Ngorongoro waishio Msomera.

### 3.2.2 Huduma za Jamii na Miradi ya Maendeleo

Katika ziara yetu tulijionea uboreshaji wa miradi ya huduma za kijamii iliyokuwepo hapo awali kwa mfano bwawa, majosho, shule ya msingi, zahanati na miradi mipya ambayo ni kituo cha afya, kituo cha polisi, shule ya sekondari, shule ya msingi Samia Suluhu Hassan, mradi wa maji, kituo cha kupokelea maziwa, eneo la mnada, huduma ya mawasiliano ya simu, majosho mapya, posta mpya na barabara.

#### 3.2.2.1 Majosho

Katika ziara yetu tuliweza kuona josho 1 kati ya 7 ambazo tuluambiwa kuwa zimejengwa na kuboreshwa kwaajili ya matumizi ya mifugo hasa ng'ombe. Majosho hayo yapo sehemu tofautitofauti katika Kijiji cha Msomera.

***Picha 3.1:*** *Josho jipya lilijengwa Msomera ambalo tuliliona wakazi wa ziara*



### 3.2.2.2 Mabwawa

Katika ziara yetu tulishuhudia bwawa moja mkubwa unayoendelea kuboreshwa kati ya mabawa mawili tuliyoelezwa kuwa yamejemngwa katika kijiji cha Msomera. Bwawa moja limejengwa Mlunduzi na jingine Msomera.

Katika ziara yetu tulielezwa kuwa yalijengwa muda mrefu na Mradi wa Benki ya Dunia katika awamu zilizopita na hivyo kwa sasa zipo katika hali ya uboreshwaji tu. Mabwa haya yamejengwa kutokana na uhitaji wa maji ya kunywa kwaajili ya mifugo.

Tulielezwa na uongozi wa wilaya kuwa kwasasa Kijiji cha Msomera kina jumla ya mifugo 86,000 na kati ya hiyo mifugo 15,000 ndio iliyohama kutoka tarafa ya Ngorongoro. Hivyo mifugo hii itatumia mabwawa hayo kupata maji ya kunywa.

Licha ya kuwa na mabwawa haya mawili, wananchi wanadai kuwa hali ya Msomera sio rafiki tena kwa ufugaji kwa sababu imejengwa kwa muundo wa mji na kufanya mifugo wengi kupelekwa katika sehemu zingine nje ya Msomera kwa ajili malisho.



***Picha 3.2:*** *Bwawa la kisasa lililojengwa Msomera*

### 3.2.2.3 Vituo vya Afya

Katika ziara hii tulifanikiwa kutembelea na kukagua ujenzi wa zahanati mpya ambayo ipo mbioni kukamilika. Katika ziara yetu tumeelezwa kuwa kituo cha afya kinachojengwa kitakuwa na vitengo mbalimbali. Ukamilifu wa kituo hiki utakuwa ni msaada mkubwa kwa wakina mama wajawazito, watoto na wagonjwa kwa ujumla waishio maeneo ya karibu.

Changamoto ni wakazi wa kitongoji cha Mkababu ambako pia wananchi kutoka Ngorongoro wamehamishiwa lakini hakuna huduma za afya hivyo wanalazimika kutembea umbali wa kilometa 16 ili kufikia huduma hiyo iliypo kitongoji cha katikati kilichopo Msomera. Changamoto nyingine ni uhaba wa watumishi pamoja na nyumba za watumishi wa afya hasa wa kituo cha afya ambacho kipo muda mrefu, kuna nyumba moja tu ya kukaa mtumishi mmoja.



***Picha 3.3**: Jengo la Kituo cha Afya kinachochengwa Msomera*

### 3.2.2.4 Kituo cha Polisi

Katika ziara yetu pia tuliona kituo kipya cha Polisi Msomera kimejengwa kwaajili ya kuimarisha ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao. Hata hivyo, baadhi ya wananchi walidai kuwa kituo hicho cha Polisi ukiachilia mbali wahalifu kimetumika pia kukamata na kuwaweka ndani watetezi wa haki za binadamu ambao wanadiriki kuongea changamoto zinazowakabili katika Kijiji hicho. Tunapongeza sana uwepo wa miundo mbinu hii katika kuboresha huduma za kwa wananchi wa msomera, lakini uwepo wa huduma hizi uende sambamba na uzingatiaji wa haki kwa wananchi wote wa msomera.

### 3.2.2.5 Huduma za Maji

Timu hii ya ufuatiliaji imefanikiwa pia kuona miundo mbinu mizuri ya maji katika Kijiji cha Msomera. Serikali imechimba visima 7 vya maji kwaajili ya wananchi wa Msomera. Hivyo kuna tenki kubwa la maji limejengwa ambalo lina uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha lita 775,000 kwa siku. Maji haya ni kwaajili ya kuwahudumia wananchi wa Kijiji cha Msomera. Baadhi ya wananchi wamevuta maji hadi kwenye miji yao isipokuwa walitueleza kwamba wakati mwingine maji hayo hayatoki kwa muda wa wiki 1 hadi 2 mfululizo.

Hatua hii ya kuhakikisha maji yanapatikana kwa wananchi ni jambo zuri kwa ustawi wa jamii. Pamoja uwepo wa huduma hizi , wananchi wote tuliowahoji walitueleza kuwa maji hayo yana chumvi nyingi na hivyo yanachangamoto kwa matumizi ya binadammu. Tatizo hili la Maji ya Chumvi viongozi wa Wilaya walisema ni tatizo la Wilaya nzima na wapo katika mikkati ya kuvuta maji yasio na chumvi kwa Wilaya nzima ya Handeni.



***Picha 3.4:*** *Kisima cha maji kilichojengwa katika kitongoji cha katikati kilichopo Msomera*

### 3.2.2.6 Huduma ya Elimu

Katika ziara yetu tuliona shule ya sekondari Msomera mpya ambayo imejengwa pamoja na shule ya msingi Samia Suluhu Hassan. Tumebaini shule hizi kuwa na ubora na tunaipongeza Serikali kwa hatua hii. S/M Samia ina jumla ya wanafunzi 883 na kati yao 674 ni wahamiaji kutoka Ngorongoro. Shule hii ina jumla ya walimu 7 (wakike 2 na 5 wa kiume).

Pamoja na uzuri wa shule hizi , zipo changamoto kadhaa zilizobainika. Mfano Changamoto katika shule ya Msingi Samia ni uhaba wa walimu 12, upungufu wa madawati 186 pamoja na upungufu wa vyumba vya madarasa. Katika kitongoji cha Mkababu ambayo ni takribani kilometa 16 kutoka katika mji wa Msomera hakuna shule ya Msingi wa Sekondari na hivyo kupelekea watoto waliokuwa shule wakiwa Ngorongoro kushindwa kwenda shule baada ya kuhamishiwa kijiji cha Msomera.



***Picha 3.5:*** *Picha ya Kamati ya Ulinzi ya Wilaya Handeni, Timu ya Ziaea wakiongea na baaadhi ya wanafunzi wa Sekondari ya Msomera wakati wa ziara. Pembeni ni moja wapo ya madarasa ya kisasa ya shule hii.*

Katika kitongoji cha Mkababu Serikali imejenga madarasa 2 kwaajili ya watoto wanaosoma darasa la awali. Katika shule ya sekondari Msomera iliyopo kitongoji cha katikati, tuliweza kuona mradi wa kompyuta kwaajili ya wanafunzi kujifunza

pia kidigitali. Shule ya Sekondari Msomera kuna jumla ya wanafunzi 205, walimu 8 ambapo wa kike ni 1 tu na anafundisha masomo yote ya sayansi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Kwa ujumla wanafunzi walieleza kuwa wameridhika na ubora wa shule hii pamoja na kwamba wana ukiwa wa kuwakosa wenzao na ndugu zao waliobaki Ngorongoro.

Changamoto zingine katika shule hii ni uhaba wa walimu, kutokuwa na mabweni ukizingatia kwamba wananfunzi wengine wanatoka mbali na ni shule pekee ya sekondari katika Kijiji kizima ambayo baadhi ya wanafunzi hulazimika kusafiri umbali mrefu. Shule hii pia ina changamoto ya nyumba za walimu.

#### 3.2.2.7 Kituo cha Kupokelea Maziwa

Tulifanikiwa pia kutembelea kituo kipya kilichojengwa kwaajili ya kupokelea, kutunza na kusambaza maziwa katika Kijiji cha Msomera. Kituo hicho kina uwezo wa kupokea lita 5,000 kwa siku. Moja ya kauli mbiu inayotumika kuhamasisha uvunaji wa maziwa katika Kijiji cha Msomera ni *vuna mifugo, ongeza tija*.

### 3.2.3 Changamoto za Wananchi waliohama kutoka Tarafa ya Ngorongoro

Katika ziara yetu na hasa baada ya kuongea na wananchi waliotoka Ngorongoro tulibaini changamoto kadhaa ambazo zinagusa maeneo ya kuanzia mchakato wa uhamishwaji, mchkato wa fidia, swala la ushirikishwaji, huduma za jamii kama vile maji safi na salama, walimu , maeneo ya kuchungia mifugo, hali ya ufugaji, hali ya usalama wa chakula , kupewa ardhi yenye kumilikiwa na wenyeji n.k.

#### 3.2.3.1 Kupewa Nyumba Moja Bila Kuzingatia Ukubwa wa Kaya

Kila kaya imejengewa nyumba moja yenye vyumba vitatu na sebule bila kuzingatia idadi ya wanafamilia. Kwa mfano, moja ya kaya tuliyoitembelea ina wanafamilia wafuatao: mume, mke, watoto wawili, mama mzazi, kaka mwenye wake wawili na watoto wawili wote hawa wamepewa nyumba moja yenye vyumba vitatu hali ambayo imeathiri utamaduni, malazi na hivyo kupelekea kutafuta hifadhi kwa wenyeji. Hali hii ipo kwa familia nyingi tulizotembelea wakati wa ziara.

***Picha 3.6:*** *Nyumba ya vyumba 3 ya mfano wa nyumba zilizojengwa Msomera*



Lakini pia katika kuongea na wananchi walitueleza kwamba kaya 48 zilihamishiwa katika Kijiji cha Msomera bila ya kuwa na nyumba za makazi. Wakati wananchi wanahamishiwa Msomera, walikuta gunia mbili za mahindi ya chakula na kuahidiwa kuwa watapewa kwa takribani miezi 18 tangu walipohamishiwa. Wananchi wamedai kwamba kwa miezi mitatu sasa bado hawajapewa chakula.

Zaidi ya hapo, wananchi ikiwemo na wanafunzi wa shule ya sekondari Msomera walitueleza kwamba maji hayatoki mara kwa mara lakini pia ni ya chunvi hivyo kwa ujumla walisema miundombinu haijakaa sawa kulingana na mahitaji yao.

### 3.2.3.2 Madai ya Kutokuwepo kwa Ushirikishwaji

Dhana ya Ushirikishwaji imeongelewa na wananchi kwa maeneo mbalimbali yanayohusu swala zima la uhamishwaji wa watu toka Ngorongoro kwenda Msomera. Wananchi wamelalamikia mchakato kwenda bila kuwashirikisha viongozi wao wa kisiasa wa ngazi mbalimbali kuanzia Kijiji hadi ngazi ya Wilaya ( Halmashauri ya Wilaya). Hadi sasa hawajui ni lini utaratibu huu ulijadiliwa na kupitishwa katika Vikao vya Halmashauri ya Wilaya na pia katika Baraza la Wafugaji la Ngorongoro ambalo ni chombo cha Kisheria chenye mamlaka ya kusimamia mambo yote wa wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro.

Matoeko ya kutokuwa na utaratabu shirikishi wa kuhamisha watu kwa hiari umechangia watu wengi kupata fidia ndogo na hata wengine kutokupata fidia hadi sasa. Mfano, Wananchi waliohamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro walidai kwamba hawakushirikishwa kikamilifu na kwa uwazi katika kukokotoa fidia zao. Walidai hawakuwahi kupewa nafasi ya kujadiliana na kukubali utaratibu utakaotumika kukokotoa fidia zao ukizingatia aina ya maisha wailiyokuwa wanaishi katika Tarafa ya Ngorongoro.

#### (a) Muundo wa Kamati ya Fidia

Wananchi walihoji kuhusu muundo wa kamati iliyopewa kazi ya kufanya tathimini ya fidia. Walieleza kuwa wao waliona tu kikundi cha watu kilichoundwa na;

(i) Katibu Tarafa,
(ii) Muwakilishi kutoka wizara ya maliasili na utalii,
(iii) Muwakilishi kutoka ofisi ya mkuu wa wilaya,
(iv) Muwakilishi kutoka mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na
(v) Muwakilishi kutoka idara ya ardhi

Kamati hii ndio ilikuwa na kazi ya kufanya tathmini na makadirio ya vitu wanavyomiliki na kuondoka. Wananchi hawakupewa nakala yoyote ya kujaza mali zao, gharama ya mali zao wala ripoti ya tathmini isipokuwa walipigiwa simu siku moja kabla ya kuondoka wakitakiwa kufika makao makuu ya mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro iliyopo Karatu ambapo walisainishwa kiasi cha fedha walichotakiwa kulipwa.

### (b) Kufunguliwa Akaunti Mpya ya Benki kwaajili ya kuwekewa Fedha

Wananchi walitueleza zaidi kwamba mamlaka ya hifadhi ndio iliwafungulia akaunti za benki kwaajili ya kuwekewa fedha za fidia. Wale ambao walikuwa na akaunti zao tayari, zilikataliwa na walifunguliwa akaunti zingine mpya na maafisa kutoka mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro. Baadaye sana fedha ziliwekwa katika akaunti zao na kutumiwa namba ya siri ya kutolea pesa. Huu ni utaratibu ambao haujawahi tokea popote duniani ukizingatia kuwa maswala ya namna ya kuhifadhi fedha ni maswala binafsi.

Hiii ni changamoto kubwa sana na imefanya watu wa Ngorongoro kuonana kama ni watoto wanaotakiwa kusaidiwa hadi kufunguliwa account za benki. Mazingira haya yanaweza changia upotevu mkubwa wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hii. Wananchi wapewe uhuru katika kuamua namna wanavyotaka kupokea pesa zao na kuwe na uwazi katika mchakato huu.

### (c) Usiri wa Fidia

Katika ziara hii wananchi tuliowafikia walitueleza kwamba mchakato wa tathmini ulighubikwa na usiri kwasababu hawakupewa mrejesho wa tathmini iliyofanyika na kiwango ambacho walistahili kulipwa. Fedha pekee iliyofahamika tangu awali ni fedha taslimu za kitanzania shilingi milioni kumi maarufu kama ***"asante mama" wanayosema ni hela ya Rais Samia.*** Lakini pia fidia haikuzingatia ukweli kwamba wananchi wa Ngorongoro walizuiliwa kufanya shughuli za kimaendeleo kama vile kujenga nyumba za kisasa, kilimo na kumiliki vyombo vya usafiri.

Hatimaye fidia walizopewa zilkuwa  za kiwango cha chini sana , na wengi walipewa fidia ya kuanzia milino moja hadi milioni tatu.  Utaratibu uliotumika kutoa  fidia walidai sio sahihi kwa kuwa  wananchi wa Tarafa Ngorongoro  wanaishi katika eneo ambalo ni tofauti na maeneo mengine ya nchi. Ni kosa kutumia sheria ya fidia kutaka kupata kiwango halali cha kufidia watu wa eneo la Ngororongoro ambao kwa muda mrefu wamezuiwa kufanya maendeleoe au kuendeleaz maeneo yao. Fidia yao ilipaswa kuwa na utaratibu wa kipekee kwa kuangalia zaidi thamani ya mali asili walizotunza na wanazoziacha zaidi na sio kuangalia mali  zisizohamishika  pekee .

Takriban wananchi 100 waliweza kutupatia kiwango chao walicholipwa kamaa inavyoonekana katika jedwali hapa chini.  Viwango hivi ni vya chini sana na kama sio hiyo milioni 10 ya Asante Mama manake wapo watu wangeondoka na laki tano hadi million tatu pekee.  Hali hii imefanya watu wengi waliopo Msomera kuingia katika umaskini mkubwa mara baada ya kuhamia Msomera.

**Jedwali 3.1: Kiwango cha Fidia ambacho kila kaya ilipewa**

| Na | Fidia kwa Mujibu wa Tathmini | Fedha iliyotolewa na Rais "Asante Mama" | Jumla |
|---|---|---|---|
| 1 | 3, 424, 211.5 | 10, 000, 000 | 13, 424, 211.5 |
| 2 | 5, 784, 217.94 | 10, 000, 000 | 15, 784, 217.94 |
| 3 | 8, 681, 393.17 | 10, 000, 000 | 18, 681, 393.17 |
| 4 | 3,865, 383.2 | 10, 000, 000 | 13, 865, 383.2 |
| 5 | 76,620.01 | 10, 000, 000 | 10, 076, 620.01 |
| 6 | 4, 794, 927.4 | 10, 000, 000 | 14, 794, 927.4 |
| 7 | 3, 759, 601.5 | 10, 000, 000 | 13, 759, 601.5 |
| 8 | 9,607, 533.36 | 10, 000, 000 | 19, 607, 533.36 |
| 9 | 12, 700, 297.44 | 10, 000, 000 | 22, 700, 297.44 |
| 10 | 2, 282, 671.3 | 10, 000, 000 | 12, 282, 671.3 |
| 11 | 6, 843, 576.9 | 10, 000, 000 | 16, 843, 576.9 |
| 12 | 4, 386, 005.5 | 10, 000, 000 | 14, 386, 005.5 |
| 13 | 2, 127, 726.71 | 10, 000, 000 | 12, 127, 726.71 |
| 14 | 4, 567, 812.84 | 10, 000, 000 | 14, 567, 812.84 |
| 15 | 3, 901, 981.8 | 10, 000, 000 | 13, 901, 981.8 |
| 16 | 4, 362, 109.88 | 10, 000, 000 | 14, 362,109.88 |
| 17 | 3, 268, 856.7 | 10, 000, 000 | 13, 268, 856.7 |
| 18 | 3, 644, 464 | 10, 000, 000 | 13, 644, 464 |
| 19 | 6, 584, 324.18 | 10, 000, 000 | 16, 584, 324.18 |
| 20 | 12, 516, 087.07 | 10, 000, 000 | 22, 516, 087.07 |
| 21 | 3, 520, 247 | 10, 000, 000 | 13, 520, 247 |
| 22 | 2, 149,333.5 | 10, 000, 000 | 12, 149, 333.5 |
| 23 | 3, 524,416.25 | 10, 000, 000 | 13, 524, 416.25 |
| 24 | 2, 496, 954.1 | 10, 000, 000 | 12, 496, 954.1 |
| 25 | 5, 886, 518.5 | 10, 000, 000 | 15,886, 518.5 |
| 26 | 5, 679, 657.44 | 10, 000, 000 | 15, 679, 657.44 |
| 27 | 3, 094,269.93 | 10, 000, 000 | 13, 094, 269.93 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 28 | 4,255,116.5 | 10, 000, 000 | 14, 255, 118.5 |
| 29 | 3,976,447.7 | 10, 000, 000 | 13, 976, 447.7 |
| 30 | 1, 985, 949.6 | 10, 000, 000 | 11, 985, 949.6 |
| 31 | 22,864,358.5 | 10, 000, 000 | 32, 864, 358.5 |
| 32 | 9,175,868.06 | 10, 000, 000 | 19, 175, 868.06 |
| 33 | 1, 455, 741.2 | 10, 000, 000 | 11, 455, 741.2 |
| 34 | 3,743, 070 | 10, 000, 000 | 13, 743, 070 |
| 35 | 22,864,358.5 | 10, 000, 000 | 32, 864, 358.5 |
| 36 | 9,175,868.06 | 10, 000, 000 | 19, 175, 868.06 |
| 37 | 22,864,358.5 | 10, 000, 000 | 32, 864, 358.5 |
| 38 | 5, 314, 769.46 | 10, 000, 000 | 15, 314, 769.46 |
| 39 | 13,581,232.72 | 10, 000, 000 | 23, 581, 232.72 |
| 40 | 3,133,867 | 10, 000, 000 | 13, 133, 867 |
| 41 | 3, 780,821.1 | 10, 000, 000 | 13, 780, 821.1 |
| 42 | 9,576, 679.81 | 10, 000, 000 | 19, 576, 679.81 |
| 43 | 1,727,325.25 | 10, 000, 000 | 11, 727, 325.25 |
| 44 | 2,332, 597.5 | 10, 000, 000 | 12, 332, 597.5 |
| 45 | 4,183,128.9 | 10, 000, 000 | 14, 183, 128.9 |
| 46 | 13,581,223.72 | 10, 000, 000 | 23, 581, 233.72 |
| 47 | 3,143,190.23 | 10, 000, 000 | 13, 143, 190.23 |
| 48 | 6, 397, 838.69 | 10, 000, 000 | 16, 397, 838.69 |
| 49 | 2,396, 800 | 10, 000, 000 | 12, 396, 800 |
| 50 | 76,620.01 | 10, 000, 000 | 10, 076, 620.01 |
| 51 | 14,822, 579.24 | 10, 000, 000 | 24, 822, 579.24 |
| 52 | 25, 640, 133.14 | 10, 000, 000 | 35, 640, 133.14 |
| 53 | 8, 628, 937.6 | 10, 000, 000 | 18, 628, 937.6 |
| 54 | 6, 991, 686.4 | 10, 000, 000 | 16, 991, 686.4 |
| 55 | 7,864, 016.44 | 10, 000, 000 | 17, 864, 016.44 |

#### 3.2.3.3 Kutokupewa Taarifa Sahihi Kuhusu Eneo la Msomera

Wakati wa ziara yetu wananchi waliohamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro walitueleza kwamba, kabla ya kuhamishwa kwao waliahidiwa kwamba sehemu wanapohamishiwa kuna mandhari mazuri, ardhi yenye rutuba na ambayo haimilikiwi na mtu yeyote. Pia waliambiwa eneo hilo ni pori tengefu linalomilikiwa na Serikali hivyo hakuna mtu anayeishi katika eneo hilo. Na pia eneo hilo ni zuri na linafaa kwa mashamba na malisho.

Wananchi walitueleza pia kuwa baada ya kufika katika eneo la Msomera walikuta ni ardhi ya kijiji na ina wamiliki wake, walitueleza kuwa hakuna maeneo ya malisho kwakua maeneo mengi ni ya watu na yaliyobakia ni mapori yasiyokuwa na nyasi. Waliendelea kutueleza kuwa eneo la Msomera ni kame na lisilofaa kwa malisho na hata mashamba waliyopewa ni maeneo ya watu na hivyo kupelekea mgogoro kati yao na wenyeji.

Katika kutembelea eneo la Msomera, tulibaini kwamba ni ardhi ya Kijiji lakini pia haina nyasi kwaajili ya malisho ya mifugo hasa ng'ombe ambao ndio mifugo mama kwa jamii ya kimaasai na wadatoga waliohamishwa kutoka tarafa ya Ngorongoro. Swala hili limejadiliwa na kuchambuliwa kwa undani zaidi katika sura zinazofuata.

#### 3.2.3.4 Uwepo wa Mgogoro wa Ardhi kati ya Wageni na Wenyeji wa Msomera

Wageni waliohamishiwa Msomera walitueleza uwepo wa mgogoro wa ardhi kati yao na wenyeji. Ardhi waliyopewa inamilikiwa kihalali na wenyeji kwani wenyeji waliwaonyesha hati za umiliki wa maeneo hayo. Hii imepelekea kutokuwa na mahusiano mazuri baina yao na wenyeji. Baadhi walisema kwamba wenyeji wamelima kwenye maeneo ambayo wageni wamepewa na wakati mwingine kung'olewa kwa mazao yaliyopandwa.

Baadhi ya wananchi waliohamisahwa kutoka Ngorongoro ambao tuliweza kuwahoji walitueleza kuwa baadhi ya maemneo waliyopewa kama mashamba ni maeneo ambayo yalikuwa yanatumiwa na wananchi wenyeji wa Msomera.
Mfano, mwananchi mmoja alitueleza kuwa:

> *"Mimi sehemu niliyopewa kama shamba ni eneo la mtu ambaye alikuwa analima. Mimi sijalima hapo kwasababu ya kuhofia ugomvi na mmiliki wa shamba hilo."*

#### 3.2.3.5 Kutokuwa na Uhuru wa Kuchagua Sehemu ya Kuhamia

Wananchi wa Ngorongoro walitueleza kwamba katika mchakato wa uhamishwaji hawakupewa chaguo kama wanataka kwenda Msomera au sehemu nyingine ambayo wao wangependa kuhamia. Pia walitueleza kuwa hawakupewa nafasi ya kuchagua kupewa fedha au kuhamia Msomera ama sehemu nyingine. Hivyo, mchakato mzima haukuzingatia maoni ama uamuzi wao.

Baadhi walisema walidai tulikuwa tuko tayari kuchukua garama ziloztumika kujenga nyumba msomera na kuhamia wanakota wenyenyewe ukizingatia sio wote walihamia msomera wana mifugo. Walieleza kuwa fedha ziliotumika kujenga maneneo ya msomera pengine wangelipewa wao wangeamua kwenda kuishi popote pale imliradi pesa watakayopewa iwe ni ya kujitosheleza..

### 3.2.3.6 Hatari ya kufa au kutoweka kwa utamaduni wa jamii ya kimaasai na Kidatoga

Katika ziara hii wananchi walitueleza wasiwasi wa kutoweka au kufa kwa tamaduni na mila zao kwani mazingira ya sasa ya Msomera hayaruhusu jamii ya wamaasai na wadatoga kufurahia na kuendeleza utamaduni wao kwa mfano utamaduni wa kukaa na mifugo nyumbani, matambiko, sherehe za kimila, maeneo ya kuabudia, kuvusha rika na kustaafisha rika.

Mfano wananchi wa Ngorongoro wanakuwa na sehemu maalum za kutambika, kuabudia na hata kufanyia shughuli zingine za kimila. Kreta ya Ngorongoro ndio sehemu pekee inayotumiwa na wananchi wa Ngorongoro katika kipindi cha kuvusha rika. Lakini kwa mazingira ya sasa ya huko Msomera, ni wazi ya kuwa hauna mazingira ya kuendeleza utamaduni wa jamii hizi ziilizokuwa zinaishi kiasili.

Utamaduni huu hauwezi kuendelea Msomera kutokana na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali zilizopo na jinsi eneo lilivyopangwa kwani Msomera imepangwa kama eneo la mji na hakuna mazingira ya wao kuweka mifugo nyumbani na hata hivyo mila na tamaduni za kimaasai na za wadatoga zinamahusiano makubwa na ardhi kwani sherehe mbalimbali hufanyika kwenye miti, mizizi na milima.

### 3.2.3.7 Usalama wa Chakula

Kwenye hii wananchi waliotoka Ngorongoro walieleza kwamba kwasasa wanakabiliwa na njaa kwani takribani miezi mitatu imepita bila ya kuletewa chakula kama ambavyo awali waliahidiwa na mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro. Wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro walituieleza kuwa kulikuwa na utaratibu wa kuletewa mahindi kila baada ya miezi mitatu wakiwa Msomera na sasa haikufanyika kwa miezi mitatu sasa. Hali hiyo imepelekea wananchi wengi kulia njaa kwa sababu ya kukosekana kwa chakula.

Hii pia ikumbukwe kuwa kwa kipindi ambacho hawa watu walihamishwa ilikuwa kipindi cha ukame. Pia kwa mwaka wa 2022 wananchi wengi wa Msomera wamenyang'anywa maeneo yao ya mashamba na hivyo kupelekea kushindwa kulima na kupelekea uhaba wa chakula kijijini hapo. Pia pesa walizolipwa kama fidia ni kidogo sana na wengi wamesema walishazimaliza toka wiki ya kwanza tu.

Mazingira pia ya ufugaji sio mazuri na mifugo yao mingi imekufa na kupelekea wengi kukosa mifugo na wengine kuhamisha. Pia wananchi hawa walikuwa ni wafugaji tu, hawakuwa na uzoefu wa Maisha mengine kama kilimo, hivyo lazima changamoto

ya usalama wa chakula ijitokeze kwa kuwa hawana tena mifugo waliyokuwa wanategemea kwa chakula. Mazingira yote haya yanapelekea kutoa picha halisi ya hali ya kimaisha itakavyokuwa kwa jamii hii iliyohamishiawa eneo hili. Kwa mazingira haya ni vyema zoezi la uhamisha wananchi likafanyiwa tathmini ya kina kabla ya kuendelea kuhamisha watu hawa.

#### 3.2.3.8 Mifugo kufa kwa kukosa Malisho

Mazingira ya Kijiji cha Msomera hayana malisho kwa mifugo hasa ng'ombe hali hii imepelekea ng'ombe wengi waliohamishwa kutoka Ngorongoro kufa kwa kukosa malisho. Hivyo, wananchi wamelazimika kuhamisha mifugo iliyobaki kwenda sehemu mbalimbali nje ya Msomera kama vile kilindi, gendagenda, kabuki, korogwe, mzeri n.k. Kwa mfano familia moja tuliyoitembelea ilitueleza kwamba wakati wanahamia Msomera walikuwa na ng'ombe 70 lakini wamekufa na kubakia 38 tu na mwingine alikuwa na ng'ombe 30 lakini wamekufa wote.

Hali ni mbaya kwa kweli kwenye ufugaji, eneo hili ni orpukeli ( semi-aridi - sio rafiki kwa ufugaji) , Mifugo mfano yangu nilikuja nayo 70 , na sasa nimebaki na 38 pekee na pia hawa 38 imebidi niwapeleke maeneo ya Mseri na maeneo mengine kuomba wapate malisho, na hali hii ni kwa wote tuliokuja na mifugo huk' Anasisitiza Mbunge Mstaafu wa Ngoorongoro aliyehamia Msomera

Sababu kubwa tuliyoelezwa kupelekea wananchi wengi kupoteza mifugo baada ya kuhamishiwa katika kijiji cha Msomera ni:

a) Eneo la Msomera ni kame (semi-arid- Orpukel kwa kimasai) kulinganisha na Ngorongoro ambayo ina ukijani mwingi na ni milimani nyanda za juu.
b) Watu walihamishiwa Msomera katika kipindi cha Kiangazi na ukame
c) Hali ya uoto Msomera ni tofauti kabisa na hali ya uoto wa Ngorongoro.
d) Hakuna sehemu ya kutosha ya kulisha mifugo katika kijijni cha Msomera.
e) Asilimia kubwa ya kanda za malisho katika kijiji cha Msomera ni pori isyikuwa na majani na ni ndogo kulinganisha na idadi ya mifugo.

#### 3.2.3.9 Ukosefu wa Zahanati na Vituo vya afya

Pamoja na kwamba kuna kituo cha afya kikubwa na kisasa kinaendelea kukamilika kama tulivoona wakati wa ziara, wananchi walitueleza kwamba kuna uhaba wa zahanati hivyo huwalazimu kutembea umbali mrefu kwaajili ya kupata huduma za kijamii. Kwa mfano wakazi wa kitongoji cha Mkababu ambapo nyumba 100 zilijengwa na kupewa wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro hawana zahanati, hivyo kulazimika kutembea takribani kilemta 16 ili kufuata huduma hizo katika Kijiji cha Msomera.

#### 3.2.3.10 Uhaba wa Walimu na Shule kulingana na Wingi wa wanafunzi

Wananchi wakazi wa kitongoji cha Mkababu hawana shule na hivyo kulazimika kutembea takribani kilemita 16 ili kufuata huduma hizo katika Kitongoji cha katikati kilichopo kijiji cha Msomera. Hii imepelekea baadhi ya wanafunzi kuacha kwenda shule. Shule ya Msingi Samia Suluhu Hassan iliyopo Msomera, ina jumla ya wanafunzi 883

(674 wamehamia kutoka Ngorongoro), ina jumla ya walimu 7 tu (5 kiume na 2 kike) hivyo kuna uhaba wa walimu 12, madawati 186 na vyumba vya madarasa.

Shule ya sekondari Msomera ina jumla ya wanafunzi 206 lakini walimu wapo 8 tu na wa kike ni mmoja tu na ndio mwalimu pekee anayefundisha masomo ya sayansi. Sekondari hii pia ina uhaba wa mabweni na walimu isipokuwa maabara ambayo tulikuta ujenzi unaendelea. Hivyo kuna uhaba wa walimu kwenye shule ya Msingi Samia Suluhu Hassan na Sekondari ya Msomera. Ukosefu wa mabweni huwapelekea kutembea umbali mrefu ukilinganisha na hali waliyokuwa nayo Ngorongoro ambapo walikuwa wanaishi shuleni.

### 3.2.4 Mahitaji ya Wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro

a) Zoezi la uhamishwaji wa watu kutoka tarafa ya Ngorongoro lisitishwe hadi kutakapokuwa na utaratibu shirikishi na uliopitishwa na Wawakilishi wa Jamii katika Baraza la Madiwani na pia Baraza la Wafugaji

b) Tathmini ya kina ya zoezi la kwanza la kuhamishwa wananchi wa Ngorongoro kwenda Msomera ufanyike

c) Pawe na uhuru wa mtu kuchagua sehemu anayotaka kuhamia na sio kulazimishwa kuhamia Msomera

d) Ujenzi wa nyumba katika Kijiji cha Msomera uzingatie miundo mbinu ya maji

e) Familia / kaya 48 ambazo hazijajengewa nyumba za makazi zijengewe

f) Wananchi 130 ambao hawajapewa fidia na wapo msomera tayari wapewe fidia zao stahiki

g) Serikali isiendelee kuchukua ardhi za wananchi wa Msomera kwa ajili ya kuwapa wao wananngorongoro kwa kuwa inawaletea migogoro.

h) Fidia wanayopewa ni ndogo sana , itafutwe utaratibu mwingine wa kufanya tathmini utakaozingatia mfumo wa maisha wa watu wa Ngorongoro. Kuwe na pesa maalum isiyopunguwa million 50 kwa ajili ya kila kaya inayotaka kuhama Ngorongoro bila kuangalia alichonancho mtu.

i) Wapewe maeneo ya kuchungia mifugo ambayo haina migogoro na yenye maji na majani ya mifugo.

### 3.2.5 Ufafanuzi wa Serikali

Baada ya kutembelea katika Kijiji cha Msomera tulibaini changamoto za watu waliohamishwa toka Ngorongoro zilizotajwa hapo juu na hivyo ilitulazimu kuandika barua kwa Serikali kuomba ufafanuzi wa hoja na malamaiko ya wananchi katika eneo hili. Mbali na kuandika barua na kukumbushia mara kwa mara, hatukufanikiwa kupata majibu ya Serikali kwa njia ya maandishi au kwa njia ya mikutano. Barua ziliekezwa kwa, Mkuu wa Mkoa Arusha, Viongozi wa Wilaya ya Ngorongoro, Mamlaka ya Ngorongoro, Wizara ya Malsili na Utalii pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu lakini hadi tunapomalizia taarifa hii miezi kadhaa badaye hatujapata majibu au ufafanuzi wowote wa hoja tulizowapa kwa ajili ya ufafanuzi.

**3.2.6 Hali ya Haki za Binadamu kwa Wenyeji wa Msomera**

Katika ziara hii tulikutana na wananchi zaidi ya 300 wenyeji wa Msomera. Idadi isiyo rasmi ya wananchi wenyeji ni 6,500 kwa mujibu wa wananachi waliohojiwa . Wananchi wote hawa walikuwa wanaishi katika Kijiji hiki na wengi wao walituonyesha hati za umiliki wa ardhi yao katikia Kijiji cha Msomera. Walitueleza kwamba mwaka 2022 waliona msafara wa magari mengi na walipofuatilia waligundua kuwa ni magari ya wakuu wa mikoa mitatu: Manyara, Tanga na Arusha. Baada ya wakuu hao wa mikoa kuondoka bila kuongea na wananchi, walifuatiwa na ujio wa vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo viliweka kambi katika Kijiji hicho na wanaolikatiza eneo hilo ama kuhoji walirukishwa kichura na wengine kuwekwa ndani.

**3.2.6.1 Changamoto walizoeleza Wenyeji wa Msomera**

Wananchi walielezea changamoto mbalimbali hasa zinazohusu namna ardhi yao ilivyotwaliwa na kuwaacha bila kuwa na maeneo ya makazi, malisho na kilimo. Upimaji na uwekwaji wa vigingi ulifanyika katika maeneo ya mashamba na makazi ya watu. Wananchi wenyeji wa Msomera walieleza pia kuwa baada ya uwekwaji wa vigingi ulifuata ujenzi wa makazi ya nyumba za kisha uhamisho wa watu kutoka tarafa ya Ngorongoro. Kwa mujibu wa maelezo ya wananchi ni kuwa kila aliyejaribu kuhoji au kupinga zoezi la uwekwaji wa vigingi alitishwa kuwekwa ndani.

Kwasasa wenyeji wa Msomera wengi wao hawana maeneo ya kilimo na malisho ya mifugo yao kutokana na maeneo yao kupewa wageni. Wananchi hawa walizunguma na watetezi wa haki za binadamu na kueleza yafuatayo kwa undani.

**(a) Kutokushirikishwa wakati wa Utwaaji wa Ardhi**

Katika ziara yetu wananchi wenyeji wa Msomera katika mkutano wa hadhara na katika usahili wa mtu mmoja mmoja, walitueleza kwamba hawakushirikishwa wakati wa uandaaji wa makazi na baadae uhamisho wa wananchi kutoka katika tarafa ya Ngorongoro kwenda kijiji cha Msomera.

> *“Ardhi yangu niliamka asubuhi na kukuta nyumba inajengwa, nilipouliza nikaambiwa ni kwaajili ya wageni kutoka Ngorongoro, nina hati ya kimila na sikupewa fidia yoyote” –* ***Alisema mkazi wa Msomera***

Wananchi wote ambao tuliweza kuwafikia katika ziara yetu katika kijiji cha Msomera walieleza kuwa maeneo yao ya makazi, mashamba, makaburi na malisho yalitwaliwa kwa nguvu na kujenga makazi ya watu wa Ngorongoro na miradi mbalimbali bila kuwashirikisha wananchi ambao ndio wamiliki halali.

> *“Mimi eneo langu lote ambalo nilifyeka Serikali imechukua na kuwapa wageni kutok Ngorongoro, sina sehemu ya kulima hivyo njaa itakuwa kali sana kwenye familia yangu, sijui hatima ya Maisha na familia yangu” –* ***Mkazi wa Msomera***

### (b) Ardhi ya Wenyeji Kutwaliwa bila Utaratibu wa Kisheria

Wananchi wenyeji wa Msomera walitueleza kwamba Kijiji kilisajiliwa mwaka 1992 na baadhi yao walikuwa wanaishi katika Kijiji hicho kabla ya uhuru, wengine walihamia baada ya uhuru. Wananchi walitueleza zaidi kuwa Msomera kabla ya kuwa Kijiji kilikuwa ni sehemu ya Kijiji cha Mbagwi kilichosajiliwa kipindi cha oparesheni vijiji miaka ya 1970. Baada ya Kijiji kusajiliwa kilikuwa na mamlaka kamili na tangu hapo miradi mbalimbali ya maendeleo kama josho, mabwawa, soko, zahanati, shule, ofisi ya Kijiji na hivi karibuni mwaka 2014 Rais wa awamu ya nne Mhe. Jakaya Kikwete alizindua mradi wa madume ya mbegu ya ng'ombe wa kisasa.

> *"Sisi mzee watu alikuwa na wake 4, jumla ya watoto tupo 37 na wajukuu Zaidi ya 50. Tulikuwa tunamiliki hekari 50 lakini eneo lote limechukuliwa na kubaki na hekari 7 tu, hatuna sehemu ya kulisha mifugo na hatujui tufanye nini maana mifugo inakufa"* ***mkazi mwenyeji wa Msomera.***

Rais aliwahimiza kuongeza maeneo kwaajili ya ufugaji na malisho. Hivyo, mwaka 2016 waliandaa na kupitisha mpango wa matumizi bora ya ardhi. Mpango huo ulitarajiwa kudumu hadi mwaka 2026. Wananchi wengi walituonyesha hati za kumiliki ardhi katika Kijiji cha Msomera ambazo walipata kihalali. Na pia kuna kesi zilizoamuliwa na Mahakama Kuu ya Tanzania juu ya umiliki wa ardhi katika Kijiji cha Msomera.

> *"Sisi familia yetu yenye zaidi ya watu 37 ilikuwa inamiliki shamba lenye ukubwa wa hekari 200 lakini kwa sasa tumeachiwa eneo la hekari mbili na nusu kama sehemu ya makazi ambalo nalo limezungukwa kila upande na hata sehemu ya njia haipo"-* ***Mkazi wa Msomera***

Kwa mfano katika kesi ya Juma Iddi Chambo dhidi ya Julius Leki [Rufaa ya Kesi ya Ardhi Na. 12 ya Mwaka 2019] Mahakam Kuu ya Tanzania, masjala ya Tanga ilitambua uhalali wa ardhi iliyogawiwa na Kijiji cha Msomera tarehe 01/02/2010, na ardhi hiyo ambayo ilikuwa ndio mjadala kwenye kesi tajwa ilichukuliwa na kujengwa kaya 27 za watu waliohamishwa kutoka Ngorongoro bila mmiliki kushirikishwa au kupewa fidia stahiki.

> *"Mimi nilinunua hekari 8 mwaka 2018 kwa Tshs. 370,000. Jumla ya hekari 3 zilichukuliwa na kujengwa shule bila fidia yoyote"* ***Mkazi wa Msomera***

Wengi walidai kwamba hati hizo walipewa na Serikali lakini mwaka 2022 ardhi yao ilitwaliwa na Serikali bila utaratibu wa kisheria, bila fidia na ardhi yao kuwekwa vigingi na kugawiwa kwa wageni kutoka tarafa ya Ngorongoro.

*"Baba, mimi na kaka zangu tulikuwa tunamiliki hekari 297, mzee alikuwa na wake 4 na watoto 21, kwenye boma moja tupo watu 30. Tulipewa hati za kumiliki ardhi mwaka 2010 lakini ardhi yetu yote imechukuliwa na kupewa hekari 7 tu"* ***mkazi wa Msomera.***

**(c) Vitisho na Kunyimwa Uhuru wa Kujieleza**

Katika kuongea na wananchi wenyeji, walitueleza kuwa tangu zoezi la wageni kuhamishiwa katika Kijiji hicho lianze, wamekuwa wakikumbana na vitisho mbalimbali ikiwemo kupigwa, kuwekwa ndani, kutishiwa kufungwa n.k. kwa mfano mmoja wa wananchi alisema...

*"Eneo langu liligawiwa kwa wageni kutoka Ngorongoro, nilipohoji, nilikamatwa na kufungiwa ndani ya nyumba yangu na askari walisimama mlangoni wakiwa wameshika bunduki kwa muda wa saa sita, niliachiwa pale ambapo eneo langu lilimaliza kugawanywa na kuwekewa vigingi"*

***Mwananchi mwingine alisema*** *"Kabla ya zoezi kuanza tuliona msafara wa magari ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Arusha na Manyara, tulizuiliwa kufanya vikao hata vya kimila, ukipita eneo la kambi iliyowekwa na wakuu hao wa mikoa unarushwa kichura chura"*

**(d) Wenyeji wa Msomera kuitwa Wavamizi**

Katika ziara hii wenyeji wa Msomera, walilalamika juu ya kauli ya Serikali ya kuwa wao ni wavamizi katika Kijiji cha Msomera ilihali wao ni wakazi halali wa Kijiji hicho. Walidai pia kwamba Serikali iliwapelekea maendeleo tangu zamani kama vile shule ya msingi, zahanati, barabara, bwawa, soko na mradi wa madume ya mbegu ya ng'ombe za kisasa mwaka 2014.

*"Walitujengea shule, zahanati, kama walitujengea shule, nani atasoma kama sio sisi? huo ni ujanja ujanja wa kutupindua ili wao wawe juu sisi tuwe chini"* ***mmoja wa wana Kijiji alitueleza.***

Wakati tunafanya kikao na Mkuu wa Wilaya ya Handeni wakati akijibu hoja hii alitueleza kwamba wananchi wenyeji wa Msomera wanaitwa wavamizi kwa sababu mwaka 1974 lilianzishwa pori tengefu la Handeni likijumuisha Kijiji cha Msomera ambacho kilisajiliwa mwaka 1992 isivyo halali.

**(e) Tishio la Uhaba wa Usalama wa Chakula**

Kwenye ziara hii wananchi wenyeji wa Msomera walitueleza kwamba kwasasa hawana mashamba ya kulima kwasababu mashamba yao yote yamegawiwa kwa wageni kutoka tarafa ya Ngorongoro na wao kubaki bila eneo lolote la kulima hivyo yawezekana mwakani wasiwe na chakula kwaajili ya familia zao. Kabla ya ujio wa wageni kutoka Ngorongoro wananchi wa Msomera walikuwa wanafanya kilimo na ufugaji kwenye maeneo yao.

Kwa mfano walikuwa wanalima mahindi, maharage n.k kwaajili ya chakula. Kutokana na ujio wa wageni na ardhi yao kugawiwa kwa wageni hawana sehemu tena ya kulima na baadhi yao wamekuwa wakilima maeneo ya wageni kwa nguvu hali inayoweza kusababisha amani na utulivu kutoweka kabisa Msomera.

> *"Mimi sina shamba la kulima kwasababu eneo langu wamepewa wageni wa Ngorongoro, sina sehemu ya kupanda mazao, nitalazimika kung'oa mazao ya aliyepanda shambani kwangu ili nipande mazao yangu maana sina eneo jingine la kulima"-* ***Mwananchi alitueleza.***

**(f) Mifugo kufa kwa kukosa Malisho**

Mazingira ya sasa katika Kijiji cha Msomera sio rafiki kwa ufugaji wa asili kwa namna ambayo ardhi ya Kijiji imepangwa. Kimepangwa kimji zaidi ambapo hamna njia ya mapito ya mifugo kwenda nyumbani kwasababu maeneo karibu yote ni mashamba na makazi ya watu. Eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho ni mbali na makazi ya watu, ni pori, ni dogo na halina nyasi kwaajili ya malisho.

### 3.2.6.2 Mahitaji ya Wananchi

a) Serikali isitishe zoezi la kuwahamishia watu katika Kijiji cha Msomera kwa kuwa hakuna maeneo tena yaliwazi bila kuwa na wamiliki wake

b) Wananchi wanaomba kulipwa fidia kwa maeneo yao ambayo yamechukuliwa na kujengwa miradi mbalimbali ya kijamii na kurudishiwa mashamba yao ambayo bado hayajajengwa

c) Wananchi wameomba kuondolewa vigingi katika maeneo yao ambayo vigingi vimewekwa na ujenzi haujaanza ili kuepuka kuwaleta watu awamu nyingine katika maeneo yenye migogoro.

d) Wananchi wametaka ifanyike tathmini na uchunguzi juu ya madhara yaliyotokana na madhara ya wageni kutoka Ngorongoro na kuhamia katika Kijiji hicho

e) Wananchi wametaka baadhi ya watendaji wa Serikali kuacha vitisho pale ambapo wananchi hao wanadai haki zao

f) Serikali ifuate utaratibu shiriki na wa kisheria katika kutwaa maeneo ya wananchi ili waweze pata stahiki zao kwa ufasaha.

### 3.2.7 Ufafanuzi na Hoja za Serikali

Baada ya kutembelea katika Kijiji cha Msomera tulibaini changamoto zilizotajwa hapo juu na hivyo ilitulazimu kuandika barua kwa Serikali kuomba ufafanuzi. Mbali na kuandika barua na kukumbushia mara kwa mara, hatukufanikiwa kupata majibu ya Serikali kwa njia ya maandishi au kwa njia ya mikutano. Barua ziliekezwa kwa Mkuu wa Wialaya Handeni, Mkuu wa Mkoa Arusha, Viongozi wa Wilaya ya Ngorongoro, Mamlaka ya Ngorongoro, Wizara ya Malsili na Utalii pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu lakini hadi tunapomalizia taarifa hii miezi kadhaa baaye hatujapata majibu au ufafanuzi wowote wa hoja tulizowapa kwa ajili ya ufafanuzi.

Hivyo ufafanuzi uliopo hapa ni ule ambao Serikali iliwahi kuutoa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Bungeni ama kwenye mikutano na wananchi kipindi cha nyuma. Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa akiwa anaongea na wananchi aliwahi kusema Serikali imekabidhi rasmi kijiji cha Msomera kwa Wilaya za Handeni na Kilindi mkoani Tanga ukiwa ni mpango wa kuendeleza kijiji hicho ambacho wakazi wake wengi ni wananchi waliohamia kwa hiari kutoka katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro mkoani Arusha.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema hayo wakati akiongea na mawaziri wa kisekta, wakuu wa mikoa ya Tanga na Arusha, viongozi wa kimila na wawakilishi wa wananchi wa Kijiji cha Msomera wilayani Handeni. *"Leo nimekuja kuwakabidhi rasmi mradi huu wa Kijiji Cha Msomera muweze kuuingiza kwenye mipango yenu ya maendeleo kama ambavyo Serikali kuu imeweza kufanya"* alisema Waziri Mkuu[4].

Waziri Mkuu wa Tanzania Kassim Majaliwa aliwahakikishia wakazi wanaohama kwa hiari yao kutoka katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kuelekea kijiji cha Msomera, Handeni mkoani Tanga kuwa hakuna shughuli zao zitakazosimama na kwamba wataendelea na ufugaji katika mazingira bora zaidi. Aliyasema hayo alhamisi, Juni 23, 2022 wakati akiwaaga wakazi wa Ngorongoro wanaohama kwa hiari yao kwenda kijiji cha Msomera na kupisha shughuli za uhifadhi katika eneo hilo.

> *"Ninawaomba msafiri kwa amani kabisa na mioyo yenu ikunjuke. Isikilizeni Serikali yenu inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan. Sasa hivi mko huru, nenda mkakae kwenye nchi yenu kwa uhuru," **alisisitiza**.*

Kwa upande wake, aliyekuwa Kaimu Mhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, Dkt. Christopher Timbuka alisema awamu ya pili ya zoezi la kuwahamisha wakazi wa eneo la Ngorongoro kwa hiari lilianza Juni 20, 2022, ambapo inahusisha jumla ya kaya 27 zenye watu 127 na mifugo 488. Aidha kaya moja kati ya hizo itahamia Karatu. Dkt. Timbuka alisema hadi sasa kaya zilizohama kwa hiari katika eneo la Ngorongoro katika awamu ya kwanza na ya pili ni 48 zenye jumla ya watu 233 na mifugo 899.

---

4 https://habarileo.co.tz/Serikali-yakabidhi-kijiji-cha-msomera-kilindi-na-handeni/

Alisema utaratibu wa kuwahamisha ulifanyika kwa kufuata hatua mbalimbali ikiwemo kuhakiki idadi ya watu. Pia, hatua nyingine ni kusainisha vitabu vya fidia vya wakazi wanaohama kwa hiari awamu ya pili, kuhakiki idadi ya mifugo na kuiweka alama ili iweze kusafirishwa pamoja na kuhakiki na kutambua aina za nyumba za wakazi hao kwa ajili ya taratibu za ubomoaji.

Dkt. Timbuka alisema mbali na kupewa nyumba, fidia na shamba kaya zote pia zitapewa magunia mawili ya mahindi kwa kwa kipindi cha miezi mitatu ili waweze kujikimu katika kipindi cha mpito wakati wakijiandaa na msimu wa kilimo.

Serikali ilitangaza rasmi kufuta pori tengefu la Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga na ardhi yake kupangiwa matumizi mengine,ikiwemo kupewa wananchi kwaajili ya shughuli za maendeleo. Taarifa hiyo ya Serikali ilitolewa katika mkutano mkuu maalum wa kijiji cha Msomera uliojumuisha wananchi wageni na wenyeji, mkuu wa wilaya ya Handeni Albert Msando alisema ardhi hiyo itakabidhiwa Serikali ya kijiji kwaajili ya matumizi mengine.

'Baada ya kuwatoa Watu kwenye eneo la pori tengefu, tufute pori tengefu iwe ardhi ya jumla tumpe mamlaka Kamishna wa Ardhi na eneo hilo wananchi wagawiwe kwa usawa na haki. Mwenyeji atapewa hekari mbili na nusu na shamba la hekari tano kama ambavyo amepewa mgeni aliefika hapa. – Mkuu wa wilaya ya Handeni Albert Msando[5].

Pia Mhe. DC. Msando wakati anawazungusha wajumbe wa ziara hii katika miradi ya maendeleo katika Kijiji cha Msomera, aliendelea kusema kwamba maagizo yaliotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mwezi uliopita wilayani Handeni mkoani Tanga kuhusu kukamilishwa kwa wakati miradi ya maendeleo iliyopo kijiji cha Msomera yameanza kutekelezwa na Serikali wilayani humo.

"Akizungumza katika ziara ya kikazi katika kijiji cha Msomera mkuu wa wilaya ya Handeni Albert Msando alisema kuwa miradi kama majosho na baadhi ya maji imekamilika na mingine ipo asilimia zaidi ya 90%"[6].

Serikali imeanza mchakato wa kuwapimia na kuwapa maeneo wananchi ambao wamekutwa ndani ya mradi wa kijiji cha Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga ili na wao waweze kumiliki ardhi. Akiongoza zoezi hilo la ukaguzi wa maeneo hayo akiwa na wataalam mbalimbali pamoja na kamati ya ulinzi na usalama mkuu wa wilaya ya Handeni alisema haki zote za binadamu zitazingatiwa.

Mhe Msando alitueleza kuwa, Mheshimiwa Rais ameelekeza walinde haki za kila mmoja katika eneo hili.

---

5 https://www.youtube.com/watch?v=gq_lirFjti8

6 https://www.youtube.com/watch?v=2uVkZXmWQZ8

'Kikubwa tunachosimamia ni kusimamia haki za kibinadamu za wananchi pamoja na kwamba wananchi wamevamia pori tengefu, walivunja sheria lakini kama tunamkuta mwananchi ambae amejenga nyumba yake katika eneo hili maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kuyatenga maeneo yao na kuyakabidhi wale tuliowakuta katika maeneo husika kwahiyo leo hii tumekuja kuangalia na kujiridhisha namna ambavyo timu tuliyoituma imefanya kazi tumeridhishwa kwa namna ambavyo timu tuliyoituma hapa ilivyofanya kazi.- Mkuu wa wilaya ya Handeni Albert Msando[7].

Serikali iliwahi kusema kwamba shughuli ya kuwahamisha wananchi kutoka Hifadhi ya Ngorongoro mkoani Arusha kwenda kijiji cha Msomera wilayani Handeni Mkoa wa Tanga ulifuata taratibu na kulinda haki za binadamu. Ufafanuzi huo ulitolewa baada ya baadhi ya asasi za kiraia kusema haki za binadamu hazikuzingatiwa katika kuwahamisha wananchi hao.
Kauli hiyo ilitolewa jijini Dodoma na baadhi ya mawaziri katika kikao kilichowakutanisha na timu ya wataalamu kutoka Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ikiongozwa na kamishna wake, Dk Litha Ogana.

Wataalamu hao walikuja nchini kufuatilia kuhama kwa wananchi wa Ngorongoro ambapo kabla ya kufanyika kwa mazungumzo hayo, Tume hiyo ilipata fursa ya kutembelea na kufanya mazungumzo na wananchi wa Ngorongoro na Msomera. Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Pindi Chana aliieleza Tume kuwa shughuli ya kuwahamisha wananchi zilifuata haki za binadamu kwani zoezi lilikuwa shirikishi na kwamba bado wananchi wanaendelea kujiandikisha kwa hiari.

> *"Serikali iliamua kufanya uamuzi kwa kuwa wananchi wa Ngorongoro walikuwa hawawezi kumiliki ardhi, kujenga makazi bora ya kudumu na kufanya mambo yao ya maendeleo kwa ajili ya mustakabali wa familia zao,''* ***Dk Pindi Chana.***

Aliieleza timu hiyo kuwa waliohamia Kijiji cha Msomera wamelipwa fidia, wamejengewa nyumba zenye staha pamoja na kupewa hati ya kumiliki ardhi, kupatiwa huduma zote za kijamii ambazo walipokuwa Ngorongoro walizikosa wamelipwa fidia inayostahili pamoja na kusafirishiwa mizigo, mali na mifugo yao kuelekea kwenye makazi mapya na huu ndio msingi wa haki za binadamu." Mwenyekiti wa kikao hicho ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Damas Ndumbaro alisema sheria zilizopo Tanzania hakuna kabila lolote linalomiliki ardhi ya mababu zao hivyo madai ya kwamba Wamasai wanatolewa kwenye ardhi ya mababu zao halina msingi wowote[8].

---

7 https://www.youtube.com/watch?v=rRgBCMvKnJc

8 https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/Serikali-utaratibu-ulifuatwa-kuhamisha-wananchi-ngorongoro-4103404

SURA YA 3
SEHEMU YA TATU

# UCHAMBUZI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI

## 3.3 UTANGULIZI

Sehemu hii inachambua kwa ujumla madai, malalamiko ya wananchi Ngoronngoro na wenyeji wa Msomera pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Serikali. Sehemu hii imezingatia misingi ya utawala bora na haki za binadamu katika kufanya uchambuzi na kufikia hitimisho na mapendekezo. Sehemu hii pia imetambua nia ya Serikali ya kuhifadhi maeneo ya hifadhi lakini inakosoa baadhi ya njia zinazotumika kufikia malengo haya mazuri kwa taifa.

Kwa jumla sehemu hii imetegemea sana hoja za wananchi, hoja za Serikali , hali halisi katika maeneo husika, uelewa wa wachambuzi, sheria na sera za nchi katika kufikia hitimisho la taarifa hiii. Mapendekezo ya sura hii ni ya jumla na yamegusa wananchi, Serikali na tasisi zake, watetezi wa haki za binadamu pamojan na wadau wa maenndeleo.

### 3.3.1 Uchambuzi wa Madai ya Wananchi wa Ngorongoro na Ufafanuzi wa Serikali

Sehemu hii ndogo ya taarifa inachambua kwa pamoja madai, malalamiko ya wananchi wa Ngorongoro waliohamia msomera pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu madai haya. Uchambuzi wa taarifa umezingaia misingi ya kitaalamu yenye kupima hoja za pande zote mbili.

#### a) Uwazi na Ushirikishwaji Katika Zoezi Zima la Uhamishwaji

Wakati wa ziara yetu wananchi walilalamikia mchakato kwenda bila kuwashirikisha viongozi wao wa kisiasa wa ngazi mbalimbali kuanzia Kijiji hadi ngazi ya Wilaya (Halmashauri ya Wilaya). Matoeko ya kutokuwa na utaratabu shirikishi wa kuhamisha watu kwa hiari ulichangia watu wengi kupata fidia ndogo na hata wengine kutokupata fidia hadi sasa. Walidai hawakuwahi kupewa nafasi ya kujadiliana na kukubali utaratibu utakaotumika kukokotoa fidia zao ukizingatia aina ya maisha wailiyokuwa wanaishi katika Tarafa ya Ngorongoro.

Serikali imekuwa ikitoa ufafanuzi mara kwa mara kuwa zoezi hili limekuwa shirikishi kupitia vyombo vya na kupitia mikutano mbalimbali. Lakini hadi tunapomalzia kuandika taarifa hii hatukupata ushahidi wowote wa kimaandishi unaonyesha ni kwa kiasi gani wananchi wa Ngorongoro na wenye wa msomera wameshirikishwa katika zoezi hili.

Katika maswali ya msingi tuliyopenda Serikali kutoa ufanunuzi ambayo hatukuweza pata majibu ni pamoja na maswali yaliyohitaji kupata ushahidi wa jinsi gani wanachi walishirikishwa katika maamuzi haya makubwa yanahusu masiha yao.

Wananchi mfano wa Ngorogoro waliandika hadi taarifa na mapendekezo yao na kuwasilisha hadi kwa Waziri Mkuu lakini hadi leo hawajawahi kuitwa kujadiliana kuhusu mapendekezo yao. Baraza la Halmashauri Ngorongoro ambalo ndio chombo kikubwa cha Maamuzi ya Wilaya halina kumbukumbu yoyote inayohusu hoja ya kuazimia kuanzisha mchakato wa kuamisha wananchi katika Tarafa ya Ngorongoro. Pia Baraza la Wafugaji Ngorongoro ambacho ni chombo cha kisheria kinachosimamia masalahi ya wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro nacho hakina taarifa yoyote rasmi ya kushirikishwa katika maamuzi haya.

Wananchi wa Msomera nao wamelalamika kuona maeneo yao yanachukuliwa bila kufuata taratibu za kisheria. Wananchi hawa kama taarifa hii inavyoenyesha wamehoji sana kwanini ardhi yao imechukuliwa bila kuwashirikisha. Serikali imetoa maelezo kuwa wananchi walishiriksihwa lakini hakuna mihutasari na kumbukumbu za kisheria za Kijiji zinazoenyesha utaratibu uliotumika kuchukua eneo hili la wananchi. Hadi tunakamilisha taarifa hii hatukuweza pata ufafanuzi wa kiushahidi kuhusu namna gani Serikali walishirikisha wenyeji wa Msomera.

Changamoto hii ya wananchi pamoja na viongozi wao kutokushirikishwa ipasavyo katika maamuzi haya yamebainika pia na matokeo ya awali ya ufuatilijiwa wa Tume ya Haki za Binadamu Barani Africa iliyotolewa tarehe 28/12023. Taarifa hii ya awali imeeleza pia katika changamoto walizokutana nazo katika zoezi hili la uhamishaji ni swala la kutokuwepo kwa ushirikishwaji na uwazi wa mchakato huu. Pia taarifa ya Mkaguzi na Mthibiti Mkuu wa Fedha za Umma inaonyesha pia kuna changamoto za kiutaratibu katika zoezi hili.

**b) Fidia Ndogo kwa Wananchi waliohamia Msomera**

Muundo wa Kamati ya Fidia ulijumuisha Katibu Tarafa, Muwakilishi kutoka wizara ya maliasili na utalii, Muwakilishi kutoka ofisi ya mkuu wa wilaya, Muwakilishi kutoka mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na Muwakilishi kutoka idara ya ardhi. Wananchi hawakuwekwa wazi katika zoezi zima la kuhamishwa hali iliyopelekea kupewa fidia ndogo isiyokidhi mahitaji ya familia. Kamati hii ilipaswa kuwa na wawakilishi wa jamii kama vile madiwani na viongozi wa Baraza la Wafugaji.

Ufafanuzi kuhusu utaratibu huu wa kuamua fidia haukupatikani kutoka kwa Serikali hivyo inakuwa vigumu kufanya uchambuzi wa kina katika changamoto hii iliyotolewa na wananchi.

Katika mazingira hayo hayo fidia za wananchi zinaonekakana kuwa ndogo sana kuanzia laki tano hadi million tatu  ni kutokana na wananchi na viongozi wao kutokushiriki katika mchakato mzima. Mfano wananchi walifunguliwa hadi  akaunti mpya za benki kwaajili ya kuwekewa fedha.

Wakati wa ziara ya Tume ya Afrika Juu ya Haki za Binadamu na Watu nchini Tanzania ilipokuwa inafuatilia zoezi lililofanyika la kuwahamisha wamaasai kutoka Ngorongoro kwenda Msomera Waziri wa Maliasili na Utalii wa wakati huo, Dk. Pindi Chana aliieleza Tume kuwa:

> *"Waliohamia Kijiji cha Msomera wamelipwa fidia, wamejengewa nyumba zenye staha pamoja na kupewa hati ya kumiliki ardhi, kupatiwa huduma zote za kijamii ambazo walipokuwa Ngorongoro walizikosa.....wamelipwa fidia inayostahili pamoja na kusafirishiwa mizigo, mali na mifugo yao kuelekea kwenye makazi mapya na huu ndio msingi wa haki za binadamu."*

Katika ziara hii wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro walitueleza kwamba utaratibu wa fidia ulikuwa wa kificho sana, haukuwa wa wazi. Hapakuwa na utaratibu maalumu wa kufanya tathmini kabla ya mtu kupewa fidia, wala hakuna mtu aliyejua atapewa kiasi gani cha fidia isipokuwa walijua siku ya kuhama ambapo waliitwa na kusainishwa Karatu yalipo makao makuu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

- Fidia waliyopewa haikuzingatia utajiri au mali walizoacha Ngorongoro kutokana na ukweli kwamba wakati wote wa Maisha yao Ngorongoro hawakuruhusiwa kujenga nyumba za kisasa au kufanya shughuli za kiuchumi isipokuwa ufugaji pekee.
- Fidia pia haikuzingatia ukubwa wa familia / boma.
- Baadhi ya familia walipewa chini ya kiasi cha shilingi laki tano, wengi wao wakipewea kati ya million moja hadi million tatu.
- Lakini pia katika ziara hii tuligundua kwamba familia / kaya 48 zilikuwa hazijajengewa nyumba na hazikupewa fidia yoyote. Kaya hizo zina jumla ya watu 130 ambao wamekuwa wakiishi Msomera bila kupwa stahiki ya fidia zao.
- Vilevile wananchi wenyeji wa Msomera walilalamika ardhi yao kuchukuliwa bila ya kupewa fidia ya aina yoyote ingawa walikuwa wanamiliki ardhi kihalali wakiwa na hati za kimila.

Kwa uchambuzi huu manake kaya moja katika kaya 500 zilizohamia Msomera , kila kaya iliweza pata Milioni kumi ya Asante Mama pamoja na hizo fidia ambazo asiliamia 80 walipata chini ya million 3.  Kitendo cha kuongeza million 10  kwa kila kaya ni kielezo sahihi kuonyesha kuwa utaratibu wa fidia kwa wananchi wa Ngorongoro haupaswi kuangalia wanacho miliki peke yake bali kuwe na fedha ya ziada ambayo itatolewa sawa kwa wote.

Tunapongeza sana hatua hii walau ya kuongeza million kumi kwani hali za kimaisha ingekuwa mbaya zaidi kama wote wangeondoka kwa kutegenmea tathmini iliyofanywa na timu iliyokuwa inafanya tathmini. Hata hiyo million kumi haifai kwa hali ya sasa ya maisha , hivyo wananchi wanapendekeza walau kuwepo na fidia ya milioni 50 hadi million 100 kwa kila kaya endapo kutakuwepo na nafasi ya kukaa nchini na wananchi na kupendekeza utaratibu bora wa kuhama kwa hiari. Fidia hii, manake mwananchi apewe 50 milion lakini apewe eneo la kujengewa nyumba, au apewe million 100 bila nyongeza ya ardhi wala nyumba ili akatafute mwenyewe eneo la kuhamia.

Wananchi walitueleza zaidi kwamba mamlaka ya hifadhi ndio iliwafungulia akaunti za benki kwaajili ya kuwekewa fedha za fidia. Wale ambao walikuwa na akaunti zao tayari, zilikataliwa na walifunguliwa akaunti zingine mpya na maafisa kutoka mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro. Hadi tunaandika taarifa hii hatukupata ufafanuzi wa Serikali kuhusu malalamiko haya pamoja na jitihada zote za kuomba ufafanuzi wa Serikali kuhusu utaratibu huu.

Lakini pia mchakato wa tathmini ulighubikwa na usiri kwasababu hawakupewa mrejesho wa tathmini iliyofanyika na kiwango ambacho walistahili kulipwa. Fedha pekee iliyofahamika tangu awali ni fedha taslimu za kitanzania shilingi milioni kumi maarufu kama **"asante mama".** Lakini pia fidia haikuzingatia ukweli kwamba wananchi wa Ngorongoro walizuiliwa kufanya shughuli za kimaendeleo kama vile kujenga nyumba za kisasa, kilimo na kumiliki vyombo vya usafiri. Hatimaye fidia walizopewa zilkuwa ndogo inavyoonekana katika jedwali katika taarifa hii.

Kutokna na hali halisi ya wananchi kutokuwa sehemu ya mchakato hii , ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kusitisha zoezi hili hadi kutakapokuwa na utaratibu shirikishi na uliopitishwa na Wawakilishi wa Jamii katika Baraza la Madiwani la Ngorongoro na pia Baraza la Wafugaji. Hii ni kutokana na wananchi kutokushirikishwa katika awamu ya kwanza ya uhamishwaji wa wananchi. Lakini pia hakuna mpango mkakati au mpango kazi wa uhamishwaji wa wananchi kutoka tarafa ya Ngorongoro.

#### c) Uhuru wa Kuchagua Pakwenda

Ni muhimu kwa mwananchi anayetaka kuhama Ngorongoro kuwa na uhuru wa kuchagua sehemu anayotaka kwenda kuishi na sio kulazimishwa kwenda Msomera. Kitendo cha wananchi kulazimishwa kwenda Msomera kinaondoa dhana ya kwamba wananchi wanahama kwa hiari.

Pia hoja hii hadi tunapoandika na kukamilisha taarifa hii haikuwa imepata maelezo na ufafanuzi kwa Serikali. Imekuwa vigumu pia kufanya uchambuzi wowote katika hoja hii kwa kuwa maalezo ya kina ya Serikali kuhusu maswala yanayohusu hoja hii hayakupatikana. Ufuatiliji wetu umebaini kuwa kutokuwepo na utaratibu mzuri wa kuhama kwa hiari na wenye nafasi mbalimbali za kuchagua namna ya kuhamaa kwa hiari una adhari nyingi kwa mchakato huu kwa pande zote mbili ( Serikali na wananchi).

Pengine utaratibu wa kuhama kwa hiari ungekuwa umeandikwa na wa wawazi na wenye kuwapa watu uhuru wa kuchagua wananchi wengi wangeamua kujitokeza baada ya kuona haki zao za msingi zimelindwa na utaratibu wa wazi wa kuhama kwa hiari.

### 3.3.2 Uchambuzi wa Madai wa Wenyeji wa Msomera na Ufafanuzi wa Serikali

Wakati wa ziara hii Mkuu wa Wilaya ya Handeni alisema kwamba haki zote za binadamu zilizingatiwa wakati wa upimaji na ugawaji wa ardhi kwa wageni na wenyeji wa Kijiji cha Msomera. Mkuu wa Wilaya huyo alisema

"Mheshimiwa Rais ameelekeza kwanza tulinde haki za kila mmoja katika eneo hili. Kikubwa tunachosimamia ni kusimamia haki za kibinadamu za wananchi pamoja na kwamba wananchi wamevamia pori tengefu, walivunja sheria lakini kama tunamkuta mwananchi ambae amejenga nyumba yake katika eneo hili maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kuyatenga maeneo yao na kuwakabidhi wale tuliowakuta katika maeneo husika"[9].

Pamoja na kwamba Mhe DC wa Handen anasema haki za binadamu zimezingatiwa, uhalisia wa mazingiria na taarifa za wananchi zilizochakatwa na taarifa hii zinazonyesha kulikuwa na tatizo kubwa la kuchukua maeneo ya wananchi wa Kijiji cha msomera bila kufuata taratibu za kisheria kwa kuwa Msomera kwa mujibu wa ufuatiliji huu kilikuwa ni Kijiji halali kilichosajiliwa. Hivyo kuchukua maeneo yao bila kuzingatia suala la ushirikishwaji na kufuata taratibu za kisheria kutwaa maeneo ni kukiuka haki za kikatiba dhidi ya wananchi hawa wa Msomera.

Hata hivyo ufuatiliaji wetu huu umebani jitahada kubwa zinazofanywa na Mkuu wa Wilaya wa sasa wa Handeni kama vile kujitahidi kukaa karibu na wananchi na kuwasililiza kwa karibu umesaidia kupunguza mvutano mkubwa uliokuwepo kati ya wenyeji na wahamiaji. Wananchi walitueleza walau kwa uongozi huu yapo mambo ambayo pengine yangekuwa mabaya zaidi kwa wana Msomera pamoja na wageni kama sio jitahada kubwa za Mkuuu wa Wilaya kujaribu kuzitatua baadhi ya changamoto.

#### a) Uwazi na Ushirikishwaji Katika Zoezi la Kutwaa Ardhi ya Msomera

Baada ya kuchambua hoja za Serikali pamoja na malalamiko ya wananchi, tarifa hii imebaini Msomera kilikuwa ni Kijiji halali cha wananchi wa Msomera. Wananchi wenyeji wa Kijiji cha Msomera wameishi miongo kadhaa katika Kijiji hicho na hivyo sio wavamizi kwa maana hata sheria iliyoanzisha mapori tengefu likiwemo pori tengefu la Handeni haikukataza wananchi kuishi na kufanya shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo.

Kijiji cha Msomera kilisajiliwa kwa mujibu wa sheria mwaka 1992 na kabla ya hapo Msomera ilikuwa sehemu ya Kijiji cha Mbagwi kilichoanzishwa kipindi cha oparesheni

---

9 https://www.youtube.com/watch?v=rRgBCMvKnJc

vijiji. Pamoja na kwamba uongozi wa wilaya ulieleza kuwa utaratibu ulizingatiwa, taarifa hii inaonyesha utwaaji wa ardhi ya Kijiji cha Msomera haukuzingatia utaratibu wa kisheria wa utwaaji wa ardhi kwa mujibu wa sheria ya utwaaji wa ardhi.

Misingi ya utawala bora, utawala wa sheria na haki za binadamu haikufuatwa katika michakato yote miwili yaani katika zoezi la kuwahamisha watu wa tarafa ya Ngorongoro na wenyeji wa Msomera juu ya ujio wa wageni na utwaaji wa ardhi yao. Sheria ya Utwaaji wa ardhi pia haikuzingatiwa kwasababu wenyeji wa Msomera hawakushirikishwa wala kupewa fidia ya aina yoyote.

Katika ziara yetu katika Kijiji cha Msomera wananchi walitueleza kuwa hawakushirikishwa wakati maeneo yao yanatwaliwa na serikali na kupewa wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongor Sababu iliyofanya wananchi wa Msomera wasishirikishwe wakati ardhi yao inatwaliwa ni madai ya kuwa wao ni wavamizi katika Kijiji hicho. Walitueleza pia kuwa serikali iliwambia wao ni wavamizi katika Pori Tengefu la Handeni na hivyo eneo hilo ni mali ya serikali.

Mnamo tarehe 26.01.2023 wakati Tume ya Haki za Binadamu na watu ilipotembelea Kijiji cha Msomera Mkuu wa Mkoa wa Tanga aliwaeleza makamishina wa tume hiyo kuwa eneo hilo ilikuwa ni Pori Tengefu na wananchi wenyeji wa Kijiji hicho ni wavamizi.

Katika utafiti wetu tuliweza kubaini kuwa Kijiji cha Msomera kilisajiliwa mwaka 1992 kikiwa na hati ya usajili yenye namba TA/KIJ/576. Kijiji cha Msomera kabla ya kujitegemea mwaka 1992, kilikuwa ni sehemu ya Kijiji cha Mbagwi ambacho kimesajiliwa katika oparesheni vijiji miaka ya 1970. Baada ya kusajiliwa mwaka 1992, kijiji cha Msomera kiliendelea kupata huduma mbalimbali za kijamii hadi sasa.

Mnamo 2016, kijiji cha Msomera kilijipatia mpango wa matumizi bora ya ardhi pamoja na kuitingia sheria ndogo. Wananchi pia wametueleza kuwa, kijiji cha Msomera kilikuwa inakaliwa na wananchi hata kabla ya uhuru. Baada ya kufanya uchambuzi wetu tulibaini kuwa Msomera ipo ndani ya Pori Tengefu la Handeni lakini hata hivyo haliwezi kufanya watu ambao wenye makazi yao ndani ya eneo hilo kuwa wavamizi.

Ni muhimu kufahamika kuwa Pori Tengufu 48 zilizo anzishwa Tanganyika mwaka 1951 ikiwepo Pori Tengefu la Handeni haikuzuia shughuli za binadamu katika maeneo hayo. Tafauti na Hifadhi za Taifa ambapo shughuli za binadamu zimekatazwa, sheria haijaweka katazo lolote la kuishi katika mapori tengefu. Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 1951(Fauna Conservation Ordinance, 1951) imeruhusu watu kuishi ndani ya mapori tengefu. Sheria hiyo imelenga tu kuzuia uwindaji katika maeneo hayo na sio makazi au shughuli za binadamu. Sheria ya mwaka 1951 ilifutwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori No. 12 ya 1974 ambayo pia iliendelea kuruhusu makazi ya watu na shughuli za binadamu katika mapori tengefu.[10]

---

10 Vifungu vya 6,7,8,9 na 10 ya Sheria ya uhifadhi wa Wanyamapori, No. 12 ya mwaka 1974.

Sheria ya uhifadhi wa Wanyamapori Sura 283 ya 2009 ilifuta sheria ya awali iliyokuwepo ya mwaka 1974. Wakati wa operesheni vijiji, maeneo mengi ya mapori tengefu pia yamesajilikuwa kuwa vijiji huku zingiendelea na hadhi ya kuwa mapori tengefu hadi 2009. Mnamo 2009, sheria iliyotungwa imekuja na suluhisho la mkanganyiko ya kihistoria kati ya vijiji, shughuli za binadamu na mapori tengefu.

Wakati sheria ya 2009 ikikataza shughuli za binadamu katika mapori tengefu iliweka pia utaratibu wa kuepusha migogoro katika maeneo ambayo yameshakuwa ni maeneo ya Kijiji. Kwakuwa Sheria hii ilitungwa mwaka 2009 na tayari kulikuwa na mapori tengefu 48 nchi nzima, kifungu cha 16 (4) kilimtaka Waziri afanye mapitio ya mapori tengefu yote nchini ili kujiridhisha ni mapori yapi yalikuwa yanasifa za kuendelea kuwa mapori tengefu na ayatangaze ndani ya miezi 12. Mapori hayo tengefu yalikuwa ni kama yafuatayo:

Burunge, Chabula Marsh, Enduleni, Gombe, Handeni, Igombe Dam, Kalimawe, Kigosi, Kihirumira Pool, Kilombero, Kitwai, Kongwa, Lake Daramatai, Lake Kwela, Lake Manka, Lake Natron, Lihogosa, Loliondo, Lolkisale, Longido, Luganzo, Lunda Mkwambi, Masasi River, Maswa, Meserani Dam, Mkungunero, Mlele, Moyowosi, Msima, Mto-Wa-Mbu, Muhuwesi, Mwadui Diamond Mine, Mwambesi, Nchwa-Nkima, Ngeju-Njiro Dam, Ngorongoro, Nyonga, Rau Forest, Rukwa, Rungwa River, Ruvu Masai, Ruvu Same, Sanya-Lelatema, Simanjiro, Speke Gulf, Ugunda, Umba River na Utengule Swamps.

Wakati huo huo, Kifungu 16(5) cha Sheria hii kilimkataza Waziri kujumuisha sehemu yoyote ya ardhi ambayo inaangukia katika eneo la kijiji kuwa pori tengefu. Hii ni kwasababu Sheria za awali zilizosimamia mapori tengefu kama vile ya mwaka 1951 na 1974 hazikuzuia watu kuishi na kufanya shughuli za kijamii, kiutamaduni na shughuli za kiuchumi ndani ya mapori tengefu. Hii maana yake ni kwamba, Waziri alitakiwa afanye mapitio ya mapori tengefu yote, na yale anayoona hayaangukii ardhi ya eneo la Kijiji ayatangaze ndani ya miezi 12. Kutokufanya hivyo, maana yake ni kwamba hakutakuwa na mapori tengefu.

Baada ya uchambuzi huu, sisi watetezi wa haki za binadamu tumeona kuwa wananchi wenyeji wa Msomera sio wavamizi katika kijiji hicho. Tunaongeza pia kuwa hatua yoyote ya utwaaji wa maeneo yao ingepaswa kufuata taratibu za kisheria ya utwaaji wa ardhi chini ya Sheria ya Utwaaji wa Ardhi na Katiba ya nchi. Tumebaini pia kuwa ardhi ya wananchi wenyeji wa Msaomera imetwaliwa na hakuna taratibu zozote za kisheria zilizofuatwa na serikali.

### b) Hali ya Ufugaji katika Kijiji cha Msomera

Mazingira ya Kijiji cha Msomera kwa sasa sio rafiki kwa ufugaji wa asili hasa ng'ombe kwani hakuna nyasi kwaajili ya malisho, Kijiji kimepangwa kimakazi zaidi na sio kifugaji ukizingatia mfumo wa maisha ya wafugaji wa asili. Kipaumbele kikubwa cha wafugaji wa asili ni eneo pana lenye malisho na Msomera haina maeneo hayo kwasasa. Hivyo ufugaji wa ng'ombe kiasili unafaa katika maeneo mengine mfano wilaya ya Ngorongoro, Kilindi nk lakini sio Msomera.

### 3.3.3 Mapendekezo Mahusus "( Specific Recommendations)

Sehemu hii inatoa mapendekezo ya watetezi wa haki za binadamu baada ya kufanya uchambuzi wa kina kuhusu madai ya wananchi na ufafanuzi wa Serikali. Mapendekezo haya yamejikita zaidi katika kuhakikisha madai ya wananchi yaliyoonekana kuwa ya msingi na taaarifa hii yanafanyiwa kazi ili kuepuka kuendelea kukiuka haki za wananchi wa msomera wenyeji pamoja na wale wanaohamia toka Tarafa ya Ngorongoro.

Mapendekezo haya yanagusa makundi muhimu kama Serikali na taasisi zake zote zinahisika na swala hili la uhamishwaji wa watu toka Tarafa ya Ngorongoro, wananchi wenyewe , watetezi wa haki za binadamu, wana Habari na wadau wa maendeleo.

#### 3.3.3.1 Mapendekezo Kuhusu Madai Ya Wananchi Wa Ngorongoro

**a) Mapendekezo Kwa Serikali na Uongozi wa Wilaya ya Handeni**

I. Tunishauri Serikali iwachukulie hatua baadhi ya watumishi wake wanatoa vitisho dhidi ya wanachi wa Ngorongoro hasa pale ambapo wanadai haki zao
II. Tunaishauri Serikali kutatua changamoto ya maji ya chunvi kule msomera
III. Tunaishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa shule mpya ya msingi mkababu na ujenzi wa bweni kwa wanafunzi wa sekondari
IV. Tunamuomba Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusitisha zoezi la kuondoa wananchi katika tarafa ya Ngorongoro ili kutoa nafasi ya kufanyia kazi changamoto hizi na pia kutoa nafasi ya kuandaa kwa pamoja mpango wa uhamaji kwa hiari wa muda mrefu na mfupi wenye kuzingatia misingi ya haki za binadamu na shirikishi.
V. Serikali kuheshimu na kuzingatia haki za binadamu kwenye masuala yanayogusa maslahi ya watu

**(b) Mapendekezo Kwa Wananchi**

I. Tunawaomba wananchi kudumisha amani na wazingatie njia ya kimahakama katika kudai haki zao
II. Tunawaomba wananchi kufanya mikutano na kujadiliana juu ya namna ya kutatua changamoto za huduma za kijamii
III. Tunawaomba wananchi kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo ambayo wamepewa
IV. Tunawaomba wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwaajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya kijamii wachukue hatua za kudai fidia

**(c) Mapendekezo Kwa wadau wa maendeleo**

I. Tunawaomba wadau wa maendeleo kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo katika Kijiji cha Msomera
II. Wahimize uzingatiwaji wa haki za binadamu na utawala wa sheria katika mchakato mzima wa uhamishwaji wa wananchi

**(d) Mapendekezo Kwa watetezi wa haki za Binadamu na Asasi za Kiraia**

I. Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika Kijiji cha Msomera
II. Kuendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wakazi wa Kijiji cha Msomera
III. Kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kutatua changamoto katika Kijiji cha Msomera na tarafa ya Ngorongoro
IV. Kuendelea kufuatilia misingi ya haki za binadamu, utawala bora, utawala wa sheria katika mchakato wa uhamishwaji wa wananchi na katika utwaaji wa ardhi katika Kijiji cha Msomera

**(e) Mapendekezo kwa Vyombo vya Habari**

I. Tunawasihi baadhi ya waandishi wa habari waache kueneza propaganda za chuki na uongo dhidi ya wananchi wa Kijiji cha Msomera na tarafa ya Ngorongoro
II. Waandishi wa habari wazingatie misingi ya taaluma yao kwa kutoa taarifa ambazo sio za upande mmoja na watoe taarifa za kweli
III. Wasikubali kutumika kwa ajili ya pesa na kuwaumiza wananchi wale badala yake wasaidie Serikali na wananchi kuwa kitu kimoja na waache tabia ya kuchonganisha wananchi na Serikali.

**3.3.3.2 Mapendekezo Kuhusu Madai Ya Wananchi Wenyeji Wa Msomera**

**a) Mapendekezo Kwa Serikali na Uongozi wa Wilaya ya Handeni**

I. Tunashauri baadhi viongozi wa Serikali waache vitisho dhidi ya wakazi wa Msomera hasa pale ambapo wanadai haki zao
II. Tunaishauri Serikali kutatua changamoto ya maji ya chumvi
III. Tunaishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa shule mpya ya msingi mkababu na ujenzi wa bweni kwa wanafunzi wa sekondari
IV. Tunamuomba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusitisha zoezi la kuondoa wananchi katika tarafa ya Ngorongoro
V. Serikali kuheshimu na kuzingatia haki za binadamu kwenye masuala yanayogusa maslahi ya watu
VI. Serikali iandae "resettlement plan" kwanza kabla ya kuhamisha watu kutoka eneo moja kwenda kwingine.

**b) Mapendekezo Kwa Wananchi**

I. Tunawaomba wananchi kudumisha amani na wazingatie njia ya kimahakama katika kudai haki zao
II. Tunawaomba wananchi kufanya mikutano na kujadiliana juu ya namna ya kutatua changamoto za huduma za kijamii
III. Tunawaomba wananchi kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo ambayo wamepewa
IV. Tunawaomba wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwaajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya kijamii wachukue hatua za kudai fidia

**c) Mapendekezo Kwa wadau wa Maendeleo**

I. Tunawaomba wadau wa maendeleo kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo katika Kijiji cha Msomera

II. Wahimize uzingatiwaji wa haki za binadamu na utawala wa sheria katika mchakato mzima wa uhamishwaji wa wananchi

**c) Mapendekezo Kwa watetezi wa haki za Binadamu na Asasi za Kiraia**

I. Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika Kijiji cha Msomera

II. Kuendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wakazi wa Kijiji cha Msomera

III. Kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kutatua changamoto katika Kijiji cha Msomera na tarafa ya Ngorongoro

IV. Kuendelea kufuatilia misingi ya haki za binadamu, utawala bora, utawala wa sheria katika mchakato wa uhamishwaji wa wananchi na katika utwaaji wa ardhi katika Kijiji cha Msomera

**a) Mapendekezo Kwa Vyombo vya Habari**

(i) Tunawaomba waandishi wa habari waache kueneza propaganda za chuki na uongo dhidi ya wananchi wa Kijiji cha Msomera na tarafa ya Ngorongoro

(ii) Waandishi wa habari wazingatie misingi ya taaluma yao kwa kutoa taarifa ambazo sio za upande mmoja na watoe taarifa za kweli

SURA YA 3
SEHEMU YA NNE

# MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO

## 3.4 UTANGULIZI

Sehemu hii ya mwisho katika sura hiii ya tatu ya Taarifa hii inatoa mapendekezo ya jumla kuhusu matokeo ya ufuatiliaji huu katika Kijiji cha Msomera pamoja na kutoa hitimisho la taarifa hii.

### 3.4.1 Mapendekezo ya Jumla

(a) Wananchi kwa upande wao wameitaka Serikali kupitia upya mchakato mzima wa kuwahamishia wananchi wa Ngorongoro katika eneo hilo kwa kuwa sio shirikishi.

(b) Wananchi wenyeji wa Ngorongoro waliohamishiwa msomera wameitaka Serikali wasitishe zoezi la kuwahamisha wananchi wenzao kutoka Ngorongoro ili watatue changamoto zinazotokana na zoezi hilo la awali.

(c) Wananchi wenyeji wa Ngorongoro wameitaka Serikali wapitie mchakato wa ulipaji fidia kwa kuwa sio shirikishi na wala hauko wazi. Na kuwa kiwango cha Milioni Kumi kama pesa ya fidia kwa kila kaya iongezeke hadi kufikia million 50 au million 100 kwa atakayetaka kuchagua kuchukua hela na kwenda anakotaka.

(d) Wananchi wenyeji wa Ngorongoro wameitaka Serikali kuangalia upya maeneo ya malisho kama mojawapo ya chanagomoto inayowakabili

(e) Wananchi wenyeji wa msomera wameitaka Serikali waangalie upya zoezi la umilikishwaji wa ardhi kwa Wananchi waliotoka Ngorongoro kwa kuwa zoezi hilo halijafuata taratibu za kisheria hali iliyopelekea wananchi kunyang'anywa maeneo yao ambayo wanazo hati miliki kisheria.

### 3.4.2 Hitimisho

Tunaushukuru uongozi wa wilaya ya Handeni kwa kutupa ushirikiano wakati wa ziara tuliyofanya kwenye Kijiji cha Msomera wilayni Handeni. Shukrani za dhati kwa wananchi waliotupatia taarifa mbalimbali zilizosheheni kwenye ripoti hii. Changamoto kubwa iliyojitokeza ni wananchi kutokushirikishwa katika zoezi la kuhamishiwa Msomera, lakininpia kwa wananchi wenyeji kutokushirikishwa juu ya ujio wa wageni kutoka Ngorongoro. vilevile pande zote mbili hawajapewa fidia stahiki na wengine kukosa kabisa hasa wenyeji wa Msomera. Zoezi la uhamishwaji wa wananchi kutoka Ngorongoro linapaswa kusitishwa kwani Msomera hakuna ardhi kwaajili ya malisho ya mifugo kutoka Ngorongoro. Mpangilio wa Kijiji ni wa kimji na sio kwaajili ya kilimo na ufugaji nhivyo sio rafiki wa wamasai kutoka Ngorongoro waliozoea kuishi kwa ufugaji.





SURA YA 4
SEHEMU YA KWANZA

# HALI YA HAKI ZA BINADAMU TARAFA YA NGORONGORO

## 4.1 UTANGULIZI

Sura hii ya nne ya taarifa hii inaelezea hali ya haki za binadamu katika Tarafa ya Ngorongoro (Hifadhi ya Ngorongoro). Pia sura hii inachambua hoja za wananchi pamoja na hoja za Serikali kwa pamoja na kuweza kutoa mapendekezo kwa makundi husika.

### 4.1.1 Kuhusu Tarafa ya Ngorongoro

Wilaya ya Ngorongoro ni moja kati ya Wilaya sita (6) na moja kati ya Halmashauri saba (7) zilizopo katika Mkoa wa Arusha iliyoanzishwa rasmi mwezi Julai mwaka 1979 baada ya Serikali kugawanya toka eneo la wilaya ya Monduli wakati huo ikiitwa wilaya ya maasai (Maasai District) ambapo pia jina wilaya ya Maasai lilitokana na neno 'Masailand', ambapo wakoloni waliita hivyo baada ya kukuta asilimia kubwa ya wenyeji katika maeneo hayo ni wamaasai. Kwa mujibu wa ripoti ya sensa ya mwaka 2022 wilaya ya Ngorongoro ina jumla ya wakazi 273, 549, ambapo tarafa ya Ngorongoro ina jumla ya wakazi 100,793.[11]

Wilaya ya Ngorongoro ina ukubwa wa kilometa za mraba 14,036. Kiutawala Wilaya imegawanyika katika Tarafa 3 (Ngorongoro/NCAA, Loliondo na Sale). Tarafa ya Ngorongoro ina jumla ya ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 8,100 kwa sasa, ikiwa na jumla ya kata 11 na vijiji 25. Kijiografia na Kisheria Tarafa hii ndio sehemu yenye Hifadhi ya Ngorongoro (Ngorongoro Conservation Area). Tarafa ya Ngorongoro inapakana na Karatu upande wa Kusini, Tarafa za Loliondo pamoja na Sale zipo upande wa Kaskazini , Hifadhi ya Serengeti pamoja na Pori la Akiba la Maswa vipo upande wa Magharibi mwa tarafa ya Ngorongoro wakati Wilaya za Longido na Monduli zipo upande wa Mashariki.

Tarafa hii ni mojawapo ya eneo lenye uoto wa asili mzuri , milima na mabonde ya kuvutia, majani, hali ya hewa nzuri na mazingira mazuri ya kuvutia , Wanyama , mifugo , binadamu pamoja na watalii. Tarafa hii ndio Tarafa kubwa katika Wilaya ya Ngorongoro yenye eneo zaidi ya nusu ya eneo lote la Wilaya.

---

11 The 2022 Population and Housing Census: Administrative Units Population Distribution Report; Tanzania Mainland, December 2022.





**Fig. 3**: The Ngorongoro Conservation Area where the review exercise targeted. This the place where the pastoralist population close to 90,000 individuals are threatened by the looming evictions.

*Ramani ya Tarafa ya Ngorongoro*[12]

#### 4.1.2 Kuhusu Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (The Ngorongoro Conservation Area **(NCA)** ni mojawapo ya hifadhi huru inayojitegemea hapa nchini- Hifadhi hii haipo chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa kuwa ina sheria yake iliyoianzisha ya Mwaka 1959. (The Ngorongoro Conservation Act). **Eneo hili linasimamiwa na Mamlaka** ya Hifadhi ya Ngorongoro (Ngorongoro Conservarion Area Authority, NCAA). NCAA ni mamlaka iliyoundwa na sheria yake mwaka 1959 kwa lengo la kusimamia eneo hili maalum lenye malengo matatu katika uanzishwaji wake, yaani: kulinda maslahi ya wenyeji, uhifadhi na utalii.

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ni eneo la kipekee lenye matumizi ya mseto ya ardhi.

Sheria ya NCA inatambua eneo hili kwa ajili ya uhifadhi, utalii lakini pia kwa matumizi ya watu hasa jamii ya wamasai ambao ni wengi na makabila mengine kama wahadzabe na wabarbaig ambao sheria imewataja.[13] Eneo hili linatumika pia kwa shughuli za

12 The Truth Falsity and Mismanagement, Need for an Interdisciplinary Community-led multifunctional landscape management model in Ngorongoro, 2022

13 Kifungu cha 6 cha Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

kifugaji na shughuli mbalimbali za kimila. Asimia kubwa ni msitu , pia kuna uoto wa asili wa nyanda za juu kaskazini lenye kuchukua asilimia 20 za NCA, pia milima ipo mingi na maeneo mengineyo ni tambarare na mabonde kama mabonde 5 ya kreta.

### 4.1.3 Historia ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)

Kabla ya kuundwa kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) jamii ya kimasai ilikuwa inaishi eneo lote la Ngorongoro hadi eneo la sasa la hifadhi ya Serengeti. Kuanzia mwaka 1951 jamii ya kimasai walianza kuwa katika majadiliano na Serikali ya Ukoloni wa Mwingereza kuhusu kuachia eneo lote la sasa la Serengeti na kulifanya hifadhi ya Taifa ya Serengeti na kuacha maeneo ya Ngorongoro na Loliondo kwa ajili ya matumizi mseto ya ardhi. Mwaka 1958 Jamii ilingia makubaliano na Serikali ya Waingereza na kuhamishiwa rasmi katika eneo la Tarafa ya Ngorongoro na kujumuika na wengine walikuwa wakiishi katika maeneo haya hadi ndani ya bonde la kreta ilikuwa na makazi ya wananchi.

Ngorongoro inafahamika zaidi kwa mabonde yake kama vile Bonde la Ngorongoro, bonde la Empakai, , Bonde la Oldupai sehemu ambayo chimbuko la historia ya binadamu. NCA pia inasifika kwa kuwa na misitu minene yenye madhari mazuri yenye kupendeza.  Pia eneo la Bonde la Kreta ilitangazwa na UNESCO kuwa ni mojawapo ya maeneo ya urithi wa dunia ( World Heritage Site) kutokana na ubora wake na upekee wake na wingi wa aina za wanyama wanaishi eneo hilo.

### 4.1.4 Malengo ya Kuanzishwa kwa NCAA

Mamlaka hii ya Ngorongoro ambayo ipo katika Tarafa ya Ngorongoro, ilianzishwa na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro mwaka 1959 ikiwa na malengo makubwa matatu[14];

(a) Na Kuendeleza Jamii ya Kifugaji katika eneo hili
(b) Kusimamia shughuli za kiuhifadhi ya wanayamapori na mimea
(c) Kusimamia na kuendeleza shughuli za kitalii

Jamii ya kimasai kutokana na utamaduni wao na historia yao ya kuishi na Wanyama bila kuwa na madhara makubwa, walionekana wanafaa kuendelea kushi katika eneo hili kwa kuwa hawana madhara yoyote kwa shuguli za huifadhi. Hivo NCAA ilipewa jukumu la kisheria la kuendeleza jamii hii sambamba na shughuli zingine za utalii na uhifadhi.[15]

### 4.1.5 Malengo ya Ufuatiliaji

Malengo ya jumla ya ufuatiliaji wa hali ya haki za binadamu katika eneo la Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro  ni kutathimini na  kuweka kumbukumbu sawa kuhusu zoezi la sasa la kuwandoa watu kwa utaratibu unaoitwa wa "Kuhama kwa Hiari",  kuangalia ukiukwaji wa sheria na haki za binadamu katika zoezi hili,   kufuatilia na kuweka kumbukumbu sawa kuhusu malalamiko ya kuzuiwa kwa huduma za kijamii katika Tarafa ya Ngorongoro pamoja na kuchukua mapendekezo ya wnanachi kuhusu nini kifanyike kutatua changamoto zinazoendelea kujitokeza lakini pia maoni yao kuhusu mchakato wa kuhamisha watu awamu ya kwanza na maoni yao kuhusu awamu zinazofuata.

---

14 Kifungu cha 4 na 6 cha Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro Surac 284.

15

### 4.1.6 Matarajio ya Ufuatiliaji

a) Kuwepo kwa taarifa sahihi na zinazojitosheleza kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu uliotokea na unaoendelea kutokea wakati wa zoezi uhamishaji wa watu katika hifadhi ya Ngorongoro wanaotoka kwa hiari

b) Kuwepo kwa taarifa sahihi kuhusu changamoto za utoaji huduma za kijamii zinazoendelea kujitokeza katika maeneo yote ya Tarafa ya Ngorongoro

c) Uwepo wa taarifa ya tathmini huru kuhusu zoezi la awamu ya kwanza ya kuhamisha watu toka Ifadhi ya Ngorongoro

d) Kuwepo kwa mapendekezo ya wananchi kuhusu nini wanataka kifanyike ili kutatua hizi changamoto zinazoendelea

e) Tunategemea baada ya kupatikana kwa taarifa hii, nafasi ya mazungumzo na majadiliano baina ya asasi za kiraia, wananchi na Serikali kwa upande mwingine utapatikana ili kutafutia ufumbuzi changamoto zinazoendelea kujitokeza

f) Amani , utulivu utarejea katika eneo hili baada ya kupatikana kwa nafasi ya kukubali na kurekebisha makosa yaliyotokea na kufanya maridhiano kati ya wananchi na Serikali.

g) Tunategemea pia baada ya Taarifa hii , zoezi la kuhamisha watu kwenda Msomera utasitishwa ili kutoa nafasi ya Serikali, Asasi za Kijamii na wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro kukaa pamoja kuandaa kwanza Mpango wa Wazi wa uhamishwaji watu kwa hiari kama ilivyokuwa miaka ya 1950 pale Waingereza walipokuja na " Serengeti Settelment Scheme".

h) Hali ya utoaji wa huduma na miradi mbalimbali katika tarafa ya Ngorongoro itaimarika na kufungua milango kwa wadau wengi wa maendeleo kwenda kufanya kazi zao bila hofu yoyote.

### 4.1.7 Methodolojia

Katika ziara yetu tulifanikiwa kuwafikia watu zaidi ya 100 wakiwa ni wananchi wenyeji, viongozi wa jamii, watetezi wa haki za binadamu, wenyeviti wa vjijiji na vitongoji, Madiwani wa kata zote 11, Viongozi wa Serikali ngazi ya wilaya na viongozi wa Serikali Mkoa. Tulitumia njia zifuatazo katika kukusanya taarifa: Vikao na Viongozi wa Wilaya, Vikao na jamii, vikao na viongozi wa jamii pamoja na watetezi wa haki za binadamu. Pia kupitia njia ya usahili, mahojiano kati ya makundi lengwa, kutembelea maeneo husika, uchambuzi wa nyaraka mbalimbali, mkutanao na wananchi.

### 4.1.8 Eneo la ziara na Muda wa Ziara

Ziara hii ya ufuatiliaji ilitumia takribani siku 2 Katika Tarafa ya Ngorongoro. Ziara hii ilijikita katika eneo la Kata zote 11 na vijiji vyenye changamoto mbalimbali za huduma za jamii.

### 4.1.9 Changamoto za ziara

Changamoto kubwa katika ziara yetu ni muda ulikuwa mchache kwani watu walikuwa ni wengi sana na walitaka kufikiwa kila mmoja kwenye maeneo yao. Hali hiyo ilipelekea kushindwa kumfikia kila mwananchi. Changamoto nyingine ni kukosekana kwa ushirikiano mzuri toka kwa Ofisi ya Serikali ya Wilaya, Serikali ya Mkoa ,Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro Pamoja na Wizara ya Maliasili. Hoja zote walizopoewa kwa ajili ya ufafanuzi hadi sasa hazikujibiwa lakini pia hakukuwa na ushirikiano wowote wakati wa ziara tofauti na kama ilivyokuwa maeneo mengine.

# SURA YA 4
## SEHEMU YA PILI

# MCHAKATO WA KUONDOA WATU KATIKA HIFADHI

## 4.2 UTANGULIZI

Sura ya hii inaelezea kuhusu michakato wa kuwaondoa watu katika hifadhi ya Ngorongoro. Inaelezea chimbuko la nia ya kutaka kuwapunguza watu, hatua na mbinu zinazotumika na pia sura hii inachambua dhana ya kuhama kwa hiari kwa kufanya tathmini ya zoezi la awamu ya kwanza la watu kuhamishiwa msomera. Katika sura hii pia tutachambua changamoto za utoaji wa huduma za jamii katika tarafa hii. Pamoja na kuwasilisha hoja za Serikali na maoni ya wananchi, sura hii inawasilisha pia mapendekezo mahususi kuhusu zoezi la kupunguza watu katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro.

### 4.2.1 Chimbuko la Nia ya Kutaka kupunguza Watu katika Hifadhi

Mikatati ya kutaka kuhamisha watu katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro ni la muda mrefu. Miaka michache tu baada ya hifadhi kuanzisha, shinikizo kutoka kwa wadau mbalimbali wa uhifadhi ilitaka watu wahamishwe katika hifadhi ya Ngorongoro ili kupisha shughuli za uhifadhi pekee. Hali ilianza kuwa mbaya kwa wenyeji wa Ngorongoro mwaka 1974 ampapo sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro ilifanyiwa marekebisho na kupiga marufuku kilimo cha kujikimu pamoja na kuipa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro mamlaka makubwa ya kuzuia shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi. Mikakati hiyo ya kuhamisha watu iliridhiwa pia kwenye halmashauri kuu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali pamoja na NCAA katika miaka ya 1980.

Tangu kipindi hicho Serikali pamoja na NCAA walianza kuweka mikakati ya muda mrefu ya kutaka kuwaondoa Wamasai katika eneo la Ngorongoro. Hoja zilizotolewa kuwa chanzo cha kuondoa watu ni ongezeko la watu, ongezeko la mifugo pamoja na shughuli za kijamii. Serikali ya Tanzania na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ziliomba UNESCO kufadhili tafiti ya kisayansi itakayo halalisha uhamishwaji wa watu ndani ya hifadhi ya Ngorongoro.[16]

UNESCO iliwatuma Katherine Homewood na Allan Rodgers ambao walifanya tafiti juu ya ikolojia ya Ngorongoro na athari za Wamasai kuendelea kuishi ndani ya hifadhi kwa muda wa miaka kumi. Katikika tafiti zao walibaini kuwa uwepo wa Wamasai ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro inachangia ubora wa hifadhi hiyo. Waliongeza pia kuwa mfumo wa maisha ya wamaasai unashabihiana na uhifadhi na kuwa haujawahi kuwa tishio kwa uhifadhi.

---

16 Homewood .K. M & Rodgers, W.A Maasailand Ecology: Pastoral development and Wildlife Conservation in Ngorongoro, Tanzania, Cambridge University Press, Cambridge, 1991

Katika hitimisho wa ripoti yao ya utafiti juu ya ardhi Mseto Ngorongoro, Homewood na Rodgers walisema kuwa:

> *"Tumeona kuwa ubora wa uhifadhi wa NCA hauwezi kutenganishwa na uwepo wa wafugaji... Binadamu na wanyama wameishi kwa amani. Pili, tunasema kutoka kwenye tafiti pana juu ya biolojia ya Ngorongoro kuwa hakuna madhara yanayosababishwa na wamasai kutumia rasilimali asili..."*[17]

Homewood na Rodgers walipendekeza kwenye tafiti yao kuwa:

> *"Tunaendelea kusema kwa nguvu kuwa hakuna sababu yoyote ya kiuhifadhi au sababu nyingine ya kuondoa Maasai. Lazima kuwepo na maamuzi dhabiti ya kisiasa na ya kiutawala ambayo inadhamini Maasai kama wafugaji ndani ya NCA hapo baadae..."*

Baada ya tafiti hiyo kuchapishwa, mpango wa kuhamisha watu katika hifadhi ulikoma. Mnamo mwaka 1992 baada ya kilio cha njaa kwa wenyeji wa Ngorongoro kufuatia kukatazwa kulimo cha kujikimu, Serikali kupitia kwa aliyekuwa Waziri mkuu John Malechela iliruhusu kilimo cha kujikimu ndani ya hifadhi ili kupunguza ukali wa njaa.

Pia, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi ndani ya NCA wanapata uwakilishi ndani ya NCAA, Serikali ya awamu ya tatu chini ya Hayati Benjamin W. Mkapa iliridhia kuwepo kwa chombo kitakachokuwa sauti ya wananchi ndani ya NCAA na pia daraja kati ya wananchi wanoishi ndani ya NCA na Serikali. Chombo hicho ni Baraza la Wafugaji Ngorongoro ambayo ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali mwaka 2000.

Serikali pia iliendelea kutoa huduma mbalimbali za kijamii kama shule, afya na huduma zingine. Kilimo cha kujikimu kiliendelea katika hifadhi ya Ngorongoro hadi mwaka 2009 ilipopigwa marufuku.

Kwahiyo mikakati iliendelea kwa muda mrefu na majaribio ya kutaka kuwaondoa watu katika eneo hili. Hatua zilikuwa zinatumika ilikuwa ni pamoja na mkakati wa kufifisha huduma za jamii, kupiga marufuku shuhguli za kilimo cha kujikimu pamoja na ujenzi wa nyumba imara na za kudumu.

### 4.2.2 Hatua zinazochukuliwa Kutatua changamoto za Uhifadhi

Changamoto mbalimbali za uhifadhi zimekuwa zikianishwa katika eneo la NCA wakati mwingine hata bila kuwashirikisha wenyeji. Pamoja na kwamba taarifa mbalimbali

---

17 Homewood.K. M & Rodgers, W.A Maasailand Ecology: Pastoral development and Wildlife Conservation in Ngorongoro, Tanzania, Cambridge University Press, Cambridge, 1991. P.265.

za watu huru pamoja na Serikali zinaonyesha kuwa changamoto za huifadhi sio ungezeko la watu pekee hadi sasa Serikali imeamua kufanyia kazi eneo moja tu la swala la kupunguza idadi ya watu na mifugo. Changamoto zingine zinazotishia uhafadhi ni pamoja na ujenzi wa mahoteli katika maeneo ya NCA, ujio wa magari mengi kwa wakati mmoja pamoja na mimea na magonjwa vamizi.

Hivyo hatua iliyoanza kuchukuliwa toka mwaka 2021 hadi sasa ni ya kupunguza watu na mifugo katika eneo la NCA. Hatua hii ilianza kwa wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro kupewa barua za siku 90 kuvunja makazi yao pamoja na majengo ya Serikali yenye huduma mbalimbali mwaka 2021 na badaye kubadilishwa uamuzi huu na kuja na mpango unaoitwa "Kuhamishwa kwa Hiari" (Voluntary Relocation).

Huu ndio mpango ambao Serikali ilianza ifanyia kazi kwa kuanza kutenga maeneo na kujenga nyumba za watu kuhamia maeneo ya msomera. Zoezi hili lilianza rasmi mwaka 2022 na maeneo ambayo Serikali imepanga kuhamishia watu ni maeneo ya Msomera Tanga na Kitwai Simanjiro. Mbinu inayotumika kwa sasa ni hiyo inayoitwa uhamisho wa hiari ("Voluntary Relocation").

### 4.2.3 Changamoto ya Zoezi la Kuhama kwa Hiari

Katika ziara hii na hasa baada ya kuongea na wananchi tulibaini changamoto kadhaa katika mchakato mzima wa zoezi la wananchi kwa kile kinachoitwa kuhama kwa hiari kama ifuatavyo.

#### 4.2.3.1 Wananchi Kutokushirikishwa

Mnamo Januari 11, 2022 Serikali kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ilitangaza wito kwa wananchi kuhama kwa hiari kutoka katika tarafa ya Ngorongoro kwenda katika Kijiji cha Msomera kilichopo Handeni mkoani Tanga. Baada ya maagizo hayo ya Mkuu wa Mkoa, wananchi kwa kushirikiana na viongozi wao wa kimila na kisiasa walifanya mikutano mbalimbali ya hadhara kuhusiana na kauli hiyo ya Mkuu wa Mkoa ambayo wao walidai kwamba hawakushirikishwa.



***Picha 4.1 :*** *Wananchi wakiwa katika mkutano wa hadhara*

Mbali na mikutano ya hadhara, wananchi walifanya vikao mbalimbali wakijadili hatua za kuchukua ili kunusuru ardhi yao kuchukuliwa bila ridhaa yao pamoja na kujadili changamoto zilizokuwa zinawakabili watetezi wa ardhi Ngorongoro. Mashirika ya haki za binadamu pia yaliratibu vikao vya wananchi, watetezi wa ardhi na haki za binadamu kwa ujumla ili kujadili kwa mapana na kuandaa mapendekezo yao kabla ya utekelezwaji wa amri ya Mkuu wa Mkoa ya watu kuhama kwa hiari katika tarafa ya Ngorongoro.

Mnamo Februari 17, 2022 Waziri Mkuu alitembelea Ngorongoro na kuongea na wananchi akifafanua kuhusu zoezi la kuhama kwa hiari. Hata hivyo, wananchi wenyeji hawakupata nafasi ya kuwasilisha hoja zao kuhusiana na changamoto zilizokuwa zinawakabili. Waandishi wa habari kutoka vyombo binafsi walizuiwa kuingia katika kikao hicho na wengine kukamatwa.

Pia, tarehe 03 na 04 mwezi Aprili 2022 kikao cha wananchi wenyeji wa Ngorongoro, baadhi ya mashirika ya haki ya kifugaji ( PWC, UCRT,PINGOs FORUM) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania kilifanyika jijini Arusha kujadili na kukusanya taarifa kuhusu asili ya mgogoro, changamoto zilizokuwepo ambazo watetezi wa haki za binadamu walikuwa wanakumbana nazo katika wilaya ya Ngorongoro. Jumla ya wananchi 60 walishiriki katika kikao hicho.

Katika kikao hicho kamati ya watu 60 iliundwa na kupewa jukumu la kukusanya taarifa kuhusiana na mgogoro wa ardhi katika wilaya ya Ngorongoro pamoja na kuandaa ripoti, changamoto kubwa ya awali iliyoonekana ni kwamba wananchi na viongozi wao hawakushirikishwa kabisa na Serikali. Hali hii iliwalazimu wanakamati kukutana na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa jijini Dodoma mnamo Aprili 06, 2022 na kuomba kupewa nafasi ya kusikilizwa.

Lengo la kwenda kumwona Waziri Mkuu ilikuwa ni kumueleza kuhusiana na changamoto ya kutokushikishwa lakini pia kumweleza jitihada mbalimbali ambazo kamati hiyo pamoja na wananchi wa Ngorongoro walikuwa wanazichukua ili kuhakikisha kwamba suluhu ya kudumu ya kutatua changamoto ya usimamizi na matumizi ya ardhi mseto inapatikana katika wilaya ya Ngorongoro.

Tarehe 25 Aprili 2022, Kamati ilifanya kikao cha siku 2 ambapo wananchi pia walishiriki kupitia rasimu ya ripoti ambayo ilikuwa imeandaliwa na kamati hiyo ndogo. Baada ya kujadiliana kwa kina kuhusu taarifa zilizokuwa zimekusanywa pamoja na mapendekezo ya kamati, washiriki walitoa tamko kwenye vyombo vya habari wakiomba Serikali kusitisha mpango wake wa kuhamisha watu kutoka Ngorongoro ili kutoa nafasi ya kamati hii ya wananchi kuwasilisha mapendekezo ambayo yangetumika kuweka mikakati yenye mapendekezo ya wananchi. Kimsingi wananchi kupitia kamati hii walikuwa wapo tayari kushirikiana na Serikali kuandaa mpango wa pamoja wa kutatua hizi changamoto ambao utazingatia haki za wananchi pia.

Vilevile wananchi waliomba Serikali kusitisha zoezi la ukamataji wa watetezi wa ardhi Ngorongoro, viongozi na baadhi ya madiwani ambao walikuwa wameshaanza kukamatwa na kutishiwa kufunguliwa kesi mbalimbali, wandishi wa habari pia walikuwa wanazuiwa kuchapisha taarifa kuhusiana na kilichokuwa kinaendelea Ngorongoro na wengine walikamatwa. Katika taarifa hiyo kwa vyombo vya Habari, wananchi pia waliomba Serikali kuendelea kutoa huduma za kijamii katika tarafa ya Ngorongoro ambazo zilikuwa zimesitishwa na mwisho waliomba Serikali iwape muda wa kukamilisha taarifa yao ambayo walipanga kuiwasilisha kwa Waziri Mkuu kuhusu namna bora ya kuhifadhi eneo la hifadhi ya Ngorongoro wakati watu wanaishi.

Tarehe 25 Mei mwaka 2022 Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikutana na wajumbe wa kamati pamoja na baadhi ya wananchi kutoka Ngorongoro akiwemo Mbunge wa Jimbo hilo waliwasilisha ripoti iliyoandaliwa na kamati huku ikiwa na mapendekezo lukuki kuhusu suluhisho la mgogoro wa ardhi Ngorongoro.



***Picha 4.2:*** *Mhe. Waziri Mkuu pamoja na Wajumbe na Wananchi kutoka Ngorongoro baada ya kuwasilisha ripoti jijini Dodoma.*

Utekelezaji wa mapendekezo katika ripoti hiyo haukufanyika na hivyo kupelekea wananchi kuhamishwa na maeneo yao kuchukuliwa kuanzia Juni 07, 2022 wananchi waliona vikosi vya askari wakiwa na silaha nyingi. Vikosi hivyo vilitapakaa katika maeneo mbalimbali vikifanya ziara ya kutembelea maeneo mbalimbali kwenye eneo la mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro. Baadhi ya wananchi tuliowatembelea wakati wa ziara walisema;

*"Jamii yoyote inajengwa kwa majadiliano na maelewano, solution zote zinapatina mezani, we should look for amicable solutions"-**Mkazi wa Ngorongoro alisema***

Kwa jitahada zote hizi za kutaka kutafuta nafasi za kushirikishwa katika mchakato wa kuhamisha watu , bado wananchi wanadai hawakusilizwa kabisa na hakuna kumbukumbu yoyote inayonyesha wananchi walishirikishwa kwa kina husu zoezi hili. Hata Vyombo vvya maamuzi kama Baraza la Halmashari Wilaya halina taarifa yoyote ya zoezi hili. Swala la kutokushirikishwa katika mambo makubwa kama haya ndio msingi wa changamoto zinazoendelea kwa sasa.

#### 4.2.3.2 Kutopewa Taarifa Sahihi Kuhusu Kijiji cha Msomera

Wakati wa ziara yetu wananchi wa tarafa ya Ngorongoro walitueleza kwamba, waliahidiwa kwamba sehemu wanapohamishiwa kuna mandhari mazuri, ardhi yenye rutuba, malisho ya kutosha kwa mifugo na ambayo haimilikiwi na mtu yeyote. Pia waliambiwa eneo hilo ni pori tengefu linalomilikiwa na Serikali hivyo hakuna mtu anayeishi katika eneo hilo. Na pia eneo hilo ni zuri na linafaa kwa mashamba na malisho.

Wananchi walitueleza zaidi kuwa baada ya ndugu zao kufika katika eneo la Msomera mwaka 2022 walikuta ni ardhi ya kijiji, haina maeneo ya malisho kwakua maeneo mengi ni ya watu na yaliyobakia ni mapori yasiyokuwa na malisho. Waliendelea kutueleza kuwa kwa mujibu wa taarifa walizopewa na ndugu zao wa Msomera ni kwamba eneo la Msomera ni kame na lisilofaa kwa malisho na hata mashamba waliyopewa ni maeneo ya watu na hivyo yamepelekea mgogoro wa ardhi.

> *"Wenzetu waliohamishiwa Msomera wametueleza kwamba hali ya kule ni shida, malisho hakuna, maji hakuna ni ukame na mifugo yao imekufa kwa wingi"* ***alisema mkazi wa Ngorongoro***

#### 4.2.3.3 Usiri wa Tathmini na Kiwango Kidogo cha Fidia

Wananchi walitueleza kwamba katika mchakato wa tathmini kwaajili ya fidia ya wao kutaka kuhamishwa hawakushirikishwa kikamilifu na viongozi. Walisema kwamba viongozi wa Serikali wakiwemo katibu tarafa, muwakilishi kutoka wizara ya maliasili na utalii, muwakilishi kutoka ofisi ya mkuu wa wilaya, muwakilishi kutoka mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na muwakilishi kutoka idara ya ardhi walifika na kufanya tathmini na makadirio ya vitu ambavyo familia inavmiliki na kuondoka. Changamoto hii imefafanuliwa na kuchambuliwa vizuri katika Sura ya Tatu ya Taarifa hii.

#### 4.2.3.4 Kunyimwa Uhuru wa Kuchagua Sehemu ya Kuhamia

Wananchi wa Ngorongoro kama ilivyo kwa wale waliohamia msomera walitueleza kwamba katika mchakato wa uhamishwaji hawapewi chaguo kama wanataka kwenda Msomera au sehemu nyingine ambayo wao wangependa kuhamia. Pia walitueleza kuwa hapewi nafasi ya kuchagua kupewa fedha au kuhamia Msomera ama sehemu nyingine. Lakini wanalalamikia pia kuwa zoezi hili halina mwongozo wowote na haijulikani kinachofanyika kinafanyika kwa utaratibu upi. Hivyo, mchakato mzima haukuzingatia maoni yao.

Wamehoji kuwa kama mchakato ni hiari kwanini wapanngiwe pa kwenda. Wananchi wa Ngorongoro wanatambua kuwa kuhama kwa hiari ni pamoja na mtu kuchagua pa kuhamia na pia kuwa na nafasi ya kujadiliana kiwango cha fidia. Kutokana na uhalisia wa Maisha ya wananchi wa Ngorongoro, ziara hii ibebaini kuwa swala hili la kutokuwepo kwa uwazi na utaratibu mzuri wa kutoa fidia inayostahili imechangia pia watu wengi kutokuwa na hari ya kuhama kwa hiari.

Mchakato huu unaendeshwa kwa usiri mkubwa na bila mwongozo wowote (No Voluntary-relocation plan) na kupelekea wananchi kuogopa kuwa wahanga kama wenzao waliokwisha tangulia. Lakini pia taarifa hii imebaini kutokana na usiri mkubwa katika zoezi hili mazingiria ya rushwa na matumizi mabaya ya rasilimali kuwemo ni mkubwa sana.

### 4.2.3.5 Kufifishwa kwa Huduma za Msingi za Jamii

Wananchi walitueleza kwamba moja ya changamoto kubwa wakati wa zoezi la kuhama kwa hiari ni kunyimwa huduma za kijamii kwa wananchi ili kuwalazimisha kuhamia katika kijiji cha Msomera au kwingineko. Huduma mbabalimbali za jamii kama vile huduma za mabweni kwa shule za msingi na secondari, huduma za vyoo mashuleni, huduma za afya , huduma za barabara, huduma za maji nk.


### (a) Njia Zinazotumika Kuzorotesha Huduma Za Jamii

Huduma hizi zimezorotoshwa kwa kuzuia ujengaji wa shule mpya, madarasa mapya, zahanati na vituo vya afya vipya, pia visima vya maji na matundu ya choo. Pia ukarabati wa majengo ya huduma hizi za msingi kwa jamii umesitishwa. Njia ingine inayotumika ni kuhamisha fedha za miradi ya maendeleo toka TAMISEMI kama vile miradi ya Burst na miradi toka wadau mbalimbali wa maendeleo.

Kwa mfano mwaka 2022 jumla ya shilingi 195,500,000 zilihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga. Tarafa ya Ngorongoro ina huduma kadhaa za kijamii japokuwa hazikidhi mahitaji ya wananchi. Kuna jumla ya shule za msingi 25 na shule za sekondari 3, hospitali 1 ya Endulen na vituo vya afya vitatu (3).

### (i) Huduma za Elimu

Kwa mfano kiasi cha shilingi za kitanzania, 355,500,000 cha fedha za mradi wa uviko-19 (Covid-19 relief funds) zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro zilihamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni bila kuazimiwa na baraza la madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Fedha hizo zilihamishwa kwa barua mbili zenye Kumb. No.NGOR/DC/F.1/02/VOLIII/68 na Kumb. No.NGOR/DC/F.1/02/VOLIII/69 za tarehe 31/03/2022.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. NGOR/DC/F.1/ 02/VOLIII/ 69

Tarehe: 31/03/2022

Wakuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Embaraway
Shule ya Sekondari Nainokanoka
Shule ya Sekondari ya Wasichana Ngorongoro
Halmashauri (W) Ngorongoro,
S. L. P 1,
**LOLIONDO - NGORONGORO**

**YAH: KUHAMISHA FEDHA ZA MIRADI YA UVIKO 19 JUMLA YA SHS. 195,500,000/- KWENDA HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu

Nimepokea barua kutoka kwa katibu Mkuu TAMISEMI yenye kumbu Na BD.291/298/03/281 ya Tarehe 14/3/2022 inayohusu mada tajwa hapo juu kuhusu fedha za Miradi ya UVIKO 19 zilizoingizwa katika Akaunti zenu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kuwa Fedha hizo zihamishiwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Hivyo kwa Barua hii Nawaelekeza kuhamisha fedha hizo kwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni katika Akaunti ya – Handeni District Council Miscellaneous Deposit Na 41410000535 benki ya NMB. Kazi hiyo ifanyike kabla ya Tarehe 05/04/2022 bila kukosa. Mchanganuo wa fedha hizo baada ya kutoa matumizi ya madawati ni kama ifuatavyo:-

1. Shule ya Sekondari Nainokanoka — Shs. 80,000,000/-
2. Shule ya Sekondari Embaraway — Shs. 66,000,000/-
3. Shule ya Sekondari ya Wasichana Ngorongoro — Shs. 49,500,000/-

Nawatakia Utekelezaji Mwema.

Dr Jumaa Mhina
**Mkurugenzi Mtendaji (W)**
**NGORONGORO**

Jengo la Utawala; S.L.P 1 Loliondo; Arusha; Simu +255272535051 ; Nukushi +255272535051/2535264
Baruapepe:ded@ngorongorodc.go.tz Tovuti: www.ngorongorodc.go.tz

***Picha 4.3:*** *Barua ya Mkurugenzi Ngorongoro Ikielekeza Million 190 za Tarafa ya Ngorongoro kwenda Wilaya Handeni*

Fedha hizo katika picha namba 4.4 zilikuwa kwaajili ya kujenga madarasa na mabweni ya wanafunzi katika shule tatu za Serikali ambazo ni Nainokanoka, Embarway na shule ya Wasichana ya Ngorongoro pamoja na shule za msingi Endulen, Misigiyo na Esere. Baada kwa barua ya Mkurugenzi wa Halmashauri zilihamishwa kwenda Wilayani Handeni Tanga.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES
DESIGN DISTRICT COUNCIL
(All letters should be sent to Executive Director)

31/03/2022

When responding please refer
Ref. No. NGOR/DC/F.1/02/VOLIII/69

Head Masters,
Embarway Secondary School
Nainokanoka Secondary School
Ngorongoro girsl secondary school
Ngorongoro District Council,
P.O.BOX 1
LOLIONDO-NGORONGORO

REF: TRANSFER OF COVID-19 PROJECT FUNDS TSHS. 195,500,000 TO HANDENI DISTRICT COUNCIL

Please refer to the headline above
I have received a letter from the Secretary General PMO-RALG with reference No. BD.291/298/03/281 dated 14/03/2022 regarding the above-mentioned subject regarding COVID-19 project Fund deposited in your accounts for the construction of classrooms and boarding hostel that the money should be transferred to Handeni District Council.

Therefore, with this Letter I direct you to transfer the funds to Handeni District Council via Handeni District Council Account Miscellaneous Deposit account No. 41410000535 NMB bank. This should be executed before 05/04/2022 without fail.

The breakdown of such funds transfer after deducting the expenses for desk is as follows

| | |
|---|---|
| 1. Nainokanoka Secondary School | Tsh 80,000,000 |
| 2. Embarway Secondary School School | Tsh 66,000,000 |
| 3. Ngorongoro girls Secondary School | TSH 49,500,000 |

I wish you all the best in execution

Dr Jumaa Mhina
District Executive Director
Ngorongoro

***Picha 4.4:*** *Barua za kuhamisha fedha za miradi ya uviko 19 kutoka Ngorongoro kwenda Msomera*

Hizi ni baadhi tu za barua nyingi ambazo zimeandikwa kuhamisha fedha za miradi ya maendeleo na huduma za msingi kwa wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro. Fedha zote za Tarafa ya Ngorngoro kwa sasa haziendi tena katika taarafa hii. Zingine zimekuwa zikihamishia katika matumizi ya miradi katika tarafa ya Loliondo na Sale. Hivyo wanafunzi katika shule zote Ngorongoro kwa sasa  hawana madarasa, mabweni pamoja vyoo hali inayoweza kupelekea madhara ya kiafya kwa wanafunzi na magonjwa ya mlipuko kwani imewalazimu wanafunzi kulala wawili kwenye kitanda kimoja kutokana na upungufu wa mabweni.



***Picha 4.5:*** *Shule ya Msingi ya Bweni Endulen ambayo kwa sasa haina vyoo na watoto takriban 700 wanalala hadi wanne kwa kitanda katika mabweni mawili pekee. Kila bweni lina uwezo wa kubeba watoto 40 pekee*

Kwa ujumla hali ya huduma ya elimu katika Tarafa ya Ngorongoro imezorota sana kupelekea Watoto wengi wa jamii hii ya Kimaasai kushindwa kupata haki yao ya kielimu kinyume na misingi ya sheria ilyoanzisha mamlaka ya Ngorongoro, kinyume na katiba ya nchi pamoja na misingi ya haki za binadamu. Kata na vijiji vingi vilivyotembelewa vinachangamoto ya kukosa ujenzi mpya huduma ya elimu, kukosekana kwa fedha za ukarabati wa majengo ya shule , kukosekana kwa vibali vya kumalizia majengo yaliyokuwa yanaendelea kujengwa, wanafunzi kukosa huduma za vyoo n.k. Changamoto hizi zinaelezewa kwa muhtasari tu katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.1 : Changamoto za Huduma za Elimu Tarafa ya Ngorongoro**

| Na | Kata | Mabweni yanayohitajika | Vyoo vinavyohitajika | Madarasa yanayohitajika | Ofisi/Nyumba za walimu zinazohitajika |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Enduleni | 4 | 42 | 10 | 8 |
| 2. | Ngorongoro | | 25 | 6 | 5 |
| 3. | Alaitole | | 4 | 4 | 6 |
| 4. | Misigiyo | | 16 | | |
| 5. | Nainokanoka | 4 | 20 | 3 | 3 |
| 6. | Olbalbal | | 15 | | |
| 7. | Kakesio | | 16 | 4 | 2 |
| 8. | Alailelai | 2 | 24 | 1 | 3 |
| 9. | Naiyobi | | 10 | | 2 |
| 10. | Eyasi | 2 | 20 | 2 | 2 |
| 11. | Ngoile | | 4 | 3 | 3 |
| | **Jumla** | **12** | **194** | **33** | **33** |

### ii) Huduma za Afya

Huduma za afya zimezorota sana katika tarafa ya Ngorongoro. Kwa mujibu wa ziara hii Tarafa ya Ngorongoro ina kituo cha afya kimoja, zahanati Nane, Hospitali Moja ya Enduleni inayosimamiwa na Kanisa Katoliki. Huduma hizi zinahudumia Tarafa nzima yenye kata 11 na vijiji 25 na takriban watu 110,000. Pia kulikuwa na huduma ya dharua pamoja na chanjo kupitia mradi wa Flying Medical Service ulioko chini ya Kanisa Katoliki ambayo initoa huduma za chanjo na huduma za dharura katika sehemu za pembezoni ikiwemo Ngorongoro.

Flying Medical Servive ilizuiliwa kuanya shughuli zake na kupelekea watu wengi sana kuadhirika. Huduma zote hizi zimezorota kwa njia mbambali zikiwemo kukosa ukarabati, kukosa majengo mapya , kuzuiwa kwa ndege kuruka, kuondolewa kwa fedha za miradi, kunyimwa vibali vya ujenzi,ukarabati na kunyimwa kuwa na makazi ya kisasa.

Mnamo 08/04/2022 Serikali ilisitisha huduma ya afya ya dharura iliyokuwa inatolewa na Flying Medical Service. Flying Medical Service ilikuwa inatoa huduma mbalimbali za afya kama vile huduma ya chanjo kwa watoto, huduma ya kliniki kwa wajawazito, wagonjwa wa kifua kikuu, na magonjwa ya dharura. Huduma hiyo ilikuwa inatolewa hasa katika maeneo ambayo hayafikiki kwa usafiri wa kawaida. Kati ya mwaka 1985 hadi mwaka 2021 Flying Medical Service iliwafikia jumla ya wagonjwa 765,947 ambapo watoto pekee ni 138, 036.

**Jedwali 4.2: Changamoto Huduma za Afya kwa baadhi ya kata za Tarafa ya Ngorongoro**

| Na | Kata | Changamoto-Zahanati | Changamoto-Kituo cha Afya | Changamoto ya Hosptali |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Enduleni | Kunyimwa vibali vya ukarabati na ujenzi mpya | Kunyimwa vibali vya ukarabati na ujenzi mpya | a. Uhaba waa Watumishi<br>b. NCAA wameon-doa huduma yad awa (300 milioni)<br>c. Kunyimwa ruhu-sa ya kukarabati majengo |
| 2. | Ngorongoro | Kunyimwa vibali vya ukarabati na ujenzi mpya | | |
| 3. | Alaitole | Ukarabati wa zah-anati unahitajika- | | |
| 4. | Misigiyo | kunyimwa kiba-li ya kujenga uzio (fence) msaada ku-toka crater lodge. | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5. | Kakesio | Kunyimwa vibali vya ukarabati na ujenzi mpya | Kituo cha afya kimesimama | |
| 6. | Alailelai | zahanati haina jen-go la wazazi | | |
| 7. | Naiyobi | Kunyimwa vibali vya ukarabati na ujenzi mpya | | |
| 8. | Ngoile | Jengo la zahanati ya Ngoile limesh-indwa kukamilika kwa sababu ya vibali kutoka NCAA | | |

**iii) Maji**

Tulipotembelea katika tarafa ya Ngorongoro wanachi walitueleza kuwa huduma maji zimezorota haswa kwenyekata zote za Ngorongoro. Wananchi walitueleza pia kuwa, hata kwenye kata ya Ngorongoro, Misigiyo na Nainokanoka ambazo zilikuwa zikipata huduma za maji baada ya kuzuiliwa kupeleka mifugo yao ndani ya kreta kwa ajili ya maji na chumvi,sasa wanadai kukatiwa huduma ya maji na NCAA.

kwa mujibu wa wananchi ni kuwa mnamo 2016, walikatazwa kupeleka mifugo yao ndani ya Kreta kwa ajili ya Maji, chumvi na malisho kwa ahadi kuwa watapelekewa maji na chumvi katika vijiji vyao. Maji hayo hata hivyo, inadaiwa kukaziuwa na NCAA baada ya mgogoro wa uhamisho wa watu kuzuka. Na hata hivyo chumvi ambayo wanachi waliahidiwa kusambaziwa baada ya kuzuiliwa kufuata ndani ya kreta ilikuja kudhihitishwa na maabara kuwa zina sumu na hivyo sio salama kwa kuwapa mifugo.

**iv) Barababara**

Katika ziara hii katika tarafa ya Ngorongoro wananchi walilamika kuwa kumekuwa na changamoto ya barabara. Kwa maelezo ya wananchi ni kwamba wakati barabara zinazoendana kwa wananchi na kuunganisha vijiji vikiwa na changamoto na wakati mwingine kutopitika kabisa na barabara zinazoenda katika maeneo ya wawekezaji kama mahoteli,loji na kambi za kitalii zinawekewa miundombinu nzuri. Kwa mfano, bararabara za kwenda maeneo ya Ndutu ambako kuna loji na kambi za kitalii ikiwa na miundombinu nzuri, barabara za kupeleka huduma kwa wananchi ni mbaya sana na wakati mwingine hazipitiki.

### 4.2.3.6 Kunyimwa Vibali vya Ujenzi

Wananchi walitueleza kuwa wakati wa zoezi la kuhama kwa hiari, mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ilisitisha vibali vya kufanya ujenzi au ukarabati wa aina yoyote kwa kwa nyumba za wananchi na taasisi zinazotoa huduma za jamii. Kwa mfano ukarabati

wa hospital, shule za msingi, nyumba za watumishi n.k. Kwa mfano shule ya msingi Endulen vyoo vimejaa na imewalazimu wanafunzi kujisaidia nje au porini.

Katika shule ya Enduleni, pia wanafunzi wanalala 4 kwenye kitanda kimoja kutokana na ujenzi wa mabweni uliokuwa unaendelea kusitishwa. Shule hii ina jumla ya wanafunzi 1,900 (wakike 785 na wa kiume 1054) ina mabweni mawili tu. Kati ya hao wanafunzi 617 wanaishi bweni (wakike 272 na wa kiume ni 345) na kuna mabweni mawili tu.

***Picha .4.5:*** *Choo ambacho hakijakarabatiwa kwasababu ya kukosa kibali S/M Endulen*



Hospitali ya Enduleni pia imeshindwa kufanya ukarabati wa nyumba zinazotumika kutoa huduma kwa wananchi kwa kukosa vibali. Swala la vibali inatumika kama silaha kubwa kuhakikisha hakuna kinachoendelea tena katika Tarafa ya Ngorongoro. Majengo ya serikai pia kama ofisi za kata zimeshindwa kufanya ukarabati wowote. Mfano shule na ofisi ya Mtendaji wa Kijiji cha Mokilal zilipata changamoto ya kuezuliwa paa na mvua na hadi tunapoandika taarifa hii ofisi hiyo haijaezekwa.



***Picha 4.6:*** *Ofisi ya kijiji cha Mokla iliyoezuliwa na upepo na hadi sasa haijakarabitwa*

### 4.2.3.7 Ng'ombe Kupewa Chumvi Yenye Sumu na Hatimae Kufa

Wakati wa ziara yetu wananchi walitueleza ya kwamba kabla ya mwaka 2016 wafugaji wa kata zilizopo karibu na bonde la kreta la Ngorongoro walikuwa wanalisha mifugo yao kwenye bonde la kreta kwani eneo lenye malisho, maji na chumvi ya mifugo. Mwaka 2016 Serikali kupitia kwa Mhe.Waziri Mkuu ilizuia wafugaji kuingiza mifugo katika bonde la kreta na Waziri Mkuu aliamuru kwamba Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro iwe inaleta chumvi mbadala, kuweka na kuboresha huduma ya maji katika maeneo hayo ambayo ni; Kata ya Ngorongoro, Kata ya Misigiyo na Kata ya Nainokanoka.

Mamlaka ilifanya hivyo lakini mwaka 2021 wananchi waligundua kwamba chumvi iliyokuwa inaletwa ilikuwa na sumu  na hili lilithibitishwa na vipimo vya maabara ikiwemo maabara ya taifa ya mifugo ambapo tarehe 27/12/2021 sampuli ya chumvi katika vijiji vya, Kayapus, Mokilal, Erkeepus na Misigiyo ilipelekwa maabara ya taifa ya mifugo na kufanyiwa uchunguzi tarehe 27/12/2021 na majibu ya kiuchunguzi yalibaini chumvi hiyo kuwa na sumu. Baada ya janga hilo kutokea mifugo mingi ilikufa hali iliyopelekea umasikini kwa wananchi, na hadi sasa hakuna hatua zozote za kisheria au kiutawala zilizochukuliwa dhidi ya mamlaka na hakuna fidia iliyotolewa kwa wananchi. Haya yote tunadhani yalifanyika ili kushinikiza wananchi kuhama katika tarafa ya Ngorongoro.

***Picha 4.7:*** *Mabaki ya ng'ombe waliokufa kutokana na kupewa chumvi yenye sumu*




#### 4.2.3. 8 Baadhi ya Kata na Vijiji Kukosa Uwakilishi wa Viongozi

Katika ziara yetu wananchi walitueleza kwamba wakati wa zoezi la kuhama kwa hiari madiwani wawili (Kata ya Eyasi na Kakesio) wamehamia Msomera. Hii ni sambamba na mwenyekiti wa Kijiji cha Olpiro naye amehama. Mpaka sasa hakuna uchaguzi uliofanyika na madiwani hao wamekuwa wakihudhuria vikao vya halmashauri ilihali wao sio wakazi wa tarafa ya Ngorongoro. Hii inaleta changamoto katika uwakilishi kwenye baraza kwani madiwani hawa kwasasa hawajui changamoto za wakazi wa Eyasi na Kakesio.

#### 4.2.3.9 Wenyeji wa Ngorongoro kunyimwa Ajira

Wakati wa ziara yetu katika tarafa ya Ngorongoro, wenyeji walitueleza kwamba katika mahoteli na maeneo mengine ya ajira ndani ya tarafa ya Ngorongoro wenyeji hawapewi kipaumbele kutokana na propaganda zilizoenezwa kuwa wenyeji wakipewa ajira wataenda kufuga ng'ombe ndani ya eneo la hifadhi ya mamlaka ya Ngorongoro.

Hii pia inadhibitishwa na barua inayotoka NCAA yenya kumb.No. DE 70/341/04/40 kwenda kwenye maloji, kambi za kitalii na mahoteli ambayo imetoa maelekezo ya kuhamishwa kwa watumishi wenyeji wanaofanya kazi katika maeneo hayo tajwa na kupelekwa katika sehemu zingine.



MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO

**Kumb. Na.** BE 76/341/04/40 **Tarehe:** 24/09/2019

Kambi/Hoteli/Lodge

**Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

YAH: **MAELEKEZO JUU YA ULINZI WA KAMBI, HOTELI NA LODGES**

Kutokana na wimbi kubwa la wizi uliokwishafanyika katika maeneo mbalimbali yanayotumika kulaza wageni, Serikali kupitia maagizo ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha ilichukua hatua za kuunda kamati maalumu ya kupitia na kukagua **Hotel** zote na **Camps** zilizoko ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kuanzia tarehe 21/8/2019 mpaka tarehe 24/8/2019.

Katika kutekeleza hilo Kamati ya ulinzi na usalama Wilaya ya Ngorongoro ilipita ili kuhakiki usalama wa maeneo na kuangalia mapungufu yaliyopo ili yarekebishwe kwa haraka.

Kamati hiyo ilipita katika maeneo yako na kubaini mapungufu kadhaa

**Kwa barua hii unaagizwa kutekeleza yafuatayo kabla ya tarehe 31 Mwezi Desemba, 2019.**

1. Kufunga CCTV camera katika maeneo ya nje kuzunguka kambi ,
   **(NB:** kamera hizo zifichwe na ziaiwekwe ndani ya vyumba)
2. Kuwe na Radio call kwa ajili ya mawasiliano kambini.
3. Kila chumba cha mgeni kiwe na mawasiliano ya dharura inapotokea tukio lolote kama ifuatavyo:
   i. Filimbi
   ii. Horn/air blows
   iii. Tochi
   iv. Radio call
   v. Simu
4. Unatakiwa kutengeneza geti la kuingilia kambini na kutoka, gari zote ziandikishwe na kujulikana ni za nani.
5. Unatakiwa kuwa na walinzi waliopitia mafunzo ya kijeshi au ulinzi mfano JKT/MGAMBO/PANSIASI NA MWEKA.

**Barua zote zielekezwe kwa Mhifadhi wa Ngorongoro**

6. Walinzi wote wapewe mikataba ya ajira na kulipwa inayopewa kisheria kwa kufuata kima cha chini cha serikali au zaidi.
7. Walinzi wako unaowatumia utawaleta ofisi ya meneja ulinzi/intelijensia ili waweze kufanyiwa ukaguzi (VETTING) kama wanavyo vigezo vya kufanya ulinzi kabla hujawatumia.
8. Unatakiwa kuwa na mawasiliano yote ya wafanyakazi wako wote pamoja na IMEI za namba za simu zao zote.
9. Unapokuwa na wageni wengi omba kupatiwa Askari Polisi au Askari kutoka NCAA
10. Unaagizwa kuwahamisha walinzi wenyeji wa Ngorongoro na kuwapeleka maeneo mengine ili ulete walinzi wasio wenyeji. Agizo hili lifanyike kazi bila kuathiri ajira za walinzi wenyeji waliopo sasa.
11. Uwe na walinzi wa kutosha kulingana na ukubwa wa kambi ,pia waaipangiwe kazi nyingine kiasi cha kuathiri utendaji wao.
12. Unatakiwa kuwa na sanduku la kutunzia vifaa vya wageni (safebox) kila chumba cha kulaza wageni au kuwa na sanduku kubwa moja ambalo vitu vya thamani vitahifadhiwa na kulindwa.
13. Hotel kubwa kama SOPA unatakiwa kuwa na ASKARI wa NCAA AU POLISI muda wote ili kuimarisha ulinzi.
14. Walinzi wako hawaruhusiwi kutumia upinde na silaha zingine za jadi kama mikuki na sime wanazoweza kutumia.
15. Unatakiwa kuwashonea sare walinzi wako zinazowatofautisha na wafanyakazi wa kawaida.
16. Unatakiwa kuwa na wafanyakazi maalumu wa kubeba mizigo ya wageni badala ya mizigo kubebwa na kila mtu.
17. Mtu mwingine au yeyote asiyehusika asiingie eneo la kambi au Hotel/lodges

Maagizo haya yanatakiwa kutekelezwa mara moja na ukaguzi utafanyika mara kwa mara kuona kama yametekelezwa.

***Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kama ulapuuzia kutekeleza.***

**SAHIHI YA MENEJA IDARA YA ULINZI NCAA**

**SAHIHI YA AFISA TARAFA NGORONGORO**

***Picha 4.8:*** *Barua kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuelekeza watumishi wenyeji kuhamishwa*

Ni muhimu kukumbuka ajira ni haki kwa kila mtu ambaye ana uwezo wa kufanya kazi hivyo wenyeji haw wa Ngorongoro wanaitaka Serikali na wenye mahoteli, NCAA, kambi za kitalii na loji kuepuka kufanya ubaguzi katika suala zima la ajira. Kabila au sehemu ambapo mtu anatoka isiwe sababu/kigezo ya kunyimwa ajira kwa kuwa ni kinyume na Katiba.

#### 4.2.3.10 Madai ya Unyanyapaa na Ubaguzi kwa Watumishi Wenyeji/Wamasai

Katika ziara yetu katika tarafa ya Ngorongoro, walitueleza kuwa kumekuwa na vitendo vinavyoashiria ubaguzi dhidi ya watumishi wenyeji wanaofanyanya kazi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro,walitueleza zaidi kuwa watumishi wenyeji ndani ya NCAA wamekuwa wakipewa dodoso za kueleza mali wanazomiliki na burua hizo inalenga watumishi wenyeji pekee na sio watumishi wote ndani ya NCAA.

Pia NCAA imekuwa ikitoa tangazo la kuitwa kwa watumishi wenyeji ndani ya NCAA kuhudhuria kikaoni ambapo waliambiwa wachague kati ya kuhama ndani ya hifadhi au kupoteza ajira.kwa maana nyingine ajira ya watumishi wenyeji ndani ya NCAA imekuwa ikitumiwa kama silaha ya kushinikiza wakazi wa Ngorongoro wanaofanya kazi ndani ya NCAA kuhama ndani ya hifadhi.

**DOKEZO SABILI**

**Kwenda:** Makamsihna Wasaidizi Waandamizi,
**Idara/Vitengo.**

**Kutoka:** Kaimu Kamishna Msaidizi Mwandamizi,
**Rasilimali Watu na Utawala.**

**Tarehe:** 27 Aprili, 2022.

Yah: **FOMU MAALUM KWA WATUMISHI WENYEJI/WAZAWA WANAOISHI NDANI YA ENEO LA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Mnajulishwa kuwa mnatakiwa kuwajulisha watumishi walio chini ya Idara zenu kujaza fomu maalum kwa watumishi wazawa/wenyeji wanaoishi ndani ya eneo la Mamalaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Katika fomu hiyoi mtumishi atapaswa kujaza taarifa zake zinazohusu umiliki wa mifugo na makazi. Fomu hii ijazwe na kuwasilishwa ofisi ya MHRA ifikapo ya tarehe 29/4/2022 siku ya Ijumaa

3. Pamoja na dokezo hili nimeambatanisha fomu husika kwa ajili ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa.

4. Naomba kuwasilisha kwa hatua zenu.

S. O. Chisonga
Ag. **SACC-HRA**

***Picha 4.9:*** *Dekezo kuhusu kuhakiki mali za Watumishi Wazawa (Wamasai) kwa lengo la Kujua Mali zao kwa ajili ya hatua zaidi hasa kushinikizwa kuhama*

Ni muhimu kuzingatia kwamba kitendo chochote kinachoashiria ubaguzi katika sehemu za kazi na pia inayolenga asili ya mtu ni kinyume cha Katiba, sheria za kazi na mikataba mbalimbali za kimataifa ambazo Tanzania imesaini na kuridhia.

**MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO**

**FOMU MAALUM KWA MTUMISHI MWENYEJI/MZAWA ANAYEISHI NDANI YA ENEO LA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO.**

Fomu hii inakutaka mtumishi/mwajiriwa wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro mwenye makazi ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kutoa taarifa zako sahihi kuhusu umiliki wa mifugo na makazi. Taarifa zako zitasaidia serikali katika kutolea maamzi dhidi ya kukabiliana na changamoto zinayohusu ongezeko la watu, mifugo na ujenzi holela ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

**A. TAARIFA BINAFSI ZA MTUMISHI:**

1. JINA KAMILI.........................................................................
2. KITONGOJI UNACHOISHI...........................................................
3. KIJIJI UNACHOISHI....................................................................
4. KATA UNAYOISHI.......................................................................
5. NAMBA ZA SIMU .......................................................................

**B. TAARIFA ZA MAKAZI NA MIFUNGO UNAYOMILIKI NDANI YA ENEO LA HIFADHI YA NGORONGORO:**

| IDADI YA NYUMBA | | | IDADI YA MIFUGO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| NYUMBA ZA ASILI | NYUMBA ZILIZOJENGWA KWA MITI NA BATI. | NYUMBA ZA KUDUMU | NG'OMBE | MBUZI | KONDOO | PUNDA |
| | | | | | | |

SAHIHI.......................................................

TAREHE.......................................................

***Picha 4.10:*** *Formu Maalum kwa Watumishi wa Kimasai katika Mamlaka ya Ngorongoro*

### 4.2.3.11 Gharama ya kupaki gari (Parking fee) kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro

Wakazi wa tarafa ya Ngorongoro wanakumbana na changamoto ya kulipia gharama ya kupaki gari ndani ya makazi yao. Mtu yeyote anayemiliki gari na ni mkazi wa tarafa ya Ngorongoro anatakiwa kulipa kiasi cha Tshs. 118,000 kwa gari binafsi na Tshs 300,000 kwa gari ya biashara kwa mwaka. Mbali na gharama ya kupaki gari, ikifika 05:30 Jioni kama mtu hajaingia getini haruhusiwi kuingia hata kama mtu huyo ni mkazi wa Ngorongoro.

Sisi kama Watetezi wa Haki za Binadamu tunadhani ni muhimu kwa Serikali kutowalipisha gharama ya kupaki gari kwa wakazi wa Ngorongoro kwa sababu ni kuwaongezea mzigo na ugumu wa maisha na pia kinyume na sheira ya NCA pamoja na katiba ya Tanzania. Kama ambavyo magari ya NCAA na Serikali hawalipi chochote wakiwa ndani ya hifadhi hiyo hivyo kwa wanyeji wa tarafa ya Ngorongoro wanapaswa kutolipishwa gharama yoyote ya kupaki magari yao

### 4.2.3.12 Kudhoofishwa kwa Shughuli za Baraza la Wafugaji

Baraza la wafugaji ni chombo iliyo anzishwa kwa Tangazo la Serikali la mwaka, 2000 kwa lengo la kusimamia maslahi ya wenyeji ndani ya NCAA.Kwa sasa shughuli za Baraza la Wafugaji zimedhofika na kusimama kabisa baada ya Baraza kunyang'anywa fedha za uendeshaji na pia baada ya miradi yote ya Baraza kuhamishiwa Halmashauri chini ya usimamizi wa Afisa Maendeleo ya Jamii.

Toka Baraza la Wafugaji kunyang'anywa miradi yake, watumishi wa Baraza ambao hawajalipwa mishahara yao hadi leo. Ni muhimu pia kuzingatia kuwa Baraza la Wafugaji ilikuwa chombo cha muhimu kwa wakazi wa Ngorongoro na imedhoofishwa bila kufuata kufuata taratibu.

### 4.2.4 Mahitaji ya Wananchi Kuhusu Zoezi la Kuondolewa Wananchi Ngorongoro

a) Zoezi la uhamishwaji wa watu kutoka tarafa ya Ngorongoro lisitishwe kwani licha ya zoezi hilo kughubikwa na ukiakwaji wa haki za biandamu lakini pia zoezi hilo /linakinzana na sheria mama ambayo imeanzisha Mmalaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inayotambua malengo makuu matatu ikiwemo uenelezaji wa masilahi ya wakazi wenyeji. Zoezi la kuhama kwa hiari liendelee baada ya jamii kukaa na Serikali na kutengeneza mpango wa pamoja ( Joint-Voluntary Relocation Plan) wa kuruhsu watu kuhama kwa hiari tofauti na ilivyo sasa ambapo nguvu nyingi inatumika kulazimisha watu kuhama.

b) Serikali ifanye tathmini ya changamoto zilizojitokeza wakati wa uhamishwaji wa wananchi katika awamu zilizopita na kurudi kukaa na jamii kuona namna bora ya kuendesha zoezi hili.

c) Kwamba kuhama kwa hiari isiwe njia ya kuwaumiza wenyeji wa Ngorongoro wanaoendelea kubaki kudhihakiwa,

d) kukemea kudhalilishwa na kubaguliwa kwa wananchi wa Ngorongoro kwa kupitia vyombo vya habari na baadhi ya viongozi wa Serikali kwa namna inayolenga tamaduni na asili ya mtu.

e) kuwa na mjadala kati ya wananchi na Serikali juu ya namna ya kuwa na Ngorongoro bora inayo zingatia maslahi ya watu na maslahi ya uhifadhi.
f) kwamba uhusiano kati ya NCAA,Serikali na wananchi wa Ngorongoro imekuwa mbaya kuliko kipindi chochote kile hivyo wananchi wanaona meza ya mazungumzo italeta suluhisho.
g) Serikali itekeleze huduma za kijamii ndani ya tarafa ya Ngorongoro kama ilivyo katika sehemu nyingine za Tanzania. Kwamba tangu kuanza kwa mgogoro, miradi za maendeleo na huduma za kijamii zimesimama.

#### 4.2.5 Ufafanuzi wa Serikali Kuhusu Changamoto za zoezi la Kuhama kwa Hiari

Kama sehemu ya kupata taarifa kuhusu zoezi la kuhamisha watu ndani ya hifadhi ya Ngorongoro, timu ya watetezi wa haki za Binadamu ilituma barua kwa viongozi wa wilaya, uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Uongozi wa Mkoa, Wizara ya Maliasili na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kupata taarifa kutoka kwao,licha ya kutuma barua lakini mpaka tunaadika ripoti hii hatukupata taatifa yoyote ya ufafanuzi toka kwa Serikali wala kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Hata hivyo, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngororongoro pamoja na Serikali zimekuwa zikisisitiza kuwa zoezi la uhamisho wa watu kutoka Ngorongoro kwenda Msomera au kwinginiko ni hiari na linakwenda vizuri. Hoja ambazo Serikali inasema kuwa ndio chanzo cha uhamishaji wa wananchi ni, uwingi wa watu,uwingi wa mifugo na makazi holela.

Hakuna sehemu yoyote Serikali ilieleza kuwa uwingi wa magari ya kitalii,ujenzi wa mahoteli, kambi na loji kama pia zina athari kwa uhiadhi. Hoja kubwa za Serikali ni kuwa wenyeji ndio wanachangia kuharibu hifadhi ya Ngorongoro. Serikali pia haijaeleza hatima ya wananchi ambao hawataki kuhama maeneo yao ndani ya hifadhi ya Ngorongoro. Kwa ujumla imekuwa ngumu kupata ufafanuzi wa serikali kuhusu changamoto zinazotoakana na zoezi hili la kuhama kwa hiari. Sehemu hii ya taarifa hii ilitengwa mahususi kwa ajili ya kutoa nafasi kwa serikali kutoa ufafanuzi wa hoja zinazohusu changamoto za uhamaji kwa hiari.

Serikali pia haijawekeka wazi sababu za kuzuia huduma za kijamii kwa wananchi wanaoishi ndani ya tarafa ya Ngorongoro tangu 2021. Jambo hili la kuzuia miradi ya maendeleo na huduma za kijamii ndani ya hikadhi ya Ngorongoro linaleta wasiwasi kama kweli uhamishwaji wa wananchi ni hiari. Mara kadhaa serikali wamekuwa wakitoa kauli kwa vyombo vya Habari na bungeni kuwa hakuna huduma za jamii zilizozuiliwa katika katarafa ya Ngorongoro.

Serikali iliwahi kutoa ufafanuzi kwamba shughuli ya kuwahamisha wananchi kutoka Hifadhi ya Ngorongoro mkoani Arusha kwenda kijiji cha Msomera wilayani Handeni Mkoa wa Tanga ilifuata taratibu na kulinda haki za binadamu. Ufafanuzi huo ulitolewa baada ya baadhi ya asasi za kiraia kusema haki za binadamu hazikuzingatiwa katika kuwahamisha wananchi hao.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dodoma na baadhi ya mawaziri katika kikao kilichowakutanisha na timu ya wataalamu kutoka Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ikiongozwa na kamishna wake, Dk Litha Ogana.

Wataalamu hao walikuja nchini kufuatilia kuhama kwa wananchi wa Ngorongoro ambapo kabla ya kufanyika kwa mazungumzo hayo, Tume hiyo ilipata fursa ya kutembelea na kufanya mazungumzo na wananchi wa Ngorongoro na Msomera. Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Pindi Chana aliieleza Tume kuwa shughuli ya kuwahamisha wananchi zilifuata haki za binadamu kwani zoezi lilikuwa shirikishi na kwamba bado wananchi wanaendelea kujiandikisha kwa hiari.

Mhe. Kassim Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akitoa hoja ya kuahirisha mkutano wa saba wa bunge la 12 tarehe 30 Juni 2022 alisema;

> *"usimamizi wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro umeshindwa kutimiza lengo la kuleta uwiano baina ya uhifadhi, ukuzaji wa utalii na maendeleo ya jamii kutokana na changamaoto mbalimbali"*

Waziri Mkuu alisitiza kuwa hali hiyo imechangiwa na changamoto nyingi za kiuhifadhi na maendeleo ya jamii hususan ongezeko la idadi kubwa ya watu na mifugo, makazi holela na shughuli za binadamu. Kwa mfano, mwaka 1959 wakati Hifadhi hiyo inaanzishwa kulikuwa na watu takriban 8,000 na mifugo 161,000. Lakini hadi sasa idadi ya watu inakadiriwa kuwa takribani 110, 000 na mifugo zaidi ya 1,000,000. Ni jukumu la Serikali kuweka miongozo itakayowezesha maisha ya watu na uhifadhi kuwa endelevu kwa maslahi ya Taifa.

Mhe. Waziri Mkuu alisema pia kwamba changamoto nyingine ni kuendelea kudorora kwa ustawi wa maisha ya wenyeji wa Ngorongoro katika nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwemo elimu, afya, uchumi, usalama wa chakula na lishe, ufinyu wa vyanzo mbadala vya mapato kwa jamii, makazi duni, kukosa haki ya msingi ya kikatiba ya kumiliki na kutumia ardhi kwa ajili ya maendeleo yao kwa sheria zilizopo, pia kumejitokeza kubadilika kwa uoto wa asili na kuenea kwa mimea vamizi. Hivyo, kuendelea kuwepo kwa mfumo uliopo, kunaathiri ustawi endelevu wa maliasili ambazo ndio chanzo kikubwa cha mapato ambayo hugharamia shughuli za maendeleo na ustawi wa Watanzania.

Kufuatia hali hiyo, Serikali kwa nyakati tofauti ilichukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto za usimamizi wa hifadhi ikiwemo kufanya tathmini ya kina tangu mwaka 2017 hadi mwaka 2021 kwa lengo la kutatua changamoto za mfumo wa matumizi mseto ya ardhi. Kutokana na tathmini hiyo, Serikali iliamua kutumia mapori Tengefu ya Handeni na Kitwai yaliyopo katika Wilaya za Simanjiro, Handeni na Kilindi kwa ajili ya wananchi wa Ngorongoro kuhamia na kuendeleza maisha yao na kujitafutia shughuli mbalimbali za uchumi.

Serikali imeendelea kusisitiza kuwa sababu ya kutumia maeneo ya Handeni na Kitwai ni pamoja na kufaa kwa ufugaji na kilimo; mwingiliano wa kimila, kitamaduni na desturi katika jamii iliyopo Handeni na Kitwai na jamii ya wafugaji wa Ngorogoro na shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo zinafanana sana ambapo shughuli kuu ni ufugaji.

Katika kuhakikisha maeneo hayo yanakidhi makusudio yaliyotarajiwa, Serikali imeendelea kujenga miundombinu muhimu katika eneo la Msomera ikiwemo upangaji na upimaji wa viwanja vya makazi na mashamba na ujenzi wa nyumba 500 za wakazi ambapo ujenzi wa nyumba zingine unaendelea kupitia JKT. Vilevile, huduma za umeme na maji tayari zinapatikana na ujenzi wa shule ya msingi na sekondari umekamilika. Ujenzi wa miundombinu ya afya, majosho na barabara tumeona vimekamilika.

Serikali inasema kuwa imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa za eneo la Msomera lililopo Handeni kiuchumi na kijamii kupitia vikao vingi na wananchi wa eneo la Ngorongoro wakiwemo viongozi wa mila (Laigwanak), waheshimiwa madiwani, watendaji wa kata na vijiji (WEO na VEO) wawakilishi wa wakina mama, vijana na wadau wengine. Lakini hali halisi katika jamii hawaoni hivyo vikao na pia hakuna kumbukumbu zozote za vikao hivi na jamii.

Serikali imeendelea kusema zoezi la kuandikisha wakazi wanaoomba kuhama kwa hiari linaendelea vizuri. Serikali imesisitiza kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliridhia kutoa motisha mbalimbali kwa wakazi hao kama ifuatavyo:-

**Moja:** Kila Kaya inayoondoka inapewa fidia ya nyumba aliyokuwa anaishi;

**Mbili:** Kaya zote zinazohamia Msomera kwa hiari zinapatiwa nyumba zenye vyumba vitatu zilizojengwa kwenye eneo la ekari 2.5, godoro, tochi, na ndoo;

**Tatu**: Kila kaya inapewa shamba lenye ukubwa wa ekari tano na zitakabidhiwa hati za kumiliki ardhi kwa ajili ya eneo la nyumba na shamba. Pia lipo eneo lingine huru la kuchungia;

**Nne**: Kila kaya inapewa fedha shilingi milioni kumi kwa ajili ya kuanzia maisha kwenye makazi mapya; na

**Tano:** Kila kaya inapewa mahindi magunia mawili kwa kipindi cha miezi mitatu kwa ajili ya kujikimu katika kipindi cha mpito wakati wakazi wakijiandaa na maandalizi ya kilimo.

### 4.2.6 Matumizi ya Vyombo vya usalama Yanayoendelea Tarafa ya Ngorongoro

Mnamo mwezi Julai,2023 hadi sasa kumeripotiwa ukiukwaji wa haki za binadamu katika tarafa ya Ngorongoro ambapo wananchi walitueleza kuwa askari wa wanyamapori wanaofanya kazi NCAA wamekuwa wakiwapiga na kujeruhi wananchi bila hatua zozote za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

Mfano, mnamo 13.07.2023 Joshua Parato,kijana mwenye umri wa miaka 15 mkazi wa Nainokanoka wilaya ya Ngorongoro,alivunjwa meno 3 na askari wa wanyamapori anayefanya kazi NCAA. Hata hivyo, japokuwa mtumishi huyo wa NCAA ametembuliwa na Joshua kwenye paredi la utambuzi la Polisi, mtu huyo hajakamatwa na kupelekwa mahakamani hadi sasa.

Vilevile, mwishoni mwa mwezi Julai 2023 na mwanzoni mwa mwezi Agusti, 2023 wananchi wa kata ya Endulen Tarafa ya Ngorongoro wamekuwa wakipaza sauti kushinikiza Serikali kutoa vibali vya kukarabati shule ya Msingi Ndian ambayo madarasa mengi yanakaribia kuanguka. Wananchi hao pia waliomba Serikali kuruhusu miradi ya maendeleo ambayo imezuiliwa tangu 2021. Lakini nguvu ilionekana kutumika kuwazuia na baadaye baadhi yao kukamatwa.

NCAA kwa upande wake badala ya kufanyia kazi kilio na malalamiko ya wananchi ilipeleka waandishi wa habari Ngorongoro ili waripoti kuwa wananchi wamechoka kuishi ndani ya hifadhi na wanaomba Serikali iweze kuwahamisha. Kwa namna ya kushangaza,hakuna mwandishi wa habari hata moja kati ya hao walio pelekwa Ngorongoro na NCAA aliyeweza kuripori kilio cha wananchi cha kunyimwa miradi ya maendeleo na vibali vya ujenzi.

Ni muhimu pia kufahamika kuwa hawa sio waandishi bali ni kikundi maalum cha propaganda kinachofadhiliwa kwa lengo la kuchafua jamii ya maasai na utamaduni wao. Kundi hili limekuwa likitumiwa kuandika habari mbaya kwa wananchi huku wakiandaa taarifa za uongo kuwadanganya viongozi wa juu kuwa kila kitu kiko sawa Ngorongoro. Kundi hili linasemekana wanatengewa fedha nyingi sana kwa ajili ya propanganda na kuaminisha umma kuwa kila kitu kiko sawa.

Mfano, mnamo tarahe 15.08.2023, watu hao wanaodaiwa kuwa ni waandishi wa habari walisemekana wamepigwa katika soko la Endulen. Kundi hili lilikuwa linafanya mikutano ya hadhara katika maeneo ya wananchi bila viongozi wa jamii kuwa na taarifa. Baada ya tukio hilo polisi na NCAA walifanya msako wa kukamata kila mwananchi ambaye wamekutana nae katika kata ya Endulen. Takribani watu 60 walikamatwa katika operesheni hiyo.

Miongoni mwa watu waliokamatwa ni, mgonjwa wa kifua kikuu (TB), Watoto wawili (moja wa shule ya msingi Ndian),watu wawili wanye ugonjwa wa akili, Mbunge wa Ngorongoro, Madiwani, wanawake wawili,viongozi wa mila, mwenyekiti wa Kijiji na wananchi wengine. Zaidi ya watu 30 walikamatwa na kushikiliwa kwa muda wa siku 8 na wengine kushikiliwa kwa wiki moja kinyume cha sheria inayokataza watu kushikiliwa zaidi ya masaa 24.

Watu wote ambao wamehojiwa na watetezi wa haki za binadamu wametueleza kuwa wameteswa sana pindi wakiwa vituo mbalimbali vya polisi. Wananchi hao walitueleza kuwa wamepigwa na askari wa NCAA na polisi katika ofisi ya NCAA

Endulen. Walitueleza pia kuwa wamemwagiwa maji ya baridi, kubebeshwa ndoo za maji na kuambiwa warukeruke, kuambiwa wabusu ukuta na kuimbia ukuta kuwa "ninakupenda" , kupigwa makofi, mateke na pia kwa kutumia vitako vya bunduki.

Wananchi tuliowahoji pia walitueleza kuwa walipofikishwa kituo cha polisi karatu walihojiwa bila ndugu au mawakili wao kuwepo wakati wa mahojiano. Wanachi walieleza zaidi kuwa, wakati wa mahojiano walilazimishwa kusaini na kuweka vidole gumba maelezo bila kupewa nafasi ya kusoma au kusomewa na hakuna anaye fahamu kilichoandikwa katika mahojiano hayo. Katika maelezo hayo wananchi pia walitueleza kuwa waliulizwa kwanini hawataki kwenda Msomera na pia uhusika wao katika kudai vibali vya ujenzi. Wananchi walieleza pia kuwa walilazimishwa kuvalishwa mabango na kupigwa picha bila kufahamu kilichoandikwa katika mabango hayo.

Katika hali ya kuendelea kutia hofu wananchi wa Ngorongoro polisi na askari wa NCAA wamekuwa wakuvunja nyumba za watu usiku wa manane na kuchukua vitu pamoja na kuwadhalilisha wanawake. Mfano, askari wa NCAA na polisi inadaiwa walivamia makazi ya mwenyekiti wa Kijiji cha Nasipooriong' usiku wa manane na kuchukua debe 10 za asali na kuwadhalilisha wanaweke na moja kudaiwa kuvuliwa nguo. Usiku huo huo pia walivunja nyumba za familia zingine mbili. Hata hivyo, hakuna hatua iliyochukuliwa hadi sasa.

#### 4.2.6.1 Kunyimwa Haki ya Shughuli za kisiasa na Kujumuika

Wananchi wa tarafa ya Ngorongoro wamenyimwa haki za kujumuika na kufanya shughuli za kiasa ambazo ni haki za kikatiba. Mfano, Mnamo tarehe 07 na 08 Agusti, 2023 polisi walizuia mikutano ya Tundu Lissu, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha CHADEMA Taifa kufanyika katika wilaya ya Ngorongoro. Polisi wengi walitawanywa katika tarafa ya Ngorongoro ili kuzuia wananchi kujumuika na kufurahia haki zao za kisiasa kama raia wengine. Msafara wa kiongozi wa upinzani Tundu Lissu ulizuiliwa kufanya kikao chake katika tarafa ya Ngorongoro kwa kuzuiliwa kupita katika Geti la Ngorongoro ambapo alikuwa anasubiriwa na maelfu ya wanachi.

Mbali na kuzuia wananchi kukutana na viongozi wa kisiasa,Serikali pia inatuhumiwa kuzuia waangalizi wa kimataifa wa haki za binadamu kutembelea Ngorongoro na Loliondo kama vile, wabunge wa Bunge la Ulaya, Mwangalizi Maalum wa Umoja wa Mataifa juu ya watu wa Asili na waangalizi kutoka UNESCO**.**

SURA YA 4
SEHEMU YA TATU

# MAPENDEKEZO MAHUSUSI

## 4.3 UTANGULIZI

Sehemu hii inaelezea uchambuzi wa hoja zilizoibuliwa na wananchi wakati wa ziara pamoja na ufafanuzi ambao Serikali iliwahi kuutoa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Bungeni ama kwenye mikutano na wananchi kipindi cha nyuma.

### 4.3.1 Ufafanuzi wa Serikali Kuhusu zoezi la Kuhama

Waziri Mkuu wa Tanzania Kassim Majaliwa aliwahakikishia wakazi wanaohama kwa hiari yao kutoka katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kuelekea kijiji cha Msomera, Handeni mkoani Tanga kuwa hakuna shughuli zao zitakazosimama na kwamba wataendelea na ufugaji katika mazingira bora zaidi. Aliyasema hayo alhamisi, Juni 23, 2022 wakati akiwaaga wakazi wa Ngorongoro wanaohama kwa hiari yao kwenda kijiji cha Msomera na kupisha shughuli za uhifadhi katika eneo hilo.

> *"Ninawaomba msafiri kwa amani kabisa na mioyo yenu ikunjuke. Isikilizeni Serikali yenu inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan. Sasa hivi mko huru, nenda mkakae kwenye nchi yenu kwa uhuru,"* ***alisisitiza.***

Kama ilivyoelezwa hapo awali, imekuwa ni vigumu kupata ufafanuzi toka kwa serikali pamoja na jitihada zote zilizofanyika kuwapa nafasi ya kufafannua hoja hizi za wananchi. Katika ziara hii tulijionea kuwa shughuli za ufugaji kwa wananchi waliohamishwa kutoka Ngorongoro zimeathirika sana kwasababu hakuna malisho, mifugo imekufa Msomera na wamelazimika kuhamisha mifugo kwenda wilaya ya Kilindi mkoa wa Tanga na maeneo mengine kwaajili ya kutafuta malisho.

Vilevile kuhusu zoezi la kuhama katika ziara hii tulibaini kuwa kinanchoelezewa inaaancha maswali mengi kwa kuwa zoezi halikuzingatia haki za binadamu kama vile haki ya kushirikishwa kikamilifu, haki ya kupewa fidia stahiki, haki ya kupewa taarifa sahihi kuhusu eneo walilohamishiwa yaani Kijiji cha Msomera. Hii ni tofauti na madai ya Serikali ambayo yalitolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Pindi Chana wakati akiwaeleza makamishna wa Tume ya Afrika juu ya Haki za Binadamu na Watu walipokuja nchini Tanzania kufuatilia suala la Ngorongoro kuwa "shughuli ya kuwahamisha wananchi zilifuata haki za binadamu kwani zoezi lilikuwa shirikishi na kwamba bado wananchi wanaendelea kujiandikisha kwa hiari". Wakati wa ziara hii wananchi walitueleza kuwa zoezi la kujiandikisha halikuwa la hiari.

Kwa ujumla zoezi hili la kuhama haliendani kabisa na kinachoelezwa na Serikali katika vyombo vya Habari au katika mikutano mbalimbali. Zoezi hili linaendeshwa bila utaratibu au mwongozo wowote na wananchi hawana taarifa sahihi kuhusu mchakato huu.

### 4.3.2 Uchambuzi kuhusu Changamoto ya Huduma za Kijamii

Tarafa ya Ngorongoro ina huduma kadhaa za kijamii japokuwa hazikidhi mahitaji ya wananchi. Kuna jumla ya shule za msingi 25 na shule za sekondari 3, hospitali 1 ya Endulen na vituo vya afya vitatu (3).

Katika ziara hii tulijioenea kwa macho juu ya changamoto ya huduma za kijamii kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro. Changamoto kubwa ni kuwa Serikali haikujibu hoja hizi kama tulivyowaandikia kuomba ufafanuzi wa Serikali. Baadhi ya taarifa tulipatiwa na wenyeji hivyo kwa ujumla tulibaini changamoto nyingi kama zilivyoelezewa hapo mwanzo kuhusiana na huduma za kijamii kwenye tarafa ya Ngorongoro tangu zoezi la kuhama kwa hiari litangazwe na Serikali.

#### (a) Kusitishwa Vibali vya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu

Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya pili ya sura hii Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro imesitisha vibali vya ujenzi au ukarabati wa shule katika tarafa yote ya Ngorongoro. Kwa mfano Parokia ya Endulen ilijenga shule ya msingi mwaka 2017 na ilianza mpango wa ujenzi wa shule ya sekondari. Kibali cha ujenzi wa shule ya sekondari kilisitishwa mwaka 2021 hivyo kanisa limeshindwa kujenga shule ya sekondari kwaajili wa wanafunzi. Si hivyo tu, nyumba ya masisita wa kanisa katoliki inavuja huu ni mwaka wa pili sasa na wamenyimwa kibali cha kufanya ukarabati.

Shule ya msingi Endulen ilianzishwa mwaka 1947 mpaka leo ina nyumba 6 tu za walimu. Kwa sasa ina walimu 17 (wakike 6 na wa kiume 11), shule hii ina jumla ya wanafunzi 1,900 (wakike 785 na wa kiume 1054) ina mabweni mawili tu. Kati ya hao wanafunzi 617 wanaishi bweni (wakike 272 na wa kiume ni 345) na kuna mabweni mawili tu.

Pia ujenzi wa mabweni 4 mapya umekwama kutokana na vibali kusitishwa hivyo wanafunzi wamelazimika kulala 4 kwenye kitanda kimoja hali ambayo sio njema kiafya na ukizingatia kuwa hawa ni watoto wadogo.Awali shule hii ilikuwa na matundu ya vyoo 42 lakini kwa sasa ni matundu 9 tu yanatumika kwa wavulana na kwa wasichana, mengine yamejaa.

Wananchi wamechanga shilingi milioni 9 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo lakini kibali kimezuiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Hadi tunapomalizia taarifa hii hakuna ufafanuzi wowote wa Serikali uliopatikana kuhusiana na changamoto hii, hivyo inakuwa ngumu kuchambua eneo hili kwa undani kuwa hatukuepewa maelezo rasmi ya Serikali kuhusu swala hili pamoja na jitihada zote zilizofanyika kuwasiliana na Serikali.

Pia ujenzi wa kituo cha afya katika Kijiji cha Sinoni kata ya kakesio, zahanati ya Alailelai pia haina miundombinu na ujenzi umesimama kutokana na kibali cha ujenzi kusitishwa, ujenzi wa zahati ya Esere na kata ya Ngoire haina kabisa zahanati kwa ajili ya kuwahudumia wananchi ingawa vifaa vya ujenzi vyote vipo.

Katika kitongoji cha Ndepesi hakuna shule wala hospitali hivyo imewalazimu wanafunzi kutembea umbali wa kilometa 30 kutafuta shule na kupata huduma ya matibabu. Wakazi wa kitongoji hicho walitafuta na kupata mfadhili mwaka 2016 lakini kibali cha ujenzi walinyimwa hivyo shule haikujengwa. Hivi sasa wanafunzi wanasomea chini kwenye ardhi kwa sababu hawana madarasa.
Hadi tunaandika taarifa hii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Serikali kwa ujumla haijawahi kutoa ufafanuzi juu ya kusitishwa kwa vibali vya ujenzi au ukarabati wa majengo na miundombinu ya wananchi. Isipokuwa wakati wa zaiara hii wananchi walitueleza kuwa kuna ujenzi wa hoteli unaendelea Ngorongoro ili hali wao wanazuiliwa kujenga au kufanya ukarabati wa aina yoyote.

Ni muhimu kukumbuka kwamba Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa wajibu kwa Serikali kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa katika kupata elimu, hivyo kusitishwa kwa vibali vya ujenzi au ukarabati wa shule, madarasa, vyoo vya wanafunzi na nyumba za watumishi ni ukiukwaji wa matakwa ya kikatiba.

Pia ni muhimu kukumbuka kwamba Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilianzishwa na kifungu cha 4 cha Sheria Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo kwenye kifungu cha 6 majukumu yake ni pamoja na kuendeleza jamii ya kifugaji katika eneo hilo hivyo kuzuia vibali ni kinyume na matakwa ya Sheria iliyoanzisha mamlaka hiyo.

Kitendo cha kuzuia vibali kwa ajili kuboresha miundo mbinu na huduma za jamii, kwa mujibu wa ufuatiliaji huu ni mbinu inayotumika kulazimisha wananchi wananchi wahame katika eneo la Ngorongoro. Kitendo hichi kimeondoa dhana ya kuhama kwa hiari ambayo imekuwa ikisisitizwa na Serikali. Kwa ujumla baada ya uchambuzi huu ni Dhahiri kuwa kwa sasa Ngorongoro hakuna uhamaji wa hiari bali wananchi wanawekewa vikwazo vingi kwa lengo la kuwalazimisha wahame.

**(b) Kusitishwa kwa huduma ya matibabu ya dharura (Flying Medical Service)**
Mnamo Oktoba 1983 Kanisa katoliki lilianza kutoa huduma ya dharula ya matibabu kwa wananchi wa Ngorongoro (Flying Medical Service) hasa katika maeneo ambayo hayafikiki kwa usafiri wa kawaida. Kati ya mwaka 1985 hadi mwaka 2021 Flying Medical Service iliwafikia jumla ya wagonjwa 765,947 ambapo watoto pekee ni 138, 036.[18]

18 Ripoti ya Flying Medical Service kuanzia 1985-2021

Huduma hii ilikuwa inatolewa bure kwa wananchi. Aprili 04, 2022 Serikali ilizuia kibali cha huduma hiyo kwa madai kuwa ndege inayotumika (CESSNA-206) imesajiliwa nchini Marekani na sio Tanzania. Watoa huduma wa Flying Medical Service walitueleza kwamba ndege hiyo ilisajiliwa Marekani kwasababu za ukarabati na urahisi wa kuiendesha kuliko ingekuwa imesajiliwa Tanzania na kwa miaka yote ndege hiyo ilikuwa inafanya kazi bila kikwazo cha aina yoyote.

Hivyo kwasasa ndege imekaa tu bila kazi na watu hawapati huduma za matibabu. Hii imepelekea watu kufariki kwa kukosa matibabu, wakina mama wanazidi kupata shida wakati wa kujifungua, na watu wamekosa dawa. Wilaya ya Ngorongoro ina vijiji 70 na baada ya huduma hii kusitishwa vijiji 30 havipati huduma ya matibabu ya dharura na chanjo kutoka na kutokufika kwa haraka kwa njia za kawadia za usafiri.

> *Mwananchi mmoja alisema yafuatayo "kama hospitali imefanya kazi over 50 years, kwanini ifungwe mwaka 2022? Jibu ni kwamba tunawasitishia huduma, you have to feel the pinch, mhamie Msomera"-* ***Mwananchi alitueleza.***

Kitendo hiki pia kinatoa picha kuwa huenda mpango wa Serikali kwa sasa ni kutumia fimbo ya kuzuia huduma za jamii kwa lengo la kuwafanya watu waondoke baada ya kuishi Maisha magumu.

Katika moja ya maelezo ya Waziri Mkuu hapo juu ni kuwa wananchi wanahamishwa kwa kuwa huduma ni duni na hafifu. Kwa kauli ilitegemewa kuwa badala ya kuendelea kuzofisha huduma hizi za msingi za jamii , Serikali ingeziboresha huduma hizi huku mbinu shirikishi na wazi zikiendelea kushawishi wananchi kuhama kwa hiari yao. Ikumbukwe hadi sasa waliohama ni 0.03 ya wakazi wote walioko tarafa ya Ngorongoro ambao kwa sasa ni 10,0000. Sasa kitendo cha kuzua huduma za msingi kwa zaidi ya watu laki moja waliopo Ngoorongoro kihalali kwa sasa ni ukiukwaji mkubwa wa haki za kibinadamu na katiba ya nchi.

**Jedwali *Namba*.4.4 hili linaonyesha huduma na kiasi cha watu waliofikiwa kwa huduma hiyo.**

**Patient Reports: 1985 to 2021**

| A | B | C | D | E | F | G | H | I | J | K |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Year | Treated | Vaccinated | PNC | TB | HIV | Evacuated | Emergency | Total | Hours | Ps/Hr |
| 1983 | 689 | 7,926 | 2,952 | * | | 165 | 43 | 17,337 | 1,368.2 | 12.7 |
| 1984 | | | | * | | | | | | |
| 1985 | 5,435 | | | * | | 105 | 22 | | 330.6 | |
| 1986 | 4,811 | 1,673 | 130 | - | | 104 | 26 | 6,744 | 262.6 | 25.7 |
| 1987 | 4,884 | 3,027 | 397 | - | | 215 | 22 | 8,545 | 398.0 | 21.5 |
| 1988 | 4,117 | 2,018 | 737 | - | | 304 | 18 | 7,194 | 380.5 | 18.9 |
| 1989 | 3,826 | 3,666 | 938 | 187 | | 246 | 16 | 8,879 | 339.8 | 26.1 |
| 1990 | 3,473 | 5,590 | 1,428 | 167 | | 213 | 19 | 10,890 | 626.4 | 17.4 |
| 1991 | 3,454 | 5,434 | 1,674 | 212 | | 122 | 23 | 10,919 | 509.4 | 21.4 |
| 1992 | 3,621 | 6,970 | 2,151 | 278 | | 155 | 38 | 13,213 | 695.7 | 19.0 |
| 1993 | 5,068 | 10,705 | 3,472 | 538 | | 193 | 41 | 20,017 | 689.0 | 29.1 |
| 1994 | 4,024 | 7,646 | 2,860 | 706 | | 196 | 43 | 15,475 | 645.9 | 24.0 |
| 1995 | 4,260 | 6,573 | 3,300 | 605 | | 249 | 40 | 15,027 | 780.8 | 19.2 |
| 1996 | 4,312 | 9,467 | 3,594 | 473 | | 166 | 51 | 18,063 | 787.6 | 22.9 |
| 1997 | 2,067 | 9,835 | 2,697 | 317 | | 117 | 67 | 15,100 | 782.5 | 19.3 |
| 1998 | 2,601 | 6,897 | 2,793 | 123 | | 179 | 63 | 12,656 | 903.7 | 14.0 |
| 1999 | 2,705 | 8,243 | 2,747 | 86 | | 88 | 55 | 13,924 | 668.4 | 20.8 |
| 2000 | 3,634 | 9,205 | 3,531 | 330 | | 114 | 75 | 16,889 | 882.7 | 19.1 |
| 2001 | 5,546 | 8,176 | 3,372 | 650 | | 128 | 95 | 17,967 | 865.6 | 20.8 |
| 2002 | 6,094 | 9,855 | 4,369 | 532 | | 84 | 121 | 21,055 | 969.7 | 21.7 |
| 2003 | 6,989 | 9,080 | 4,377 | 421 | | 121 | 74 | 21,062 | 818.0 | 25.7 |
| 2004 | 6,872 | 9,260 | 3,609 | 373 | | 126 | 96 | 20,336 | 859.8 | 23.7 |
| 2005 | 6,928 | 9,217 | 4,317 | 530 | | 79 | 149 | 21,220 | 1,150.9 | 18.4 |
| 2006 | 5,280 | 10,317 | 4,135 | 498 | | 105 | 147 | 20,482 | 1,218.8 | 16.8 |
| 2007 | 7,250 | 13,434 | 5,301 | 474 | | 119 | 113 | 26,691 | 1,072.8 | 24.9 |
| 2008 | 6,662 | 16,404 | 5,405 | 431 | | 83 | 87 | 29,072 | 793.1 | 36.7 |
| 2009 | 5,356 | 16,151 | 5,139 | 544 | | 65 | 93 | 27,348 | 764.6 | 35.8 |
| 2010 | 7,011 | 15,710 | 4,939 | 390 | | 44 | 138 | 28,232 | 1,080.9 | 26.1 |
| 2011 | 5,034 | 18,331 | 5,020 | 413 | | 37 | 160 | 28,995 | 1,192.0 | 24.3 |
| 2012 | 4,693 | 17,612 | 5,235 | 441 | | 19 | 97 | 28,097 | 959.6 | 29.3 |
| 2013 | 4,148 | 19,861 | 5,185 | 495 | | 24 | 107 | 29,820 | 824.7 | 36.2 |
| 2014 | 1,980 | 11,733 | 3,733 | 109 | | 11 | 36 | 17,602 | 467.6 | 37.6 |
| 2015 | 5,470 | 19,557 | 5,801 | 178 | | 11 | 82 | 31,099 | 871.2 | 35.7 |
| 2016 | 3,228 | 18,258 | 5,805 | 176 | | 8 | 89 | 27,564 | 894.8 | 30.8 |
| 2017 | 3,368 | 16,447 | 4,498 | 160 | | 18 | 70 | 24,561 | 759.0 | 32.4 |
| 2018 | 5,633 | 18,917 | 5,772 | 187 | | 20 | 91 | 30,620 | 880.0 | 34.8 |
| 2019 | 5,372 | 23,013 | 5,957 | 157 | 102 | 13 | 85 | 34,699 | 796.2 | 43.6 |
| 2020 | 6,961 | 23,722 | 5,395 | 174 | 75 | 15 | 68 | 36,410 | 703.5 | 51.8 |
| 2021 | 5,604 | 20,918 | 5,271 | 174 | 77 | 9 | 95 | 32,143 | 801.6 | 40.1 |
| | | | | | | | | | | |
| **Total** | **178,460** | **430,848** | **138,036** | **11,529** | **254** | **4,070** | **2,755** | **765,947** | **29,796** | **25.7** |

* Information not available

Clinic Definitions:

A. Year of operation: 1 January through 31 December
B. Patients treated for medical problems.
C. The number of children vaccinated for infectious diseases.
D. Pre-natal care: The number attending the pregnant women's clinic (also known as Ante Natal Clinic)
E. Tuberculosis patients treated.
F. HIV patients treated.
G. Evacuated: patients seen at, but too sick to be treated in, the under-the wing-of-the-airplane clinics and who were flown to a nearby hospital.
H. Emergency: Critically ill patients not seen on a scheduled clinic and who require immediate attention and usually a special emergency flight transfer to a higher level hospital.
I. Total Patients seen
J. Total hours flown
K. The average number of patients seen per hour flown.

***Picha 4.9:*** *Ripoti ya Flying Medical Service 1985-2021*

### (d) Tishio la Kushushwa hadhi kwa Hospital ya Endulen

Mwaka 1975 kanisa katoliki chini ya usimamizi wa Padre Herbert Watschinger lilianzisha hospitali ya Endulen kwaajili ya kutoa huduma ya matibabu kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro. Mwaka 2012 kanisa katoliki na Serikali waliingia ubia wa kuendesha hospitali ya Endulen. Serikali ilikuwa inachangia hela ya mafuta ya magari ya hospoitali, chakula cha wagonjwa, na walikuwa wanatoa dawa zenye thamani ya Tshs 80,000,000/= kwa mwaka.

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilikuwa inatoa kiasi cha shilingi 300,000,000/= kati ya mwaka 2015 hadi 2020 ilipositisha. Tangu mwaka 2018 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro iliacha kupeleka dawa katika hospital ya Endulen na imeacha kupeleka chakula cha wagonjwa kwenye hospitali.

Wafanyakazi wa hospitali ya Endulen na kanisa walifanya mazungumzo mwaka 2018 juu ya wingi wa wagonjwa wanaowapokea na kujadiliana namna ya kuboresha huduma za hospitali. Mwaka 2022 Bodi ya hospitali ilimuomba Askofu wa kanisa katoliki jimbo la Arusha aongee na Mkuu wa Mkoa ili kujadiliana namna ya kutatua changamoto zilizokuwepo. Walikubaliana waunde tume kwaajili ya kufanya tathmini na ushauri wa nini kifanyike. Kamati iliyoundwa ilijumuisha Mganga Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye alikuwa mwenyekiti, maofisa kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa, wenyeji na Kanisa katoliki Endulen.

Wajumbe wa kamati hiyo walitembelea hospitali ya Endulen na kutoa maelekezo kuwa kuna uwezekano wa kushushwa hadhi ya hospitali hadi kuwa dispensary, kupunguza wafanyakazi na kupunguza baadhi ya huduma, kitu ambacho hayakuwa makubaliano ya kikao cha wajumbe wote wa kamati.

Kwa mujibu wa taarifa tulizopata ni kwamba kamati hiyo ilijipa mamlaka ambayo haikuwa nayo na sio wajumbe wote walishiriki kwenye maamuzi. Ni kweli kwamba kama Kanisa ilikuwa na nia ya kupunguza wafanyakazi kwasababu hospitali haina uwezo wa kujiendesha kutokana na wafadhili kupunguza ufadhili na Serikali kusitisha baadhi ya huduma kama hela za dawa na chakula cha wagonjwa.

Kufikia Desemba 2022 jumla ya wafanyakazi 17 walipunguzwa kazini kwani mikataba yao haikufanyiwa marejeo baada ya muda wake kuisha.  Kwa maoni yetu, ni muhimu Serikali kutambua kwamba nchi yetu imeridhia mikataba mbalimbali kuhusu utoaji wa huduma za kijamii kama vile Mkataba wa Kimataifa juu ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni pamoja na Katiba yetu ambayo inatoa wajibu kwa Serikali kuhakikisha upatikanaji wa matibabu bora kwa wananchi wote.

Hivyo, Serikali inapaswa kuendelea kutoa fedha za dawa, fedha za chakula kwa wagonjwa na huduma zingine ikiwemo kuiboresha hospitali ya Enduleni na sio kuishuhsa hadhi kwa sababu hii ndio hospitali pekee katika tarafa ya Ngorongoro ambayo imekuwa inahudumia watu kwa miaka mingi.  Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inaingiza.

### (e) Fedha za Miradi ya Maendeleo Kuhamishwa bila Utaratibu

Wakati wa zaiara tulibaini kuwa kiasi cha Tshs. 355,500,000 cha fedha za mradi wa uviko-19 (Covid-19 relief funds) zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro zilihamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni bila kuazimiwa na baraza la madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Fedha hizo zilihamishwa Machi 31, 2023.

Fedha hizo zilikuwa kwaajili ya kujenga madarasa na mabweni ya wanafunzi katika shule tatu za Serikali ambazo ni Nainokanoka, Embarway na shule ya Wasichana ya Ngorongoro pamoja na shule za msingi Endulen, Misigiyo na Esere. Baada ya fedha hizo kuhamishwa imepelekea wanafunzi kukosa madarasa, mabweni pamoja vyoo. Sisi kama watetezi wa haki  tuliona kwamba fedha hizo zilihamishwa kama njia ya shinikizo ili watu wahamie katika Kijiji cha Msomera. Ushahidi wa fedha hizo kuhamishwa ni barua 3 ambazo zimeambatanishwa katika taarifa hii.

Fedha zingine takriban million 600 zilihamishwa kutoka shule ya Enduleni na kuelekezwa katika Kata Soitsambu Loliondo.  Taarifa hii haikuweza kupata jumla ya fedha zilizohamishiwa lakini taarifa zisizo rasmi zinaonyesha zaidi ya billion mbili zimehamishwa kutoka miradi ya kijamii na huduma za kijamii kwa ndani ya miaka miliwil pekee 2021/2022. Misingi ya haki za binadamu inakataza ubaguzi wowote wa kupangwa dhidi ya jamii au kundi lolote katika jamii. Hali hii inayoendelea Ngorongoro imefikia kiwango cha hali ya juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu (High level of human rights abuse). Mikakati yote hii inaonekana inapangwa ili kuidhoofisha jamii hii ya kimasai katika eneo la Ngorongoro kijamii, kisiasa ,kiuchumi na kitamaduni kwa lengo la kuwafaya walazimike kuondoka eneo hili.

### (f) Kukosekana kwa huduma msingi kama barabara, umeme na maji

Kutokana na ziara ambayo tumefanya tulibaini ya kwamba tarafa ya Ngorongoro haina barabara nzuri zilizochongwa kwaajili ya matumizi ya biandamu wanaoishi ndani yae neo hilo isipokuwa barabara inayotumika kwa shughuli za utalii. Katika vijiji na mitaa ambayo wananchi wanaishi tulijionea ukosefu wa barabara zilizochongwa. Huduma ya umeme hata wa solar haupo katika tarafa ya Ngorongoro na hakuna miundo mbinu ya maji kabisa.

Sisi tunadhani ni muhimu kwa wananchi kupatiwa umeme wa solar na kuunganishiwa huduma ya maji. Kwa mfano Baraza la Wafugaji walipata mfadhili wa mradi wa maji wa dola za Marekani 300,000/=, lakini Serikali iliamuru kwamba mwekezaji huyo alete pesa bila kufika eneo la mradi hali ambayo ilipelekea mwekezaji huyo kuahirisha uwekezaji.

*Mwananchi mmoja alihoji kwamba "sisi hatuna barabara, tumezuiwa kufanya shughuli za ujenzi na huduma mbalimbali tumesitishiwa. Lakini cha kushangaza tumeona miradi mikubwa ya ujenzi wa mahoteli na uwekaji umeme kwenye mahoteli hayo unafanyika"*

### (g) Zoezi la Anwani ya Makazi Halikufanyika Katika Tarafa ya Ngorongoro

Katika ziara yetu tulibaini kuwa zoezi la kuweka anwani za makazi halikufanyika katika tarafa nzima ya Ngorongoro. Hali hii iliwaacha wananchi katika hali ya sintohamu na mpaka sasa hawajui hatima ya zoezi hilo. Sisi tunaamini kwamba kwa vile zoezi hilo ni la nchi nzima bado tunaona kuna haja ya Serikali kufanya zoezi hilo katika tarafa ya Ngorongoro ili wananchi wapate haki ya anwani yao ya makazi.

### (h) Miradi ya Maendeleo Kusimamiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama

Tangu kuanza kwa zoezi la kuhama kwa hiari, miradi ya maendeleo ndani ya tarafa ya Ngorongoro imekuwa inasimamiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya tofauti na chombo chenye mamlaka ambalo ni baraza la madiwani. Hii ni kinyume na utaratibu kwani kisheria baraza la madiwani ndio chombo halali chenye mamlaka ya kupanga na kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika halmshauri husika.

Wananchi wa Ngorongoro wamelalamika kuwa maamuzi ya kuondoa miradi ya maendeleo Ngorongoro imekuwa ikifanywa zaidi kamati ya usalama ya Wilaya na sio ofisi ya Mkurugenzi na Baraza la Madiwani.

### (i) Uhaba wa Majosho kwa ajili ya Mifugo

Wananchi hawana majosho ya kutosha kwa ajili ya kuogeshea mifugo yao. Ni muhimu Serikali kujenga majosho ya kisasa ili kukidhi mahitaji ya wananchi ambao wanajishughulisha na ufugaji.

### (j) Nyumba kwenda na upepo na kunyimwa ruhusa ya kufanya ukarabati

Katika Kijiji cha Mokilal nyumba zaidi ya 60 ziliezuliwa na upepo ikiwemo ofisi ya Kijiji. Mapaa yaliezuliwa na nyumba zimekaa bila kupauliwa. Katika ofisi ya Kijiji tulikuta pia kuna magunia ya mahindi ambayo ikinyesha mvua yanalowana na mahindi kuharibika. Ukarabati wowote haujafanyika kwasababu ya kukosa vibali. Hali hii ni hatari sana kwa usalama wa watu lakini pia ni taswira mbaya kwa Serikali kuzuia watu waliopatwa na janga la kupoteza makazi yao kuanya ukarabati ya nyumba zilizobomolewa na upepo.

Changamoto zote hizi zinakiuka haki za binadamu za wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro. Ni kinyume na misingi ya haki za binadamu kama ilivyoelezewa katika Azimio la Haki za Binadamu la Ulimwengu la Mwaka 1948, Mikataba mbalimbali ya haki za binadamu kama ilivyofafanuliwa katika sura ya pili ya taarifa hii.

#### 4.3.3 Mapendekezo Mahususi

#### 4.3.3.1 Kwa Serikali

a) Tunaishauri Serikali kwa ngazi ya Wilaya na Mkoa kuendelea kupeleka miradi/ huduma za kijamii zinazotengwa katika bajeti ya TAMISEMI katika tarafa ya Ngorongoro kwa kuwa suala la kuzuia miradi lina madhara makubwa kwa wananchi na linaleta taswira mbaya kwa Serikali.

b) Serikali na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro zitoe vibali kwa ajili ya huduma muhimu za kijamii kwa maisha ya wanadamu kama vile ujenzi wa vyoo, majengo ya huduma za jamii, hospitali ya Endulen, vituo vya afya, zahanati, madarasa, makazi na mabweni ya wanafunzi.

c) Tunaishauri Serikali iruhusu huduma ya afya ya dharura kwa jamii iliyokuwa inatolewa na Flying Medical Service katika maeneo ambayo hayafikiki kwa usafiri wa kawaida ili tuendelee kuendana na mpango wa taifa ya kupunguza vifo vya wakina mama wajawazito na watoto na mpango wa taifa wa utoaji chanjo kwa watato.

d) Tunaishauri Serikali kusitisha zoezi la uhamishwaji wa wananchi kwani zoezi hilo limeghubukwa na kasoro nyingi lakini pia linapingana na sheria ilianzisha hifadhi ya Ngorongoro kuwa ni eneo mesto. Zoezi hili liendeleea baada ya serikali kukaaa na wananchi, viongozi wa jammii ya watetezi wa jamii ili kupanga mpango shirikishi wa namna ya watu watakavyoondoka kwa hiari.

e) Tunaishauri Serikali kuacha baraza la wafugaji Ngorongoro ( NPC) lijitegemee kama lilivyoanzishwa badala ya sasa ambapo chombo hicho pekee kilichokuwa nguzo ya kuunganisha wenyeji na NCAA pamoja na Serikali hakipo huru na hivyo kupelekea changamoto mbalimbali kwa wenyeji kushindwa kupata utatuzi.

f) Tunaisihi Serikali kuwachukulia hatua za kisheria na kuwaamuru maofisa wa Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kulipa fidia kwa wananchi waliopoteza mifugo yao baada ya kula chumvi iliyothibitishwa na wataalamu kuwa na sumu katika kata ya Ngorongoro, Misigiyo na Nainokanoka.

g) Tunaisihi Serikali pamoja Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro waruhusu kwa asasi za kiraia na wadau wengine kwenda kutoa huduma za msingi kwa jamii katika Tarafa ya Ngorongoro

h) Tunaiomba Serikali kuitaka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro warudishe na kutoa msaada wa chakula na dawa kwa Hospitali ya Endulen kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa katika hospitali hiyo kama ilivyokuwa awali.

i) Tunaishauri Serikali kujenga majosho ya kisasa kwaajili ya wafugaji kuogesha mifugo yao. Kama Serikali ina upungufu wa fedha basi itoe vibali kwa wananchi au mfadhili yeyote ambaye anaweza kufadhili ujenzi wa majosho na huduma zingine za kijaami.

j) Tunaiomba Serikali kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro iondoe usumbufu kwa wakazi wa Ngorongoro pale wanaporudi kutoka nje ya eneo katika kufuata huduma mbalimbali ili kuepuka uvunjifu wa haki za wenyeji kwenye mazingira ya geti la kuingia Ngorongoro.

k) Tunaisihi Serikali kuingilia kati na kutoa adhabu kali za kisheria kwa wote waliohusika kugawa dawa za trakoma ambazo zilionekana kuisha muda wake.

l) Tangu mwaka 2010 wananchi wa tarafa ya Ngorongoro walizuiliwa kuwa na kilimo cha kujikimu hali ambayo imepelekea janga kubwa la njaa, tunaiomba Serikali itoe msaada wa chakula kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro na kurudishiwa kilimo cha kujikimu ili kuwanusuru wananchi kuondokana na janga la njaa kipindi hichi wakati tunajaribu kutafuta suluhu ya kudumu.

m) Serikali kuwarudishia wananchi wa tarafa ya Ngorongoro fedha ya mradi wa Covid-19 zilizohamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

n) Serikali ikae na watetezi wa haki za binadamu , jamii pamoja na viongozi wa jamii kuandaa mpango wa pamoja wa kuhama kwa hiari (Voluntary-Relocation Plan)

o) Wananchi wa Tarafa ya Ngorogoro wasisizuiwe kushiriki shughuli zozote za kijamii kama watanzania wengine hasa swala la siasa.

p) Serikali iondoe huduma za jamii pale tu itakapoona Kijiji kizima kimeshaondoka na kuhamia kwingine na sio kuondoa huduma za jamii wakati bado kuna binadamu wengi katika kata na vijijiji.

#### 4.3.3.2 Kwa Wananchi

a) Tunawaomba wananchi waendelee kutumia njia halali za kimahakama katika kudai haki zao pale ambapo zimekiukwa au zitakiukwa.

b) Tunawaomba wananchi kufanya mikutano na kujadiliana juu ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabili bila kufanya uhabiribifu wowote.

c) Tunawaomba wananchi waendelee kutunza mazingira pamoja na kuendeleza utamaduni wao wa kuishi na wanyamapori bila kuwadhuru.

d) Tunawaomba wananchi kuyatunza maeneo yote yanayotumika kwa shughuli za kiutamaduni, kimila na kuabudia ili kuendeleza uhai na uhalisia wa Ngorongoro kama eneo nyeti lenye matumzi mseto.

e) Tunawaomba wananchi kutokaa kimya pale uvunjivu wa haki zao kama binadamu unapotokea. Hivyo waripoti Katika mamlaka husika, kwa watetezi, polisi n.k matukio yote yanayoashiria uvunjivu wa haki za binadamu na unyanyasaji.

f) Tunawasihi wananchi wasiwabuguzi wenzao wanaojitokeza kwa hiari yao bila shinikizo lolote kuhama kwa hiari

#### 4.3.3.3 Kwa Wadau wa Maendeleo

a) Tunawaomba wadau wa maendeleo kuwezesha miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro. Katika wilaya nzima ya Ngorongoro hakuna miradi mingi ambayo inatekelezwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi hivyo ni muhimu wadau kushiriki katika kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inapatikana kwa wananchi wa Ngorongoro.

b) Tunawaomba wahimize uzingatiwaji wa haki za binadamu na utawala wa sheria katika masuala mazima ya uhamishwaji wa wananchi wa tarafa ya Ngorongoro ambao wako tayari kuhama kwa hiari kutoka Ngorongoro.

c) Tunawaomba wadau kutembelea tarafa ya Ngorongoro ili kujionea hali halisi ya kile kilichotokea na kinachoendelea kwa wananchi wa Ngorongoro.

#### 4.3.3.4 Kwa Watetezi /Mashirika yasiyo ya Kiserikali

a) Tunaziomba asasi za kiraia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro. Kwa mfano miradi ya afya, maji, elimu, kuwawezesha kiuchumi hasa kwa wakina mama n.k.

b) Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Ngorongoro.

c) Kuendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wakazi wa tarafa Ngorongoro kwa wale wenye mahitaji

d) Kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kutatua changamoto katika tarafa ya Ngorongoro.

e) Kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kuendelea na kudumisha matumizi bora ya ardhi mseto ya Ngorongoro.

SURA YA 4
SEHEMU YA NNE

# MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO

### 4.0 Utangulizi

Sura hii ya mwisho katika eneo la Ngorongoro inaelezea hitimisho na mapendekezo ya jumla yaliyotokana na ziara. Ni muhimu kwa mapendekezo haya kuzingatiwa na kufanyiwa kazi ili kuleta nafuu kwa wananchi kutokana na ukweli kwamba bila ya mapendekezo haya kufanyiwa kazi hali itakuwa ngumu Zaidi kwa wananchi wa tarafa ya Ngorongoro.

### 4.1 Mapendekezo ya Jumla

a) Serikali katika ngazi ya Wilaya na Mkoa inapaswa kupeleka miradi /huduma za kijamii zinazotengwa katika bajeti ya TAMISEMI katika tarafa ya Ngorongoro kwa kuwa suala la kuzuia miradi lina madhara makubwa na ni unyanyasaji wa wananchi na linaleta taswira mbaya kwa Serikali. Pia ni jambo la aibu kuwaumiza wananchi ambao ndio wametunza maeneo hayo kwa miaka yote.

b) Tunaishauri Serikali,Wizara ya maliasili na utalii, Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro, mashirika yanayojihusha na uhifadhi kujadili na kutathmini upya hoja zinazoisukuma Serikali kupunguza idadi ya watu Ngorongoro, kwani imebainika kuwa hoja hizo likiwemo swala la kuenea kwa mimea vamizi na uharibifu mwingine wa kuhifadhi lina vyanzo vingine ambavyo NCAA hawataki kubainisha badala yake wameelekeza nguvu kuwatuhumu watu na mifugo yao kuwa ndio chanzo cha uharibifu huo, Dhanio ambalo halina uhakika ikizingatiwa kuwa kuna maeneo ambazo ni no go zone kama kreta ya Ngorongoro na Ndutu lakini mimea vamizi imetapakaa zaidi maeneo hayo kuliko hata maeneo wanamoishi watu. Pia kupitia ripoti ya jamii, imebainika kuwa wenyeji wanaishi asilimia 5 tu ya eneo lote kinyume na malalamiko ya wahifadhi kuwa uwezo wa eneo (carrying capacity) imekuwa ndogo kulinganisha na idadi ya watu.

c) Tunaisihi Serikali kuruhusu vyombo huru vya habari kuchunguza na kupata ukweli katika eneo la Ngorongoro, yaani upande wa jamii na uhifadhi, ili kuja na matokeo ambayo yatasaidia kupata ufumbuzi wa changamoto zinazoikumba jamii na uhifadhi.

I. Kwani kwa kuanzia mwaka 2022 uhuru wa vyombo vya habari uliingiliwa ambapo hakuna chombo chochote chenye kuweza kuchukua na kurusha habari ya wenyeji wa Ngorongoro pindi tu swala la kuhama kwa hiari lilipaloanza.

II. Badala yake ni vyombo vya habari tu vinavyoonyesha upande wa Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na Serikali walipata ruhusa ya kuchukua habari za matukio Ngorongoro ambazo mara nyingi huwa ni za upande mmoja. Hali hii iliongeza propaganda nyingi dhidi ya jamii, kuziba changamoto za upande wa jamii na kuzidi kuleta mvutano kati ya wananchi na Serikali yao.

d) Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro inapaswa kuboresha nyumba za asili zilizopo Ngorongoro kwani ni kivutio cha utalii, haziaribu mazingira na zimependesha eneo hilo.

e) Kwamba mamlaka husika kama wizara ya Habari na mawasiliano, iwahoji na kuwachukulia hatua wamiliki na wahariri wa baadhi ya magazeti na vyombo vingine, ambavyo kwa nyakati tofauti zimetumia muda mwingi kueneza chuki na uongo, kutoa kauli za kudhalilisha dhidi ya wenyeji wa Ngorongoro

f) Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ione umuhimu wa kutoa vibali kwa ajili ya huduma muhimu za kijamii kwa maisha ya wanadamu kama vile ujenzi wa vyoo, majengo ya huduma za jamii, hospitali ya Endulen, vituo vya afya, zahanati, madarasa, makazi na mabweni ya wanafunzi.

g) Ili kuepusha watu kufa kwa kukosa matibabu Serikali iruhusu huduma ya afya ya dharura kwa jamii iliyokuwa inatolewa na Flying Medical Service katika maeneo ambayo hayafikiki kwa usafiri wa kawaida ili tuendelee kuendana na mpango wa taifa ya kupunguza vifo vya wakina mama wajawazito.

h) Serikali isitisha zoezi la uhamishwaji wa wananchi ili kufanya tathimini shirikishi juu ya changamoto zilizojitokeza katika awamu ya kwanza ya kuhamisha watu kwa hiari. Serikali inapaswa kuandaa Mpango wa kuhamishwa (Relocation Plan) kwa kushirikiana na wananchi, Serikali za vijiji, Baraza la wafugaji, Baraza la Madiwani, asasi za kiraia, wadau wengine pamoja na watetezi wa haki za binadamu. Mpango huu utatoa dira na mwongozo wa namna bora ya kusimamia maslahi ya hifadhi pamoja na maslahi ya wananchi kwaajili ya vizazi vya sasa na vinavyokuja.

i) Tunaomba Serikali kuwachukulia hatua za kisheria na kuwaamuru maofisa wa Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kulipa fidia kwa wananchi waliopoteza mifugo yao baada ya kula chumvi iliyothibitishwa na wataalamu kuwa na sumu katika kata ya Ngorongoro, Misigiyo na Nainokanoka.

j) Tunaiomba Serikali iwashauri na kuwataka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itoe vibali kwa asasi za kiraia na wadau wengine kwenda kutoa huduma za msingi kwa jamii katika Tarafa ya Ngorongoro

k) Tunaiomba Serikali kuingilia kati na kutoa adhabu kali za kisheria kwa wote waliohusika kugawa dawa za trakoma ambazo zilionekana kuisha muda wake.

l) Serikali inapaswa kufuta takwa la wakazi wa Ngorongoro kulipa gharama ya kupaki gari kwa wale ambao ni wakazi wa tarafa ya Ngorongoro kwasababu ni kuwabebesha mzigo usiokuwa na faida kwa wananchi hao.

m) Serikali ione umuhimu wa kuwarudishia wananchi wa tarafa ya Ngorongoro fedha ya mradi wa Covid-19 zilizohamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

n) Wananchi wanapaswa kudai haki zao kwa kutumia njia za kimahakama katika kudai haki zao pale ambapo zimekiukwa au zitakiukwa.

o) Serikali ya wilaya iandae na kutangaza utaratibu wa uchaguzi wa nafasi za madiwani na viongozi wengine waliohama ili wananchi wapate uwakilishi sahihi wa viongozi katika vyombo mbalimbali vya maamuzi.

p) Serikali iache kutoza faini wafugaji amabo wanasafirisha mifugo yao kwenda kwenye minada.Wananchi wanaosafirisha mifugo yao kwa ajili ya kwenda kuuza hawastahili kutozwa faini na madai ya vibali lukuki ambavyo awali havikuwepo. Sambamba na hilo, Serikali inapaswa kuanzisha masoko ya uhakika katika tarafa ya Ngorongoro.

q) Wadau wa maendeleo wanapaswa kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro. Katika wilaya nzima ya Ngorongoro hakuna miradi mingi ambayo inatekelezwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi hivyo ni muhimu wadau kushiriki katika kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inapatikana kwa wananchi wa Ngorongoro.

r) Asasi za kiraia zinapaswa kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro. Kwa mfano miradi ya afya, maji, elimu, kuwawezesha kiuchumi hasa kwa wakina mama n.k.

s) Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Ngorongoro.

t) Kuendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wakazi wa tarafa Ngorongoro kwa wale wenye mahitaji

u) Serikali ifanye uhifadhi wa mazingira unazozingatia maarifa ya asili ya uhifadhi wa mazingira (Indigenous Conservation Knowledge). Nchi nyingi duniani zinadhamini sana utaalam wa kiasili wa kuhifadhi mali asili hasa zile zenye jamii zinazoishi kwa kutegemea mazingiria asili kama ilivyo kwa wamasai wa Ngorongoro.

### 4.2. Hitimisho

Katika ziara kwenye tarafa ya Ngorongoro tuliona hali halisi ya eneo la Ngorongoro na namna ambavyo wakazi wa eneo hilo wamehifadhi mazingira yao. Eneo linavutia kwa utalii na nyumba za asili zilizopo katika eneo hilo zinavutia zaidi kwani zinapendesha mazingira hivyo ni muhimu nyumba hizo kuendelea kuwepo na kuboreshwa zaidi ili kuendelea kudumisha utamaduni wa wamaasai wa Ngorongoro.

Tulijionea pia hali ya miundombinu na changamoto zinazowakabili wananchi. baadhi ya changamoto hizi ni kama vile kunyimwa vibali vya kufanya ujenzi au ukarabati wa majengo, kusitishiwa huduma ya dharula ya matibabu iliyokuwa inatolewa na Flying medical Service tangu mwaka 1983, kutokuwepo kwa huduma za kijamii kama umeme, maji, vyoo mashuleni, uhaba wa madarasa na mabweni kwaajili ya wanafunzi. Sisi kama Mtandao tunasisitiza kuwa wananchi wana haki ya kupata huduma za kijamii hata kama kuna baadhi yao wameamua kuhama kwa hiari, hivyo ni muhimu huduma za kijamii kuendelea kutolewa kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro.

Tunahitimisha pia kuwa hakuna sababu zozote za kisayansi na kisheria za kuwahamisha watu kutoka katika makazi yao ya kudumu ndani ya hifadhi ya Ngorongoro kwenda kwingineko.
Ngorongoro bado ina hali nzuri inayo vutia na kwa watu wote wanao tembelea. Ulazima wowote wa kupunguza watu unaweza ukafanyika lakini kwa kupitia mikakati ya pamoja na wananchi, na wananchi wamesisitiza wapo tayari kukaa na kupanga na serikali mikakati yoyote.

Taarifa zote tulizozieleza katika ripoti hii tumekusanya kutoka kwa wananchi na kwa viongozi wao ndani ya eneo la tarafa hivyo tunawashukuru wananchi na viongozi waliotoa ushirikiano kwetu wakati wote wa ziara yetu. Taarifa hii isingeweza kukamilika bila kupata taarifa sahihi kutoka kwa wananchi, wahanga wa kukosa huduma za kijamii, tunawashukuru kwa kutupatia taarifa mbalimbali na muhimu kwa ajili ya uandishi wa taarifa hii.

Mwisho, tunawashukuru wadau mbalimbali ambao wamekuwa katika mstari wa mbele katika kuhamasisha uhifadhi unaozingatia haki za binadamu katika tarafa ya Ngorongoro. Tunawashukuru wale wote ambao wamekuwa wakitoa huduma kwa wananchi bila kujali ugumu wa mazingira yaliyopo.



SURA YA 5
SEHEMU YA KWANZA

# HALI YA HAKI ZA BINADAMU TARAFA YA LOLIONDO NA SEHEMU YA SALE

## 5.1 Kuhusu Tarafa ya Sale na Loliondo

Wilaya ya Ngorongoro ina eneo la kilometa za mraba zipatazo 14,036 ambapo Tarafa ya Ngorongoro ina jumla za kilometa za mraba 8,100, Tarafa ya Sale ina jumla ya kilometa za Mraba 3,518 na tarafa ya Loliondo ina ukubwa wa kilomita za mraba 2,218. Kwa mujibu wa ripoti ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 tarafa ya Sale na Loliondo ina jumla ya watu 166,553. Wakazi wa eneo lenye mgogoro shughuli yao kubwa ni ya ufugaji wa asili kama chanzo kikuu cha uchumi na ambao huchangia zaidi ya asilimia 50 ya mapato yote ya ndani ya Halmashauri.[19]

Tarafa ya Loliondo na Sale kwa ujumla zina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 5,744 ambayo kwa wilaya ya Ngorongoro pekee ni sawa na asilimia 41 ya eneo lote la wilaya. Kati ya kilometa za mraba 5,744 za Sale na Loliondo, kilometa za mraba 4,000 ndio zilikuwa na pori tengefu kwa mujibu wa sheria kabla ya mabadiliko ya 2009 ambayo ilifuta mapori tengefu ndani ya ardhi ya vijiji. Kati ya eneo lote la kilometa za mraba 5,744 eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,744 linajumuisha eneo lote la tarafa ya Sale isipokuwa kata za Malambo na Piyaya ambazo ni sehemu ya eneo la kilometa za mraba 4000 zinazojumuisha eneo lote la tarafa ya Loliondo. Eneo hili la kilometa za mraba 4000 ilikuwa ni eneo la ardhi ya vijiji na mji mdogo wa Loliondo na maeneo ya Sale kabla ya kuchukuliwa kwa nguvu na kinyume cha sheria eneo la kilometa za mraba 1,502 mwaka 2022 na kufanywa kuwa Pori tengefu la Pololet bila ridha ya wananchi wenyewe.

### 5.1.1 Kuhusu Pori Tengefu la Pololeti

Eneo lenye kilomita za mraba 1,502 ndani kilometa za mraba 4000 ndio limekuwa na mgogoro wa ardhi kwa muda mrefu ikijumuisha kata mbili (2) za Malambo na Piyaya vya tarafa ya Sale, na kata sita (6) za tarafa ya Loliondo ambazo ni kata za Arash, Oloipiri, Maaloni, Oloirien, Soitsambu na Ololosokwan zenye jumla ya vijiji 23.

---

19 Ripoti Ya Mapendekezo Ya Wananchi Juu Ya Utatuzi Wa Mgogoro Wa Ardhi Tarafa Za Loliondo Na Sale Wilaya Ya Ngorongoro Arusha (2022)

Eneo hili limekuwa likiitwa Pori Tengefu la Loliondo toka mwaka 1950 na limeendelea kuwa na matumizi mseto, ikimaanisha kuwa shughuli za usimamizi wa wanyamapori Pamoja na makazi ya wananchi katika vijiji rasmi pamoja na makao makuu ya wilaya kwa kuwa sheria za Wanyama pori kuanzia mwaka 2009 kurudi nyuma hazikundoa uwepo wa vijiji katika mapori tengefu hapa nchini. Eneo hili ( lililobatizwa jina "Pori Tengefu ka Pololeti" kinyume cha sheria), lilikuwa na ukubwa wa kilometa za mraba **4000 sawa na asilimia** (29%) ya eneo lote la Wilaya linalojumuisha sehemu yote ya Tarafa ya Loliondo na sehemu ya Tarafa ya Sale ambapo ndani ya Tarafa ya Loliondo linakadiriwa kuwa na ukubwa wa kilomenta za Mraba **2216** sawa na 55.4% ya eneo lote lililomegwa na Tarafa ya Sale inachangia eneo linalokadiriwa kuwa na ukubwa wa kilometa za mraba **1784** sawa na 44.6% ya eneo lote lililomegwa.

Eneo linalodaiwa kuwa ni eneo la km za mraba 1,502 ilikuwa ni eneo la vijiji ambalo lilitengwa rasmi na jamii kwa ajili ya shughuli za ufugaji zaidi kutokana na ukweli kuwa asilimia 100% ya jamii katika eneo hili la km za mraba 4000 walikuwa wanategemea eneo hili kwa malisho , chumvi, maji ya mifugo pamoja na maeneo machache kwa ajili ya makazi na pia kwa shughuli za kiutamaduni na kimila. Eneo hili ni sehemu ya Vijiji zaidi ya 14 katika kata nane ( Arash , Oloipiri, Malambo, Piyaya, Soitsambu, Ololosokwan , Oloirien and Maaloni) zilizokuwa zinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Matumizi mseto ya ardhi (Multiple Land Use), yaliwezekana kabisa katika eneo hili kutokana na shughuli ya kiuchumi ya jamii ya kimasai (pastoralism) ambayo iliwaruhusu wao kutenga eneo hilo kwa ajili ya shughuli za kifugaji na hivyo kuwawezesha wanyamapori kama Nyumbu, pandamilia n.k. kukimbilia na kufanya mazalia yao. Mbali na eneo kubwa kubakizwa kwa ajili ya malisho, utamaduni pia wa Wamasai wa kutowinda na kutokula nyamapori uliimarisha uhusiano kati ya wanyamapori, mifugo na binadamu.

Eneo hili pia ndio limekuwa likitumika na kampuni ya Uwindaji ya watu kutoka Falme za Kiarabu (OBC) toka mwaka 1992. Migogoro katika eneo hili la km 1,502 ilianza rasmi baada ya ujio wa kampuni hii ya uwindaji katika eneo hili. Kwa muda mrefu zimekuwa zikifanyika jitihada za kuchukua eneo hili la wananchi lakini zimekuwa zikikwama kutokana na sababu mbalimbali kama ilivyoelezwa katika Taarifa ya Wananchi wa Loliondo juu ya mapendekezo ya namna ya kutumia eneo hili la km za mraba 1,502.

Eneo hili la km za mraba 1,502 lilichukuliwa rasmi kwa nguvu za dola mwaka 2022 na Serikali katika operesheni ya kuweka vigingi iliyoanza tarehe 16 June 2022 na kuhusisha vikosi mbalimbali vya usalaam. Baada ya operesheni hii Serikali moja kwa moja bila majadiliano na bila kufuata utaratibu wa sheria wa kutwaa maeneo ya vjijiji na bila kuwashirikisha wananchi ilitoa Notisi ya kutangaza hadhi mpya ya eneo hili la vijiji la kilometa za mraba 1502 kuwa ni pori tengefu jipya liitwalo "**Pololeti Game Controlled Area ( PGCA)**" na baadaye mwezi Oktoba 2022 kupandishwa hadhi na kuwa **Pori la Akiba la Pololet (Pololet Game Reserve).**

### 5.1.2 Malengo ya Ufuatiliaji Katika Eneo la Kilometa za Mraba 1,502

(a) Malengo ya jumla ya ufuatiliaji wa haki za binadamu katika eneo la kilometa za mraba 1,502, ni kuweka kumbukumbu sawa kwa matukio yote ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu yaliyotokea wakati wa operesheni ya kuweka vigingi ,

(b) Kufuatilia hali ya haki za binadamu na kasoro/makosa zilizojitokeza na zinazoendelea kujitokeza baada ya eneo la km za mraba 1,502 za vijiji 14 kuchukuliwa

(c) Pamoja na kuchukua mapendekezo ya wananchi kuhusu nini kifanyike ili kulinda Haki za Binadamu na kutatua kasoro zinazoendelea kujitokeza.

### 5.1.3 Matarajio ya Ufuatiliaji

a) Kuwepo kwa taarifa sahihi na zinazojitosheleza kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu uliotokea wakati wa zoezi la kuweka mipaka ya eneo la km za mraba 1,502

b) Kuwepo kwa taarifa sahihi kuhusu changamoto zinazoendelea kujitokeza katika maeneo yote yaliyokosa ardhi baada ya eneo la km za mraba 1,502 kuchukuliwa na kugeuzwa eneo la Pori la Akiba

c) Kuwepo kwa mapendekezo ya wananchi kuhusu nini wanataka kifanyike ili kulinda haki za Binadamu na kutatua hizi dosari/mapungufu/makosa zilizojitokeza na zinazoendelea kutokana na eneo km za mraba 1,502 kugeuzwa Pori la Akiba

d) Tunategemea baada ya kupatikana kwa taarifa hii, nafasi ya mazungumzo na majadiliano baina ya wananchi, viongozi wa kijamii na kiserikali pamoja na wadau wengine kama Asasi za Kiraia (CSOs) itapatikana ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto za hali ya haki za binadamu zilizojitokeza na zinazoendelea kujitokeza.

e) Amani , utulivu utarejea katika eneo hili baada ya kupatiakana kwa nafasi kukubali na kurekebisha makosa yaliyotokea na kufanya maridhiano kati ya wananchi na Serikali.

f) Hali ya utoaji wa huduma na miradi mbalimbali katika tarafa ya Sale na Loliondo itaimarika na kufungua milango kwa wadau wengi wa maendeleo kwenda kufanya kazi zao bila hofu yoyote.

g) Hali ya uchumi wa wananchi hasa jamii ya kifugaji katika Tarafa ya Loliondo na Sale itaimarika na hivyo kuondokana na umaskini/hali duni ya maisha iliyojitokeza kwa kuruhusiwa kutumia eneo la kilometa za mraba 1,502 kwa shughuli yao ya kiufugaji ( pastoralism) ambayo kimsingi haina athari kwa uhifadhi.

h) Wananchi kuendelea kulitumia eneo hilo kwa shuguli za ufugaji kwa utaratibu ambao utawekwa baina ya wananchi na Serikali.

### 5.1.4 Methodolojia

Katika ziara yetu tulifanikiwa kuwafikia watu zaidi ya 100 wakiwa ni wananchi wenyeji, viongozi wa jamii, watetezi wa haki za binadamu, wenyeviti wa vijiji na vitongoji, Madiwani wa kata zote nane, Viongozi wa Serikali ngazi ya wilaya (Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya) na viongozi wa Serikali Mkoa.

Tulitumia njia zifuatazo katika kukusanya taarifa: Vikao na Viongozi wa Wilaya , Vikao na jamii, vikao na viongozi wa jamii pamoja na watetezi wa haki za binadamu. Pia kupitia njia ya usahili, mahojiano kati ya makundi lengwa, kutembelea maeneo husika, uchambuzi wa nyaraka mbalimbali, mkutano na wananchi.

### 5.1.5 Eneo la ziara na muda wa ziara

Ziara hii ya ufuatiliaji ilitumia takribani siku 2 Katika kata zote nane (8) ambazo kilometa za mraba 1,502 zilizochukuliwa zilikuwa sehemu ya kata hizo katika Tarafa ya Loliondo na Sale. Ziara yetu ilijikita katika Kata 8 na vijiji 14 vilivyopoteza maeneo yao baada ya km za mraba 1500 kuchukuliwa na kisha kufanywa eneo la Pori Tengefu na baadaye kuwa eneo la Pori la Akiba la Pololeti.

### 5.1.6 Changamoto za Ziara

Changamoto kubwa katika ziara yetu ni muda ulikuwa mchache kwani watu walikuwa ni wengi sana na walitaka kufikiwa kila mmoja kwenye maeneo yao. Hali hiyo ilipelekea kushindwa kumfikia kila mwananchi. Changamoto nyingine ni kukosekana kwa ushirikiano mzuri toka kwa Mkuu wa Wilaya pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwani baada ya kuwasiliana nao na kuwatumia barua kuhitaji kukutana nao na kupata ufafanuzi hawakuwa tayari kukutana na sisi wala kujibu barua zetu za kuhitaji ufafanuzi kuhusu hoja na malalamiko ya wananchi kuhusu hali ya haki za binadamu kwenye maeneo yao.

SURA YA 5
SEHEMU YA PILI

# MCHAKATO WA KUTWAA ENEO LA KM ZA MRABA 1,502 NA KULIFANYA KUWA ENEO LA PORI LA AKIBA LA POLOLETI

### 5.2 Utanngulizi

Sehemu hii inaelezea jinsi mchakato wa kutwaa eneo la km za mraba 1,502 na kulipa hadhi ya kuwa Pori la Akiba la Pololeti. Katika tathmini hii sura hii itaangazia njia zilizotumika, sura hii pia inagusia maswala ya kisheria ya utwaaji wa ardhi za vijiji. Ukiukwaji wa haki za binadamu uliotokea wakati wa zoezi hili pia vinaelezewa kwa undani katika sura hii, maoni ya wananchi juu ya zoezi hili pamoja na hoja za Serikali.

#### 5. 2.1 Chimbuko la Nia ya Kutaka Kutenga Eneo la Kilometa za Mraba 1,502

Eneo la km za mraba 1,502 ilikuwa ni sehemu ya Pori tengefu la Loliondo na pia eneo la ardhi ya vijiji 14 vya Tarafa ya Loliondo na Sale. Pori hili kama mapori mengine ya Tanzania yalianzishwa kisheria mwaka 1951 na Serikali ya Waingereza chini ya Agizo la Hifadhi ya wanyama (The Fauna Conservation Ordinance, section 32). Kwa nchi nzima kulikuwepo na mapori Tengefu 49, Ngorongoro ikiwa na mapori manne (Endulen, Ngorongoro, Lake Natron na Loliondo) ambapo kati ya Mapori hayo, mawili (Endulen na Ngorongoro) yapo ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCA).

#### 5.2.2 Uwepo wa Vijiji Kisheria

Haya maeneo yalikuwa ndani ya ardhi za vijiji kwa kuwa sheria hazikutenganisha ardhi ya vijiji na maeneo ya mapori tengefu. Iliwezekana kuwa na vijiji pamoja na mapori tengefu kwa kuwa lengo la mapori haya yalikuwa ni kusimamia shughuli za Wanyama pori pekee katika maeneo yenye watu na sio kuchukua ardhi za vijiji. Haya maeneo yalianzishwa hasa karibu na maeneo ambayo yamehifadhiwa (protected areas) ili kulinda Wanyama na kusimamia suala la uwindaji.

Agizo la Uhifadhi wanyama la mwaka 1951 pamoja na Sheria ya wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 ilitambua uwepo wa vijiji pamoja na shughuli za kibinadamu (**Makazi**, **Kilimo**, **Ufugaji**, **Matambiko n,k**) ndani ya mapori Tengefu chini ya sheria mbalimbali ikiwemo taratibu za kimila kwa jamii zinazoishi maeneo hayo, sheria za Serikali za mitaa, na sheria za ardhi.Miaka yote eneo hili la km za mraba 1,502 limekuwa likitumiwa kwa shughuli za Wanyama, uwindaji pamoja na shughuli za kibinadamu hasa ufugaji.

Taarifa ya wananchi wa Loliondo inaonyesha kuwa kabla ya ujio wa wakoloni wa Kijerumani na baadae Waingereza jamii ya kimasai ilikuwa inamiliki na kutumia ardhi hii kwa taratibu za kimila chini ya usimamizi na uangalizi wa viongozi wa mila (Malaigwanani) kwa niaba ya jamii. Kimsingi kabla ya ujio wa wakoloni, eneo la kilometa za mraba 1,502 ilikuwa ni sehemu ndogo sana ya ardhi ya ufugaji iliyotumiwa na wamasai kabla ya kupoteza ardhi kubwa ya hifadhi ya Serengeti, Ngorongoro Creater na maeneo mengine yaliyohifadhiwa.

Hali hiyo ilipelekea kubakiwa na eneo dogo sana kwa ajili ya shughuli yao ya kiufugaji na hivyo kuamua kutumia maeneo machache yakiwemo eneo la kilometa za mraba 1,502 kwa ufugaji, ndio ikawa chanzo cha eneo hilo kubaki na uasilia na kuwezesha matumizi mseto ya ardhi kwa kuwa matumizi makubwa ya kibinadamu ni ufugaji tu. wakoloni walileta utaratibu mwingine ambao ulikuwa chini ya sheria za kikoloni hasa wakati wa Wajerumani na baadae Waingereza walipokuja na sheria ya Ardhi namba 3 ya mwaka 1923 na kufuatiwa na sheria zingine ikiwemo za Uhifadhi wa Wanyama pori. Umiliki wa ardhi kimila ulitambuliwa pia na Sheria ya Ardhi ya 1923 na iliyofanyiwa marekebisho 1928, ili kutambua zaidi haki za wenyeji.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1923 katika kifungu cha 9, ilitoa mamlaka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Maendeleo ya Ardhi kutoa hati za kumiliki ardhi za Vijiji. Baada ya mabadiliko ya sheria za Ardhi za Tanzania hasa mwaka 1999, Sheria Mpya ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 illibainisha kuwa, kutakuwa na vyeti vya ardhi vya Vijiji tofauti na hati za kumiliki ardhi zilizotolewa kwa Vijiji kwa mujibu wa Sheria ya ardhi ya mwaka 1923.Vilevile Sheria hizo mpya za ardhi zimeendelea kutambua hati hizo ambazo zilitolewa kwa Mujibu wa Sheria zingine kabla ya kutungwa kwa Sheria hiyo.

### 5.2.3 Vichocheo vilivyo Pelekea Kutwaliwa kwa Eneo la Kilometa za Mraba 1,502

Nia ya kutaka kuchukua eneo la kilometa za mraba 1,502 na kuondoa kabisa katika ardhi ya vijiji ilishamiri zaidi kuanzia mwaka wa 1990 na kuendelea kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo zaidi sababu za uwekezaji. Sura hii ndogo inamwelezea msomaji wa taarifa hii historia na vichocheo vilivyopelekea ardhi ya vijiji yenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa.

#### (a) Kugawa Eneo la Vijiji kwa OBC bila Kufuata Utaratibu

Kwa mujibu wa wananchi na wazee wa Loliondo pamoja na taarifa mbalimbali za kijamii na ripoti mbalimbali za Serikali kuwa nia ya kutaka kuchukua hili eneo la kilometa za mraba 1,502 ilianza kushamiri zaidi kuanzia mwaka 1992 baada ya eneo la vijiji kupewa kampuni ya Ortello Business Corporation ya Umoja wa Falme za Emirati kama kitalu cha uwindaji. Mwaka 1992 Serikali ya Tanzania ilimilikisha kwa mkataba usio na ukomo, kitalu cha uwindaji eneo lote la pori Tengefu la Loliondo (km.sq 4000) kwa Kampuni ya Uwindaji ya Ortello Business Corporation (OBC) inayomilikiwa na Mfalme za Kiarabu. Tangu hapo, kumekuwa na mgogoro usioisha kati ya jamii ya eneo la Loliondo, Serikali na mwekezji (OBC) ikichangiwa zaidi na mahusiano hafifu kati ya jamii na kampuni ya OBC.

Ripoti ya Rushwa ya Tume ya Rais Juu ya Masuala ya Rushwa Tanzania ya Mwaka 1996, maarufu kama Tume ya Warioba ilibainisha kuwa ugawaji wa eneo la vijiji vya Loliondo kwenda kampuni ya watawala wa Falme za Emirati uligubikwa na rushwa. Ukurasa wa 281 na 282 katika aya 706 (k) ya Ripoti ya Warioba ilieleza kuwa;

*"Baadhi ya viongozi wa juu wamekuwa wakijuhusisha na ugawaji wa vitalu vya uwindaji kwa manufaa yao binafsi. Wamekuwa wakihadaa watu katika maeneo haya kuingia katika mikataba ya kilaghai na makampuni ya uwindaji kwa manufaa binafsi yao binafsi. Ripoti ya Kamati ya Bunge juu ya tuhuma isiyo ya kimaadili zinazohusishwa idara ya Wanyamapori imeelezea tatizo hili vizuri sana, hasa eneo la Loliondo ambalo amegawiwa Ortello Business Corporation (T) Limited."(Tafsiri yetu).*

Sehemu ya Ripoti ya Warioba pia imeeleza katika ukurasa wa 284 aya ya 716 mambo yafuatayo:

*"...Vilevile, waziri wa kipindi kile wa Maliasili na Utalii, Mh. Dkt. J. Ngasongwa alitoa leseni kwa niaba ya Rais (Presidential License) kwa watu wasio stahili kama ifuatayo:*

(a) Brigedia Mohamed Abdulrahim Al-Ali, ambaye ni Waziri Msaidizi katika Umoja wa Falme za Kiara Emirati alipewa leseni No: B 00158 na B 00159 ambayo bado inatumika. Anamiliki eneo la uwindaji la Loliondo. Ambapo kwa mujibu wa taratibu za utoaji wa leseni ya Rais hastahili leseni hiyo kwa sababu anaweza kutumia kukodisha wawindaji wengine kufanya shughuli zao katika eneo lake kwa fedha za kigeni bila ya Serikali kupata mapato. Aliruhusiwa kuwinda nyati mmoja na kware thelathini. ( Tafsiri yetu)

(b) Mtukufu Sheikh Maktoum bin Rashid Al Maktoum, Naibu Waziri Mkuu wa Umoja wa Falme za Kiarabu alipewa leseni No.: B 0039 na B 00397 aliruhusiwa kuwinda pofu moja, nyati moja na kware hamsini. (Tafsiri yetu).

Taarifa ya Tume ya Warioba imethibitishwa pia na aliyekuwa waziri wa Maliasili na Utalii Dk. Hamisi Kigwangalla kuwa mgogoro wa Loliondo umechangiwa kwa uwepo wa kampuni ya uwindaji ya OBC. Waziri Kigwangalla aliwahi pia kunukuliwa akikiri kuwa, OBC iliwahi kutaka kumhonga na kutamka kuwa mwekezaji huyo hatapewa tena leseni ya uwindaji.[20]

---

20 "OBC ipo nyuma ya vurugu hizi, siku zao zinahesabika, hawatapewa leseni mpya ya uwindaji Januari mwakani," alisema Waziri Kigwangala Oktoba 29, 2017 https://mtanzania.co.tz/kigwangala-siku-za-kampuni-ya-obc-zinahesabika/

Tangu eneo la Loliondo lipewe kampuni ya Emirati kumekuwa na mgogoro usiokwisha ambalo pia limeghubikwa na ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya wananchi wenyeji wa maeneo haya. Kampuni ya OBC imejenga miundombinu za kudumu kama majengo na kiwanja cha ndege kikubwa eneo la Lima.

### (b) Nia ya Kuweka Eneo la Kilometa Mraba 1,502 chini ya Usimamizi wa NCAA

Katika ziara yetu katika tarafa za Loliondo na Sale wananchi walitueleza kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) imeshirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama katika operesheni iliyofanyika Loliondo Mwezi June 2022. Wananchi pia walitueleza kuwa NCAA ndio imekuwa ikikamata mifugo ndani ya eneo la kilometa za mraba 1,502 na kutoza faini ya laki moja kwa ng'ombe.

katika uchambuzi wetu juu ya nyaraka mbalimbali, tumebaini pia kuwa katika Ripoti yake juu ya Ardhi Mseto (Multiple Land Use Report ) ya Mwaka 2019, Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro imependekeza kuwa eneo la kilometa za Mraba 1,502 la Loliondo na Sale pamoja na Ngarasero kuwekwa chini ya usimamizi wa NCAA.

Tumebaini pia kuwa mnamo 28/09/2022, aliyekuwa waziri wa Mali Asili na Utalii Pindi Chana alitangaza kuwa eneo la Kilometa za Mraba 1,502 iliyotwaliwa itawekwa chini ya NCAA.

vilevile katika ziara yetu tumebaini kuwa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imekuwa ikikamata mifugo ya wananchi na kuachia baada ya kutoza faini kubwa ya laki moja kwa ng'ombe na elfu ishirini na tano kwa kondoo/mbuzi. Hii pia inadhibitishwa na Kesi ya **Raphael Kesoi na Mwenzake V. NCAA na Wenzake 3, Rufaa No. 9 ya 2023** katika Mahakama Kuu kanda ya Arusha. Katika kesi hii, warufani miongoni mwa mambo mengine wanapinga yafuatayo:

a) Faini ya Shilingi laki moja kwa Ng'ombe na 25000 kwa kondoo ni kinyume cha sheria.
b) Kwamba,NCAA haina mamlaka kisheria ya kufanya shughuli zake katika mapori tengefu na mapori ya akiba kwani ni Mamlaka yaliyowekwa na sheria chini ya TAWA.

Ikumbukwe pia, kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro,Sura 284 inaeleza bayana kuwa maeneo ya kiutawala ya NCAA ni ndani ya hifadhi ya Ngorongoro peke yake. Ni kweli pia kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 8 cha Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori, Sura 283 inaeleza wazi kuwa maeneo ya Mapori Tengefu na Mapori ya Akiba yatakuwa chini ya TAWA.

Hii ndio kusema kuwa kitendo cha kuweka eneo la kilometa za Mraba 1502 chini ya NCAA ni kinyume cha Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro na Pia Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori.

#### (c) Shinikizo Kutoka kwa Wadau wa Uhifadhi (Conservation Lobbying Groups)

Sababu nyingine iliyoelezwa na wananchi kuwa chanzo cha utwaaji wa ardhi ya vijiji yenye kilometa za Mraba 1,502 ni shinikizo kutoka kwa wadau wa uhifadhi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali, OBC, NCAA kushinikiza kushawishi wananchi kukubali eneo hilo kutengwa.

Mfano, wananchi walitueleza kuwa baada ya kutwaliwa kwa eneo la vijiji lenye kilometa za mraba 1502 bila kufuata utaratibu kumekuwa na juhudi nyingi za kuhalalisha kilicho fanyika kwa kuleta Mpango wa Matumizi Bora wa Ardhi usiyojumuisha eneo lililotwaliwa. Mpango huu unafadhiliwa na Frankfurt Zoological Society (FZS)

Kwa maana nyingine ndio kusema kuwa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kama njia ya kuhalalisha ardhi iliyotwaliwa bila kufuata utaratibu. Wadau wa uhifadhi kama FZS wanadaiwa na wananchi kuwa nyuma ya utwaaji wa Ardhi. Taasisi hii ya Kijerumani imeonekana kuwa sehemu ya changamoto ambazo zinaendelea kuwakumbuka wananchi wa Ngorongoro kwa sasa kutokana na ukweli kuwa taasisi hii imekuwa ikifadhili mipango mingi iliyoshiriki kudhulumu ardhi ya wananchi.

### 5.2.4 Kubadilishwa kwa Sheria ya Wanyamapori Mwaka 2009

Baada ya njia zingine kushindwa kutimiza hadhma ya kutwaa eneo hili la km za mraba 1,502, mwaka 2009 Sheria ya Wanyamapori No.05 ilitungwa na kubadilisha hadhi ya mapori tengefu Tanzania kwa kutenganisha vijiji na maeneo ya mapori tengefu. Sheria hii mpya imekataza shughuli za kibinadamu (Makazi, Kilimo, Ufugaji na Matambiko) kufanyika ndani ya mapori Tengefu kwa msisitizo kwamba hakuna ardhi ya kijiji itakayokuwa ndani ya mapori Tengefu.

Sheria hii haikurithi moja kwa moja mapori haya badala yake, sheria ilimtaka Waziri mwenye dhamana kupitia upya mapori Tengefu yote nchi nzima ndani ya miezi 12, kwa lengo la kubaini mapori Tengefu yenye sifa ya kuendelea kuwa maeneo ya Hifadhi (GCAs) na kuyatangaza, na yale ambayo hayatakuwa na sifa kupendekezwa kufutwa na Serikali.[21] Zoezi hili halikufanyika kwa wakati na kufanya maeneo yote ya Loliondo kutokuwa na hadhi ya kisheria tena kuendelea kuitwa ni mapori tengefu kwa kuwa sheria ya sasa haitambui uwepo mapori tengefu kwenye ardhi ya vijiji. Sheria hii hii ilikuja kutumika mwaka 2022 pasipo kuzingatia taratibu zilizoainishwa kisheria za kubadilisha ardhi yenye matumizi ya vijiji kuwa pori tengefu kwa mujibu ya sheria ya sasa ya wanyama pori.

### 5.2.5 Kukiukwa kwa Makubaliano ya Mwaka 1958

Eneo hili la Loliondo na Sale hadi eneo la Ngorongoro lilijumuisha eneo la sasa la Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Lakini kuanzia mwaka 1950 Serikali ya wakoloni wa Waingereza walianza majadiliano na wananchi ya kuhifadhi eneo la sasa la Hifadhi

---

21 Ripoti Ya Mapendekezo Ya Wananchi Juu Ya Utatuzi Wa Mgogoro Wa Ardhi Tarafa Za Loliondo Na Sale Wilaya Ya Ngorongoro Arusha (2022)

ya Serengeti na hivyo kukubaliana na wananchi wahamie maeneo ya Loliondo na Ngorongoro. Wananchi waliridhia japo sio kwa uhuru uliopaswa , kuachia eneo hilo na kuja maeneo ya Ngorongoro na Loliondo kuungana na wenzao waliokuwemo katika maeneo hayo.

Mwaka 1958 makubaliano yalifikiwa baada ya mazungumzo ya miaka zaidi ya 8 kwa Jamii ya wamasai kukubaliana na kuridhia mipaka na maslahi mengine kupitia "Serengeti Compensation Scheme". Mwaka mmoja baada ya makubaliano kufikiwa Hifadhi ya Serengeti ilianzishwa rasmi mwaka 1959, sambamba na Hifadhi ya Ngorongoro (1959) ambako Serikali ya kikoloni ilikubaliana na wananchi kuwa na hifadhi yenye matumizi mseto ya ardhi (wanyamapori, shughuli za binadamu, na utalii).

Katika makubalino hayo moja ya masharti ya wananchi yalikuwa ni kuwepo na kifungu cha kuwa hawatahamishwa tena katika maeneo ya sasa na pia ikitokokea mgongano wowote kati ya maliasili na wananchi basi haki za wananchi zitapewa kipaumbele.

"**Kwanza**, tuliaihidiwa kupewa huduma za mifugo kama majosho, maji, na huduma zingine za kijamii. ***Pili, tuliahidiwa kuwa huko tuendako upande wa mashariki mwa Serengeti (Loliondo) endapo patatokea mgogoro baina ya Wamasai na shughuli za uhifadhi, haki zetu zitapewa kipaumbele zaidi***. Baada ya sisi kuhamishwa baadhi ya ahadi hizo hazikutekelezwa na Serikali hiyo ya Kikoloni lakini na zingine kwa sasa haziheshimiwi na Serikali ya sasa." [22]

Kutokuheshimiwa na kutotambuliwa kwa makubaliano haya ndiyo yamesababisha eneo hili la kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa bila ridhaa ya wananchi mwaka 2022. Hali hii imechangia jamii ya Kimasai kuendelea kufukuzwa katika maeneo yao ya asili kwa lengo la uwekezaji na uwindaji.

### 5.2.6 Utaratibu Uliotumika Kutwaa Ardhi ya Vijiji `( Kilomita za Mraba 1,502)

Sehemu hii inafafanua kwa undani njia zilizotumika kumega eneo la kilometa za mraba 1,502. Tathmini ya taarifa hii imechambua pia sheria zinazohusika na njia zinazotakiwa kutumika kisheria kutwaa ardhi ya vijiji. Njia zilizotumika katika utwaaji wa eneo hili ni pamoja na zoezi la kuweka vigingi, operesheni ya vikosi vya usalama, ukamataji wa viongozi wa jamii, propaganda kupitia baadhi ya vyombo vya habari na baadaye kutangaza kwa eneo kupitia Notisi ya Serikali. Njia zilizotumika ni kama ifuatavyo.

---

22 Ripoti Ya Mapendekezo Ya Wananchi Juu Ya Utatuzi Wa Mgogoro Wa Ardhi Tarafa Za Loliondo Na Sale Wilaya Ya Ngorongoro Arusha (2022)

### (a)Kauli Mbalimbali za Viongozi wa Serikali

#### i). Kauli kabla ya uwekaji wa vigingi

Mnamo Tarehe 11 Januari 2022, Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella alinukuliwa akiwaeleza wa viongozi wanaotoka katika vijiji 14 vilivyopo ndani ya eneo la kilometa za mraba 1,502 kuwa eneo hilo litamegwa kwa maslahi mapana ya taifa.

Kauli ya Mkuu wa Mkoa imepingwa na wananchi kwa kufanya maandamano katika kata ya Oloirien tarehe 13 na 14 Januari 2022.

Mnamo Tarehe 14 Februari 2022, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitembelea Loliondo Loliondo na kujaribu kutuliza hali baada kauli za bungeni ambazo zimetafsiriwa kulenga jamii ya Maasai na tamaduni zao. Hata hivyo, alipotembelea 17/02/2022 akiwa katika hifadhi ya Ngorongoro Waziri mkuu Kassim Majaliwa alisema eneo la Loliondo lenye Kilometa za Mraba 1500 itaweka alama ili kulinda maji na mazallia ya wanyama.Hii pia imerudiwa na aliyekuwa waziri wa Mali Asili na Utalii Damas Ndumbaro alipohojiwa na DW Kiswahili tarehe on 08/03/2022.

Mnamo tarehe 03.06.2022, Waziri wa Mali Asili na Utalii Pindi Chana alieleza kwenye hotuba yake bungeni kusudio la Serikali la kupandisha hadhi mapori tengefu kadhaa ikiwemo Loliondo kuwa Mapori ya Akiba..

Mnamo tarehe 6,7 na 8 vikosi mbalimbali vya usalama zilionekana katika maeneo mbalimbali za Loliondo ambacho wananchi wanadai kuwa sio kawaida kwani haikuwa ni polisi peke bali na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. Wananchi walieleza pia kuwa wameshangaa kuona msafara wa kijeshi katika maeneo yao kwasababu hakukuwa na uvunjivu wowote wa amani wala shida yoyote ya kiusalama.

Baada ya taharuki hiyo wanachi walienda kumlililia Mungu katika eneo la Kirtalo ili awaokoe katika jambo ambalo hawakufahamu litaishia wapi. Mnamo tarehe 09.06.2022 viongozi wote wanawakilisha vijiji 14 ambavyo zipo ndani ya eneo la kilometa za mraba 1502 waliitwa na Mkuu wa Wilaya na hawakurudi tena nyumbani na kutoweka kwa siku saba.

#### ii.) Kauli za viongozi baada ya kuwekwa vigingi

Wananchi walitueleza kuwa mnamo tarehe 10.06.2022 kulikuwa na matumizi makubwa ya nguvu kutoka kwa vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo vimehusisha uwekaji wa vigingi na ushambuliaji wa wananchi. Mnamo tarehe 10.06.2022 alivyoulizwa bungeni kuelezea kinachoendelea Loliondo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alinukuliwa akisema yafauatayo:

> *"Kilichotokea si uhalisia, hakuna tishio lolote, wale wameenda msituni kuweka alama katika eneo ambalo liko mbali sana kijiji cha karibu kipo umbali wa kilomita nane, wananchi waendelee na shughuli zao,*

*wasisikilize upotoshaji unaofanywa na baadhi ya watu wasiopenda maendeleo ya nchi hii, hakuna mapambano yoyote, hakuna askari yeyote aliyekwenda huko kijijini  kutishia amani."* ***Kauli ya Waziri Mkuu  Majaliwa Kasimu Juni 10 2022 Bungeni Dodoma.***

Mnamo tarehe 11.06.2022 Mkuu wa Mkoa wa Arusha alieleza kuwa askari moja ameuwawa katika zoezi la uwekwaji wa vigingi ulioleta mvutano kati ya askari na wananchi. Tarehe 13.06.2022 Inspekta Mkuu wa Polisi, Simo Sirro alifika Loliondo na kuwaonya watu wote ambao wanapinga zoezi la uwekaji wa vigingi.

Tarehe 15.06. 2022, Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni,alifika Loliondo na kurudia maneno yaliyo semwa na Simon Sirro na kuamuru mashirika yanayo jihusisha na utetezi wa haki za binadamu katika maeneo hayo kufuatiliwa mienendo yao na uraia wa wamiliki wa mashirika hayo.

Ni muhumu pia kuzingatia katika hatua hii kuwa maswala yote haya yamefanyika bila kuwa na Tangazo la Serikali na hivyo kwa tafsiri ya kisheria ni kuwa operesheni ya kuweka vigingi, kukamata  wananchi ilifanywa bila taratibu za kisheria.

Mnamo tarehe 22.06.2023 Kamishna wa Uhamiaji  aliamuru kufanyika kwa operesheni ya siku 10 na kuwakamata waliodaiwa kuwa ni wahamiaji haramu ambao ndio wanakwamisha zoezi la uwelkwaji wa vigingi. Hii ilipelekea wananchi zaidi ya 100 kukamatwa na 62 kati yao walifikishwa mahakamani kwa madai kuwa sio watanzania. Wananchi hao hata hivyo walikuja kuachiwa baada ya kukosekana kwa ushahidi.

### (b) Propaganda kwenye baadhi ya  vyombo vya Habari

Wakati wa ziara yetu, wananchi walieleza kwamba baadhi ya vyombo vya habari vilitumika kueneza propaganda ikiwa ni pamoja na baadhi ya watu wenye ushawishi mitandaoni ambao pia walitumika kueneza hizo propaganda kwa lengo la kuhakikisha kuwa ardhi ya wananchi inatwaliwa na pia kusababisha taharuki kubwa kwa wananchi. Propaganda hizo zilipelekea kuwepo kwa viashiria vya ubaguzi, uwepo wa taarifa za uongo kutoka kwa vyombo hivyo vya habari na baadhi ya watu maarufu, taarifa za uongo  kama vile, 'Loliondo yametimia' Asasi za kiraia kupewa hela loliondo' 'Wamasai hawazikani' (Balile na Maulid Kitenge, 'Wamasai wameenda kuandamana ubalozi wa kenya'' baadhi ya vyombo hivyo vya habari ni kama vile; Jamvi la habari, Jamhuri media na ITV.

Nukuu kutoka kwa Christopher Ole Sendeka (Mbunge wa Simanjiro),  Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba ninukuu maneno haya ya gazeti la Jamhuri la tarehe 1 mpaka 7 Februari 2022, linasema hivi: "Loliondo na Ngorongoro kwa ujumla wake ni za Watanzania. Hivyo sote tuna wajibu wa kuona ikiendelea kuwepo ili iwe na manufaa kwa Watanzania na walimwengu wote. Haiwezekani kabila moja katika nchi likatae kutii mipango ya Serikali hasa ikizingatiwa kuwa kinachofanywa na dola kina manufaa makubwa kwa Umma na kwa nchi." (Narudia), "haiwezekani kabila moja likatae kutii." Mwisho wa kunukuu.

### (c) Vitisho dhidi ya Viongozi wa kijamii na Wananchi na Kuwekwa Ndani kwa Viongozi wa Jamii

Kabla ya ardhi kutwaliwa, baadhi ya viongozi na watetezi wa haki za binadamu walitishwa na wengine kukamatwa hasa waliokuwa wanapinga kutwaliwa kwa ardhi yao kinyume na utaratibu wa kisheria. Pia kauli za viongozi wa Serikali zilipingwa na wananchi katika kata ya Arash tarahe 19 Machi 2022 na kupelekea diwani wa kata ya Arash kuitwa kituo cha Polisi, kuwekwa ndani kwa siku kadhaa na baadae kuachiwa kwa masharti ya kuripoti kituoni mara kwa mara. Lakini pia diwani wa kata ya Malambo aliitwa mara kadhaa kwenye kituo cha Polisi kutokana na msimamo wake wa kupinga ardhi yao kutwaliwa kinyume cha Sheria.

Vilevile Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Ndirango Tajewo Olesenge aliitwa katika ofisi za uhamiaji tarehe 14 Aprili 2022 kwaajili ya mahojiano kuhusu uraia wake. Mnamo Juni 07, 2023 wananchi wa Loliondo waliona vitisho vya vikosi vya askari vikizunguka maeneo yao hadi tarehe 08 Juni ambapo askari hao waliweka kambi katika maeneo mbalimbali. Tarehe 09 Juni, 2023 askari hao walianza kuweka zoezi la vigingi kwenye eneo la kilometa za mraba 1,502.

Baada ya zoezi hilo kuanza, baraza la madiwani liliitisha kikao siku hiyo ya tarehe 09 Juni 2023 na wakati kikao kinaendelea, Mkwenyekiti wa Kikao hicho alipokea ujumbe kwenye simu yake kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ukiwa na orodha ya majina ya baadhi ya madiwani amabo walikuwa wanatakiwa kwenda kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Kwa vile walioitwa ni madiwani wenzao waliamua kusindikizana kwenda kwa Mkuu wa Wilaya na baada ya kufika waliambiwa kuwa wanahitajika kwenye kikao cha kamati ya ulinzi na usalama. Baada ya kuingia kwenye kikao hicho, walihojiwa kuhusu kikao walichokuwa wanafanya kabla ya kuitwa, baadhi ya maswali waliyoulizwa ni; mlikuwa mnapanga nini? kupinga kuhusu oparesheni na eneo kutwaliwa?

Viongozi hao waliendelea kuwepo kwenye kikao bila mwelekeo na baadae Katibu Tawala wa Wilaya aliwaambia wasiondoke kuna watu wanataka kuongea nao. Muda mrefu haukupita askari wengi waliingia na kuwaamuru kuwa wapo chini ya ulinzi na kuingizwa katika chumba maalumu. Simu zao zote walinyang'anywa. Ilipofika majira ya saa saba usiku, viongozi hao walisafirushwa hadi kituo cha Polisi Chekereni, Arusha mjini ambapo walifika majira ya saa 06:00 asubuhi.

Viongozi hao baadae walipewa taarifa za kifo cha askari aliyedaiwa kuuwawa kwa kupigwa mshale Juni 11, 2022. Viongozi hao waliendelea kukaa kwenye kituo hicho hadi Juni 16, 2022 ambapo walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha na kufunguliwa kesi ya mauaji ya askari aliyedaiwa kuuwawa tarehe 11 Juni 2022.

### d) Matumizi makubwa ya nguvu ya vyombo vya dola dhidi ya raia

Wakati wa zoezi la uwekaji wa vigingi ,vyombo vya dola vilitumia nguvu ikiwemo mabomu,risasi za moto dhidi ya raia ambao walikusanyika kupinga kutwaliwa ardhi yao.Katika matumizi hayo wananchi walitueleza mkwamba wananchi walipigwa

risasi,mzee Oriasi Oleng'iyo wa mkazi wa kijiji cha Ololosokwan alipotea na pia kwenye kijiji cha Piyaya kuna mtoto alipotea na mpaka leo hajaonekana na pia baadhi ya vifo viliripotiwa katika kijiji cha Piyaya ambapo mtoto alifariki baada ya kuangukiwa na wanawake waliokuwa wanakimbia kuingia ndani na kumwangukia mtoto na pia kijiji cha Malambo.

kuna mtu moja alikanyagwa na magari ya oparesheni. Wanawake wamelalamika kwamba kuna wenzao ambao mimba zao ziliharibika kutokana hofu ya milio ya bunduki na mabomu na pia kuna taarifa kwamba baadhi ya wanawake walibakwa

**e) Uwekaji wa vigingi**

Zoezi la awali kabisa ni zoezi la uwekaji mipaka (vigingi ) kwenye eneo hili la kilometa za mraba 1,502. Zoezi hili hapo awali kwa mujibu wa Waziri mkuu lilikuwa ni zoezi la kubaini mipaka ya eneo la kilometa za mraba 1,502 pekee na sio kuchukua eneo hilo. ( Hakuna kijiji kinaondolewa, hakuna mwananchi anaondolewa - kauli ya Waziri Mkuu Majaliwa Majaliwa Bungeni Dodoma. Zoezi hili lilianza bila ushirikishwaji wowote wa wananchi. Zoezi hili liliendeshwa na vyombo vya usalama likijumuisha askari kutoka majeshi mbalimbali hapa nchini.

Oparesheni hii iliendeshwa kwa matumizi makubwa ya mabomu na silaha za moto zilikuwa zinapigwa angani kwa mujibu wa wananchi waliohojiwa. Magari mengi ya askari pamoja na askari wengi walitanda pembezoni mwa vijiji vinavyopakana kwa sasa na eneo hili la kilometa za mraba 1,502. Vigingi viliwekwa kuanzia kata ya Ololosokwan hadi kumalizia katika kitongoji cha Sanjan kata ya Malambo. Utaratibu huu ndio uliotumika kutenga eneo la kilometa za mraba 1,502.
Mnamo Juni 10,2022 Serikali ilianza rasmi zoezi la uwekaji wa vigingi kwenye eneo la ardhi ya Vijiji 14 Tarafa ya Loliondo na sehemu ya Tarafa ya Sale katika kata ya Piyaya na Mlambo,zoezi ambalo lilisimamiwa na vyombo vya dola chini ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella**.** Zoezi hilo lilikamilishwa tarehe 23 Juni,2022 kwa kuwekwa jumla ya vigingi 424.[23]

**f) Upimaji upya wa eneo la vijiji**

Hatua zingine ziliendelea kuchochea nia ya kutaka kuchukua hili eneo la km za mraba 1,502 ni pamoja na mipango mbalimbali ya matumizi ya ardhi ya Wilaya iliyokuwa na ajenda ya kuhakikisha eneo la km za mraba 1,502 zinatolewa katika ardhi ya vijiji. Mfano mpango wa kwanza wa mwaka 1993-2008 (Ngorongoro District Land Use Framework Plan (1993 – 2008) ilitayarishwa kwa msaada wa OBC na kuanisha eneo (linalokadiriwa sasa kuwa ni km za mraba 1,502) kuwa eneo linalopaswa kutumika kwa madhumuni ya Uhifadhi wa wanyama pori na utalii pekee.

Mpango huu pmaoja na mingine iliyofuata mara zote kumekuwa na nia ya kutaka kuchukua eneo hili kwa kisingizio kuwa ni kulinda ikolojia, mazalia ya nyumbu pamoja na mapitio ya wanyama. Mfano **Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Wilaya ya mwaka 2010-2030** ilikuwa na mkakati ule ule wa kutaka kumega eneo hili, Mipango yote hii

23 https://www.pmo.go.tz/news/waziri-mkuu-akagua-zoezi-la-uwekaji-alama-loliondo-apongeza

imekuwa ikishawishiwa zaidi na kampuni ya OBC na pia baadaye uwepo wa Shirika La Kijerumani Frankfurt Zoological Society. Hatua zote hizi zimekuwa zikpingwa na wananchi kupita baraza lao la madiwani.

### g) Kutangazwa kwa Pori Tengefu la Pololeti na baadaye kuwa Pori la Akiba la Pololeti

Kwa mujibu wa Sheria ya Wanyama Pori ya Mwaka 2009, zoezi lolote la kutaka kutangaza Pori Tengefu toka kwenye ardhi ya vijiji ni sharti masharti yote ya msingi yazingatiwe na moja ya takwa la kisheria ni Waziri mwenye dhamana kufanya mashauriano na Serikali mitaa mahalia jambo ambalo halikuzingatiwa wakati wa utwaaji wa ardhi ya vijiji na kufanywa kuwa Poei Tengefu na baadaye kuwa Pori la Akiba la Pololeti. Eneo la km za mraba 1,502 ilikuwa ni sehemu ya vjiji vilivyosajiliwa na vingine vyenye hati ya umiliki ardhi.

Kwa maelezo ya awali ya Waziri Mkuu , zoezi la uwekaji vigingi haikuwa ndio zoezi la kuchukua eneo moja kwa moja , alisisitiza kuwa mara baada ya kuweka vigingi kutakuwa na vikao shirikishi na jamii kujadili kuhusu hatma ya eneo hilo , lakini sicho kilichofanyika. Eneo hili lilitangazwa kuwa pori tengefu maramoja baada ya kumalizika kwa zoezi la uwekaji vigingi bila kuzitatia taratibu za kisheria za kutwaa maeneo ya vijiji.

### h) Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi

Hatua zingine ziliendelea kuchochea nia ya kutaka kuchukua hili eneo la km za mraba 1,502 ni pamoja na mipango mbalimbali ya matumizi ya ardhi ya Wilaya iliyokuwa na ajenda ya kuhakikisha eneo la km za mraba 1,502 zinatolewa katika ardhi ya vijiji. Mfano mpango wa kwanza wa mwaka 1993-2008 (Ngorongoro District Land Use Framework Plan (1993 – 2008) ilitayarishwa kwa msaada wa OBC na kuanisha eneo (linalokadiriwa sasa kuwa ni km za mraba 1,502) kuwa eneo linalopaswa kutumika kwa madhumuni ya Uhifadhi wa wanyama pori na utalii pekee. Mpango huu pmaoja na mingine iliyofuata mara zote kumekuwa na nia ya kutaka kuchukua eneo hili kwa kisingizio kuwa ni kulinda ikolojia, mazalia ya nyumbu pamoja na mapitio ya wanyama.

Mfano **Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Wilaya ya mwaka 2010-2030** ilikuwa tena na mkakati ule ule wa kutaka kumega eneo hili, Mipango yote hii imekuwa ikishawishiwa zaidi na kampuni ya OBC na pia baadaye uwepo wa Shirika La Kijerumani Frankfurt Zoological Society. Hatua zote hizi zimekuwa zikpingwa na wananchi kupita baraza lao la madiwani.

### 5.2.7 Changamoto za Zoezi la Uwekaji Mipaka

Sehemu hii inaelezea kwa ufupi ukiukwaji wa haki za binadamu uliojitekeza wakati wa zoezi la uwekaji mipaka katika eneo la km za mraba 1,502. Changamoto hizi ni pamoja na matukio mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria na uvunjifu wa haki za binadamu kama watu kupigwa, kuchomewa nyumba,kubomolewa makazi,uharibifu wa mali,mauaji,watu kupotea.

**a) Utwaaji wa eneo la Km 1502 halikuwa zoezi shirikishi**

Kwa mujibu wa matokeo ya ufuatiliaji huu , zoezi hili la kumega eneo la km za mraba 1502 halikuwa shirikishi na kwa maana hiyo halikuwa na ridhaa ya wananchi wala viongozi wao. Taratibu za utawala bora na pamoja na taratibu za utawala wa sheria unalazimisha zoezi lolote linalogusa maeneo yanayotumiwa na wananchi kihalali kuwe na mchakato shirikishi na kisheria katika kufanya maamuzi yoyote.

Katija jamii zipo ngazi za utawala kama Serikali za vijiji, Serikali za kata pamoja na baraza la madiwani lakini vyombo vyote hivi vya kijamii havijawahi kukaa na kuridhia zoezi hili. Hakuna kumbukumbu zozote kwa ngazi ya wilaya au vijji zinazoonyesha kuwa vjiji husika na eneo hili vilihusishwa kikamilifu katika zoezi hili.

Mchakato ambao ulikuwa ni jitahada ya jamii kutafuta nafasi ya ushirikishwaji kabla ya zoezi hili kufanyika ni zoezi la taarifa ya mapendekezo ya jamii iliyoandaliwa na kamati ya jamii. Wanannchi kupitia kamati yao , walifanikiwa kuwasilisha mapendekezo yao kwa jamii May 17 Mwaka 2022 lakini mapendekezo haya hayakufanyiwa kazi badala yake wiki tatu badaye wananchi waliona magari ya vikosi mbalimbali vya usalama vikingia Loliondo tayari kwa zoezi la kutoa eneo hilo bila maelezo yoyote kuhusu hatma ya mapendekezo ya jamii.

Wananchi zaidi ya 7000 waliweza kushiriki kutoa maoni na mapendekezo kwenye taarifa yao hii kwa njia mbalimbali. Wananchi walitumia Kamati maalumu ya jamii kutoka katika kata 8 iliyoundwa na wananchi kwa kuongozwa na Mh. Mbunge wa Wilaya Ngorongoro na Mwenyekiti wa CCM Wilaya kwa lengo la kuandaa mapendekezo ya utatuzi wa mgogoro huu wa ardhi katika eneo la Kilomita za mraba 1,502. Kamati hii iliundwa na wajumbe zaidi ya 40 kutoka katika kata zote 8 wakiwemo Madiwani, viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Ngorongoro, wenyeviti wa vijiji, viongozi wa mila, wawakilishi wa Wanawake, vijana na wataalamu wa jamii kwa lengo la kuratibu mapendekezo ya wananchi.




***Picha 5.1:*** *Sehemu ya Wajumbe wa Kamati ya Wananchi kutoka Tarafa za Loliondo na Sale wakiwa katika Mapitio ya rasimu ya Kwanza ya Taarifa.*



***Picha 5.2:*** *Sehemu ya Wananchi kutoka tarafa ya Loliondo na Sale katika Kikao cha pamoja kujadili mgogoro wa Ardhi*

Wawananchi kupitia kamati yao walitumia mikutano ya jamii, mikutano ya kimila iliyowakutanisha makundi yote ya jami kutoa maoni. Jedwali lifuatalo kutoka katika taarifa ya wananchi wa Loliondo and Sale ikionyesha jinsi wananchi walivyokuwa tayari kutoa maoni yao na pia kuwa tayari kujadiliana kuhusu eneo hili.

***Jedwali 5.1 : Orodha ya mikutano ya ukusanyaji wa tarafa ya Loliondo na Sale***

| Na | Eneo | Tarehe | Aina ya Mkutano | Idadi ya watu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kijiji cha Ormanie | 29 Machi 2022<br>2 Aprili, 2022 | kupitia maresho toka kamati ya mapendekezo ya Arusha | 545<br>707 |
| 2. | Kijiji Piyaya | 15 Feb, 2022<br>7 Aprili, 2022<br>19 Aprili, 2022 | Majadiliano ya mgogoro wa ardhi (1500 sqkm)<br>Kupokea mrejesho wa kikao cha Arusha<br>Ms TCDC, Kikao cha kujumuisha mapendekezo ya jamii | 295 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Kijiji cha Arash | 15 Januari, 2022,<br><br>5 Februari, 2022<br><br>26 Februari, 2022<br><br>5 Marchi, 2022<br><br>19 Machi, 2022 | Majadiliano na kutoa mapendekezo juu ya mapendekezo ya mgogoro wa km 1500 | 1516 |
| 4. | MS-TCDC-Arusha | 3-4 Aprili, 2022 | Mapitio ya rasimu ya Kwanza ya Taarifa | 60 |
| 5. | Lush Garden -Arusha | 24 Aprili, 2022 | Mapitio ya Rasimu ya pili ya Taarifa | 65 |
| 6. | Kijiji cha Ormanie | 28 Aprili, 2022 | Mkutano Mkuu kuwasilisha na kupitia rasimu ya pili ya taarifa | 258 |
| 7. | Malambo | Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 745 |
| 8. | Madukani | Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 328 |
| 9. | Kirtalo | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 373 |
| 10. | Ololosokwan | March-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 652 |
| 11. | Oloipiri | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 379 |
| 12. | Maaloni | March-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 415 |
| 13. | Mbuken | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 314 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14. | Loosoito | March-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 296 |
| 15. | Olalaa | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 225 |
| 16. | Engobereti | March-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 271 |
| 17. | Oloiswashi | Machi-Aprili 2022 | Mkutano Mkuu wa kuwasilisha na kupitia rasimu ya taarifa | 259 |
| | **Jumla** | | | **7,703** |

Baadhi ya Mapendekezo ya wananchi katika taarifa hii ya Loliondo yalitoa nafasi ya mazungumzo kati ya wananchi na Serikali katika kupanga namna ya kutumia eneo hili kwa pamoja. Kwa maana hiyo kama haya mapendekezo ya wananchi yagepewa nafasi ya mazungumzo kusingekuwa na sababu ya kupeleka vikosi Loliondo na kuchukua eneo kwa njia ya umwagaji damu.

**b) Matumizi makubwa ya nguvu za vyombo vya usalama**

Taarifa mbalimbali za wananchi katika kata zote nane ambazo operesheni hii imepita inaonyesha kuwa kulikuwa na matumizi makubwa ya nguvu katika zoezi hili la utwaaji wa eneo la km za mraba 1502. Takriban magari zaidi ya 50 ya vikosi mbalimbali vya usalama yanasadikiwa kuwa yalikuwa yanasimamia zoezi hili katika ukanda wote huu wa kata nane zenye eneo hili la km za mraba 1502.

Vikosi vingi vyenye silaha za moto, mabomu ya machozi yalionekana yakizingira maeneo yote ambayo vigingi vilipangwa kupitishwa. Katika zoezi hili wananchi wamelalamika kuwa kulikuwa kuna matumizi holela ya risasi na mabomu. Risasi zilipigwa mara kwa mara juu na mabomu pale palipoonekana kuna watu. Milio ya silaha iliweza zua taharuki na mshtuko mkubwa kwa jamii. Wapo waliokimbia walitoa mimba kutokana na mshtuko, mifugo kupigwa risasi na mingine kupotea.

**c) Kupoteza uhai na kupotea kwa watu**

Zifuatazo ni baadhi ya taarifa za kupotea kwa watu siku ya oparesheni na vifo vilivyotokana na oparesheni hiyo kama ilivyoelezwa na waathirika katika kila kata.

I. Kutokana matumizi makubwa ya nguvu katika zoezi hili, watu Katika zoezi hili hadi sasa kutokana na matokeo ya ufuatiliaji huu , tumebaini uwepo wa taarifa za kifo cha Askari Polisi mmoja anayedaiwa kupigwa mshale katika mvutano wa wannchi na askari katika kata ya Ololosokwan.

II. Imebainika kuwa yupo mzee Oriasi ole Ng'iyo, mwenye umri wa miaka 80 aliyekeruhiwa na vikosi vya Operesheni na kupotea hadi leo
III. Imebainika kuwa pia kuna mtoto mmoja kutoka Kijiji cha Piyaya alipotea wakati wa oparesheni hii na hadi leo hajulikani alipo.
IV. Pia wananchi wa Piyaya walitueleza kuhusu mtoto aliyepoteza uhai wakati wanawake waliokuwa wanakimbia kumwangukia mtoto na hatimaye kupoteza maisha.
V. Wapo pia watu zaidi ya 30 waliopigwa na kuumizwa na kulazimika kutafuta matibabu nje ya nchi.
VI. Kuna taarifa pia zinadaiwa na wananchi kuwa yupo Mtu mmoja wa kata ya Malambo aliyegongwa na magari ya Oparesheni na kupoteza maisha

**d) Kukamatwa kwa watu wengi wakiwemo viongozi wa kisiasa na jamii**

Zoezi hili la uwekaji vigiingi ulikwenda sambamba na ukamataji holela wa wananchi katika maeneo husika. Ufuatiliaji huu umebaini kuwa walau kila kata ilikuwa na watu wasiopungua 30 waliokamatwa wakati wa zoezi hili. Toka zoezi hili lianze takriban jumla ya watu 200 walikamatwa na kupewa makosa mbalimbali kama ya mauaji, makosa ya uraia, makosa ya kuingia linalotengwa pamoja na makosa mengine. Wengi walishia katika vituo vya polisi na kulipa kila mtu hongo ya million tatu kwa polisi.

Takribani kesi 100 ndio zilifanikuwa kufika mahakamani na badaye kuachiwa kwa kukosa ushahidi. Wananchi 27 pamoja na viongozi walibambikiziwa kesi ya mauaji katika Mahakama ya Hakimu mkazi Arusha (Kesi ya Awali Na 11 ya Mwaka 2022 Jamhuri dhidi ya Molongo Daniel Paschal na wenzake 26) na kukaa gerezani kwa muda wa Zaidi ya miezi sita na badaye Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini kuiondoa kesi hiyo mahakamani. Pia wananchi 62 walikuwa kesi tofauti tofauti wakituhumiwa kuwa wao sio raia wa Tanzania na badaye kuamuliwa na mahakama kwa kuwaachia huru watuhumiwa baada ya upande wa mashitaka kushindwa kuthitibtisha madai yao (Mfano kesi ya Jamhuri dhidi ya Paulo Yale Mako na wenzake 4, Kesi na 15 ya mwaka 2022, Kesi na 16 ya 2022 Jamhuri dhidi ya Samson Joseph Kipukya na wenzake 6 nk, kesi hizi zilifunguliwa katika mahaka ya wilaya ya Ngorongoro iliyopo Loliondo).

**e) Watu kukimbia Nchi**

Kutokana na nguvu kubwa iliyokuwa inatumika wakati wa oparesheni hii, wananchi takriban elfu mbili (2,291) waliweza kukimbilia nchi Jirani ya Kenya kuepuka kupigwa , kukamatwa na kuunganishwa katika kesi mbalimbali. Katia ya wananchi hawa 2,291 (Watoto walikuwa 1,652 Wanawake 528 Wanaume 100 na Watetezi wengine 30). Pi kuliwa na wagonjwa 30 waliondoka pamoja na ndugu zao. Kati ya watu waliokimbia walikuwepo pia watetezi wa haki za binadamu takribani 30 ambao walikuwa katika hali ya kutafutwa pengine kuunganishwa na shauri la mauaji liliokuwa mahamani. Hadi sasa hakuna taarifa kamili kama watu wote hawa wamesharudi katika jamii na kuendelea na shughuli zao za kawaida.

### f) Watu kupigwa na majeruhi kunyimwa matibabu

Kutokana na mvutano uliojitokeza kati ya vikosi na wananchi, wapo wananchi walioumizwa na kupelekea kuhitaji matibabu ya haraka. Mfano katika kata ya Olosokwan pekee watu 30 pekee walipigwa na kujeruliwa kwa silaha za mpira pamoja na risasi za moto. Wengi wanaeleza walikosa ushirikiano wa matibabu katika vituo vya afya vya Loliondo kwa kuwa walitakiwa wawe na PF3 form ya polisi kitu ambacho kwenda polisi wao waliona ni kujipeleka kwenye shida zaidi.

Hatimaye wengi walikwenda nchi jirani ya Kenya na kupata matibabu katka hosptali za huko Posmoru ilikoko Narok nchini Kenya. Baadhi ya wananchi hadi sasa wengine wanachechemea na wengine bado wanaendelea na kliniki za matibau kutokana na majeraha waliyokuwa nayo.

### g) Kuibuka kwa zoezi la Watu kuwa sio raia

Changamoto nyingine iliyoambatana na zoezi la uwekaji vigingi au inayofanya zoezi hili kuwa na sura ya matumizi makubwa ya nguvu ili kutisha watu ni swala la uraia. Kutokana ukweli kuwa jamii ya kimasai ipo pande zote mbili za mpaka (Kenya na Tanzania). Swala hili limekuwa likitumika sana kujenga hofu kwa wananchi katika eneo hili. Swala hili la uraia lilisababisha watu wengi kukamatwa takriban 150 kwa swala la uraia. Wengi waliishia katika hatua za awali lakini waliofika mahakamani na mashauri yao kusikilizwa ni watu 62.

Tarehe 31mwezi Mei 2023 kupitia bunge la Jumuiya ya Ulaya, Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji Bwana Jestas Nyamanga aliyeambatana na baadhi ya maafisa wa Tanzania akiwenmo Profesa Malebo toka kmisheni ya UNESCO Tanzania aliendelea kuongelea upotoshwaji katika swala hili la uraia akituhumu baadhi ya makundi ya wamasai katika wilaya ya Ngorongoro kama Purko, Loita na Laitayok sio wenyeji/raia wa Tanzania bali ni wakenya.

Ukweli ni kuwa asilimia 99.9% ya wakazi wa kata za Arash, Maaloni, Oloirien, Soitsambu na Ololosokwan ni Purko, Loita na Laitayok na ni raia wa Tanzania halali waliokuwepo katika maeneo katika karne nyingi kama ilivyokuwa kwa Serengeti na Ngorongoro. .

### h) Kukosekana kwa uhuru wa Habari

Katika ziara hii tumebaini pia kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa uhuru wa kujieleza na pia uhuru wa vyombo vya habari kutoa taarifa za operesheni hii. Vyombo vingi vya ndani vilipata vitisho na maelezo yasiyo rasmi kuwa taarifa zozote zinazonyesha uhalisia wa zoezi hili zisitolewe badala yake zipo baadhi ya vyombo vya habari vilitumika kufanya propaganda dhidi ya wananchi wa Loliondo. Waandishi wengi walishindwa kwenda Loliondo kutoa taarifa za kweli kutokana na hali ya vitisho wakihofi usalama wao.

Kwa mfano Februari 03, 2022 jumla ya waandishi wa Habari 6 walikamatwa na askari wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro baada ya kufuatilia mkutano wa wanakijiji Zaidi ya 200 waliofanya mkutano katika kata ya Nainokanoka katika tarafa

ya Ngorongoro. Wananchi hao walikuwa wanajadili namna ya kukabiliana na vitisho dhidi yao kuhusu kuhama Ngorongoro.

Waandishi hao walikamatwa na kutishiwa kuwa waliingia katika eneo la mamlaka bila ya kuwa na kibali wakati kiuhalisia walikuwa na vibali vyote.

Waandishi hao ni: Janeth Mushi wa Mwananchi, Julius Sagati wa Star Tv, Amina Ngahewa wa Mwananchi Digital, Allan Isack wa gazeti la Nipashe, Profit Mmanga wa Wasafi Tv na Apolo Benjamin wa Daily News Digital. Lakini pia mwandishi Thobias Mwanakatwe wa gazeti la Nipashe Newspaper na Joseph Kimambo wa Dar Mpya pamoja na dereva wao Majuka Ngisaayo aliyekuwa mfanyakazi wa shirika la PINGOs Forum walikamatwa Februari 17, 2022. Lakini pia mwandishi wa Watetezi Tv Hilda Ngatunga alinusurika kukamatwa kutokana na kufanya kazi ya kufuatilia na kurusha juu ya kile kilichokuwa kinatokea Ngorongoro.

#### i) Kukosekana kwa uhuru wa Watetezi wa Haki za binadamu

Watetezi wa haki za binadamu pamoja na mashirika ya utetezi wa haki za wafugaji wamekuwa katika wakati mgumu sana kufanya kazi zao za utetezi kipindi chote cha zoezi hili hadi hivi sasa.  Baadhi ya watetezi wa jamii walijikuta wakikimbia nchi kunusuru maisha yao huku wengine wakiunganishwa katika kesi ya mauaji. Kila kiongozi wa Serikali aliyefika katika eneo la Loliondo alitamka wazi wazi kupambana mashirika ya utetezi wa jamii pamoja na watetezi waengine wa jamii. Mashirika haya yalipekuliwa mara kwa mara na viongozi wao kutakiwa kwenda kuripoti katika vyombo vya usalama.

Mwezi Februari mwaka 2022 Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) kwa kushirikiana na mashirika 20 ya kidini na ya haki za binadamu ulizuiwa kufanya ziara katika wilaya ya Ngorongoro kufuatilia hali ya haki za binadamu. Lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kufuatilia hali ya haki za binadamu, kufanya vikao na wananchi wenyeji pamoja na idara mbalimbali za Serikali katika tarafa ya Loliondo, Sale na Ngorongoro ili kukusanya taarifa sahihi kutoka ngazi ya chini kuhusu mgogoro wa ardhi katika wilaya ya Ngorongoro.

Hata hivyo, ziara hiyo ilizuiliwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha baada ya mashirika hayo kufika Arusha kwa madai ya kwamba hayakuwa na kibali cha kufanya zaiara hiyo kutoka ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mtandao uliandika barua kwenda ofisi ya Waziri Mkuu  lakini haikujibiwa hadi sasa.

Mashirika ya utetezi wa jamii pamoja na watetezi wa jamii wamekuwa wakionekana kuwa ni tishio katika mikakati kama hii hasa pale wanaposimama kutetea haki za jamii. Swala la utetezi wa haki za jamii katika eneo hili la Loliondo limekuwa na madahara makubwa kwa kazi za mashirka na kazi za watetezi wa haki za binadamu. Watetezi wengi wamekimbia Wilaya ya Ngorongoro kutokana na mazingiria magumu ya kufanya kazi za utetezi.

Changamoto za kutishia watetezi wa haki za biandamu zilianza hata kabla ya zoezi hili la kuweka mipaka. Watetezi wa jamii walianza kusumbuliwa kukamatwa na kuitwa mara kwa mara katika vituo vya polisi. Mfano wakati wa uwaandaji wa taarifa na mapendekezo ya wananchi viongozi wa kisiasa, wa kimila na watetezi wa haki za binadamu kukamatwa, kuitwa vituo vya polisi na kuhojiwa wakati zoezi hili la uandishi wa ripoti likiendelea.

**Jedwal 5.2: Baadhi ya Viongozi wa kisiasa, wa kimila na watetezi wa haki za binadamu walioendelea kukamatwa, kuitwa vituo vya polisi na kuhojiwa wakati wa zoezi la kukusanya maoni ya wananchi (Machi-Aprili 2022).**

| Na | Kiongozi | Kata/Kijiji | Cheo | Tarehe ya kukamatwa | Alikopelekwa | Hali ya Shauri |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Joel Clemence | Malambo | Diwani | | Loliondo na Arusha | - |
| 2. | Motiko Risando | Malambo | Mwenyekiti wa Kijiji | | Loliondo | - |
| 3. | Simon Ndari | Malambo | Laigwanani | | Loliondo | - |
| 4. | John Kulinja | Malambo | Laigwanani | | Loliondo | - |
| 5. | Simon Ole Nairiamu | Piyaya | Diwani | | Loliondo | - |
| 6. | Moloimet Saing'eu | Ololosok-wan | Diwani | | Loliondo | - |
| 7. | Ndirango Olesenge | Loliondo/ Orgosorok | Mwenyeki-ti wa CCM Wilaya ya Ngorongoro | | | - |
| 8. | Mathew Siloma | Arash | Diwani | | Loliondo-Aru-sha | - |
| 9. | Mbeka Rago | Maaloni | Diwani | | Loliondo | - |

Mtandao wa watetezi pamoja wadau wake walitumia muda mwingi kuhakikisha watetezi wa haki za binadamu wanabakia katika hali yao ya usalama na kuendelea kazi zao za utetezi.

### j) Kupotea kwa mifugo na kuliwa na Wanyama wakali

Zoezi hili la kuweka vigingi pamoja na utwaaji wa eneo hili la km za mraba 1500 ulisabisha pia maumuvu makali kwa wanachai wa kata hizi nane. Kwa kuwa zoezi hili lilikuwa linafanyika matumizi ya silaha na katika maeneo yenye watu na shughuliz ufugaji ulisababisha mifugo mingi kupotea na wengine kuliwa na Wanyama wakali. Wananachi waliohojiwa na ziara hii walielezea kwa uchungu jinsi zoezi hili lilipowanya wapoteze baadhi ya mifugo yao kama mbuzi , kondo, ngombe na punda.

Watu hawa walikokuwa wanaweka viginngi walipokuwa wanawakuta watu aidha katika makazi yao au wakiwa wanachunga walipiga rasasi juu na kuwapa masaa chache ya kuondoka ndani ya eneo la km za mraba 1500. Pia wapo ngombe na punda waliopigwa risasi kwa mujibu wa wananchi katika eneo hili linalozunguka Pori la sasa la Pololeti. Mfano kata ya Arash ng'ombe 17 walipigwa risasi.

### k) Watu kuvunjiwa makazi yao na wengine kuacha mali zao

Katika zoezi zoezi hili wapo pia wanachi waliovunjiwa makazi yao ya kudumu. Kata zilizoadhirika zaidi na watu kuvunjiwa nyumba zao wakati wa zoezi hili ni pamoja na kata ya Arash, Ololosokwan na Malambo. Wananchi katika kata hizi walipoteza nyumba zao pmaoja na mali ziliokuwa katika nyumba zao. Kwa mujibu wa maelezo yao, wananchi wanandai watu wa operesheni waliweka mipaka hadi maeneo yasiyohusika na km za mraba 1500, ambayo ni makaazi ya kudumu ya wananchi.

Mfano katika kata ya Malambo, vitongoji viwili vya ndinyeka na Sanjan ndio vilivyoathirika zaidi na zoezi hili. Vitongoji hivi vimepoteza mifugo mingi, nyumba , maeneo ya huduma za jamii kama makanisa, vituo vya afya pamoja na visima vya maji. Mfano kitongji cha Sanjani nyumba 120 (81 maboma ya kiasili pamoja na nyumba za bati 40) zilibolewa zilokuwa na kaya 450 sawa na jumla ya watu 1982, shule za awali mbili , zahanati 4 na kanisa moja kubwa., matenki matatu ya maji ya mvua.

Kitongoji kingine katika kata hiyo hiyo ya malambo kilichoadhirika ni cha Ndinyeka , kilikuwa na nyumba 100 ( Maboma 89 nyumba za bati 11) yenye kaya 287 sawa na watu 1468. Kulikuwa na shule moja ya awali, vituo viwili vya kutolea huduma za chanjo kwa wanawake na watoto mbili , kanisa kubwa ambalo hadi sasa halijavujnwa; mabwawa saba ya maji.

**Jedwali 5.3 : Makazi na Miundo Mbinu iliyobomolewa**

| Na. Kata. | Makazi/Kaya/ Idadi | Shule | Clincis/Zahanati/Vituo vya kutolea huduma kwa Wanawake na Watoto | Makanisa | Visima / Mabwawa |
|---|---|---|---|---|---|
| Malambo | Nyumba 220 ( Maboma ya Kiasili 169 na nyumba za bati 51) zenya jumla ya kaya 737 na idadi ya watu 3442 | Shule tatu za awali | Clnics 6 | Makanisa mawili | Visima vitatu na mabwawa saba |
| Arash | - | - | - | - | - |
| Ololosokwan | - | - | - | - | - |

Kitendo hiki cha kubomoa makazi ya watu kimesababisha watu takriban 4000 elfu kukosa makazi na kupoteza huduma za msingi. Watu waliathirika zaidi ni watu wa kata Malambo ambao hadi sasa hawana makazi wala huduma za msingi walizokuwa wanazitgemea katika maeneo yaliyochukuliwa.

### 5.2.8 Mahitaji ya Wananchi kuhusu Zoezi la Uwekaji Mipaka

Sura hii ndogo inawasilisha maoni ya wananchi kuhusu zoezi hili kama walivyatoa kwa ziara hii. Maoni yao yanajikita zaidi katika zoezi zima la uwekaji vigingi pamoja na chagamoto zote zilizojitokeza wakati wa zoezi hili.

(a) Kuwepo na nafasi ya pamoja baina ya Serikali na Wananchi kuweka ukweli na mardhiano ya matukio yaliyotokea

(b) Kwamba wananchi wa tarafa ya Loliondo na Sale hawana ardhi mbadala kwa ajili shughuli yao kuu ya kiuchumi ambayo ni ufugaji. Hivyo kupoteza eneo hilo ni kuangamiza jamii moja kwa moja. Wananchi katika baadhi ya kata kama Malambo na Piyaya, wameeleza kuwa maeneo ya kata zao ni maeneo kame (semi-arid land) hivyo shughuli nyingine ya kiuchumi kama kilimo haiwezekani isipokuwa ufugaji tu. Kwa maana hiyo kupoteza ardhi ya malisho ni kutengeneza janga kubwa la umaskini na njaa kwa jamii, kitu ambacho imeshashuhudiwa kwa siku chache tu baada ya eneo kutengwa. Hivyo wanaomba Serikali iwarushie sehemy ya maeneo yao yaliyomegwa kwa kuwa hawana eneo jingine wanalotegemea.

(c) Kwakuwa zoezi hili liliumiza wengi kuwe na fidia kwa wale waliomizwa pamoja na wale walipoteza ndugu zao hadi leo

(d) Kwa kuwa zoezi hili halikuwa shirikishi, wananchi wanapendekeza kuwe na mazungumzo ya pamoja baina ya Serikali na wananchi wa kata hizi nane zinazopaka na Pori la Pololet kujadili namna ya kutumia hili eneo kwa pamoja hasa wananchi kulitumia wakati wa kaingazi pekee kwa ajili ya malisho.

### 5.2.9 Ufafanuzi wa Serikali Kuhusu Changamoto Zoezi la Uwekaji Mipaka

Baada ya kutembelea katika Tarafa ya Loliondo na Sale tulibaini changamoto zilizotajwa hapo juu na hivyo ilitulazimu kuandika barua kwa Serikali kuomba ufafanuzi. Mbali na kuandika barua na kukumbushia mara kwa mara, hatukufanikiwa kupata majibu ya Serikali kwa njia ya maandishi. Hivyo ufafanuzi uliopo hapa ni ule ambao Serikali iliwahi kuutoa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Bungeni ama kwenye mikutano na wananchi kipindi cha nyuma.

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa mnamo Juni 23, 2022 alizipongeza taasisi zote zilizokuwa zinaratibu zoezi la uwekaji wa alama katika eneo la Pori tengefu la Loliondo kwa kukamilisha uwekaji wa vigingi 424 vilivyokusudiwa kuwekwa. Waziri Mkuu alitoa pongezi hizo alipotembelea eneo hilo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,500 kuona maendeleo ya uwekaji wa alama kuzunguka eneo la hifadhi.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Mheshimiwa Majaliwa alisema kuwa eneo hilo lina umuhimu mkubwa kwa Watanzania na hata nchi jirani.

"Hii ni tunu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, uwepo wa wanyama ni kivutio kikubwa kwa shughuli zetu za utalii, ni muhimu tuilinde." "Ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini unatokana na kodi ambazo Serikali inakusanya kutoka maeneo tofauti ikiwemo sekta hii ya utalii," Alisema kuwa zoezi lililofanyika ni uwekaji wa alama tu, na hakuna mtu yeyote atakayeondolewa katika vijiji vinavyozunguka eneo hilo. "

Tofauti na kauli ya Waziiri Mkuu kuwa wanaaweka mipaka tu, Waziri wa Maliasili na Utalii kipindi hicho, Balozi Dkt. Pindi Chana alisema kuwa eneo hilo ni muhimu katika sekta ya utalii na ni wajibu wa Wizara kuhakikisha eneo hilo linalindwa. "Tumeshapitisha GN, sasa itaitwa Pori tengefu la Pololeti la kilomita za mraba 1,500." Kwa upande wake, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Bw. Mashimba Ndaki alisema kuwa Serikali inaendelea na ujenzi wa lambo kubwa litakalotumika kunyweshea mifugo katika eneo la Loliondo.

Alisema kuwa Serikali inajenga majosho 10 ya kuogeshea mifugo na tayari majosho mawili yameshakamilika huku mengine manane yakiwa katika hatua mbalimbali za ujenzi. "Serikali inawajali na inawaangalia sana wafugaji," alisisitiza. Na kwa upande wake, Waziri wa Maji, Bw. Jumaa Aweso alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kupeleka huduma ya maji safi na salama katika maeneo yote nchini ikiwemo Loliondo[24].

---

24 https://www.vaticannews.va/sw/world/news/2022-06/zoezi-wakazi-ngorongoro-ku-hamia-msomera-handeni-tanga-maasai.html

Lakini pia Serikali kupitia kikao cha Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Kamati ya Ulinzi na Usalama, Wataalamu kutoka Tume na Halmashauri ya Wilaya, pamoja na Wenyeviti na Watendaji wa Vijiji ilifanya kikao na kutoa ufafanuzi kuhusu kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi pamoja na upimaji wa ardhi ya vijiji 14 baada ya kilometa za mraba 1,502 kutwaliwa na Serikali. Kwenye kikao hicho Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro Mhe. Raymond Steven Mwangwala aliishukuru-Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kwa kufanya kazi ya kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika Vijiji 14 vilivyoko kwenye kata 8 katika Tarafa ya Loliondo. Kazi hii pia ilihusisha upimaji wa mipaka ya Vijiji, utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji, uandaaji wa Mipangokina pamoja na utoaji wa Hatimiliki za Kimila kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya alidai kwamba wananchi wa Vijiji hivyo kwa nyakati tofauti walifika ofisini kwake kupeleka maombi ya kupimiwa vijiji vyao. Aidha, Mkuu wa Wilaya alisema uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi utasaidia wananchi wa vijiji hivyo kutumia ardhi kwa ajili ya shughuli zao mbalimbali ili kuleta mafanikio katika nyanja za kiuchumi na kijamii sambamba na kuhifadhi mazingira[25].

Mbali na hilo, naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro Dkt. Jumaa Mhina alisema kuwa zoezi la uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji hivyo litasaidia kuwahakikishia wananchi umiliki wa ardhi za vijiji pamoja na kuondoa migogoro ya mipaka baina ya kijiji na kijiji. "Zoezi la Upimaji na Upangaji wa Vijiji hivi pia litasaidia kuondoa migogoro ya ardhi na dhana potofu kuwa Serikali ina mpango wa kuchukua maeneo yao kwa kuwa Vijiji vinaenda kupata vyeti vya ardhi vitakavyowasaidia kuwa na uhakika wa umiliki wa ardhi yao" alisema Dkt. Jumaa Mhina

Mkurugenzi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Usimamizi na Uratibu, Bw. Jonas Masingija Nestory kutoka Tume alisema kuwa kazi hiyo imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu hizo ni Upimaji wa mipaka ya Vijiji, Utoaji wa Vyeti vya Ardhi vya Vijiji, uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Uandaaji wa Mipangokina ambao utahusisha kupima vipande vya ardhi na kutoa Hatimiliki za Kimila. "Sambamba na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, pia kutakuwa na upimaji wa mipaka ya vijiji, lengo ni kuwa kila kijiji kujulikana mipaka yake, kubainisha matumizi mbalimbali yaliyopo kwenye kila kijiji, ikiwa ni pamoja na maeneo ya makazi, kilimo, malisho, hifadhi za misitu na vyanzo vya maji, ili kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili hapo awali" alisisitiza Bw. Masingija.

Akizungumza bungeni mjini Dodoma Mhe. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alisema 'hakuna mapambano yoyote, hakuna askari yeyote aliyekwenda huko kwenye kijiji kutishia, kwa sababu katika mipango yote hakuna kijiji kinaondoka, hakuna mwananchi anayeondolewa, wananchi wa Loliondo watulie', alisema Majaliwa na kuongeza, "eneo lile ni letu sote na tutaliratibu vizuri baada ya kuweka hizo alama, kuashiria

25 https://www.nlupc.go.tz/news/vijiji-loliondo-kupimwa-na-kuandaliwa-mipango-ya-matumizi-ya-ardhi

tu kwamba huku ndani ndo tumehifadhi, tuweze kuratibu kwa pamoja, hayo ndiyo malengo ya Serikali kwa eneo la Loliondo"

Lengo hasa la Serikali kuendelea na zoezi hilo la Loliondo ni kutokanana na umuhimu wake kwa ikolojia na uhifadhi wa wanyamapori nchini Tanzania. Kwa muda mrefu mpango na nia ya Serikali ya Tanzania katika mapori tengefu na hifadhi zake ikiwemo Ngorongoro, Serengeti na Pori Tengefu Loliondo ni kulinda maeneo hayo, ikiwemo kuondoa maboma na mifugo pamoja na kuweka mipaka na alama ili kutenganisha maeneo hayo na yale ya vijiji kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

Zoezi la uwekaji wa alama Loliondo lililosababisha kifo cha askari mmoja, na baadhi ya wanakijiji kujeruhiwa katika mivutano ya kupinga zoezi hilo, ni muendelezo wa nia ya Serikali ya kuchukua eneo hilo la vjiji. Hata hivyo, msemaji mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alipozungumza na BBC mara mbili alisisitiza hali ni shwari Loliondo na kwamba kilichotokea hadi kusababisha mauaji ni wakazi kuwafuata askari polisi na si polisi kuwafuata wakazi, wakati wa zoezi la kuweka mipaka, umbali wa takribani kilomita 8, kutoka yalipo makazi ya watu.[26]

26 https://www.bbc.com/swahili/articles/c726w2gg7zlo

SURA YA 5
SEHEMU YA TATU

# CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA BAADA ENEO LA KILOMITA 1,502 KUGEUZWA KUWA HIFADHI

## 5.3 UTANGULIZI

Changamoto mbalimbali zimekuwa zikijitokeza baada ya eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa na Serikali na baadae kugeuzwa kuwa pori tengefu la Pololeti. Ni muhimu kukumbuka kwamba eneo lililochukuliwa ndio lilikuwa eneo pekee ambalo wananchi walikuwa wanalitegemea katika kulisha mifugo yao, maji ya kunywa kwa wote binadamu na mifugo na lilikuwa ni eneo la makazi kwa baadhi ya wananchi. Hivyo baada ya eneo hilo kutwaliwa na Serikali changamoto kadhaa zimekuwa zikijitokeza kama zilivyoelezwa kwenye sura hii.

### 5.3.1 Changamoto Zinazoendelea Kujitokeza Baada ya Eneo la Vijiji Kutwaliwa

#### (a) Mifugo kukamatwa, kutaifishwa na kutozwa faini

Hii ni changamoto kubwa sana kwa wakazi wa maeneo ya Kirtalo, Soitsambu, Arash, Malambo, Sale, Piyaya, Loliondo, Ololosokwan, n.k. Mifugo yao imekamatwa kwa wingi, kuuzwa kwa mnada na mingine kutaifishwa. Wananchi walitueleza kuwa wahusika wa mifugo wakigundulika wamekuwa wanafunguliwa kesi mahakamani na kutozwa faini ya shilingi laki moja (Tshs. 100,000) kwa ng'ombe na shilingi elf ishirini na tano (Tshs. 25,000) kwa mbuzi au kondoo.

Kwa mfano kwa mwezi Novemba pekee mwaka 2022 ng'ombe 2,276 walitaifishwa katika kata ya Arash kwa kudaiwa kuingia katika hifadhi ya taifa ya Serengeti. Kwa kata nzima ya Arash kuanzia Juni 2022 hadi Aprili 2023 faini iliyolipwa na wafugaji ni milioni 860 kwa kudaiwa mifugo yao kuingia katika pori tengefu la Pololeti na hifadhi ya taifa ya Seerengeti.

**Jedwali 5.4: Idadi ya Mifugo iliyokamatwa pamoja na Fedha zilizotumika kukomboa kwa kila Kata**

| Na. | Kata | Idadi ya Mifugo illyokamatwa na kukombolewa | Fefha iliyolipwa kuomboa mifugo | Mifugo iliyotaifishwa na kupigwa Mnada | Idadi ya Kaya zilizobaki bila ng'ombe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Arash | Zaidi ya 5000 | 860,000,000 | 2, 276 | 180 |
| 2. | Piyaya | 600 | Hakuna Kumbukumbu | Hakuna kumbu kumbu | Hakuna kumbukumbu |
| 3. | Malambo | 2,820 | 118,525,000 | 124 | 60 |
| 4. | Olorien | 400 | Hakuna Kumbukumbu | Hakuna Kumbukumbu | Hakuna Kumbukumbu |
| 5. | Maaaloni | 300 | Hakuna Kumbukumbu | Hakuna Kumbukumbu | Hakuna Kumbukumbu |
| 6. | Ololosokwan | 3,846 | 789,800,000 | 55 | |
| 7. | Soit Sambu ( Kijji cha Kritalo) | Zaidi ya 10,000 | Zaidi ya bilioni moja | hakuna kumbukumbu | hakuna kumbukumbu |
| 8. | Oloipiri | 1200 | hakuna kumbukumbu | 400 | hakuna kumbukumbu |
| | **Jumla** | **25,166** | **2,768,325,000/=** | **2,855** | **240** |

Kwa ujumla wananchi wa kata hizi nane wameumia sana kiuchumi kwani ufuatiliaji huu umebaini wameshapoteza zaidi ya nusu ya mifugo yote katika eneo hili na pia tayari kwa kata zote nane wananchi wameshatoa zaidi ya billion 3 kama faini na pia kama hongo kwa njia zisizo rasmi kukomboa mifugo yao inayoingia katika eneo hili liliotengwa la vijiji. Mfano kata ambazo zimeathirika sana na kufa kwa mifugo na kulipa faini nyingi zaidi ni Kata za Arash, Ololosokwan, Soitsambu na Malambo.

### (b) Askari Kuswaga Mifugo na Kuwaingizwa kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti

Wakati wa ziara yetu, wananchi wa tarafa ya Loliondo na Sale walieleza kwamba askari wanaolinda pori tengefu la Pololeti wamekuwa na tabia ya kuswaga mifugo na kuwaingiza kwenye pori tengefu la Pololeti na hatimaye kwenye hifadhi ya taifa ya Serengeti kwa lengo la kutoza faini au kutaifisha mifugo endapo mmiliki hatajitokeza.

Kwa mfano, Solio Toroge mkazi wa Loliondo alishitakiwa katika Mahakama ya Wilaya ya Serengeti kwa tuhuma za kuingiza ng'ombe 440 kwenye hifadhi ya taifa ya Serengeti mnamo Machi 2023. Mahakama ya wilaya iliamua kwamba Bw. Toroge arudishiwe ng'ombe zake kwa sababu hakukuwa na ushahidi kwamba ng'ombe waliingiaje katika hifadhi ya taifa ya Serengeti pasipo kupita au kukamatwa kwenye pori tengefu la Pololeti. Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini alikata rufaa katika Mahakama Kuu ya Tanzania na Bw. Toroge kuamuriwa kulipa faini ya shilingi elfu tano kwa kila ng'ombe kwa kila siku ambazo ng'ombe walikuwa wanashikiliwa na askari wa hifadhi ya taifa ya Sererengeti. Alilipa zaidi ya shilingi milioni 70 kwa ng'ombe wote.

### (c) Mifugo Kufa kutokana na Ukame na Kukosa Maji

Katika ziara hii wananchi walitueleza kwamba mifugo mingi imekufa kwa wingi kutokana na ukame ndani ya miezi 8 toka eneo hili litwaliwe. Eneo lililochukuliwa na Serikali ndio lilikuwa chanzo cha maji na malisho kwa mifugo kwa tarafa nzima ya Loliondo na Sale hasa wakati wa kiangazi.. Ni eneo ambalo lilikuwa na vyanzo vya maji hasa mito ya maji safi na salama kwa mifugo na binadamu. Mito hiyo yenye vyanzo vya maji ni ormungushi, orkereyani, esiyaiti na emurgur na yote imechukuliwa. Kabla ya eneo la Pololeti kutwaliwa na Serikali kulikuwa na mifugo takriban 973,745 lakini mara baada ya eneo kutwaliwa kata zote zinazo zunguka eneo hili la km za mraba 1502 zilipungua karibu nusu ya mifugo hasa ng'ombe. Mfano kata ya Arash ilikuwa na ng'ombe 56,000, lakini baada ya eneo kutwaliwa na Serikali ng'ombe 25,000 wamekufa kutokana na ukame.

### (d) Wananchi Kukosa Makazi ya Kuishi

Wakati wa zoezi la uchukuaji wa eneo la kilometa za mraba 1,502, wananchi walitueleza kwamba walipewa notisi ya kuhama kwenye maboma yao ndani ya saa 24. Nyumba zao zilizungukwa na askari waliokuwa wanafanya oparesheni na kuwataka wahame mara moja. Hivyo wengi iliwalazimu kuhama bila kujua kuwa wanaenda kuishi wapi hali ambayo imewasababishia kutokuwa na nyumba na hivyo hawana makazi ya kuishi. Pia hakuna maeneo kwaajili ya wao kujenga nyumba kwani eneo liliobaki ni dogo sana.

Mfano katika kata ya Malambo pekee , zaidi ya kaya 600 zimekosa mahali pa kuishi baada ya makazi yao kubomolewa wakati wa zoezi la uwekaji mipaka. Hadi sasa zipo familia zimeshindwa kurudi katika hali yao ya kawaida kimaaisha na wanahitaji kupata msaada wa dharura kuwarudisha katika hali waliyokuwa nayo. Hali hii imechangi umaskini katika jamii kuongoza zaidi.

### (e) Watoto Kushindwa kwenda Shule kwa sababu ya kukosa ada

Matokeo ya ziara hiii inaonyesha kwamba hivi sasa wananfunzi wameshindwa kwenda shule kutoakana na umasikini uliosababishwa na mifugo kutaifishwa, kupigwa mnada na kupigwa faini na mifugo kufa kutokana na kukosa malisho. Asilimia 90 ya shughuli za kiuchumi kwa jamii ya kifugaji katika eneo hili ni shughuli za ufugaji asili unaotegemea sana eneo liliochukuliwa.

Wafugaji wamekuwa wakitumia mifugo yao kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za msingi kama vile matibabu, chakula elimu na kadhalika. Wananchi wengi sasa wanapta changamoto ya kulipa ada za Watoto wao waliokuwa wanasoma katika shule mbalimbali.

### (f) Kukosekana kwa maeneo ya malisho, maji na chumvi

Wakati wa ziara wananchi walitueleza kuwa kwasasa hawana maeneo ya malisho kutokana na kwamba eneo ambalo walitenga kwa ajili ya malisho limechukuliwa na Serikali. Kwa mfano ukubwa wa Kijiji cha Ololosokwan ulikuwa ni hekari 51,230 kabla ya kuchukuliwa na Serikali. Serikali imechukua hekari 25,000 na kuwa sehemu ya pori tengefu la Pololeti na eneo hili lote ndio lilikuwa la malisho tu na sio makazi.

**Jedwali 5.5: Eneo Kata Mbili kabla na baada ya kuchukuliwa na Serikali**

| Kata | Vijiji 3 | Ukubwa wa eneo kabla ya kuchukuliwa (hekari) | Eneo lililochukuliwa (hekari) | Eneo liliobaki (hekari) |
|---|---|---|---|---|
| Soitsambu | Kirtalo | 53,000 | 33,000 | 20,000 |
| Ololosokwan | Ololosokwa | 51,230 | 25,000 | 27,130 |

### g) Miradi na Huduma Mbalimbali Kusitishwa

Wananchi wa kijiji cha Ololosokwan walitueleza kuwa walikuwa wamewekeza kwenye mradi wa ubia na kampuni ya kitalii ya **And Beyond** ambapo walikodisha ardhi yao kabla ya eneo kuchukuliwa. Kutokana na uwekezaji huo kjiji kilikuwa kinapata faida ya shilingi milioni 240 hadi 250 kwa mwaka na walikuwa wanalipia bima za afya kwa kaya masikini 30 katika kila Kijiji kwa mwaka, gharama ya matibabu kwa wagonjwa mahututi, na kusomesha wanafunzi wanaotoka kaya masikini ,hadi kufikia mwaka 2022 wanafunzi 600 walinufaika na mpango huo. Baada ya ardhi yao kuchukuliwa vijiji vimekosa mapato na huduma zilizokuwa zinatolewa kusitishwa.

### h) Njaa na Umasikini Kuongezeka

Wakati wa ziara yetu wananchi walitueleza kuwa wao ni wafugaji kwa asili na ndio shughuli pekee iliyokuwa inawaingizia kipato ikiwa ni pamoja na kupata chakula kama nyama na maziwa. Baada ya eneo kuchukuliwa na mifugo kufa, wamepoteza uchumi

wao hali ambayo imewaletea umasikini mkubwa na hivyo wanakabiliwa na njaa. Hali hii imewalazimu kuchangiana chakula ili wasife njaa na kuna madai kuwa baadhi ya watu wamefariki kwa kukosa chakula.

#### i) Wananchi Kukosa Huduma ya Maji

Baada ya eneo la kilometa za mraba 1,502 kuchukuliwa ambalo ndio sehemu ya chanzo cha maji ya kunywa kwa binadamu, wananchi hawana huduma ya maji ya kunywa kwasasa. Hivi sasa wamama hutembea umbali wa kilometa za mraba 18 kutafuta maji ya kunywa na maji hayo mengi yanapatikana kwenye madimbwi. Hakuna visima vya maji kwaajili ya matumizi ya binadamu. Eneo lililochukuliwa ndio lina mito ya maji tiririka kwaajili ya matumizi ya binadamu.

### 5.3.2 Hoja za Wananchi

a) Wananchi hawana maeneo ya malisho ya mifugo yao hivyo wameomba eneo la kilometa za mraba 1,502 watumie kwaajili ya malisho ya mifugo wakati wa kiangazi. Kwa mfano eneo lililobaki la Piyaya ni la miamba hivyo halina malisho kwaajili ya mifugo.

b) Eneo lililochukuliwa ndio chanzo kikuu cha maji ya kunywa kwa binadamu na Wanyama. Wananchi wameomba waruhusiwe kuchota maji ya kunywa kwenye pori tengefu la Pololeti lakini pia waruhusiwe kunyweshea mifugo yao kwenye pori hilo

c) Wananchi wanahitaji Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aweze kwenda Ngorongoro akawasikilize kero zao ili ziweze kutatuliwa. Kwa ujumla wananchi wanahitaji mazungumzo na Serikali kuhusu matumizi bora na ya pamoja ya pori la Pololeti.

d) Wanyamapori wamekuwa na tabia ya kwenda kwenye maeneo ya makazi ya watu na kula nyasi hata zile ambazo ni kidogo zilizobaki. Wananchi hawana tabia ya kudhuru wanyamapori na hawajawahi kufanya hivyo, hivyo wanaomba hata mifugo ikienda kwenye pori la Pololeti isikamatwe kwasababu wanyamapori na mifugo wamezoea kuishi kama ndugu.

e) Wananchi wanaomba kauli ya Waziri mkuu itekelezwe, Waziri mkuu alisema mnamo mwanzoni mwa mwaka 2022 kuwa "tunaweka vigingi, kama kuna vijiji vitaathirika tutaakaa mara moja". Wananchi wanaomba kukaa na Serikali.

f) Wananchi wamedai kuwa wameathirika kisaikolojia kutokana na madhira waliyoyapata wakati wa oparesheni. Hivyo ni muhimu sana kupatikana tume ya pamoja ya majadiliano na mardhiano.

### 5.3.3 Ufafanuzi wa Serikali kuhusu Changamoto Hizi

Jitihada nyingi zimefanyika kupata ufafanuzi wa hoja hizi za wananchi kwa njia ya mikutano na Serikali au kwa njia ya maandishi lakini barua zote hazikuwaji jibiwa hadi taarifa hii inapokamilika. Barua zilielekezwa kwa ofisi za Wilaya, Mkoa, NCA, Wizara ya Maliasili na ofisi ya Waziri Mkuu. Hoja zinazonekana hapa ni zile zinazopatikana katika vyombo vya Habari.

SURA YA 5
SEHEMU YA NNE

# UCHAMBUZI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI

## 5.4 UTANGULIZI

Sehemu hii inaelezea uchambuzi wa hoja zilizoibuliwa na wananchi wakati wa ziara pamoja na ufafanuzi ambao Serikali iliwahi kuutoa katika kipindi cha oparesheni ya Juni 2022.

### 5.4.1 Kukosekana kwa maeneo ya malisho, maji na chumvi

Wakazi wa Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale (jumla ya vijiji 14) wameathirika kwa kukosa eneo la malisho baada ya ardhi yao kuwekwa vigingi na kuchukuliwa na Serikali. Katika hotuba ya Waziri Mkuu wakati akitoa hoja ya kuahirisha mkutano wa saba wa bunge la 12 tarehe 30 Juni 2022 alisema.

"Serikali imesimamia kwa umakini mkubwa zoezi la uwekaji vigingi kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500 ambalo ni muhimu kwa ikolojia ya Hifadhi ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Halikadhalika, Serikali imeendelea kushirikiana na wananchi wa Loliondo katika kuboresha malisho ya mifugo, uchimbaji wa visima vya maji, ujenzi wa majosho pamoja na miundombinu ya kunyweshea mifugo kwenye eneo la kilometa za mraba 2,500".

Lakini pia kabla ya zoezi la uwekaji vigingi kwenye eneo la kilomita 1,502 kuanza Mhe. Waziri Mkuu alisema "tunaweka vigingi, kama kuna vijiji vitaathirika tutaakaa mara moja". Katika ziara hii tuligundua kwamba baada ya vigingi kuwekwa wananchi walikosa maeneo ya malisho, maji na makazi lakini bado Serikali haijawahi kukaa na wananchi walioathirika na zoezi hilo. Hakuna maboresho ya malisho ya mifugo yaliyofanyika kwani eneo lililochukuliwa wananchi wenyewe ndio walilihifadhi kwaajili ya malisho ya mifugo yao na ndio eneo pia lililokuwa chanzo cha maji ya kunywa binadamu na mifugo yao.

Wakati wananchi wakihangaika kutafuta maeneo ya malisho ili mifugo yao isife kwa kukosa malisho, Serikali imekuwa ikikamata mifugo ambayo hukutwa kwenye pori la akiba la pololeti na wakati mwingine askari wanaolinda maeneo hayo wamedaiwa kuswaga mifugo ili iingie katika eneo hilo ili mifugo itaifishwe, ipigwe mnada au vinginevyo.

### 5.4.2 Wananchi Kukosa Makazi ya Kuishi

Mhe. Kassim Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akitoa hoja ya kuahirisha mkutano wa saba wa bunge la 12 tarehe 30 Juni 2022 alisema

"zoezi hili la uwekaji wa vigingi **ambalo limekamilika kwa asilimia 100** halitoathiri maendeleo ya wakazi wa eneo la vijiji 14 vinavyopakana na eneo hilo. Aidha, hakutakuwepo na Kijiji kitakachofutwa na hakuna miundombinu itakayoondolewa kwa kuwa ndani ya eneo la kilometa za mraba 1,500 la Pololeti hakuna miundombinu yoyote".

Katika ziara hii tuligundua kwamba eneo hilo lilikuwa ni mali ya vijiji hivyo 14 na hivyo kulikuwa na miundo mbinu ya makazi ya watu. Kutokana nae neo hilo kuwekwa vigingi kwa asilimia 100, baadhi ya wananchi hawana makazi ya kuishi kutokana na eneo lao kuchukuliwa na Serikali bila ya kuwepo mpango mbadala na bila kushirikishwa kikamilifu.

Baadhi ya wananchi imewalazimu kujibanza kwenye maboma ya ndugu zao. Mfano katika kata ya Malambo pekee zaidi ya kaya 600 zimekosa mahali pa kuishi baada ya makazi yao kubomolewa wakati wa zoezi la uwekaji vigingi. Hadi sasa zipo familia zimeshindwa kurudi katika hali yao ya kawaida kimaaisha na wanahitaji kupata msaada wa dharura kuwarudisha katika hali waliyokuwa nayo. Hali hii imechangia umaskini katika jamii kuongezeka zaidi. Mbali na uwepo wa kilio na malalamiko ya wananchi kukosa sehemu za kuishi, Serikali haijawahi kuchukua hatua zozote kunusulu hali hiyo.

### 5.4.3 Mifugo Kufa kutokana na Ukame na hakuna vyanzo mbadala vya maji

Mhe. Kassim Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akitoa hoja ya kuahirisha mkutano wa saba wa bunge la 12 tarehe 30 Juni 2022 alisema;

> *"shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji na makazi zimekuwa chanzo cha uharibifu wa ikolojia... ambayo ni muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa hifadhi zetu hususan Serengeti. Vilevile, shughuli hizo zimechangia uharibifu wa uoto wa asili na kusababisha kukosekana kwa malisho na maji, kupungua uwezo wa kiuchumi kwa wafugaji. Aidha, ongezeko la mifugo limesababisha maeneo yote ya vyanzo vya maji na mito kuharibika. Uharibifu huo mkubwa wa mazingira, pia, umekuwa chanzo cha wanyamapori kutoweka".*

Katika ziara hii tuligundua kwamba wamaasai ni watu walioyatunza maeneo yao kwa miaka mingi na wamekuwa wakiishi na wanyamapori bila kuwadhuru kwa miaka yote walioishi nao. Kutokana na hali hiyo, wanyamapori pia huenda hadi kulala kwenye Mazizi ya ng'ombe ya wamaasai. Lakini baada yae neo hilo kuchukuliwa mifugo imekufa sana kutokana na ukame.

Serikali haijachukua hatua zozote kunusuru hali hii. Hakuna mabwawa yaliyojengwa kwaajili ya mifugo au binadamu. Eneo lililochukuliwa na Serikali ndio lilikuwa chanzo cha maji na malisho kwa mifugo kwa tarafa nzima ya Loliondo na Sale hasa wakati wa kiangazi. Ni eneo ambalo lina vyanzo vya maji hasa mito ya maji safi na salama

kwa mifugo na binadamu. Hivyo hata binadamu waishio Loliondo hawana maji safi na salama kwaajili ya matumizi ya nyumbani. Kwa mfano katika kata ya Arash ilikuwa na ng'ombe 56,000, lakini baada ya eneo kutwaliwa na Serikali ng'ombe 25,000 wamekufa kutokana na ukame.

### 5.4.4 Mifugo kukamatwa, kutaifishwa na kutozwa faini

Wananchi wakazi wa Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale hasa maeneo ya Kirtalo, Soitsambu, Arash, Malambo, Sale, Piyaya, Loliondo, Ololosokwan, n.k. wameendelea kuteseka kutokana na mifugo yao kukamatwa kwa wingi, kuuzwa kwa mnada na mingine kutaifishwa au kutozwa faini ya shilingi laki moja (Tshs. 100,000) kwa ng'ombe na shilingi elf ishirini na tano (Tshs. 25,000) kwa mbuzi au kondoo.

Mfano katika Kijiji cha Kirtalo, wananchi wamelipa faini zaidi ya bilioni moja ya fedha za kitanzania kutokana na mifugo yao kukamatwa kwenye pori la akiba la pololeti. Serikali katika ngazi ya wilaya, mkoa au kitaifa haijawahi kutoa kauli au ufafanuzi wa aina yoyote juu ya utozaji mkubwa huu wa faini. Hali hii imeendelea kuongeza umasikini kwa wamaasai wakazi wa ameneo tajwa siku hadi siku.

### 5.4.5 Uamuzi wa Mahakama dhidi ya Tangazo la Waziri

Mnamo tarehe 19.09.2023, Mahakama kuu ya Tanzania masijala ya Arusha imeamua kuwa Waziri wa Mali Asili na Utalii hajafuata utaratibu wakati anatangaza eneo la vijiji 14 vya Loliondo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1502 kuwa pori tengefu la Pololeti. Mahakama imeweka bayana kuwa tangazo hilo la Waziri No. 421 la 2023 halikufuata utaratibu wa kuwashirikisha viongozi wa eneo husika kuhusu kusudio la kutwaa eneo hilo na hivyo ni batili. Katika kesi hiyo iliyo funguliwa na wananchi 5 wa Loliondo mahakama imeweka bayana kuwa ni takwa la lazima kisheria kwa Waziri kushirikisha viongozi na wadau kabla eneo lao kutwaliwa kuwa pori tengefu.

Mahakama hata hivyo baada ya kuona kuwa Waziri hakufuata utaratibu wa kisheria wa kushirikisha wadau ambao ndio waathirika wa tangazo lake, haikuweza kufuta tangazo hilo kwakua eneo hilo limekwisha tangazwa kuwa pori la Akiba la Pololeti na Rais kwenye tangazo No. 604 la 2022 na kupelekea tangazo la Waziri kukoma.

Badala yake, mahakama imesema njia sahihi ni kufungua shauri dhidi ya tangazo la rais kwa kuwa tangazo la Waziri limekoma tangu tangazo la Rais lilipotangazwa.Hata hivyo, kwenye kesi dhidi ya Tangazo la Rais ambalo limefunguliwa na wananchi 8 wa Loliondo, mahakama imesimamisha operesheni ya Tangazo la Rais No. 604 la 2022 hadi shauri hilo litakapo amuliwa na mahakama.

Kwa tafsiri hiyo ya mahakama ni kwamba, wananchi wanaweza kuendelea kutumia eneo lao kwa ilivyokuwa awali. Na hivyo Serikali inapaswa kuheshimu uamuzi wa mahakama kwa kuacha wananchi kutumia eneo leo kama ilivyokuwa awali kabla ya eneo hilo kutwaliwa. Maamuzi ya mahakama katika mashauri kadhaa ya wafugaji yamekuwa yakipuuzwa na kutotekelezwa kinyume na misingi ya utawala wa sheria. Wananchi wameona njia ya amani na ya kistarabu ya kueleza malalamiko yao ni kwenda mahakamani lakini bado maamuzi ya mahakama hayaheshimiwi.

### 5.4.6 Mapendekezo Mahususi

#### 5.4.1.1 Kwa Serikali

a) Tunashauri Serikali iingilie kati na kusitisha utaratibu wa sasa wa kukamata mifugo katika eneo la Pololeti na kutoza fedha nyingi kwa wananchi. Hadi sasa Katika Kata zote nane, za tarafa ya Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale wananchi wametozwa na kulipa zaidi ya Bilioni tatu tangu eneo hilo kutangazwa kuwa pori tengefu na pori la akiba. Fedha zote hizi zililipwa na wananchi ili kukomboa mifugo yao iliyoshikiliwa hifadhini pamoja na kununua zile zilizotaifishwa na kupigwa mnada. Suala hili limeshusha sana hali ya kiuchumi kwa jamii kwa kuwa wanategemea ufugaji pekee kuendesha maisha yao.

b) Serikali itengue Tangazo lake la Julai 2022 (GN 420) lililofanya eneo la Kilometa 1502 ardhi ya vijiji kuwa eneo la Pori Tengefu la Pololeti ili eneo hilo liendelee kuwa mali ya vijiji na liendelee kuwa eneo la matumizi mseto kama ilivyokuwa hapo awali kwani kwa muda wote wananchi wamekuwa wakitumia eneo hilo hakujawahi kuwa na madhara yoyote kwa wanyamapori.

c) Kwa kuwa wananchi wa kata hizi nane kwa sasa wamekumbwa na janga la njaa kutokana na mifugo kufa kwa kukosa malisho na maji, kutaifishwa na mingine kuuzwa ili kupata fedha za kukombolea mifugo yao. Tunashauri hizi fedha zilizokusanywa zirudishwe katika vijjiji husika kwa ajili ya kutoa huduma za chakula, kulipia ada za wanafunzi ambao kwa sasa wanashindwa kuendelea na masomo pamoja na kutatua changamoto zingine zilizotokana na kumegwa kwa eneo la kilometa za mraba 1,502 zilizokuwa zinatumika kulisha mifugo wakati wa kiangazi.

d) Serikali iruhusu wananchi kuchunga katika eneo la Pololeti wakati wa kiangazi ili ng'ombe wapate malisho na maji ili kuepusha janga la mifugo kufa kwa kukosa malisho kama ilivyotokea kuanzia mwezi Juni mwaka 2022 hadi hivi sasa.

e) Serikali ifanye majadiliano na wananchi juu ya matumizi ya eneo la kilometa za mraba 1,502 ambalo ndio lilikuwa tegemeo pekee kwa wafugaji wa Loliondo na Sale na kwasasa wananchi hawana eneo la malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

f) Ili kurudisha amani, kuondoa hofu na kutibu majeraha yaliyotokana na oparesheni ya kuweka vigingi, tunapendekeza kuwepo na mazungumzo ya maridhiano baina Serikali na wananchi waliaothirika na zoezi lile. Hatua hii itasaidia kubainisha changamoto zilizojitokeza wakati wa zoezi lile na kuhakikisha hazitajirudia katika siku za usoni hapa Ngorongoro au kwingine nchini. Suala hili linaweza kuja na mpango wa ujirani mwema ambao utazingatia pia mambo ambayo wananchi wanaweza kuendelea kunufaika nayo katika eneo hilo kama malisho, kazi za utalii n. k.

g) Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa zifungue milango na kuweka mazingira mazuri kwa mashirika ya watetezi wa Haki za Binadamu kufanya kazi Wilayani Ngorongoro, hasa kupeleka miradi ya maendeleo kwa jamii.

h) Serikali kufanya tathmini shirikishi juu ya changamoto zilizojitokeza wakati wa oparesheni ya kuwaondoa watu na kuweka vigingi katika tarafa ya Sale na Loliondo.

#### 5.5.6.2 Kwa Wananchi

a) Tunawaomba wananchi waendelee kutumia njia za kimahakama katika kudai haki zao pale ambapo zimekiukwa.

b) Tunawaomba wananchi kufanya mikutano na kujadiliana juu ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabili.

c) Tunawashauri wananchi kuendelea kudumisha utamaduni wao unaofaa kwa utunzaji wa mazingira kama ambavyo wamekuwa wakifanya katika maisha yao ya kawaida. Ufugaji wa mifugo, wenye mipango ya matumizi bora ya ardhi, unaoruhusu wanyamapori kama nyumbu kuzaliana na baadae wafugaji kutumia nyumbu na wanayama wengine wakihama kwenda upande mwingine wa hifadhi, ni ufugaji unaofaa kuendeleza na usio hatarishi kwa mazingira.

d) Tunawashauri wananchi wajikite kuboresha ufugaji kwa kujikita kwenye ufugaji wa kisasa kwa kuwafuga wanyama wachache lakini wenye tija. Pia tunawashauri wajihusishe na shughuli zingine za Kiuchumi na ujasiriamali kama ufugaji wa nyuki, biashara na kilimo.

#### 5.5.6.3 Kwa Wadau wa Maendeleo

a) Tunawaomba wadau wa maendeleo kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Loliondo na Sale. Katika wilaya nzima ya Ngorongoro hakuna miradi mingi ambayo inatekelezwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi hivyo ni muhimu wadau kushiriki katika kuiendeleza wilaya ya Ngorongoro.

b) Tunawaomba wahimize Serikali na wadau wengine uzingatiwaji wa haki za binadamu na utawala wa sheria katika masuala mazima ya utwaaji wa ardhi ya wananchi hasa wafugaji ambao wameonekana kuathirika zaidi katika kipindi hiki.

c) Tunawaomba wadau wa Haki za Binadamu na wadaue wengine wa Maendeleo wawe wanatembelea maeneo yanayoathiriwa na zoezi la utwaaji wa ardhi wakiwa kama watu huru na wawe wanafanya mikutano na wananchi. Hii itasaidia kupata taarifa sahihi kuhusu mchakato mzima.

#### 5.5.6.4 Kwa Watetezi wa Haki za Binadamu /CSOs

a) Tunaziomba Asasi za Kiraia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Loliondo na Sale. Kwa mfano miradi ya maji, afya, elimu, uwezeshaji wa kiuchumi hasa kwa Wanawake na Vijana

b) Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Loliondo na Sale

c) Kuendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wakazi wa tarafa ya Loliondo na Sale

d) Kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kutatua changamoto katika tarafa ya Loliondo na Sale.

SURA YA 5
SEHEMU YA TANO

# MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO

## 5.0 UTANGULIZI

Sehemu hii ya tano inaelezea mapendekezo ya jumla kwa tarafa ya Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale. Mapendekezo haya yanatokana na yale tuliyoyaona wakati wa ziara. Hivyo, sura hii inatoa mapendekezo ya jumla kuhusu matokeo ya ufuatiliaji wa yale yaliyotokea wakati na baada ya kufanyika kwa zoezi la utwaaji wa ardhi ya vijiji pamoja na kutoa hitimisho la taarifa hii.

### 5.1 Mapendekezo ya Jumla

a) Serikali inapaswa kuingilia kati na kusitisha utaratibu wa sasa wa kukamata mifugo katika eneo la Pololeti na kutoza fedha nyingi kwa wananchi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba suala hili limeshusha sana hali ya kiuchumi kwa wananchi kwa kuwa wanategemea ufugaji pekee kuendesha maisha yao.

b) Tunapendekeza Tume Huru ya Majaji iundwe kuchunguza ukiukwaji wa Haki za Binadamu uliotokea wakati wa zoezi la utwaaji wa ardhi ya Vijiji na kugeuzwa kuwa eneo la Pori la Akiba.

c) Serikali ione umuhimu wa kurudisha fedha zilizokusanywa kwenye vijiji husika kwa ajili ya kutoa huduma za chakula, kulipia ada za wanafunzi ambao kwa sasa wanashindwa kuendelea na masomo pamoja na kutatua changamoto zingine zinazowakabili.

d) Kutokana na ukweli kwamba wamasai wamekuwa mstari wa mbele katika kutunza mazingira, basi Serikali iwaruhusu wananchi kuchunga katika eneo la Pololeti wakati wa kiangazi ili ng'ombe wapate malisho na maji ili kuepusha janga la mifugo kufa.

e) Serikali ione umuhimu wa kufanya majadiliano na wananchi juu ya matumizi ya eneo la kilometa za mraba 1,502 ambalo ndio lilikuwa tegemeo pekee kwa wafugaji wa Loliondo na Sale na kwasasa wananchi hawana eneo la malisho na maji kwaajili ya mifugo.

f) Serikali ikamilishe ujenzi wa barabara ya Loliondo - Mto wa mbu kwa kiwango cha lami ili isaidie kuvuta vichocheo vya kiuchumi ambavyo vinaweza kutoa shughuli mbadala za kiuchumi kwa wafugaji.

g) Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa ifungue milango na kuweka mazingira mazuri kwa mashirika na watetezi wa haki za binadamu kufanya kazi Wilayani Ngorongoro, hasa kupeleka miradi ya maendeleo kwa jamii.

h) Serikali kufanya tathimini shirikishi juu ya changamoto zilizojitokeza wakati wa oparesheni ya kuwaondoa watu na kuweka vigingi katika tarafa ya Sale na Loliondo. Kuwepo na tume ya kuanzisha majadiliano na maridhiano ili watu wakae kwa amani.

i) Wananchi pamoja na viongozi wa kimila na kisiasa watafute fursa ya kufanya majadiliano na Serikali ya wilaya, mkoa na wizara husika ili waweze kutatua changamoto ya mifugo kukamatwa na suala zima la faini na eneo la malisho ya mifugo yao.

j) Wananchi wanapaswa kufanya mikutano mbalimbali na kujadiliana juu ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabili.

k) Wananchi wanapaswa kubuni shughuli nyingine mbalimbali za kufanya ili kukuza uchumi wao tofauti na kutegemea ufugaji pekee ambao kwa kiasi kikubwa umezuiliwa na mazingira yalivyo kwasasa.

l) Serikali ya Wialya iache kusumbua wananchi kwa swala la uraia na kuwapa vitambulisho vyao vya taifa.

m) Tunawaomba wadau wa maendeleo kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Loliondo na Sale. Katika wilaya nzima ya Ngorongoro hakuna miradi mingi ambayo inatekelezwa kwaajili ya maendeleo ya wananchi hivyo ni muhimu wadau kushiriki katika kuiendeleza wilaya ya Ngorongoro.

n) Kwa upande wa asasi za kiraia ni wakati sasa wa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika tarafa ya Loliondo na Sale. Kwa mfano miradi ya maji, afya, elimu, kiuchumi hasa kwa wakina mama n.k.

o) Tunawahimiza watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia kuendelea kufuatilia hali ya haki za binadamu katika tarafa ya Loliondo na Sale

p) Wananchi wenyeji wa Ngorongoro wameitaka Serikali wapitie mchakato wa ulipaji fidia kwa kuwa sio shirikishi na wala hauko wazi. Na kuwa kiwango cha Milioni Kumi kama pesa ya fidia kwa kila kaya iongezeke hadi kufikia million 50 au million 100 kwa atakayetaka kuchagua kuchukua hela na kwenda anakotaka yeye

### 5.2. Hitimisho

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania pamoja na wanachama wake walioshiriki katika kufanya ziara, tunatoa shukrani kwa wananchi na viongozi waliotoa ushirikiano wakati wa ziara. Tunawashukuru kwa kutupatia taarifa mbalimbali na muhimu kwaajili ya uandishi wa taarifa hii. Pia tunawashukuru wadau mbalimbali ambao wamekuwa katika mstari wa mbele katika kuhamasisha, kuhifadhi, kulinda na kuendeleza haki za binadamu, utawala bora na utawala wa sheria nchini. Sisi kama watetezi wa haki za binadamu tumetimiza wajibu wetu wa kufuatilia swala hili na kuandaa haya mapendekezo kwa makundi husika. Uwezo wetu kama watetezi unaishia hapa kwenye kushauri, hivyo endapo mapendekezo haya hayatafanyiwa kazi tunaomba wananchi waelewe kuwa majukumu yetu yanaishia kwenye kushauri.




Mikocheni B, Eyasi Road, P.o.box 105926,
Dar Es Salaam, Tanzania
+255 769 642208
info@thrdc.or.tz
www.thrdc.or.tz

Like us on
TANZANIA HUMAN RIGHTS DEFENDERS COALITION

Follow us on
@thrdccoalition

Follow us on
@thrdccoalition